# MATESO YA DHURIA YA MTUME

**Mwandishi:**
Ayatullah Murtadha Mutahhari

**Mtarjumi:**
Salman Shou

**Kimehaririwa na:**
Al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo

**ترجمة**

# مقتل المطهر

تأليف

**مرتضى المطهري**

من اللغة الإنجليزية إلى اللغة السواحلية

©**Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

**ISBN:** 978 - 9987 - 512 - 34 - 8

**Kimeandikwa na:**
Ayatullah Murtadha Mutahhari

**Kimetarjumiwa na:**
Salman Shou

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Julai, 2013
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@raha.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** w.w.w.alitrah.info

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji ........ 13
Utangulizi ........ 14
Falsafa na Umuhimu wa Kusimulia Mateso ya Ahlul-Bayt (a.s) ........ 16
**MAJILISI 1 ........ 18**
Imam Ali (a.s.) anangojea Usiku wa Shambulizi ........ 18
**MAJILISI 2 ........ 19**
Kufa Kishahidi kwa Mtazamo wa Imam Ali (a.s.) ........ 19
Siku za Mwisho za Uhai wa Ali ........ 20
Ndoto ya Imam Ali (a.s.) Katika Usiku wa Shambulizi ........ 21
Mabata Yalalamika ........ 22
Adhana ya Mwisho ya Imam Ali (a.s.) ........ 23
**MAJILISI 3 ........ 25**
Imam Ali (a.s.) Anajitayarisha Kukutana na Mola ........ 25
Ee Mola! Nichukuwe haraka ........ 25
"Nimefaulu, kwa Mola wa Kaaba!" ........ 26
"Namshukuru Allah, Matakwa yangu ya siku nyingi hatimaye yametimizwa ........ 27
Wosia wa Imam Ali Katika Kitanda alichofia Kishahidi ........ 29
**MAJILISI 4 ........ 33**
"Nilikuwa naingojea Siku hii." ........ 33
**MAJILISI 5 ........ 34**
Nyakati za mwisho za Imam Ali (a.s.) ........ 34
Tabibu wa Kufa amfanyia vipimo Ali (a. s.) ........ 34
Ummu Kulthum azungumza na Ibn Muljim ........ 35
Mapendekezo ya Imam Ali (a. s.) kuhusu muuaji wake ........ 35
Kikombe cha maziwa kwa ajili ya Ibn Muljim ........ 36
Nini kinaweza kuwa bora zaidi kuliko Shahada wakati wa ibada? ........ 36
Ushauri wa mwisho wa Imam Ali (a. s ) ........ 37
**MAJILISI 6 ........ 39**
Thamani ya Mahari – Damu ya Ali (a.s.) ........ 39
Msimuue huyo Khawarij baada yangu ........ 40
Kuhudhuria Maziko wakati wa Usiku ........ 41
Kuonewa kwa Ali (a.s.) ........ 43

**MAJILISI 7 ........................................................................................ 44**
Imam Ali (a.s.) alizikwa kwa siri ........................................................................ 44
Shairi la huzuni la Sasa`ah kwenye kaburi la Imam Ali (a.s.) ......................................... 45
**MAJILISI 8 ........................................................................................ 47**
Sasa`ah, Sahaba Mashuhuri wa Imam Ali (a.s.) ................................................................ 47
Siku ya Kwanza ya Ukhalifa wa Ali........................................................................ 47
Baada ya Kujeruhiwa kwa Imam Ali (a.s.) ...................................................................... 47
Baada ya mazishi ya Ali ................................................................................. 48
**MAJILISI 9 ........................................................................................ 50**
Ali (a.s.) na Haki wana maana ya karibu sana ................................................................ 50
Darmiyya amsifu Ali (a.s.) mbele ya Muawiyah ............................................................ 50
Adi asoma shairi la kumsifu Ali (a.s.) ..................................................................... 51
**MAJILISI 10 ........................................................................................ 55**
Tabasamu Lenye maana la Bibi Fatimah ........................................................................ 55
Ujasiri wa Bibi Zahra ................................................................................... 56
Ujasiri wa Bibi Zainab ................................................................................... 57
**MAJILISI 11 ........................................................................................ 59**
Bibi Zahra amhuzunikia baba yake ........................................................................ 59
**MAJILISI 12 ........................................................................................ 60**
Wosia wa Bibi Zahra ..................................................................................... 60
Mahusiano ya Adabu ya Fatimah na Ali (a.s.) ................................................................. 61
Kukosa utulivu kwa Imam Ali (a.s.) kwa kutenganishwa na Bibi Zahra ......................... 62
**MAJILISI 13 ........................................................................................ 63**
Kwa Nini Bibi Fatimah Alizikwa wakati wa Giza la Usiku? ............................................ 64
Ewe Ali, baada ya mazishi, bakia nami kwa muda kidogo ............................................. 64
Ali anaelezea hisia zake ................................................................................. 65
**MAJILISI 14 ........................................................................................ 67**
Mtindo wa maisha rahisi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ................................................ 67
Usahili (ukawaida) wa Bibi Fatimah ....................................................................... 68
Vazi la Usiku wa Siku ya Harusi .......................................................................... 69
Basi kwa nini Bibi Fatimah alikwenda kudai Fadak? ...................................................... 70
Nyakati za mwisho wa Bibi Fatimah ....................................................................... 70
**MAJILISI 15 ........................................................................................ 72**
Ukatili juu ya Imam Hasan (a.s.) ........................................................................ 72
Ukatili na Uhalifu wa Muawiyah ........................................................................... 72
Amri ya kumlaani Ali (a.s.) mbele ya Imam Hasan (a.s.) ............................................. 74

**MAJILISI 16 ........................................ 76**
"Usiondoke kwenye mimbari" ........................................ 76
Huduma ya Mkuu wa Mashahidi ........................................ 76
**MAJILISI 17 ........................................ 78**
Imam Sadiq aomboleza kifo cha Husain (a.s.) ........................................ 78
**MAJILISI 18 ........................................ 80**
**MAJILISI 19 ........................................ 82**
Binti yake Muslim apewa taarifa ya Shahada ya Muslim ........................................ 85
Watoto wa Aqiil waahidi utii ........................................ 85
**MAJILISI 20 ........................................ 86**
Hadhi ya Masahaba wa Husain ........................................ 86
**MAJILISI 21 ........................................ 88**
Masahaba Watiifu Sana ........................................ 88
Hali ya Ujasiri ........................................ 90
Dini na Dunia ........................................ 90
Mwanzo wa vita na matokeo yake ........................................ 91
Kifo cha Kishahidi cha Abis bin Abi Shabiib Shakri........................................ 92
Mama mwenye kujitoa muhanga wa Abdullah bin Umair ........................................ 94
Mtoto anayestahili Kusifiwa ........................................ 95
**MAJILISI 22 ........................................ 97**
"Yeyote ambaye hana moyo wa kujitoa muhanga asije." ........................................ 97
Masahaba wa Husain watahiniwa ........................................ 98
Mafanikio makubwa sana ya harakati za Imam Husain ........................................ 98
Hurr, mfano wa dhamira iliyozinduka ........................................ 99
Hurr atubia ........................................100
"Je, toba yangu inaweza kukubaliwa?" ........................................101
Kwa nini Hurr hakuingia kwenye hema la Imam? ........................................102
Mazungumzo baina ya jeshi la Umar bin Saad na Hurr ........................................102
Imam Husain (a.s.) amwendea Hurr wakati wa mwisho wa uhai wake ........................................103
Uhai wangu nauwe muhanga kwa ajili ya Abbas ........................................104
Imam auendea Mwezi wa Bani Hashim ........................................104
**MAJILISI 23 ........................................ 106**
Mkesha wa Ashura ulikuwa kama Miraj kwa wale wafuasi ........................................106
Mvumo wa sauti za wafuasi ........................................106
Toba yakubaliwa ........................................107
Hurr alikuwa na dhamira hai ........................................108
Huruma na upole wa Husain (a.s.) ........................................108

**MAJILISI 24 ........................................................................................ 110**
Ushauri wa mke wa Zuhair ........................................................................ 110
Nguvu ya mvuto ya Husain ........................................................................ 111
Zuhair sasa awa juu ya orodha ya masahaba wa Imam Husain ....................................112
**MAJILISI 25 ........................................................................................114**
Imam Husain amwendea Mtumwa wa ki-Habeshi [Ethiopia] ......................................114
Kifo cha Kishahidi cha mtumwa kutoka Rumi ..............................................................115
**MAJILISI 26 ........................................................................................117**
Nichukue pamoja nawe ..............................................................................117
**MAJILISI 27 ........................................................................................ 120**
**MAJILISI 28 ........................................................................................ 121**
**MAJILISI 29 ........................................................................................ 123**
Wito wa Imam Husain (a.s.) kwa ajili ya msaada ........................................................ 124
Kifo cha Kishahidi cha Mtoto Mchanga ........................................................ 125
Imam Husain (a.s.) alijipaka damu hiyo usoni mwake ............................................... 125
Alasiri ya tisa Muharamu .............................................................................. 125
Mkesha wa Ashura ..................................................................................... 125
Utiifu wa Muhammad bin Bashir Hadhrami ..................................................... 127
Mtukufu, Qasim bin Hasan ............................................................................ 127
"Mimi ni mwana wa Hasan" ........................................................................... 129
Kichwa cha Qasim kwenye mapaja ya ami yake ......................................................... 129
"…..Usisimulie sehemu hii ya mateso ya Qasim." ...................................................... 130
**MAJILISI 30 ........................................................................................ 132**
Wallahi, mimi sitamuacha Ami yangu ............................................................ 132
**MAJILISI 31 ........................................................................................ 134**
"Kuamrisha mema" Na "Kukataza maovu – Misingi ya harakati za Husein (a.s.) ........ 134
Mtoto anayenyonya anatengana na Imam Husain (a.s.) ............................................. 134
**MAJILISI 32 ........................................................................................ 136**
Nguvu za mvuto wa Mihemuko na hisia za Husain .................................................. 136
Kutambuliwa kwa Ali Akbar .......................................................................... 136
Kifo cha kishahidi cha Ali Akbar .................................................................... 137
**MAJILISI 33 ........................................................................................ 139**
Kuaga kwa Vijana wa Bani Hashim ................................................................. 139
Ali Akbar, mwenye kufanana sana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ............................... 140
Kuondoka kwa Ali Akbar kwenda kupambana ............................................................ 140
Laana ya Imam Husain(a.s.) .......................................................................... 140
Kiu ya Ali Akbar ..........................................................................................141

**MAJILISI 34 .......... 143**
Mihemuko ya binadamu waliokamilika .......... 143
Haiba kubwa ya Ali Akbar .......... 144
**MAJILISI 35 .......... 145**
Mwezi wa Bani Hashim - Mfano Halisi wa Muhanga .......... 145
**MAJILISI 36 .......... 147**
Utiifu wa Abbas .......... 147
Ujasiri wa Mtukufu Abbas .......... 148
Mwezi wa Bani Hashim na Usawa .......... 148
Abbas, Mwangalizi wa kambi ya Imam Husain (a.s.) .......... 149
Nauha ya Ummul Banin ndani ya Baqii .......... 150
**MAJILISI 37 .......... 152**
Vitendo viovu vya Dhalimu Yazid .......... 152
Ufalme wa Bani Umayyah watikiswa .......... 153
Athari ya harakati za Husein yaenea kwenye nyumba ya adui .......... 153
Mtoto wa Yazid ajitenga na baba yake .......... 154
Mashahidi walionea wivu daraja la Abbas .......... 155
Barua ya Msamaha kwa watoto wa Ummul Banin .......... 155
Mashairi ya kuhuzunisha ya Ummul Banin .......... 156
**MAJILISI 38 .......... 158**
Ashura, ile Siku ya Mashahidi .......... 158
Mantiki ya Kufa Kishahidi (ufia dini) .......... 158
Mkesha wa Ashura .......... 158
Viriba vya maji vitupu .......... 159
Hotuba ya Imam Husain (a.s.) kwenye Mkesha wa Ashura .......... 159
Majibu ya Imam Husain (a.s.) kwa Farazdaq .......... 160
Ushuhuda wa Imam Husain (a.s.) kuhusu masahaba na Ahlul-Bayt (a.s.) .......... 161
Yeyote anayetaka kuondoka yuko huru kufanya hivyo .......... 161
Furaha ya Imam Husain (a.s.) yaongezeka maradufu .......... 162
Masahaba waonyesha utiifu wao .......... 162
Kwa nini Imam Husain (a.s.) aliruhusu masahaba kubakia? .......... 163
Kifo cha mfiadini kinatia uhai kwenye jamii .......... 164
**MAJILISI 39 .......... 166**
Tisa (*Tasua*) ya Imam Husain (a.s.) .......... 166
Nini kilitokea mnamo alasiri ya Tisa? .......... 167
Hali ya Bibi Zainab mnamo mkesha wa Ashura .......... 167
Kwa nini Imam aliomba kuahirishwa kuanza vita? .......... 170

Utambuzi wa Qasim ........................................................................................ 172
Ewe ami yangu! Nisaidie ................................................................................ 173
**MAJILISI 40 ........................................................................................ 175**
Imam Husain (a.s.) ni Muhajiri na Mujahidi pia ......................................... 175
Kifo cha kishahidi ni taji la kujivunia kwetu sisi ......................................... 176
Ni wale tu walio safi ndiyo walibaki ............................................................ 177
Hao walikuwa taji la mashahidi wote ........................................................... 177
Heshima kwa masahaba wa Husain ............................................................ 178
**MAJILISI 41 ........................................................................................ 179**
Umashuhuri wa Roho ya Imam Husain ...................................................... 179
Semi za Imam Husain (a.s.) wakati wa mwisho wa uhai wake ................................... 179
Viashirio vya ujasiri kwenye hotuba za Husain ......................................... 180
**MAJILISI 42 ........................................................................................ 184**
Swala – Nguzo ya dini .................................................................................... 184
Swala ya mwisho ya Imam Husain (a.s.) ..................................................... 184
Said bin Abdullah - shahidi wa Swala ........................................................... 185
Imam Husain (a.s.) anarukuu na kusujudu kwa mara ya mwisho ............................. 186
**MAJILISI 43 ........................................................................................ 187**
Maneno ya Imam Husain (a.s.) wakati akiwa anaondoka kwa mara ya mwisho ........ 187
Zainab al-Kubra azungumza kwenye baraza ya Yazid .................................. 188
**MAJILISI 44 ........................................................................................ 189**
Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alimlilia Khadija ........................................... 189
Wosia wa Khadija kwa Asma ......................................................................... 189
Mapenzi ya Imam Husain (a.s.) kwa Bibi Rabab na Sakina .......................................... 190
Rabab aomboleza kifo cha Imam Husain (a.s.) ..............................................191
“Binti yangu Sakina, usiufanye moyo wangu uteseke zaidi.” .......................................191
**MAJILISI 45 ........................................................................................ 193**
Fedheha haivumiliki ........................................................................................ 193
Aliyelelewa kwenye mapaja ya Fatimah hawezi kuvumilia fedheha .......................... 194
Kiu ya Imam Husain (a.s.) mnamo siku ya Ashura .................................................... 195
Mashairi ya *Nauha na Matam* ......................................................................... 195
Falsafa ya kuhuisha Ashura ........................................................................... 197
Ashura ni siku ya kuhuisha maisha .............................................................. 198
Ishara za kuambatana na roho ya Imam Husain (a.s.) ............................................... 198
Kauli Mbiu ya Husain ........................................................................................ 199
Kumlilia Imam Husain (a.s.) ........................................................................... 200
Ushujaa wa Imam Husain ................................................................................201

Roho ya Ali ndani ya mwili wa Husain ....201
Hisia za heshima za U-Husain .... 202
Kauli Mbiu ya Kumpwekesha Mungu .... 202
Imam Husain (a.s.) anaaga .... 203
Mazungumzo ya Sakina na Dhuljanah .... 204
*Nauha* ya Imam wa zama zetu (a.t.f.s.) .... 204
**MAJILISI 46 .... 205**
Mashindano baina ya sifa za ki-Husain Siku ya Ashura .... 205
Utulivu wa Imam Husain (a.s.) .... 205
Mapinduzi ya Imam Husain yalichochea mapinduzi mengine .... 206
Shambulio la kwanza dhidi ya utawala wa Bani Umayyah .... 206
Hisia ya heshima ya Imam Husain .... 207
Bishara njema za Imam Husain (a.s.) wanafamilia wake .... 207
Imam Husain ni dhihirisho la hali ya heshima Tukufu .... 208
Dhuljanah wa Imam Husain (a.s.) .... 209
Mshale wenye sumu wachoma moyo wa Imam Husain (a.s.) ....210
Abdullah bin Hasan alijitoa muhanga kwa ajili ya ami yake .... 211
**MAJILISI 47 .... 213**
Maneno ya mwisho ya Imam Husain (a.s.) ....213
**MAJILISI 48 .... 214**
Kifo kwa ajili ya mtu shujaa ....214
"Mfungwa wa dunia hii hatambui yalioko dunia zingine" ....215
Hisia za kuvunjika vipande vipande katika njia ya Allah ....216
Nyanda za chini za ufiadini ....216
**MAJILISI 49 .... 218**
Furaha ya Imam Husain (a.s.) wakati wa Shahada yake ....218
Kulinda kambi hadi dakika za mwisho ....219
"Mtu yeyote asitoke nje ya mahema wakati ningali hai" ....219
Familia ya Imam wasoma Nauha wakimzunguka Dhuljanah .... 220
Swali la kuhuzunisha la Sakina kwa Dhuljanah .... 220
**MAJILISI 50 .... 222**
Wakati mgumu sana kwa Ahlul-Bayt wa Imam (a.s.) .... 222
Ufidhuli wa adui .... 223
Kifo cha kishahidi cha Ali Asghar .... 223
Bibi Zainab alihisi ana deni kwa Husain (a.s.) .... 224
Mama ambaye mwanawe alikatwa kichwa mbele yake .... 225

**MAJILISI 51 ........................................................................................ 227**
Bibi Zainab aongoza msafara ........................................................................ 227
"Tupitishe katikati ya uwanja wa vita" ........................................................ 227
Bibi Zainab aomboleza kwenye mwili wa kaka yake .................................. 228
Wajibu wa Bibi Zainab ................................................................................... 228
Hadithi iliyosimuliwa na Ummu Aiman ...................................................... 229
Msafara wa mateka wa kivita ndani ya Kufa ............................................... 230
Hotuba ya Bibi Zainab ilikumbusha moja ya hotuba za Ali (a.s.) ................ 230
Hadhi na Staha ya Bibi Zainab .......................................................................231
**MAJILISI 52 ........................................................................................ 235**
Bibi Zainab kwenye baraza ya Ibn Ziyad ..................................................... 235
**MAJILISI 53 ........................................................................................ 236**
Wauaji wa Imam Husain (a.s.) waliupa uhalifu wao sura ya kidini ............ 236
Kipofu hakuruhusu hila ya Ibn Ziyad ifaulu ............................................... 237
Mantiki ya Ibn Ziyad iliegemezwa kwenye mabavu .................................... 238
Kiwango cha fedheha kulingana na maneno ya Bibi Zainab ....................... 240
Ibn Ziyad aliamuru Bibi Zainab auawe ..........................................................241
Jina la Ali lawachukiza maadui .......................................................................241
Ngao ya Imam Sajjad (a.s.) ............................................................................ 242
**MAJILISI 54 ........................................................................................ 243**
Roho zetu haziwezi kufungwa nyororo ........................................................ 243
Bibi Zainab kwenye ukumbi wa Yazid .......................................................... 243
"Mtume alikuwa na desturi ya kubusu midomo ile." .................................. 245
**MAJILISI 55 ........................................................................................ 246**
Zainab - mrithi wa umaarufu wa Ali na Fatima ........................................... 246
Wafungwa ndani ya kasri ya Yazid ................................................................ 247
Hotuba ya Bibi Zainab ndani ya ukumbi wa Yazid ...................................... 247
Bibi Zainab aleta mapinduzi Syria ................................................................. 248
**MAJILISI 56 ........................................................................................ 250**
Familia ya Imam ndani ya gereza la Syria .................................................... 250
**MAJILISI 57 ........................................................................................ 252**
Wafungwa waliohuisha historia ya Karbala ................................................. 252
Imam Sajjad (a.s.) ahutubia mkusanyiko wa swala ya Ijumaa ..................... 252
Ewe Muadhini! Nyamaza ............................................................................... 254
**MAJILISI 58 ........................................................................................ 255**
Gereza la Syria ................................................................................................. 255

**MAJILISI 59 ........ 257**
Imam Sajjad (a.s.) – mfano halisi wa Upendo ........ 257
Kuhudumia msafara unaokwenda Hijja ........ 257
Kulia na Kusoma Dua kwa Imam Sajjad (a.s.) ........ 258
**MAJILISI 60 ........ 260**
Kifo cha kishahidi cha Imam Musa Kadhim (a.s.) ........ 260
Athari za gereza kwa uhalifu wa kupenda uhuru ........ 263
Sheria ya vinyume na migongano ........ 264
Bibi Zainab Kubra ........ 265
Kusema na kupenda ukweli ........ 266
Gereza la Basra ........ 267
Gereza la Baghdad ........ 268
Afisa mkubwa amtembelea Imam ........ 269
Kutosheka kwa Imam Musa Kadhim (a.s.) ........ 269
**MAJILISI 61 ........ 271**
Kifo cha kishahidi cha Imam Ridha (a.s.) ........271
*Hadith Silsilatudh-Dhahab* ........271
Imam Ridha (a.s.) asipitishwe sehemu zenye Shia wengi ........ 272
Imam Ridha (a..s.) akiwa Nishapur ........ 272
Ngome ya Tauhidi ........ 273
Hotuba ya Bibi Zainab Kubra katika soko la Kufah ........ 274
**BIBLIOGRAFIA ........ 277**

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjumi ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho, *Sufferings of the Prophet's Descendants*, kilichoandikwa na Ustadh Murtadha Mutahhari. Sisi tumekiita, *Mateso ya Dhuria ya Mtume.*

Ni jambo la kusikitisha na kuhuzunisha sana kuona kwamba historia ya Uislamu imejaa mateso waliyofanyiwa Dhuria ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w), Mtume ambaye ni rehema kwa ulimwengu lakini kwa Kizazi chake imekuwa kwao ni mateso yasiyomithilika. Sababu ya kufanyiwa mateso hayo kunatokana na kutaka kwao kusimamisha haki katika ulimwengu kwa kufuata nyayo za Mtukufu Mtume.

Makafiri walimfanyia Mtume (s.a.w.w) vitimbi vya kila aina, lakini hatimaye kwa uwezo wa Allah aliweza kuwashinda na Uislamu ukasimama na kuwa imara. Lakini baada tu ya kufariki Mtume (s.a.w.w) waliibuka watawala madhalimu ambao walipinga mafundisho ya Uislamu ya kuleta usawa na haki kwa watu wote. Hivyo, ili kutekeleza malengo yao ya kidhalimu, waliwatesa na kuwauwa Dhuria ya Mtume (s.a.w.w) au kwa jina lingine Ahlul Bayt (a.s) ambao ndio waliokuwa na dhamana ya kuhakikisha kwamba Uislamu unaendelea kusimama na kustawi.

Kitabu hiki kimekusanya maelezo ya mateso ya Ahlul-Bayt (a.s.) kutoka kwenye majilisi 61 (hotuba za maombolezo) za Ustadh Shahid Murtadha Mutahhari ambazo zinaweza kukidhi haja ya wasomaji wa majilisi kwa kiwango fulani.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Salman Shou kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki kwa Kiswahili kutoka lugha ya Kiingereza. Aidha tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

# UTANGULIZI

بِسْمِ اللهِ الرَحْمـنِ الرَحِيم

**Amani iwe juu yenu, Enyi Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w.)**

Siku moja nilikuwa nimekaa peke yangu nikijihesabu mwenyewe na kupitia orodha ya matendo yangu. Kila nilivyozidi kufikiria juu ya hilo ndio nilivyozidi kugundua hasara kubwa katika matendo yangu na ilielekea kuwa vigumu mimi kupita katika njia za Akhera. Nikajiambia mwenyewe 'msafara umeondoka wakati wewe ulikuwa umelala. Sasa huko uendako kuna jangwa pana lisilokuwa na mwisho. Utakwenda wapi? Utamuuliza nani akuelekeze njia ya kukufikisha uendako? Na utaokoka vipi? Utawezaje kuvuka hatua za kutisha zilizoko mbele ukiwa huna kitu chochote?'

Nilikuwa nimezama kwenye mawazo haya wakati nuru ya matumaini ilipotokeza. Kutoka kwenye kina cha moyo wangu uliokuwa umedhikika, mara sauti ilisema: "Ewe uliyechanganyikiwa kwenye mashaka, kama unataka kufika kwenye kingo za matumaini yako, kwa nini usipande Safina ya Wokovu? Umesahau kwamba wale wanaopanda humo wataokolewa na wale wanaoitelekeza watakufa maji?[1] Kwa nini usichukue msaada wa wale ambao ni wacha Mungu wa kweli na kimbilio halisi? Hao ndio nuru inayoongoza msafara wa kumpwekesha Mwenyezi Mungu (*Tawhidi*). Wao wamepita katika mizani za hali ya juu za uongozi halisi. Hao ni milango ya Mwenyezi Mungu, watakuongoza hadi kwa Mwenyezi Mungu. Katika baraza tukufu la waombezi hawa wa hapa duniani na akhera onyesha mapenzi asilia kwa namna ambayo itaondoa vizuizi vyote vilivyomo kwenye njia iliyonyooka na njia hiyo inakuwa nyeupe na safi kwa ajili yako, kwa sababu kama viongozi watakatifu wa msafara huo wanaongoza njia yako, utafaulu kufika kule unakotaka kwenda bila kushindwa; lakini ukisafiri bila ya uongozi wao kamwe hutaweza kupata njia yako."

[1] Imetolewa kutoka kwenye Salawat iliyosimuliwa kutoka kwa Imam Zainul Abidiin (a.s.), ambayo husomwa kila siku ndani ya mwezi wa Shaaban.

Katika miezi michache iliyopita, ilikuwa ni tamaa ya moyo wangu kwamba inanibidi kufanya kazi ya kuandika kama ilivyo kawaida ya wanazuoni wa dini na wasafiri, ili niweze kutoa, hayo matunda ya kazi yangu kama zawadi kwa hao watu watakatifu. Labda zawadi hii ya unyenyekevu itakubalika na huyu mtu muovu akapata kutazamwa kwa jicho la huruma na wema ili mng`aro wa moyo na macho yake ungerejea, na moyo wake uliochafuka ungeweza kupata utakaso, na nafsi yake isiyo na thamani ibadilike na kuwa yenye thamani tena.

Hivyo, nikamkumbuka yule mwanazuoni mkubwa maarufu ambaye ameandika kwa kuaminika kabisa juu ya mada mbali mbali na ambaye vitabu vyake ni chanzo cha maarifa ya kidini, naye ni Ustadhi Shahid Murtaza Mutahhari. Kwa kiasi nilivyokuwa ninajua, katika vitabu vyake vyote ambavyo vimechapishwa, hakuna hata kitabu kimoja kinachozungumzia mateso ya Ahlul-Bayt (a.s.). Kwa hiyo nilifikiria, ni jambo gani lingekuwa bora zaidi kuliko kukusanya taarifa kuhusu mada hii kutoka kwenye vitabu mbalimbali vya mwanafikra huyu?

Nikiwa na kusudio hili akilini mwangu, nilianza kupitia vitabu vya Ustadhi Shahid na nikakusanya kazi hii iliyopo sasa. Baada ya hapo, nikafanya utafiti na kuongeza rejea ili kuweza kupata kitu kamili hiki cha mwisho.

Mambo yafuatayo ni muhimu kuyazingatia:

1. Katika kitabu hiki tumekusanya mateso ya Ahlul-Bayt (a.s.) kutoka kwenye Majilisi 61 (hotuba za maombolezo) za Ustadhi Shahid, ambazo zinaweza kukidhi haja ya Wahutubiaji wa Majilisi, kwa kiwango fulani.
2. Katika kukusanya na kutafiti taarifa hizi, sisi tumejaribu kadiri iwezekanavyo kuendeleza mtindo wa asili wa Ustadhi Shahid.
3. Taarifa nyingi zaidi zilikuwa kwenye kanda za sauti, kwa hiyo kuna uwezekano wa maneno yaliyokosekana au vifungu vya maneno. Kwa hiyo, tumelinganisha na vyanzo vya asili, na kama jambo limetajwa katika namna iliyo tofauti tumelionyesha kwenye tanbihi chini ya kurasa.
4. Katika zama hizi, kufuatana na mashambulizi ya kitamaduni ya maadui wa Uislamu, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba kizazi cha sasa kinatambua fikra za mwanazuoni huyu mashuhuri. Kwa hiyo, ingekuwa ni vizuri zaidi kama Wahadhiri wetu watasoma matukio ya msiba wa Karbala kwa mujibu wa Ustadhi Shahid ili kwamba huduma hii isiyolinganishika iliyotolewa naye

itambulike ipasavyo. Tuna matumaini kwamba kupitia kazi hii, kiwango cha usomi wa vijana wetu kitaongezeka na mihadhara yetu itapata uthibitisho wa kisomi.

5. Sifa zote za kitabu hiki ni matokeo ya mapambano ya kisomi na kivitendo ya Ustadhi huyu, uaminifu wake, utakaso wa ndani wa nafsi yake, na msimamo wake, ambapo kama kuna dosari zozote ni kwa sababu ya mtumishi huyu mnyenyekevu.

Mwishoni mwa utangulizi huu, tunawasilisha majibu ya Ustadhi Shahid kuhusu swali aliloulizwa wakati wa siku za maombolezo ya Imam Husain (a.s.) na humo ameeleza haja na umuhimu wa kusimulia mateso ya Ahlul-Bayt; na pia amefafanua falsafa iliyo nyuma ya mateso hayo.

## FALSAFA NA UMUHIMU WA KUSIMULIA MATESO YA AHLUL-BAYT (A.S.)

Ustadhi anasema: "Jana kijana mmoja aliniuliza swali kwa hiyo hapa nitasema jambo kuhusu swali hilo. Kwa kweli, kamwe sijasisitiza kwamba mateso ya Ahlul-Bayt (a.s.) lazima yasomwe katika kila mwisho wa Majilisi. Kama mazungumzo yapo katika jambo ambalo mimi ninaweza kuendelea mbele kuelekea upande mwingine, huwa sisimulii mateso hayo; lakini katika hotuba nyingi, hususan wakati wa msimu wa maombolezo, huamua kutaja baadhi ya mambo ya kusikitisha hata kama yawe kwa ufupi namna gani.

Kijana huyu aliniuliza kama ipo haja yoyote na manufaa ya kusimulia mateso hayo? Iwapo kama lengo letu ni kuhuisha Madhehebu ya Husain (a.s.), hivi ni muhimu kusimulia msiba wa Karbala? Nilimwambia kijana huyo: "Ndiyo ni jambo ambalo Maimamu wetu Watukufu (a.s.) wametuamuru na kuna falsafa katika jambo hili. Kama hakuna vuguvugu la mhemuko wa kweli katika harakati za Madhehebu na inakuwa ni mkusanyiko tu wa mawazo makavu na misingi isiyokuwa na mwelekeo thabiti, haitaathiri nafsi za watu na haitaweza kudumu daima. Hata hivyo kama madhehebu yana nguvu ya kuhamasisha nyoyo na kuwavutia watu,mvuto huu huu unayafanya madhehebu hayo yawe hai. Falsafa ya Madhehebu  ina wajibu wa msingi katika kueneza Madhehebu hayo na inaipatia maneno: kwamba inaifanya inazungumza yenyewe.

Bila shaka, Madhehebu ya Husain ni Madhehebu ambayo falsafa yake huwasha hisia na ndiyo maana yamedumu hadi leo hii. Tunapaswa kuelewa falsafa hii na kuipenda. Kama tukiyawasilisha Madhehebu haya yenye kuleta uhai kama Madhehebu ya kifikra tu, mwale wa Madhehebu haya ambao hugawa ulimi kwenye hisia za watu, utazimika pole pole na Madhehebu haya yatapitwa na wakati na kukosa maana. Ndiyo maana lazima tuendelee kusimulia mateso ya Karbala."

Utambuzi wa kina na uelewa mpana wa mwanazuoni huyu msomi unadhihirika kutokana na matamko ya hapo juu. Kweli, masimulizi ya mateso ya Imam Ali (a.s.), Imam Husain (a.s.), Imam Hasan (a.s.), au Bibi Zahra (a.s.) hugusa hisia za watu na hugawa maneno katika hisia hizo. Watu hupata vuguvugu kutoka kwenye mwale wa hisia hizi, na hisia hizi huwasha tena ndani mwao utambuzi wa wajibu na uelewa wao wa kulinda, jambo ambalo wakati wote tunatakiwa kulifanyia jitihada.

**3, Shawwal 1420 A.H.**
***Ja`far Salihan***

# MAJILISI 1

## IMAM ALI (A. S.) ANANGOJEA USIKU WA SHAMBULIZI

Enyi waombolezaji wa Mtukufu Amiri wa Waumini (a.s.)!

Leo ni tarehe 13 ya mwezi mtukufu wa Ramadhani. Tunakaribia ile mikesha ya kukaa macho na kufanya ibada, na siku ya kufa kishahidi Amiri wa Waumini. Inasimuliwa kwamba Amiri wa Waumini alikuwa anatoa hotuba mnamo tarehe 13 ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, ambayo ilikuwa siku ya Ijumaa. Watoto wake, Imam Hasan (a.s.) na Imam Husain (a.s.) walikaa miongoni mwa wasikilizaji.

Wakati hotuba inaendelea, ghafla alimuuliza Imam Hasan (a.s.): "Mwanangu Hasan! Siku ngapi za mwezi huu zimepita hadi sasa?"

Akajibu: "Baba, zimepita siku 13."

Inaelekea kana kwamba Imam alitaka kufikisha ujumbe muhimu kwa sababu tayari alikuwa anajua siku ngapi zilikuwa zimepita. Baada ya hapo, alimuuliza Imam Husain (a.s.): "Mwanangu! siku ngapi zimebaki katika mwezi huu?" Imam Husain (a.s.) akasema: "Zimebaki siku kumi na saba baba."

Aliposikia hivi, Imam Ali (a.s.) alishikilia ndevu zake na kusema: "Muda mfupi sana umebaki kwa ndevu hizi kupakwa rangi ya damu ya kichwa hiki."[2]

Amiri wa Waumini hakutaja muda kamili na mazingira ya kifo chake cha kishahidi lakini alikuwa akionyesha hali fulani ambayo iliwafanya watu kwa ujumla na hususan familia yake, kufadhaika na kuwa na wasiwasi.[3]

**"Hakuna Nguvu na Uwezo isipokuwa kwa Allah Mwenyezi aliyeko Juu na Muweza wa Yote."**

[2] *Muntahaiul Amaal*, Jz. 1, uk. 330 na *Manaqib Murtazwiyah*, uk. 390.

[3] *Ashnai ba Quran*, Murtaza Mutahhari, Juzuu,6, uk. 146-147

# MAJILISI 2

## KUFA KISHAHIDI KATIKA MTIZAMO WA IMAM ALI (A.S.)

Ramadhani ya mwisho ya uhai wa Imam Ali (a.s.) ilikuwa imejaa mfadhaiko kama ambavyo ilidhihirishwa na tabia ya Imam. Mwezi huu ulikuwa tofauti na miezi yote ya Ramadhani ya miaka iliyopita. Tofauti hii ilionekana wazi katika hisia za watu wa familia ya imam (a.s.). Hata hivyo, ningependa kutaja hiyo hali inayotofautisha, ambayo pia imesimuliwa kwenye *Nahjul-Balaghah*, Imam Ali (a.s.) alisema: Pale Allah Aliyetukuka alipoteremsha aya ifuatayo:

أَحَسِبَ النَّاسُ أَن يُتْرَكُوا أَن يَقُولُوا آمَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ

**Je, watu wanadhani wataachwa waseme "tumeamini," nao wasijaribiwe?"**
**[Surah Al-Ankabut 29 : 2][4]**

Nilipata kujua kwamba usumbufu huo haungetupata almuradi tu Mtume (s.a.w.w.) yu miongoni mwetu. Kwa hiyo nilisema: "Ewe Mtume wa Allah (s.a.w.w.), ni fitina gani hiyo, ambayo Allah amekufahamisha wewe?"[5] Na alijibu, "Ewe Ali, Umma wangu utapita kwenye mitihani mara baada yangu."

Ali aliposikia hayo kwamba baada ya kufariki Mtume (s.a.w.w.) wao watapata majonzi, alikumbuka kitu cha siku za nyuma na akauliza:

"Ewe Mtume (s.a.w.w.), je, mnamo siku ya Uhud wewe hukuniambia kwamba wale Waislamu ambao walikuwa wafe kishahidi tayari wamekwisha pata hadhi ya shahidi?" Siku ile Waislamu sabini walikufa kishahidi, miongoni mwao Mkuu wa Mashahidi, Mtukufu Hamza alikuwa ndiye muhimu zaidi. Pale ambapo kifo cha kishahidi kilinikwepa, jambo ambalo lilinikasirisha sana,[6] na nilikuuliza: Kwa nini mimi nimenyimwa heshima hii?"

---

[4] Qur`ani Surah Ankabuut [29:1-2]

[5] Chapisho la *Faiz al-Islam* la *Nahjul-Balaghah* halina neno *'taa'la.'*

[6] Imam Ali (a.s.) alikuwa kwenye ujana wake wakati wa vita vya Uhud. Alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano tu wakati huo. Ndio kwanza amemuoa Bibi Fatima na Imam Hasan (a.s.) amezaliwa tayari. Kwa kawaida, maharusi vijana matakwa yao ni kuishi pamoja kwa muda mrefu lakini matakwa makubwa kabisa ya Imam Ali (a.s.) yalikuwa kufa kishahidi. [Ustadhi Mutahhari]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: Furahi kwani kifo cha kishahidi kinakufuatilia. Kwani kuna nini kama wewe hukuuliwa kishahidi? Kifo cha kishahidi tayari kimekwisha kuandikwa kwenye majaaliwa yako." Aliposema hivi Mtukufu Mtume aliniuliza:

Kweli jambo hili litakuja kupita, lakini niambie subira yako itakuwaje wakati wa Shahada yako?" Imam Ali (a.s.) akasema: "Ewe Mtume wa Allah (s.a.w.w.) kipindi hicho si kipindi cha subira, bali kwa usahihi zaidi ni kipindi cha furaha na shukrani"[7]

## SIKU ZA MWISHO WA MAISHA YA IMAM ALI (A.S.)

Watu wa familia na masahaba wa Imam Ali (a.s.) hawakuwa na utulivu na walihangaika kwa sababu ya habari ambazo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizitoa na kwa sababu ya ishara hizo zilizoonyeshwa kwa dhahiri na Imam Ali (a.s.) kwa sababu alikuwa anazungumza juu ya mambo yasiokuwa ya kawaida. Wakati wa Ramadhani hii alikuwa na kawaida ya kuhitimisha saumu yake (kufuturu) nyumbani kwa mmojawapo wa watoto wake.[8] Kila siku usiku alikuwa na desturi ya kuwa mgeni wa mmojawapo wa watoto wake. Usiku mmoja alikula nyumbani kwa Imam Hasan (a.s.) na usiku uliofuata alikula nyumbani kwa Imam Husain (a.s.) na halafu nyumbani kwa Bibi Zainab na kuendelea hivyo. Lakini alikuwa anakula chakula kidogo sana.[9]

Kwa mtindo huu watoto wa Imam walikuwa wanaingiwa na huzuni. Kuna wakati walikuwa wakizidiwa na huzuni hadi wanalia. Wakati fulani mmojawao aliuliza: "Ewe baba! Kwa nini unakula chakula kidogo hivi?" Imam alijibu: "Nataka kukutana na Allah tumbo langu likiwa halina kitu"[10] (Watoto wake walikuwa wakielewa kwamba Mtukufu Ali alikuwa anangojea tukio fulani). Wakati mwingine alikuwa na kawaida ya kutazama juu angani na kusema: "Mpendwa wangu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameniarifu na yale aliyoniambia ni ya kweli kabisa. Hawezi kukosea. Muda umekaribia.[11]

Mnamo tarehe 13 Mwezi wa Rajab, alisema jambo fulani, ambalo lilizidisha utata. Ilikuwa siku ya Ijumaa na Imam alikuwa anahutubia. Wakati

[7] *Nahjul-Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 155, Uk. 1481 na *Nahjul-Balaghah*, Subhi Salih, Hotuba ya 156.

[8] Huenda labda hiyo ilikuwa ni desturi yake katika miezi iliyopita ya Ramadhani, (Ustaadh Mutahhari).

[9] *Muntahaiul Amaal,* Juzuu ya 1, Uk. 329.

[10] *Biharul Anwar*, Juzuu ya 42, uk. 224.

[11] *Biharul Anwar,* Juzuu ya 42, uk. 277.

anaendelea kuhutubia alimuuliza Imam Husain (a.s.) "Mwanangu siku ngapi zimebaki katika mwezi huu?" Imam akajibu: "Zimebaki siku kumi na saba baba." Imam Ali (a.s.) akasema: "Ndiyo, baada ya muda mfupi ndevu zangu zitatapakaa damu yangu. Muda wa ndevu hizi kupakwa damu yangu unakaribia."[12]

## NDOTO YA IMAM ALI (A.S.) KATIKA USIKU WA SHAMBULIZI

Enyi waombolezaji! Watoto walipitisha muda kiasi na Mtukufu Ali (a.s.) mnamo mkesha wa tarehe 19. Baada ya watu wote kuondoka, Imam Ali (a.s.) alisogea kwenye mkeka wake wa kuswalia.[13] Imam Ali (a.s.) alikuwa kwenye mswala wake na mapambazuko yalikuwa bado hayajawadia. Imam Hasan (a.s) aliwasili na aliketi karibu naye. Ama ilikuwa ni kwa sababu ya wasiwasi wake au ilikuwa ni tabia yake ya kawaida.

Amiri wa Waumini alikuwa akiwapa heshima maalum Imam Hasan (a.s.) na Imam Husain (a.s.) kwa sababu walikuwa watoto wa Bibi Zahra (a.s.). Yeye alikuwa akichukulia kwamba akiwaheshimu wanawe hao ni sawa na kumheshimu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Bibi Zahra (a.s.). Alimwambia Imam Hasan (a.s.): "Nilikuwa nimeketi pale nikiwa ninasinzia kwa muda fulani. Nikamuona Mtume wa Allah akitokeza mbele yangu nami nikasema, 'Umma wako umenifanya nilie machozi ya damu.'"[14] Kwa kweli ni jambo la kustaajabisha kwamba watu walimpinga Amiri wa Waumini Ali (a.s.) na hawakutaka kutembea katika njia aliyowaonyesha. Watu wamekuwa wakimsumbua mfululizo bila mwisho. Masahaba wa Aisha walivunja kiapo cha utii, na Muawiyah wakati wote alikuwa akila njama dhidi yake. Hali ilikuwa ngumu sana kwa Amiri Ali (a.s.) kuhimili yote haya. Muawiyah alikuwa mkatili hodari sana. Alijua ni kitu gani kinachomkera Amiri wa Waumini (a.s.). Kwa hiyo, naye alikuwa akilifanya hilo. Ni nini kile ambacho Khawarij na wale waliojiita makundi ya Kidini, ambao walikuwa na desturi ya kumshutumu Imam Ali (a.s.) na kumuita kafiri walichokifanya mwishoni?

---

[12] *Muntahaiul Amaal*,Jz. 1, uk. 330; *Manaqib Murtazviyah*, uk. 490.

[13] Inapendekezwa kwamba mtu anatakiwa kutenga sehemu kwa ajili ya ibada tu ndani ya Makazi yake. Mswala wa Imam Ali (a.s.) ulihifadhiwa wakati alipokuwa anaishi Darul Imarah akiwa Khalifa na alikuwa akiswalia juu yake huo. Ilikuwa kawaida yake kwamba alikuwa halali wakati wa usiku na alikuwa akianza ibada zake kwenye msala huu baada ya kumaliza shughuli zake zote. [Ustaadh Mutahhari]

[14] *Nahjul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 69, uk.156; *Nahjul Balaghah*, Subhi Salih, Hotuba ya 70.

Ni jambo la ukweli kwamba mtu atashangaa baada ya kuangalia na kuona yale maisha ya kuhuzunisha ya Imam Ali (a.s.). Hata mlima hauna uwezo wa kuhimili majanga mengi kama alivyofanya Imam Ali (a.s.). Katika hali hiyo Imam Ali (a.s.) angemwambia nani kuhusu mateso yake haya? Alipomuona Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika ndoto, Imam Ali (a.s.) aliufungua wazi moyo wake na akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Umma wako umenisumbua sana. Niambie nifanye nini kuhusu suala hili?" Halafu akamwambia Imam Hasan (a.s.); "Ewe kipenzi cha baba yake! Babu yako ameniamuru, akisema: 'Ewe Ali! Ulaani umma huu'. Na nikiwa katika ndoto hii nikasema,'Ee Mola wangu! Nichukue kutoka katika dunia hii haraka iwezekanavyo na uwateulie mtu mwingine wa kushika nafasi yangu ambaye ni mbaya zaidi yangu mimi.'" Unaweza kukisia ukubwa wa tatizo na kutokuwepo kwa utulivu kutokana na tamko hili.

## MABATA YALALAMIKA

Imam alipoanza kuondoka kwenda msikitini, mabata walianza kupiga kelele kwa sauti ya juu sana. Imam akasema: " Sasa hivi ni hawa mabata tu ndiyo wanalia lakini baada ya muda mfupi ardhi na mbingu zitatetemeka na watu wataanza kuomboleza."[15]

Baada ya kusikia haya, watoto walimwendea na wakasema: "Ewe baba! Hatutakuruhusu uende msikitini. Tafadhali tutume sisi au mtume mtu mwingine akuwakilishe." Imam Ali (a.s.) akasema: "Sawa, mwiteni binamu yangu, Juada Hubaira." Halafu akabadili nia ghafla na akasema; "Hapana nitakwenda msikitini mimi mwenyewe." Watoto wakamwomba Imam awaruhusu wafuatane naye lakini alikataa na kusema; "Sitaki mtu yeyote afuatane nami."[16]

Jinsi gani usiku huu ulivyomfurahisha Imam (a.s.)! Ni Mwenyewzi Mungu peke Yake ndiye anayejua hisia zake zilifika kwenye upeo gani!! Akasema [Imam Ali (a.s.)]: "Mimi nilijaribu sana kutaka kujua siri hiyo niliambulia kujua muhtasari tu; kwamba msiba mkubwa ulikuwa unatarajiwa kutokea." Ni wazi kabisa kutokana na maneno yake mwenyewe yaliomo kwenye *Nahjul-Balaghah*:

[15] *Kashful Ghumma*,Juz. 2, uk.62; *Manaqib Ibn Shahr Aashob*, Juz. 3, uk. 310.
[16] *Biharul Anwar*, Juz. ya 42, uk. 226; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 335.

"Nilijaribu sana kuifikia siri hiyo iliyofichika lakini Mwenyezi Mungu alikataa, kwa sababu alitaka ibakie kuwa ni siri."[17]

## ADHANA YA MWISHO YA IMAM ALI (A.S.)

Imam alikuwa na desturi ya kuadhini adhana ya Swala ya Asubuhi. Mapambazuko yalikuwa yanakaribia wakati Imam alipokwenda kwenye sehemu ya kuadhini na akaadhini.[18] Baada ya hapo, aliuaga mwanga mweupe wa alfajiri kwa kusema: "Ewe mwanga wa mapambazuko ya alfajiri! Umewahi kushuhudia siku ambapo Ali (a.s.) alikuwa amelala ulipochomoza katika anga tangu wakati Ali amefumbua macho yake?" Maana yake ni kwamba kabla ya hapo hilo halijapata kutokea lakini sasa macho ya Ali yatafumba daima milele. Baada ya kurudi kutoka kwenye sehemu ya muadhini, Imam alisoma beti zifuatazo:

"Tengeneza njia Muumini mpiganaji shujaa

anayepigana katika njia ya Allah.[19]

"Ni muumini anayefuata amri za Mwenyezi Mungu.

"Na anaingia kwenye medani ya vita ya ufiadini kwa hiari yake.

"Yule ambaye hamuabudu yeyote isipokuwa Mwenyzi Mungu na huwaamuru watu kusimamisha Swala."

Hapa Imam anajitambulisha yeye mwenyewe kama muumini na mpiganaji.

Watu wa familia yake hawakuruhusiwa kuondoka kwenye sehemu zao. Imam Ali (a.s.) alikwishasema kwamba baada ya kilio chake, watu wataanza kuomboleza. Bibi Zainab, Bibi Ummu Kulthum na watu wengine wa familia walikuwa macho na wenye wahaka. Nyoyo zao zilikuwa zinakwenda mbio na kasi huku wakiwa na wasiwasi kwa sababu walikuwa hawajui ni janga gani litakalotokea kabla ya giza la usiku huo halijatoweka. Ghafla sauti ilisikika na kukamata nadhari ya watu, ikisema:

"Enyi waombolezaji! Enyi waombolezaji wa Ali!"

Sauti hii ilikuwa inatoka kila kona na upenu katika saa hii ya msiba:

"Wallahi, nguzo za uongozi zimebomolewa. Wallahi, ishara za ucha Mungu

[17] *Nahjul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 149, uk. 445; *Nahjul Balaghah*, Subhi Salih, hotuba ya 149.

[18] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 279.

[19] *Manaqib Ibn Shahr Aashub*, Juz. 3, uk. 310; *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 238.

zimefutwa. Kamba madhubuti ya ukweli imekatika. Binamu yake Mustafa ameuawa Shahidi. Ali al-Murtaza ameuawa Shahidi. Mtu muovu kuliko wote waliopita na wanaokuja ndiye aliyemuua."[20]

***Kwa Jina la Allah na kwa Allah na juu ya dini ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).***

[20] *Muntahaiul Amaal*,Juz. 1, uk. 238; *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 282.

# MAJILISI 3

## IMAM ALI (A.S.) AJITAYARISHA KUKUTANA NA MOLA

Imam Ali (a.s.) alikuwa amechagua programu maalum katika Ramadhani ya mwisho katika uhai wake. Alikuwa na tabia ya kwenda nyumbani kwa mmojawapo wa watoto wake wa kiume au wakike kufuturu. Hakuwa akila zaidi ya matonge matatu ya chakula.[21] Kwa msisitizo wa watoto wake kwamba awe anakula chakula cha kutosha, alikuwa anajibu kwa kusema:"Sitaki kukutana na Allah tumbo langu likiwa limejaa."[22]

Mara kwa mara alikuwa akisema: "Kufuatana na ishara alizoniashiria Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ni kwamba baada ya muda si mrefu ndevu zangu zitapakwa damu ya kichwa changu."[23]

Alimtembelea binti yake mdogo, Ummu Kulthum, katika mkesha wa mwezi 19. Dalili za kusubiria zilidhihirika zaidi kwake zikilinganishwa na kila usiku wa siku zilizopita. Wakati kila mtu alikuwa ameondoka kwa ajili ya mapumziko ya usiku, Imam alikwenda kwenye mswala wake wa ibada na akaanza kuswali.[24]

### EE MOLA! NICHUKUE HARAKA

Imam Hasan (a.s.) alimwendea kwake muda mfupi kabla ya mapambazuko. Imam Ali (a.s.) alimwambia mwanawe mpendwa: "Sikulala usiku kucha na nimewaamsha watu wote wa nyumba yangu kwa sababu leo ni mkesha wa siku ya Ijumaa na usiku wa leo ni sawa na Usiku wa Badri (au Usiku wa *Laylatul-Qadr*).[25] Nilikuwa nimeketi ambapo nilisinzia kwa muda mfupi. Nilimuona babu yako kwenye ndoto yangu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alin-

[21] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 329
[22] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 224
[23] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 227
[24] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 226
[25] Vita ya Badr vilipiganwa tarehe 17 au 19 ya mwezi wa Ramadhani, mwaka wa 2 A.H., rejea Historia ya Mtume wa Uislamu, uk. 253

iambia. 'Ulaani Umma huu'. Mimi nikasema. 'Ee Mola wangu! Niondoe kutoka kwa watu hawa haraka na unikusanye miongoni mwao wale ambao ni wema kuliko wao. Mpe mamlaka ya uongozi yule ambaye ni muovu kuzidi mimi kwa sababu hivyo ndivyo wananvyostahili watu hawa."[26]

Mwadhini aliwasili na kutoa taarifa kwamba muda wa Swala umewadia. Imam Ali (a.s.) aliondoka kwenda msikitini.[27] Nyumbani kwa Imam walikuwepo mabata wachache waliokuwa wanapendwa sana kwa ajili ya watoto, mabata walianza kupiga kelele kama vile wanalia. Wakati mmoja wa wanafamilia hiyo alipojaribu kuwanyamazisha Imam alisema: "Usiwanyamazishe kwani wanaomboleza."[28]

## "NIMEFAULU, KWA MOLA WA KAABA!"

Abdur Rahman Ibn Muljim na waovu wenzake walikuwa wanangojea kuwasili kwa Imam Ali (a.s.) msikitini kwa shauku kubwa sana. Hakuna aliyejua mpango wao isipokuwa Quttam na Ash'ath bin Qais, ambao walikuwa na tabia mbaya na ambao walikuwa wanakula njama na Muawiyah kwa sababu alikuwa hapendi tabia ya Imam Ali (a.s.) ya kuwatendea watu haki sawa bila upendeleo.

Ilielekea kwamba tukio dogo lingeweza kufichua njama ya mauaji lakini wakati huo huo tukio jingine lilizuia. Ash'ath alikuja akikimbia kwenda kwa Muljim na kusema: "Muda mfupi umebakia kuwa mapambazuko. Mwanga ukishakuwa mkubwa, utafedheheka. Kwa hiyo kamilisha kazi hii haraka iwezekanavyo."[29]

Hujr bin Adi, ambaye alikuwa sahaba wa karibu wa Imam Ali (a.s.) alisikia mazungumzo hayo na akahisi kwamba watu hao walikuwa na mpango wa hatari. Muda mfupi uliopita Hujr ndiyo alikuwa amerudi kutoka katika kukamilisha kazi zake za kitaratibu na farasi wake alikuwa nje ya msikiti. Ilielekea kama vile alitaka kumpa taarifa Amiri wa Waumini kuhusu jambo hili.

Hujr aliposikia maneno ya Ash'ath, haraka alikwenda nyumbani kwa Imam Ali (a.s.) kumtahadharisha kuhusu hatari hiyo. Hata hivyo, alipofika

[26] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 226
[27] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 335
[28] *Kashful Ghumma*, Juz. 2, uk. 62; *Manaqib Ibn Shahr Aashub*, Juz. 3, uk. 310.
[29] *Irshad,* Shaykh Mufid, uk. 17.

nyumbani kwa Imam Ali (a.s.) alikuta amekwishaondoka kwenda msikitini kupitia njia nyingine.[30]

Hata hivyo, wanawe na masahaba wa Imam Ali (a.s.) walisisitiza kwamba asindikizwe na mlinzi. Kila mara Imam Ali (a.s.) alikuwa akikataa ombi lao hilo. Imam (a.s.) alikuwa akikaa bila kulindwa binafsi. Mnamo usiku wa siku hiyo walitoa pendekezo hilo hilo kwa Imam (a.s.) lakini hakulikubali.[31]

Imam Ali (a.s.) alipoingia msikitini alitoa wito akasema: " Enyi watu! Swala! Swala!" Alikuwa ametembea hatua chache tu kuelekea kwenye mswala wake baada ya kusoma Adhana ambapo mapanga mawili yalimulika ghafla kwenye giza na watu walishtuka kusikia kilio cha: *"Hukumu ni ya Mwenyezi Mungu ewe Ali na si yako."* [32] Pigo la kwanza la upanga lilitoka kwa Shabib, aliyelaaniwa, lakini upanga huo ulipiga ukutani kwa hiyo haukufakiwa. Pigo la pili lilitoka kwa Muljim, ambalo lilipiga kichwa kitukufu cha Imam Ali (a.s.). Hujr alirudi haraka kadiri alivyoweza na akakuta tu watu wanalia na kuomboleza tu ndani ya msikiti wa Kufa. Watu walikuwa wanalia: "Amiri wa Waumini ameuawa! Amiri wa Waumini ameuawa."[33]

## "NAMSHUKURU ALLAH, MATAKWA YANGU YA SIKU NYINGI HATIMAYE YAMETIMIZWA"

Maneno ya kwanza ya Imam Ali (a.s.) baada ya kushambuliwa ni haya: "Nimefaulu, kwa Mola wa Kaaba."[34] Katika maneno ya mshairi, Imam Ali alikuwa akisema:

"Namshukuru Allah, Matakwa yangu ya siku nyingi hatimaye yametimizwa." Halafu akasema kwa sauti kubwa "Msimuache mtu huyu awatoroke."[35]

Abdur Rahman, Shabib na Wardan,[36] walijaribu kukimbia ili wasikamatwe. Wardan hakujitokeza kwenye shambulio hili na yeye hakutambuliwa.[37] Mara tu Shabib alipojaribu kutaka kutoroka, sahaba wa Mtukufu Ali (a.s.)

[30] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk.17. *Tatmah al-Muntaha*, uk. 39.
[31] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 336.
[32] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 239.
[33] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 230.
[34] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 239.
[35] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 230.
[36] Jina lake kamili lilikuwa Wardan bin Mujalid; *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 16.
[37] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 17. *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 231.

alimkamata na kunyakua upanga wake kutoka mkononi mwake. Alimtupa chini na kupanda juu ya kifua chake akiwa amenuia kumuua hapo hapo. Hata hivyo, alipoona watu wanakuja kuelekea pale walipo, alihofia watu wangekosea na kudhani kwamba yeye ndiye muuaji. Kwa hiyo alishuka kutoka kifuani mwake. Shabib akapata fursa ya kukimbia na kujificha ndani ya nyumba. Binamu yake Shabib alipopata uthibitisho kwamba Shabib alihusika katika Shahada ya Imam Ali (a.s.), alikwenda nyumbani kwake na kumuua Shabib kwa upanga wake.[38]

Abdur Rahman Ibn Muljim alikamatwa na watu na kufikishwa msikitini huku mikono yake ikiwa imefungwa nyuma yake. Watu walikasirika sana hivyo kwamba wangeweza hata kumnyonga.[39]

Imam Ali (a.s.) aliwaamuru watu wamlete Abdur Rahman mbele yake. Alipofikishwa kwa Imam, aliuliza: "Je, sijakufanyia jambo jema wewe?" Akasema: "Ndiyo, kwa nini isiwe hivyo?" Imam akauliza: "Kwa nini basi ukafanya hivi?"[40] (Muljim) akasema: "Lile lililokuwa limeelekea kutokea limetokea. Nilichovya upanga huu kwenye sumu kwa muda wa siku arobaini na nilimuomba Allah Mtukufu niweze kumuua mtu mbaya kuliko wote kwa upanga huu." Imam akasema: "Maombi yako yamejibiwa. Baada ya muda mfupi tu wewe utauawa kwa upanga huu."[41]

Halafu Imam Ali (a.s.) aliwaambia ndugu zake waliokuwa wamekusanyika hapo: "Enyi wana wa Abdul Muttalib! Chukueni tahadhari! Msifanye kifo changu cha kishahidi kuwa kisingizio cha kumshutumu mtu yeyote kwa kula njama na msije mkaanzisha umwagaji wa damu."

Halafu akamwambia Imam Hasan (.a.s): "Ewe mwanangu! Endapo nikipona na kuishi, nitalipa kisasi dhidi ya mtu huyu. Kama nitakufa, lipeni kisasi kwa kumpiga pigo moja tu la upanga kwa sababu yeye amenipiga

[38] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 230
[39] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 231, 284.
[40] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 287.
[41] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 239.

pigo moja tu. Jiepusheni kufanya uharibifu wowote kwenye maiti yake[42] kwa sababu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ametuamuru tusikatekate maiti hata kama ni ya mbwa mwenye kichaa.[43] Mtunzeni vizuri na mumlishe vizuri mfungwa huyu."[44]

Baada ya kuamuriwa na Imam Hasan (a.s.) tabibu mzoefu na mashuhuri, Athir bin Amr aliitwa. Baada ya kupima jeraha la Amiri wa Waumini akasema: "Upanga uliotumika kumshambulia Imam, ulipakwa sumu na athari yake imekwishafika kwenye ubongo. Hakuna tiba inayoweza kusaidia."[45]

## WOSIA WA IMAM ALI (A.S.) KATIKA KITANDA ALICHOFIA KISHAHIDI

Imam aliendelea kuwa hai kwa muda wa saa 48 baada ya kushambuliwa kwa upanga. Hata hivyo hakupoteza muda huu pia. Hapakuwepo na muda ambapo Imam alikuwa hatoi ushauri. Aliusia kama ifuatavyo:

"Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye Kurehemu."

Haya ni mambo ambayo kwayo Ali Ibn Abi Talib (a.s.) anawausieni.

"Ali anashahidilia kwamba mungu ni Mmoja na anashahidilia kwamba Muhammad ni mja na mtume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu amemtuma aje kuifanya dini Yake iwe juu ya dini zingine. Kwa kweli, Swala yangu, ibada yangu, uhai wangu na kifo changu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu huyu. Ambaye hana mshirika. Nimeamriwa kuhusu hili tu na ninajisalimisha kwa Mwenyezi Mungu.

"Kwako wewe. Ewe mwanangu Hasan, kwa wanangu wengine, kwa ndugu zangu na kwa wote waliokuja kutaka kujua kuhusu huu wosia wangu, kuhusiana na mambo yafuatayo:

---

[42] Chuki ya Bani Umayyah dhidi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa mbaya sana hivyo kwamba Hindu bibi yake Yazid hakuwa ameridhika hata baada ya kufanya Mtukufu Hamza kuuawa kishahidi ambapo alitafuna moyo wake kama kisasi na alivaa pua na masikio ya Mtukufu Hamza baada ya kuyakata kutoka kwenye kiwiliwili chake. Wafuasi wa Yazid hawakuridhika hata baada ya kumchinja Imam Husain (a.s.) na wakakanyaga maiti yake kwa kutumia farasi waliokuwa wamewapanda. Moyo wa Yazid haukutosheka hadi alipotikisa roho ya Mtukufu Mtume kwa kugonga midomo na meno ya Imam Husain (a.s.) kwa vimbo. (*Ridwani*).

[43] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 288.

[44] *Biharul Anwar*,Juz. 42, uk. 206, 248.

[45] *Biharul Anwar*,Juz. 42, uk. 234.

1. Katika hali yoyote ile msije mkapuuza kumuogopa Allah Mwenyezi na mjaribu kuwa katika dini ya Mwenyezi Mungu hadi kufa kwenu.

2. Nyinyi wote kwa pamoja shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu. Wote nyinyi wakati wote mshikamane juu ya misingi ya dini na kumtambua Mwenyezi Mungu na epukeni utengano na kusambaratika. Mtume wa Allah (s.a.w.w.) amesema: 'Kuondoa uadui, uhasama, na chuki ni vema zaidi kuliko Sala na Saumu zilizopendekezwa. Na kile kinachoharibu imani ni utengano na msambaratiko.

3. Watunzeni ndugu wa damu na wale wa karibu. Dumisheni uhusiano mzuri nao kwa sababu kuhesabiwa kwa yule anayemfanyia wema ndugu kunakuwa rahisi mbele ya Mwenyezi Mungu.

4. Watunzeni yatima kwa ajili ya Mwenyezi. Msiwaache wakiwa na njaa na bila matunzo na uangalizi.

5. Kwa ajili ya Allah Mwenyezi, muwe wasimamizi wa ustawi wa jirani zenu. Mtume wa Allah (s.a.w.w.) alisisitiza sana kuhusu majirani hivyo kwamba tulidhani angeweza hata kuwajumuisha miongoni mwa warithi wa mtu.

6. Muogopeni Mwenyezi Mungu kuhusu Qur'ani Tukufu, wasije wengine wakaweza kuwapiku na kuwapita katika kufuata mafundisho yake na kufuata kwa vitendo yale inayoyaamrisha.

7. Muogopeni Allah Mwenyezi kiasi Sala zinavyohusika, kwa sababu Sala ni nguzo za dini yenu.

8. Muogopeni Mwenyezi Mungu katika jambo la Nyumba Yake Takatifu (Kaaba). Msiifanye ikawa ni nyumba iliyotelekezwa kwa sababu kama ikitelekezwa, (ninyi) Waislamu mtapotea.

9. Msimsahau Mwenyezi Mungu, jitahidi katika njia Yake kwa ulimi wako, kwa mali yako na uhai wako.

10. Lipeni Zaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wakati unaotakiwa. Kulipa Zaka kunapunguza hasira za Mwenyezi Mungu.

11. Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu jiepusheni na kuwadhulumu dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

12. Kwa ajili ya Allah wapeni heshima masahaba wa Mtume. Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w.w.) amewapendekeza wao.

13. Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, watunzeni masikini na wasiojiweza na muwaruhusu kushiriki maisha yenu.

14. Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, muwatendee mema watumwa kwa sababu mapendekezo ya mwisho ya Mtume wa Allah (s.a.w.w.) yalikuwa ni kuhusu wao tu.

15. Fanyeni yale yanayompendeza Mwenyezi Mungu na msijali lawama za wenye kulaumu kuhusu suala hili.

16. Washughulikieni watu kwa upendo muwe wema kwao kama Qur`ani Tukufu ilivyoamuru.

17. Wahimizeni watu kufanya mema na muwaonye wajiepushe na kufanya uovu, vinginenvyo mafisadi na waovu watawatawaleni na kama kwa hiari zenu wenyewe mtawaruhusu watu wa aina hiyo kuwa viongozi wenu, Mwenyezi Mungu hatasikia du'a zenu.

18. Endelezeni kupendana na urafiki na mapenzi baina yenu. Muwe na tahadhari kwamba hamsukumiani mbali, na kufanyiana ubaya na kutohurumiana.

19. Shirikianeni kwenye kazi nzuri na mzifanye katika njia ya pamoja. Na msisaidiane katika vitendo viovu na vitendo ambavyo husababisha chuki na uadui.

20. Ogopeni adhabu kali ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu mshiko wa Mwenyezi Mungu ni madhubuti sana. Mwenyezi Mungu awawekeni nyinyi nyote kwenye hifadhi yake na aupatie Umma wa Muhammad Mustafa hisia nzuri ili uendelee kuwashikeni nyinyi na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwa heshima.Ninawakabidhini wote kwa Mwenyezi Mungu. Amani iwe kwenu wote." [46]

Baada ya wasia huu hakuna mtu aliyesikia maneno mengine yoyote kutoka kwa Amiri wa Waumini (a.s.) isipokuwa shahada mbili za imani ya Kiislamu, hadi hatimaye pale aliposalimisha roho yake kwa Muumba.[47]

**"Hakuna nguvu wala uwezo ila ni kwa Mwenyezi Mungu aliye juu na Mtukufu."**

[46] Wosia huu wa Imam unaonyesha jinsi umoja na mshikamano ulivyo muhimu katika Uislamu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Mwenyezi Mungu analinda ushirika wa Umma." Uislamu unataka kuona mshikamano miongoni mwa watu licha ya kuwepo kwa imani kila mahali kwa sababu maendeleo na mafanikio yanatokana na umoja na mshikamano tu. Kuvunja umoja na kuendekeza utengano ni kinyume cha Uislamu. Hakika, Uislamu unao utajiri ambao unaweza kuwaamsha watu wote duniani na kuwakusanya mahali pamoja kwa sababu hii ni dini ya Mola wa wanadamu. Profesa wa fasihi ya Kiarabu katika Chuo Kikuu cha Cairo, Dkt. Hamid Hanafi Dawood anasema:"Siri za Uislamu zimejificha kwenye misingi ya Uislamu na siri ya misingi imejificha ndani ya Uislam." Jamii hufuzu tu kama imeungana na kushikamana. Kuwa mmeungana ni kwamba watu hufanya kazi kwa ajili ya manufaa ya wote na matabaka tofauati ya kijamii yana msingi madhubuti wa mawasiliano miongoni mwao na jamii nzima kwa jumla hunufaika kwayo. Kwa hiyo, mtu anayewakusanya Waislam mahali pamoja, huyo anastahili kupongezwa, na mtu anayevunja umoja na mshikamano wao (Waislamu) anastahili kulaumiwa.(Riziwani)

[47] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 15-18; *Kamiil Ibn Athiir*, Juz. 3. Uk. 387-392, *Muruj al-Dhahab*, Juz. 2. uk. 423-426; *Biharul Anwar,* Juz. 42. uk. 248; *Sharh Nahjul Balaghah*, Ibn Abil Hadid, Juz. 6, uk. 120; *Nahjul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 47, uk. 967; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 332-341; *Dastan Raastan*, Juz. 2, uk. 268-274.

# MAJILISI 4

## "NILIKUWA NININGOJEA SIKU HII"

Enyi waombolezaji!

Pale Ibn Muljim aliyelaaniwa, alipompiga upanga Imam Ali bin Abi Talib (a.s.) kichwani, mchaniko ulifanyika kwenye fuvu hadi kwenye nyusi zake. Imam (a.s.) akasema: Wallahi! Kifo cha ghafla na shambulio la ghafla ni vitu ambavyo sio vitu ninavyovichukia. Hali yangu ni kama ile ya mpenzi ambaye amekutana na yule ampendaye.[48] Katika maneno ya mshairi:

**"Unajua faraha ya kukutana na rafiki mliyepoteana? Ni furaha kama ile ya mtu mwenye kiu jangwani, pale wingu lianzapo kumnyeshea."**

Amiri wa Waumini alitoa mfano ambao ulikuwa unajulikana sana miongoni mwa Waarabu. Waarabu waliokuwa wanaishi jangwani walikuwa ni wahamiaji. Walikuwa na tabia ya kufanya Makazi popote pale ambapo paliweza kupatikana maji na uoto wa majani. Maji na majani vikiisha na wao walikuwa wanahama mahali hapo. Mnamo majira ya kiangazi, walikuwa wakisafiri wakati wa usiku wakitafuta sehemu yenye maji. Amiri wa Waumini aliwaambia masahaba wake: Hali yangu ni kama ile ya mtu ambaye amekutana na mpenzi wake. Hali yangu ya furaha ni kama ile ya mtu anayetafuta maji wakati wa usiku kwenye upweke wa msitu na anapata furaha ya kupita kiasi anapoyapata maji hayo. Imenukuliwa vizuri sana kama ilivyo hapa chini:

**"Jana asubuhi nilipewa uhuru kutokana na huzuni na leo hii kwenye giza la usiku nilipewa kioevu cha maisha."[49]**

**Kwa Jina la Mwenyezi Mungu na kwa Mwenyezi Mungu na Juu ya Dini ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).**

[48] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 254; *Nahjul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 23, uk. 865; *Sharh Nahjul Balaghah*, Ibn Abil Hadid, Juz.15. uk. 143; maneno ya Amiri wa Waumini, ambamo alimlaani Ibn Muljim baada ya kushambuliwa na kabla ya kufa kishahidi ni dondoo ambazo zimeandikwa kwa ufupi.

[49] *Hamasa Husaini*, Juz. 1 (toleo la lugha ya Urdu la kitabu hiki huchapishwa na Dar al- Thaqafiyatul Islamiya, Karachi)

# MAJILISI 5

## NYAKATI ZA MWISHO ZA IMAM ALI (A.S.)

Enyi waombolezaji!

Saa 25 za mwisho za uhai wa Imam Ali (a.s.) ni za kustaajabisha sana licha ya kwamba maisha yake yote yamejaa masomo muhimu, tangu kuzaliwa hadi kutangazwa kwa Uislamu, na kutangazwa kwa Uislam hadi kuhamia Madina, uhamiaji hadi kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambapo hicho kilikuwa kipindi cha tatu cha maisha ya Imam Ali na kilikuwa tofauti kabisa. Kipindi cha nne cha maisha ya Imam Ali (a.s.) kilianza alipokufa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hadi alipoteuliwa kuwa khalifa. Baada ya hapo, kilikuja kipindi cha utawala wake cha miaka minne na nusu, ambacho kilikuwa mojawapo ya vipindi muhimu vya maisha ya Imam (a.s.).

Hata hivyo, kipindi kingine cha maisha ya Imam Ali (a.s.) cha siku mbili na mikesha yake ni cha kushangaza mno. Ni kile kipindi tangu Imam (a.s.) aliposhambuliwa hadi kufariki kwake, ambacho kilithibitisha kwamba Imam alikuwa mtu mkamilifu. Hata pale ambapo mwisho wake ulikuwa umekaribia, ni kazi zipi alizoshiriki? Imam alipopigwa upanga kwenye kichwa chake kitukufu, alitoa matamko mawili ambayo yalisikika. Kwanza ilikuwa, “Ninaapa kwa Mola wa Kaaba, hakika nimefuzu. Nimepata Shahada na huu ni uthibitisho wa kufuzu kwangu.” Tamko la pili lilikuwa, “Msimuache mtuhumiwa akawatoroka.”

### TABIBU WA KUFA AMFANYIA VIPIMO ALI (A. S.)

Imam Ali (a.s.) aliondolewa msikitini na kupelekwa nyumbani kwake baada ya kushambuliwa. Alilazwa kitandani. Mwarabu mmoja aliyejulika kwa jina la Athir bin Amr[50] ambaye alisomea utabibu huko Jundi Shahpur alikuwa anafanya kazi ya utabibu mjini al-Kufa. Aliletwa kuja kumtibia Amiri wa

[50] Miongoni mwa madaktari mashuhuri wa Kufa hakuna aliyekuwa mzoefu kama Athir bin Amr. Alikuwa miongoni mwa vijana tisa waliotiwa nguvuni na Khalid bin Walid wakati wa ukhalifa wa Abu Bakr. Alikimbia na kujihifadhi Kufa. *Biharul Anwar*, Juz. 42. uk. 234.

Waumini. Alianza kufanya uchunguzi wa hali ya Imam.[51] Tabibu huyu alielewa kwamba sumu ilikwisha kupenya na kuingia kwenye mishipa ya damu ya Imam (a.s.) na akasema kwamba hakuna tiba itakayofaa. (Kwa kawaida wagonjwa kama hawa hawajulishwi kwamba hakuna tiba itakayofaa kuwatibu. Ni ndugu wa mgonjwa tu ndiyo hufahamishwa.) Hata hivyo daktari alijua kwamba si vizuri kuficha ukweli huo kwa mtu kama Imam Ali (a.s.) na kuwajulisha ndugu zake tu kuhusu afya yake inayoendelea kuwa mbaya. Kwa hiyo, alimwambia:

"Ewe Amiri wa Waumini! Kama unataka kuacha wosia fanya hivyo sasa."[52]

## UMMU KULTHUM AZUNGUMZA NA MULJIM

Pale Bibi Kulthum alipokuja kujua kuhusu huyu mlaaniwa kuanzia mwanzo hadi mwisho, alimwambia kwa kuchukia mno: "Baba yangu alikukosea nini wewe? Kwa nini ulimshambulia?" Halafu Bibi Ummu Kulthum akasema:"Inshaallah, baba atapata nafuu baada ya muda mfupi na wewe utapatwa na ukosefu na kushindwa." Hapa mlaaniwa huyu akamwambia Bibi Ummu Kulthum:

"Usitarajie kwamba baba yako atapata kupona, kwa sababu nilinunua upanga huu kwa dirham (au dinari) elfu moja na nikatumia dirham (au dinari) zingine elfu moja zaidi kwa ajili ya kuupaka sumu. Nimeupaka upanga huu aina ya sumu ambayo kwamba kwayo upanga huu unaweza kuua watu wote wa Kufa."[53]

## MAPENDEKEZO YA IMAM ALI (A.S.) KUHUSU MUUAJI WAKE

Muujiza wa ubinadamu na utu wa Imam Ali (a.s.) ambao hushangaza watu wengine, ulionekana pale alipoamuru kwamba matunzo mazuri yafanyike kwa mfungwa wake. Halafu akasema: "Enyi wana wa Abdul Muttalib! Msipite huku na huko mkisema: 'fulani bin fulani anahusika na kifo cha kishahidi cha Amiri wa Waumini' na 'fulani naye pia anahusika katika njama hii.'" Isije

---

[51] Inasimuliwa kwamba daktari huyu alipasha moto kongomeo la kondoo dume na akaweka kwenye jeraha.

[52] Ewe Amirul-Mu'minin! Tafadhdli kamilisha wosia wako kwa sababu athari ya shambulio la adui wa Mwenyezi Mungu imefika kwenye ubongo wako. *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 234; *Mutahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 343.

[53] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 231

ikawa kwamba mnaanza kushutumiana. Sitaki muangukie kwenye mambo haya kwa sababu muuaji wangu ni mmoja tu naye ni mtu huyu."[54]

## KIKOMBE CHA MAZIWA KWA AJILI YA IBN MULJIM

Yeye (Imam Ali a.s.) alimwambia Imam Hasan (a.s.): "Ewe mwanangu! Unayo haki ya kuamua hatima ya mtu huyu baada yangu. Unaweza kumwachia huru au unaweza kumwadhibu. Kama ukitaka kumuadhibu basi mpige pigo moja tu la upanga kwa sababu amempiga baba yako pigo moja tu. Kama hatakufa kwa pigo moja, mwacheni huru. Halafu akauliza tena: "Je mmekwisha kumpatia chakula mfungwa wenu? Je, amekunywa maji? Mmempatia matunzo mazuri yanayostahili?"[55]

Imam alipoletewa kikombe cha maziwa ili anywe, yeye alikunywa kidogo tu yaliyobaki akampa Ibn Muljim anywe ili asishinde njaa.[56]

Akisherehesha kuhusu jinsi Imam alivyokuwa anamtendea adui yake, Maulana Rumi anasema:

**"Hakuna awezaye kulingana na Ali katika uthubutu na ushujaa. Hakuna ambaye angefikia kiwango cha tabia zake bora sana na uvumilivu."**

## NINI KINAWEZA KUWA BORA ZAIDI KULIKO SHAHADA WAKATI WA IBADA?

Imam alikuwa kwenye kitanda chake alichofia. Afya yake ilizidi kuwa mbaya jinsi muda ulivyokuwa unazidi kwenda. Sumu ilikuwa imeenea mwili mzima. Masahaba zake walikuwa na huzuni kubwa. Wote walimzunguka na walikuwa wanalia. Hata hivyo, Imam alikuwa mtulivu na alikuwa anatabasamu kwa ustahamilivu. Akionyesha furaha yake kuhusu haya yaliyotokea alisema:

"Wallahi, lolote lile ambalo limenitokea hakika silichukii kwa sababu ni jambo ambalo nimekuwa nikilitamani tangu zamani kwamba nife katika njia ya Allah. Ni jambo gani linaweza kuwa bora zaidi kwangu kuliko kuawa wakati nikiwa kwenye ibada.....?"

[54] *Nahajul Balaghah*, Subhi Salih, Hotuba ya 47; *Nahajul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 47, uk. 969 - neno '*yaqtulna*' limejumuishwa kwenye *Nahajul Balaghah* ya Faizul Islam.

[55] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 289.

[56] *Mathnawi Manawi*, (toleo la Nicholson) Juz.1, uk. 229.

Imam Ali (a.s.) anatoa mfano ambao Waarabu walikuwa wanautambua vizuri. Jamii ya mabedui wahamaji ilikuwa ikiishi mahali kutegemeana na hali ya hewa. Waliishi mahali almuradi tu palikuwepo na maji na chakula kwa ajili yao na mifugo yao. Vinginevyo, waliondoka na kutafuta sehemu nyingine ambako wangepata maji na chakula. Kwa kuwa hali ya hewa ilikuwa joto sana wakati wa msimu wa kiangazi, ilikuwa ni kawaida yao kusafiri wakati wa usiku (Waarabu waliwaita watu kama hao waliokuwa wakisafiri usiku kutafuta maji –"Qaarib"). Imam Ali (a.s.) alisema:

"Enyi watu ! Fikirieni juu ya hili. Mtu ambaye anatafuta maji wakati wa giza la usiku na ghafla anapata maji, atakuwa na furaha kiasi gani? Furaha yangu pia ni sawa na ile ya mpenzi aliyekutana na mpendwa wake au kama mtu ambaye anatafuta maji wakati wa usiku na ghafla anayapata."[57]

**"Jana asubuhi nilitolewa kwenye huzuni na nikapewa kioevu cha maisha kwenye giza la usiku wa leo. Ni jinsi gani kubarikiwa kwa alfajiri hiyo! na jinsi gani kubarikiwa kwa usiku huo, Usiku huo wa Mamlaka ambamo nilipewa kibali kipya cha wokovu."**

Beti hizi za Hafiz pia zanadokezea kile alichosema Imam: "Naapa kwa Mola wa Kaaba, Nimefuzu."[58] Maneno ya kustaajabisha zaidi ya Imam Ali (a.s.) ni yale aliyoyazungumza katika saa 45 za mwisho wa uhai wake. (Imam ) Alipigwa upanga mnamo tarehe 19 ya Mwezi wa Ramadhani dakika chache baada ya alfajiri na alifariki dunia mnamo usiku wa manane wa tarehe 21 Mwezi wa Ramadhani.

## USHAURI WA MWISHO WA IMAM ALI (A.S.)

Katika nyakati zake za mwisho, wakati shani ya kifo ikiwa mbele yake na watu wamezunguka kitanda chake, athari ya sumu ilikuwa imeenea mwili wake wote. Kuna wakati alisononeka kwa maumivu na wakati mwingine alipoteza fahamu. Wakati wowote alipopata fahamu lulu za ushauri zilizojaa hekima zilitoka mdomoni mwake. Wosia wa nukta ishirini wa Imam, ambao tumeutaja katika majilisi iliyopita, umejaa hamasa ya imani. Kwanza aliongea na Imam Hasan (a.s.) na Husain (a.s.) na halafu ndugu zake wengine:

[57] *Diwan-e-Hafiz*, uk. 114.
[58] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 239.

"Mwanangu Hasan, Mwanangu Hasan! Baada ya hapo Imam aliongea na wanawe wote wa kiume na vizazi vyote ambavyo vitakuja hadi Siku ya Hukumu na akawaambia kuhusu upana wa Uislamu:

**Muogopeni Allah Mwenyezi kuhusu yatima.**

**Muogopeni Allah Mwenyezi kuhusu Qur`ani.**

**Muogopeni Allah Mwenyezi kuhusu majirani.**

**Muogopeni Allah Mwenyezi kuhusu nyumba ya Mola wenu.**

**Muogopeni Allah Mwenyezi kuhusu Taratibu za Ibada.**

**Muogopeni Allah Mwenyezi kuhusu kodi ya Zakat."**

Imam alitia msisitizo katika kila jambo.[59]

Imam aliendelea kusisitiza nukta zilizokuwa mbele yake. Watu wale ambao macho yao yalikuwa yanaelekea uso wa Imam Ali (a.s.) uliong`aa nuru, waliona kwamba katika kipindi kifupi hali ya Imam ilibadilika. Matone ya jasho jembamba yalianza kung`aa juu ya paji la uso wake mpana na akaondoa mazingatio yake kwa watu hao waliokuwa wamemzunguka. Watu wote walingojea kuona midomo ya Imam kutikisika tena, ili waweze kusikia neno kutoka kwake. Watu walingojea kutoka kwa mtu mashuhuri wa historia na kipenzi cha Mtume aseme kauli ya mwisho ya maisha yake:

**"Ninashahidilia kwamba hapana mungu ila Allah na ninashahidilia kwamba Muhammad ni mjumbe na Mtume Wake."**

[59] *Nahjul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 47, Uk. 967; *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 249.

# MAJILISI 6

## DAMU YA ALI NDIYO THAMANI YA MAHARI

Abdur Rahman alikuwa mmojawapo wa wale watu tisa waliojulikana kwa sifa ya kuwa `mashuhuri, watakatifu na wacha-Mungu` waliokwenda Makkah kutoa kiapo kijulikanacho sana. Watu hawa waliamini kwamba, Ali, Muawiyah na Amr bin Aas ndiyo walikuwa wahusika wakuu juu ya matatizo katika ulimwengu wa Uislamu.[60]

Ibn Muljim alipewa kazi ya kumuua Ali (a.s.) huko Kufa. Walipanga usiku wa mwezi 19 Ramadhani kwa lengo hili. Ibn Abil Hadid anasema kwamba wajinga hawa walichagua tarehe ya 19 mkesha wa Ramadhani kwa sababu kutokana na dhana yao potovu,kwamba kama wangetekeleza kitendo hicho (kama walivyokiita wao cha `ibada`) wakati wa Usiku wa *Laylatul-Qadr* wangepata thawabu nyingi zaidi.[61]

Ibn Muljim aliwasili Kufa na akawa anatembea huko na huko akingoja usiku huo uliopangwa kwa kazi hiyo. Katika kipindi hiki, alitokea kumpenda binti mmoja bikira, jina lake Quttam[62] (binti Akhzar) pia wa madhehebu ya khawariji. Ibn Muljim alimpenda sana binti huyo hadi alisahau kazi aliyotumwa. Alipomposa binti huyo, yeye alisema: "Nipo tayari kuolewa na wewe lakini nitataka mahari kubwa na ngumu kutoka kwako." Ibn Muljim alitaka kumuoa binti huyo kwa gharama yoyote na alikubali kutimiza matakwa yake yote.

Quttam alitoa masharti manne kwa ajili ya ndoa hiyo:

1. Dinari elfu tatu taslimu.
2. Mtumwa wa kuime (mvulana).
3. Mtumwa wa kike (msichana).

[60] *Sharh Nahjul Balaghah*, Ibn Abil Hadid, Juz. 6, uk. 112-113

[61] *Sharh Nahjul Balaghah*, Ibn Abil Hadid, Juz. 6, uk. 112-113

[62] Quttam alikuwa mjanja sana. Alidai mahari ya damu ya Ali kwa sababu ndugu zake wengi waliuawa kwenye vita ya Nahrawan (Rizwani).

4. Kumuua Ali bin Abi Talib (a.s.)

Ibn Muljim alikubali masharti matatu ya kwanza kwa furaha kabisa lakini alikuwa na mashaka kuhusu sharti la nne na akasema: "Kumuua Ali inaweza kuwa kikwazo katika maisha yetu ya ndoa." Quttam akasema: "Kama unanitaka mimi utalazimika kumuua Ali. Baada ya hapo, kama ukipona utanipata na kama hapana, basi itakuwa ndiyo mwisho."[63] Ibn Muljim alishikwa na bumbuwazi aliposikia masharti ya Quttam na mshairi ametunga beti zifuatazo kuhusu jambo hili:

**"Ilikuwa ni elfu moja dirham,**
**mtumwa na mtumishi kijana,**
**Na Ali kumpiga dhoruba,**
**kwa upanga mkali wenye kupenya.**

**Haijatokea mahari yenye thamani**
**Wala hakuna vurugu kamwe,**
**isipokuwa ndogo kuliko ya Ibn Muljim."[64]** Ukweli ulioje wa mshairi huyu

## MSIWAUWE KHAWARIJ BAADA YANGU

Ikiwa tumelizingatia jambo hilo hapo juu, naturejelee kwenye wosia wa Imam Ali (a.s.). Imam Ali alipokuwa kwenye kitanda alimofia, alikuwa anayakumbuka makundi mawili ya watu waliojivisha utukufu ambayo aliyaponda siku za nyuma. Mojawapo ya makundi hayo lilikuwa kundi la wanafiki, lililojulikana kwa jina la *Qasitiin*. Muawiyah alikuwa kiongozi wa kundi hili. Kundi lingine lilikuwa kundi liitwalo *Mariqiin* au Khawarij waliokuwa wamevaa pazia la utakatifu. Makundi haya yalikuwa na tofauti zao za kawaida. Kwa hiyo, Imam anawashauri masahaba wake kuhusu jinsi ya kupigana na makundi haya mawili:

---

[63] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 16; *Sharh Nahjul Balaghah* , Ibn Abil Hadid. Juz. 6, uk. 115

[64] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 266; *Irshad*, Shaykh Mufid, uk 18. pia ina beti ifuatayo kabla ya zile za juu: "Sijapata kamwe kuona mahari, iliyotolewa na mtu mkarimu, kama mahari ya Quttam (iwe mtu huyo alikuwa) tajiri au alikuwa masikini."

"Msiwaue watu hawa baada yangu. Ni kweli kwamba wameniua mimi lakini msiwaue baada yangu. Mkiendelea kumwaga damu, mtajumuishwa katika kundi la wasaidizi wa Muawiyah. Hamtajumuishwa katika kundi la watu wanaopigania ukweli. Hatari kwa Muawiyah ni jambo lingine zaidi." Imam Ali (a.s.) akasema: "Msipigane na Khawarji baada yangu, kwa sababu mtu anayeitafuta haki lakini haipati si sawa na yule anayetafuta batili na akaipata."[65] Sayyid ar-Radhi anasema: Amirul-Mu'minin alimaanisha Mu'awiyah na kundi lake.

Imam Ali (a.s.) hakuwa na nia mbaya na mtu yeyote wala hakuwa na uadui na yeyote. Wakati wote alikuwa akisema kweli. Fikiria mfano wa Ibn Muljim. Alipokamatwa na kupelekwa mbele ya Imam aliuliza kwa sauti ya uchungu kwa sababu ya maumivu: "Kwa nini ulifanya hivi? Hivi mimi nilikuwa Imam mbaya kwako?" (Sijui kama Imam Ali (a.s.) alisema maneno haya mara moja au mara mbili lakini kila mtu amesimulia maneno hayo hayo). Mkandamizaji huyu aliguswa na hali ya kiroho ya Imam na aksema: "Unaweza kumuokoa mtu mwenye bahati mbaya kutoka kwenye moto?[66] Nilikuwa fidhuli kutenda kitendo hiki."[67] Pia imeandikwa kwenye vitabu kwamba Imam Ali (a.s.) alipokuwa akisema naye, muuaji alizungumza na Imam kwa ukali sana na akauliza:

"Ewe Ali! Niliponunua upanga huu, nilimuomba Mwenyezi Mungu kwamba mtu mbaya sana miongoni mwa viumbe wa Allah auawe kwa upanga huu."

Imam Ali (a.s.) akasema: "Kwa bahati nzuri maombi yako yamepokelewa na kujibiwa kwa sababu baada ya muda si mrefu wewe utauawa kwa upanga huu."[68]

## KUHUDHURIA MAZISHI USIKU

Imam Ali (a.s.) aliuawa kishahidi katika mji wa Kufa ambapo watu wote isipokuwa Khawarij wa Nahrawan walitaka kuhudhuria mazishi na kumuomboleza. Watu walikuwa hawana habari ya kifo cha kishahidi cha Imam Ali (a.s.) hadi usiku wa manane wa tarehe ishirini na moja ya mwezi wa Ramadhani kwa sababu alikufa baada ya usiku wa manane.

[65] *Nahajul Balaghah*,Faizul Islam, Hotuba ya 60, uk. 141; *Nahjul Balaghah*, Subhi Salih, Hotuba ya 61 ina *'laa tuqaatiluu'* imewekwa mahali pa *'laa taqtuluu'*

[66] Surah Zumar [39:19]

[67] *Muntahaiul Amaal*,Juz. 1, uk. 340; *Biharul Anwar*,Juz.42, uk. 287.

[68] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 239-244.

Watoto wa Imam Ali, yaani Imam Hasan na Imam Husain (a.s.), Muhammad bin Hanafiyyah na Abul Fazl al-Abbas na baadhi ya masahaba wa karibu waliofika idadi ya watu sita au saba walimkosha, wakamvisha sanda na wakamzika kwa siri mahali ambapo Imam Ali (a.s.) mwenyewe aliusia. Alipelekwa mahali alipozikwa leo wakati wa giza la usiku na hapana mtu aliyejulishwa kuhusu jambo hili. Kwa mujibu wa hadithi ni pale ambapo baadhi ya mitume wakubwa wamezikwa. Mahali halisi pa kaburi la Imam palikua siri na hakuna mtu aliyeambiwa.[69]

Siku iliyofuata, watu walikuja kufahamu kwamba Ali (a.s.) alizikwa usiku uliopita. Watu walipotaka kujua mahali alipozikwa, waliambiwa haikuwa na umuhimu wao kupajua mahali hapo. Pia imeandikwa kwenye baadhi ya vitabu kwamba Imam Hasan (a.s.) alitayarisha kilili cha jeneza na akakipeleka Madina ili watu wadhani na kuamini kwamba kilili cha jeneza la Ali (a.s.) kilipelekwa Madina kwa ajili ya mazishi huko.[70]

Kwa nini ilifanyika hivi? Ilikuwa ni kwa sababu ya hawa Khawarij tu. Kama hawa wao wangejua kaburi la Imam Ali (a.s.) wangechukua maiti hiyo maasumu na kuichafua.

Madhali Khawarij walikuwepo hapa duniani na walikuwa na mamlaka, hapana mwingine isipokuwa dhuria wa Imam Ali (a.s.) na Maimam watukufu waliojua mahali halisi pa kaburi lake. Baada ya miaka mia moja, Khawarij walipoteza mamlaka na kuondolewa kwenye utawala na kwa hiyo hapakuwepo na uwezekano wa kukashifu kaburi la Imam Ali (a.s.). Ndipo Imam Ja`far Sadiq (a.s.) alipowaonyesha watu mahali alipozikwa Imam Ali (a.s.) kwa mara ya kwanza.

Dua tunayosoma kwenye Ziarat ya Ashura ina jina la sahaba mashuhuri wa Imam, Safwan Jamal kama mmoja wa wasimlizi. Safwan anasimulia: "Nilikuwa na Imam Ja`far Sadiq (a.s.) huko Kufa, ambapo alitupeleka na kutuonyesha kaburi tukufu la Imam Ali (a.s.). Imam Ja`far (a.s.) alionyesha kaburi tukufu la Imam Ali (a.s.) na huenda alifanya mpango wa kujenga banda kwa ajili ya kaburi hilo tukufu. Baada ya hapo siri ya kaburi la Imam

[69] *Biharul Anwar*,Juz. 42, uk. 239.

[70] Mtukufu Mtume alikwisha sema kuhusu Fatima Zahra: "Fatima ni kipande cha moyo wangu." (*Sahih Bukhari*, Juz. 5, Tr. 209). Pia Mtukufu Mtume alikwisha sema kuhusu Ali Murtaza, "Ewe Ali! Hivi wewe huridhiki na kwamba wewe kwangu ni kama Harun alivyokuwa kwa Musa, isipokuwa tu ni kwamba hapatakuwepo na mtume baada yangu?" (*Sahih Bukhari*, Juz. 6, Tr. 408). Hivi Umma haushangai kwa nini mazishi yao yalifanyika usiku badala ya kufanya hivyo mbele ya jamii yote? (Rizwani) *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 353.

Ali ilijulikana.[71] Uovu dhidi ya Imam Ali (a.s.) haukuwa na mpaka hadi kufa kwake. Sehemu ya kaburi la Imam Ali (a.s.) ilifanywa ni siri kwa zaidi ya miaka mia moja baada ya kifo chake cha kishahidi.

## KUONEWA KWA ALI (A.S.)

**Aman iwe juu yako, Ewe Abul Hasan! Amani iwe yako, Ewe Amir-ul-Mu'minin!**

Ni kwa kiasi gani Imam na wanawe wameonewa! Sijui kama mawla wangu, Amiri wa Waumini ndiye aliyeonewa zaidi au mwanawe mpendwa, Imam Husain (a.s.). Kama vile tu ambavyo mwili mtukufu wa Imam Ali (a.s.) haukuwa salama kutokana na madhara ya utukutu wa maadui, mwili mtukufu wa mwanawe na mwana wa Bibi Zahra pia haukuwa salama kutokana na madhara ya maadui. Huenda ikawa hiyo ndiyo sababu iliyomfanya aseme: "Hakuna siku ambazo ni mbaya kama zile siku za kusikitisha za Husain wangu madhlumu." Kwa nini Imam Hasan (a.s.) aliificha maiti tukufu ya baba yake? Kwa sababu hakutaka mtu yeyote aidhuru; lakini cha kusikitisha, hali ilikuwa tofauti kabisa huko Karbala. Imam Sajjad (a.s.) hakuwa na msaada kabisa hivyo kwamba hakuweza kuficha maiti ya Imam Husain (a.s.) baada ya kuuawa kishahidi. Matokeo yake yalikuwaje? Sitaki kuyasema. Mtu mmoja amesema:[72]

**"Kuna manufaa gani kuwa na nguo ya zamani ambapo aliyeivaa anakanyagwa na kwato?**

**Hakuna mtu aliyebaki pale ili aufunike nguo."**

[71] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 12; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 271, na *Safinatul Bihar*, Juz. 2, uk. 37. (Safwan alikuwa muongoza ngamia na alikuwa na tabia ya kukodisha ngamia wake. Alimchukua Imam Ja`far Sadiq (a.s.) kutoka Madina kwenda Kufa wakati mmoja siku za nyuma. Ndipo alipopata fursa ya kuzuru kaburi la Imam Ali (a.s.) akiwa pamoja na Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.). Alikuwa na ufahamu kamili juu ya kaburi la Imam Ali (a.s.) na imeandikwa kwenye uk. 37 wa *Kamiluz Ziyaraat* kwamba Safwan alikuwa akizuru (Ziaraat) kaburi la Imam Ali (a.s.) mara kwa mara kwa kipindi cha miaka sitini. Alikuwa akiswali karibu na kaburi la Imam (a.s.).

[72] *Siiri dar Siirat-e-Aimma-e-Athaar*, uk. 49-54.

# MAJILISI 7

## IMAM ALI (A.S.) ALIZIKWA KWA SIRI

Enyi Waombolezaji wa Amiri wa Waumini!

Kwa nini tumekusanyika hapa leo? Tumekusanyika hapa leo kuomboleza kifo cha yule mtu mkamilifu aliyezikwa kwa siri wakati wa usiku. Jambo hili lilifanyika hivi kwa sababu mtu huyu mkamilifu yaani Ali bin Abi Talib (a.s.) alikuwa na maadui wengi kama alivyokuwa na ndugu na marafiki wengi. Nimelizungumzia jambo hili kwa kina katika kitabu changu, *Jaziba wa Dafia-e-Ali (a.s.)* kwamba duniani humu kuna watu wenye uwezo mkubwa sana ndani mwao. Pia wapo watu wenye uwezo pinzani usiokuwa na mipaka ndani mwao. Wafuasi wa wale wenye uwezo usiokuwa wa kawaida wa mvuto kwa watu wamejitolea nafsi zao kabisa hivyo kwamba hujivunia kitendo cha kujitoa mhanga kwa ajili ya kiongozi wao.

Pia, maadui wa watu kama hao, huonekana ni wachungu sana. Hususani wale ambao wapo karibu naye au maadui zake wa ndani. Maadui wa Imam Ali (a.s.) walikuwa wa aina hiyo. Walizivisha nyuso zao pazia la usafi na wakasimama dhidi ya Imam Ali (a.s.). Khawarij ni wale ambao walikuwa na imani, lakini walikuwa wajinga na kaidi sana. Imam Ali (a.s.) mwenyewe aliwahi kukiri kwamba watu hawa wanayo imani lakini walikuwa wajinga na wapumbavu. Imam Ali aliwalinganisha Khawarij na wanafiki kwa kusema: "Msiwapige Khawarij baada yangu kwa sababu ipo tofauti baina yao na wafuasi wa Muawiyah. Hawa khawarij wao wanatafuta ukweli lakini ni wapumbavu. Wamekuwa mateka wa kutokuelewa ambapo wanafiki wanajua ukweli lakini wanataka kupingana nao."

Kwa nini Imam Ali (a.s.) alizikwa kwa siri usiku wa giza licha ya kuwa na wafuasi wengi?[73] Ilikuwa ni kwa sababu ya khofu ya Khawarij tu kwa sababu walikuwa na tabia ya kusema kwamba Ali (a.s.) si Mwislamu. Kwa hiyo, palikuwepo na hatari kwamba watu hawa wangechimbua kaburi wakati wa usiku na kufukua mabaki ya maiti yake safi.

[73] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 222.

Wakati wa kuelekea mwisho wa kipindi cha Imam Ja`far Sadiq yaani takribani miaka mia moja hivi,[74] kwa nini hakuna mtu mwingine yeyote aliyejua kaburi la Imam Ali (a.s.) lilipo isipokuwa Maimam watukufu na masahaba maalum tu?

Mnamo asubuhi ya tarehe ya 21 ya mwezi wa Ramadhani Imam Hasan (a.s.) alitayarisha kilili cha jeneza na akawapa kundi la watu kupeleka Madina ili kwamba watu wadhanie kwamba Imam Ali (a.s.) amezikwa Madina.[75]

Watoto wa Imam Ali (a.s.) na Shi'ah wake wa karibu walijua mahali halisi lilipo kaburi lake kwa sababu walimzika mkesha wa tarehe 21 mwezi wa Ramadhani. Walikuwa na tabia ya kwenda Ziarat sehemu hiyo, iliyokuwa karibu na Kufa. Khawarij walipopoteza mamlaka ya utawala wakati wa kipindi cha uhai wa Imam Ja`far Sadiq, hatari ya kuharibiwa kwa kaburi la Imam Ali (a.s.) ilitoweka. Hatimaye, Imam Ja`far Sadiq (a.s.) alimuamuru Safwan ambaye ni msimulizi katika sanadi ya wasimulizi wa *Du'a Alqamah* kutayarisha kibanda cha kivuli kwenye kaburi ili watu waweze kulitambua. Baada ya hapo, watu walikuja kujua mahali lilipo kaburi la Imam Ali (a.s.) na ikawa ni sehemu ya watu wote kufanya Ziarat.

## SHAIRI LA HUZUNI LA SASA`AH KWENYE KABURI LA IMAM ALI (A.S.)

Ni watu wachache sana walihudhuria mazishi ya Imam Ali (a.s.). Ni watoto wake tu na masahaba wachche wa karibu sana ndiyo waliokuwepo. Mmoja wa masahaba, ajulikanaye kwa jina la Sasa`ah bin Sauhan[76] ambaye alikuwa

---

[74] Imam Ali aliuawa kishahidi mnamo mwaka wa 40 A.H. ambapo Imam Ja`far Sadiq alikufa kishahidi mnamo mwaka wa 148 A.H.

[75] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 353.

[76] Msimulizi wa hadith Shaykh Abbas Qummi ameandika katika sehemu ya *Amaal* cha Msikiti wa Sahla kwamba Msikiti wa Zaid ni mojawapo wa misikiti mitukufu zaidi ya Kufa. Unahusiana na Zaid bin Sauhan. Alikuwa ni sahaba mwandamizi wa Imam Ali. Amejumuishwa miongoni mwa watu waaminifu. Aliuawa kishahidi akiwa upande wa Imam Ali (a.s.) wakati wa vita vya Jamal. Kuna msikiti uitwao *Masjid Sasa`ah* karibu na msikiti huu, ambao unahusishwa na kaka yake, Sasa`ah bin Sauhan. Huyu naye alikuwa sahaba mwandamizi wa bwana wa waumini. Amejumuishwa miongoni mwa waumini waliokuwa wanamtambua sana Imam Ali (a.s.). Alikuwa stadi sana wa kuhutubia hivyo kwamba Imam Ali (a.s.) alimpa cheo cha `*Khatib-e-shashah*` na alikuwa akisifia umahiri wake wa uzunguzaji na ufasaha. Mnamo usiku wa tarehe ishirini na moja, ambapo jeneza lake lilipobebwa kupelekwa Najaf Sharif kutoka Kufa, Sasa`ah alikuwepo katika msafara huo. Baada ya Imam Ali (a.s.) kuzikwa, Sasa`ah alichukua udongo uliojaa kwenye kiganja chake kutoka kwenye kaburi la Imam Ali (a.s.) na akaweka udongo huo juu ya kichwa chake na kusema: "Ewe kiongozi wa waumini! Wazazi wangu nawawe kafara yako. Ewe Abul-Hasan! Rehema za Allah ziwe juu yako. Hakika, sehemu yako ulipozaliwa ni

rafiki wa kuaminika pia alikuwepo. Alikuwa mzungumzaji mzuri sana.[77] Aliwahi kuhutubia mara kadhaa wakati wa Imam Ali (a.s.).

Wote wale waliokuwepo kwenye mazishi ya Imam Ali (a.s.) walijaa huzuni, masikitiko na hasira. Moyo wa Sasa`ah ulijaa Majuto. Alichukua udongo kwenye kiganja chake kutoka kwenye kaburi la Imam Ali (a.s.) na kuweka kichwani mwake. Alidhibiti hisia zake na akasema: "Amani iwe juu yako, Ewe Amiri wa Waumini! Uliishi maisha ya kufuzu na ukafariki katika namna ya kufuzu."[78] Ulizaliwa ndani ya Kaaba Takatifu na ukanywa sehemu ya kifo cha kishahidi ndani ya nyumba ya Allah.

Fikra hii imeelezwa vizuri sana na mshairi katika beti zifuatazo:

**"Ulizaliwa ndani ya Kaaba na ukauawa kishahidi ndani ya msikiti. Ninajivunia mwanzo wako mzuri sana na mwisho wako mzuri sana."**

Ewe Bwana wangu! Ulikuwa mashuhuri mno na watu walikuwa duni kabisa. Wallahi, kama watu wangefuata njia ulioionyesha wewe, neema zingemwagikia vichwani mwao na fadhila zingebubujika chini ya miguu yao.[79] Wangepata rasilimali na fadhila zisizo na ukomo. Lakini wapi, watu hawakujali kuhusu wewe. Walidhuru hisia zako kwa njia nyingi badala ya kufuata misingi yako iliyo bora sana. Hatimaye walipasua kichwa chako kitukufu katika vipande viwili na kukuchovya kwenye udongo na damu.[80]

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**"Na punde watajua waliodhulumu ni mgeuko gani watakaogeuka?"** [Sura Ash-Shu'araa 26 : 227]

takatifu. Subira yako na jihadi yako ni madhubuti na mashuhuri. Ulipata chochote kile ulichotaka kukipata. Biashara yako ilikuwa na manufaa na ilirejelea ukweli." Alitamka maneno mengi ya aina hiyo na alilia sana na alisababisha na watu wengine walie. Kwa kweli, Majilis-e-Aza ilifanyika kwenye kaburi la Imam Ali (a.s.) kwenye giza la usiku huu. Sasa`ah alikuwa ndiye msemaji na wasikilizaji walikuwa ni pamoja na Imam Hasan, Imam Husain, Muhammad bin Hanafiyyah, Mtukufu Abbas,na watoto wengine na masahaba wakuu wa Imam Ali (a.s.). Baada ya Majilisi hii, alimgeukia Imam Hasan, Imam Husain, na watoto wengine wa Imam Ali (a.s.) na akatoa salam zake za rambirambi. Baada ya hapo kila mtu alirejea Kufa.

[77] Jahiz amesimulia kutoka kwake kwenye *al-Bayan wa al-Tibiyyin.*

[78] *Bihar Anwar*, Juz. 42, uk.295; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 352.

[79] *Bihar Anwar,* Juz. 42, uk.296;

[80] *Insan-e-Kamil*, uk. 144-146.

# MAJILISI 8

## SASA`AH, SAHABA MASHUHURI WA ALI (A.S.)

Enyi Waombolezaji wa msimamizi!

Sasa`ah bin Sauhan Abdi alikuwa sahaba mashuhuri wa Amirul-Mu'minin. Imam alikuwa anampenda sana. Alikuwa mhutubiaji mashuhuri ambaye hotuba zake zilikuwa na athari nzuri. Jahiz amesifia uwezo wake mkubwa wa kuhutubia na jinsi ya kujieleza kwenye kitabu chake, *Al-Bayan wa al-Tibbiyyin* kwa maneno yafuatayo: "Sasa`ah alikuwa msemaji mzuri hivyo kwamba wakati fulani, Imam (a.s.) alikuwa anamwalika kuzungumza kwenye hadhara na alikuwa akizungumza mbele ya Imam (a.s.) kama msikilizaji."[81]

Sasa`ah alikuwa amezungumza kwa ufupi kuhusu Imam mnamo siku yake ya kwanza ya Ukhalifa wake. Alizungumza kuhusu Imam kwa mara ya pili pale Imam Ali (a.s.) alipopigwa upanga na Ibn Muljim. Baada ya hapo, alizungumza kwa kina kuhusu Imam baada ya mazishi yake.

### SIKU YA KWANZA YA UKHALIFA WA ALI

Mnamo siku ya kwanza ya ukhalifa wa Imam Ali (a.s.), Sasa`ah alimgeukia Imam na kusema: "Ewe Amirul-Mu'minin! Umeupamba ukhalifa na ukhalifa haujakupamba wewe. Heshima ya ukhalifa imeongezeka baada ya wewe kuwa khalifa na ukhalifa haujaongeza heshima yako. Ukhalifa unakuhitaji wewe na wewe huuhitaji huo ukhalifa."[82]

### BAADA YA KUJERUHIWA KWA IMAM ALI (A.S.)

Sasa`ah alizungumza kuhusu Imam kwa mara ya pili baada ya Amirul-Mu'minin kujeruhiwa. Pigo hilo lilikuwa na athari mbaya sana kwake kama

[81] Jahiz, *al-Bayan wat Tibiyyin*, Juz. 1, uk. 266.
[82] *Al-Sawarim al-Muhriqa*, uk.6; *Usudul Ghaba*,Juz. 4, uk.32.

ilivyokuwa kwa masahaba wengine mahsusi wa Imam Ali (a.s.). Kwa kweli, Sasa`ah alikwenda kumtembelea Imam (a.s.) hata hivyo, hakuweza kupata fursa ya kuonana naye. Hatimaye, aliwasilisha beti mbili kupitia kwa mtu ambaye aliruhusiwa kuingia kwenye chumba alichowekwa Imam. Sasa`ah alionyesha huzuni kwa kuwasilisha salamu kwa Imam na kwa kusoma beti mbili zifuatazo: "Rehema ya Allah iwe kwako katika uhai wako na kifo chako. Ewe Amiri wa Waumini! Unamfikiria Mwenyezi Mungu kuwa na ukubwa usio na mfano na unao utambuzi uliotukuka wa Dhati ya Pekee hiyo."[83]

Imam Ali (a.s.) alipopokea ujumbe huo, alimjibu Sasa`ah akasema: 'Rehema ya Allah iwe kwako pia, Ewe Sasa`ah ! Wewe ni rafiki yetu mwema na msaidizi wetu mzuri sana. Hukutarajia makubwa, ulikuwa na matatizo madogo na ulitumia kidogo sana. Pia ulikuwa mchapakazi kwa bidii; ulitoa huduma kubwa sana na ulijitolea muhanga sana."[84]

## BAADA YA MAZISHI YA ALI (A.S.)

Shairi la tatu lililosomwa na Sasa`ah lilikuwa ni baada ya mazishi ya Imam Ali (a.s.). Sasa`ah alikuwa sahaba mahsusi wa Imam aliyekuwepo wakati wa mazishi yake. Baada ya mazishi ya Imam, Sasa`ah aliweka mkono wake mmoja kwenye kifua chake na akachota udongo mkononi mwake kutoka kwenye kaburi na kuuweka kichwani kwake. Halafu akasema : "Wazazi wangu wote wawe kafara kwa ajili yako, Ewe Amiri wa Waumini! Ewe Abul Hasan! Na uweze kuziona ni zenye kufurahisha heshima zote na mafanikio yote uliyoyapata kupitia kifo hiki cha kishahidi na daraja ulilopata karibu na Allah."

Halafu akasema: "Hakika, sehemu uliyozaliwa ni takatifu, uvumilivu wako ni madhubuti na Jihadi yako ni kubwa. Umefanya biashara yenye manufaa na umemfikia Mola Wako. Ninamuomba Mwenyezi Mungu atupe hisia na uelewa mzuri wa kufuata nyayo zako. Umefika mahali ambapo hakuna anayeweza kufika. Umepata heshima hiyo, ambayo hakuna ambaye angeweza kuipata." Halafu akasema tena: "Ewe Abul-Hasan! Nina furaha kwa ajili yako. Allah amelifanya daraja lako kuwa la heshima zaidi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu asituweke mbali na thawabu hizo kubwa, ambazo

[83] *Biharul Anwar*,Juz. 42, uk. 234; *Safinatul Bihar*, Juz. 2,uk. 31.
[84] *Biharul Anwar*, Juz. 42, uk. 234; *Safinatul Bihar*, Juz. 2, uk. 30.

tunazitafuta kupitia kwako. Allah asituache tukapotea baada yako. Wallahi, maisha yako matukufu yalikuwa ni ufunguo wa kuelekea kwenye wema na kufuli la fitina.[85] Kama watu wangekutii wewe na kutafuta kukutambua wewe, mbingu zingemwaga rehema na ardhi ingetapika hazina zake. Lakini wapi, watu hawakujali kuhusu wewe. Dunia hii ya mpito imewapotosha."[86] Baada ya kusema haya, Sasa`ah alianza kulia kwa nguvu sana na watu wote waliokusanyika pale walijawa na huzuni. Walianza kulia kwa sauti kubwa wakiwa na huzuni ya kupindukia.[87]

[85] *Bihar Anwar*, Juz. 42, uk. 295
[86] *Bihar Anwar*, Juz. 42, uk. 295
[87] Sukhan, *Jame Talimaat-e-Islami*, Pakistan.

# MAJILISI 9

## ALI (A.S.) NA HAKI WANA MAANA YA KARIBU SAWA

Jina la Imam Ali (a.s.) lilikuja na maana sawa na haki baada kufariki kwake. Ali akawa mfano bora wa haki ya binadamu miongoni mwa watu wa kawaida na waungwana. Umar bin Abdul Aziz alisema: "Ali aliwapuuza waliomtangulia na kuwafanya waliomfuata waangukie kwenye hali ngumu. Watu walipolinganisha tabia za makhalifa na tabia bora na adilifu ya Imam Ali (a.s.) hawakuweza kujizuia kuwashutumu makhalifa waliomtangulia.

## DARMIYYA AMSIFU ALI (A.S.) MBELE YA MUAWIYAH

Muawiyah alikwenda Makkah kwa ajili ya Hijja na akagundua kuhusu Darmiyya Hujuniya ambaye alikuwa maarufu kwa kumuunga mkono Ali (a.s.) na kumpinga Muawiyah. Muawiyah alijulishwa kwamba mwanamke huyo alikuwa bado hai na akaamuru aitwe. Yeye (Muawiyah) alimuuliza mwanamke huyo: "Unajua nimekuita kwa sababu gani? Nataka kujua sababu inayokufanya wewe umpende Ali na unichukie mimi." Darmiyya alijibu: "Ni vema zaidi usingeniuliza swali hili?" Muawiyah akasema: "Itabidi ujibu swali hili kwa hali yoyote ile."

Darmiyya akasema: "Kwa sababu Ali alikuwa mshika bendera ya haki na usawa. Ulipigana naye bila ya haki. Ninampenda Ali kwa sababu aliwajali mafukara. Ninakuchukia wewe kwa sababu ulisababisha damu ya watu kumwagika kinyume cha sheria. Ulitengeneza mfarakano miongoni mwa Waislamu, ulifanya maamuzi batili na ukatekwa nyara na matamanio yako ya kilafi na choyo."

Muawiyah aliona aibu aliposikia haya na alikasirika. Hakuweza kudhibiti hasira yake na akamtukana Darmiyya. Halafu akadhibiti hasira zake na kama ilivyo kawaida alimwambia kwa upole: "Usijali, je umewahi kumuona Ali wewe mwenyewe binafsi?"

Darmiyya akajibu: "Ndiyo."

Muawiyah: Je, ulimuonaje?"

Darmiyya: "Wallahi, nilimuona katika hali ambayo kwamba yeye hakuwa amelewa na ufalme kama wewe."

Muawiyah akauliza: "Ulisikia sauti ya Ali?"

Darmiyya akasema: "Ndiyo, nilimsikia. Sauti yake hung`arisha na kuondoa uchafu kwenye nyoyo za watu kama mafuta ya zeituni yanavyoondoa kutu."

Muawiyah akauliza : "Unataka kitu chochote?"

Darmiyya akasema: "Utanipa kile nitakachoomba?"

Muawiyah akajibu: "Ndiyo, kwa nini nisikupe?"

Darmiyya akasema: "Nataka ngamia mia moja wenye manyoya mekundu."

Muawiyah akasema: "Kama nikikupa ngamia hawa, utanilinganisha mimi kuwa sawa na Ali.?"

Darmiyya akasema: "Kamwe."

Muawiyah aliamuru ombi la Darmiyya litekelezwe. Darmiyya akapewa ngamia mia moja. Muawiyah akasema: "Wallahi, kama Ali angekuwa hai, asingeweza kukupa hata ngamia mmoja."

Darmiyya akasema: "Unazungumzia kuhusu ngamia mmoja? Ninaapa kwa jina la Allah, Ali asingeweza kunipa hata unyoya mmoja wa ngamia mmoja kwa sababu ni mali ya umma wa Waislamu."[88]

## ADI ASOMA SHAIRI LA KUMSIFU ALI

Adi bin Hatim Tai alikuwa mmojawapo wa masahaba wakuu na wacha Mungu wa Kiongozi wa Wacha-Mungu. Alikuwa akimpenda Imam Ali (a.s.) kwa dhati ya moyo wake. Alisilimu kuwa Mwislamu wakati wa siku za mwisho za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Yeye kukubali kuwa Mwislamu kulimletea

[88] *Al-Iqdul Farid*, Juz. 2, uk. 113. Tamko hili: "Tunapaswa kufuata nyayo za Mtukufu Ali," linaonyesha kufurahisha (kimzaha) linapotamkwa na wale wanaokopesha malaki na marundo ya rupia zilizokusanywa kama kodi kutoka kwa watu kwa yoyote wampendaye na kisha wakasamehe madeni yao. (Ridhwani)

bahati njema nyingi sana. Alikuwa karibu sana na Imam Ali (a.s.) wakati wa kipindi chake cha ukhalifa. Watoto wake watatu wa kiume –Tariif, Tarfa na Taarif walikuwa bega kwa bega na Imam Ali (a.s.) kwenye vita vya Siffiin na wote walikufa kishahidi kwenye vita hivyo. Adi alipata fursa ya kukutana na Muawiyah uso kwa uso baada ya kuuawa kishahidi kwa Imam Ali (a.s.). Muawiyah alijaribu kutonesha vidonda vya Adi kwa kumfanya akumbuke vifo vya kishahidi vya wanawe na kumfanya Adi aseme alichotaka kusema.

Muawiyah akauliza: "Wapo wapi Tariif,Tarfa na Taarif?"

Adi alijibu kwa ujasiri: "Walikufa kishahidi mbele ya Imam Ali bin Abi Talib (a.s.) kwenye vita vya Siffiin." Adi alisisitiza maneno haya: "mbele ya Ali," katika kuonyesha furaha yake.

Muawiyah akasema: "Ali hajakufanyia haki wewe. Aliwapeleka wanao msitari wa mbele ili wauawe lakini hakuwapeleka wanawe msitari wa mbele ili waendelee kuishi."

Adi akasema: "Hapana, ukweli ni kwamba mimi ndiye ambaye sijamtendea haki Ali (a.s.) kwa sababu aliuawa kishahidi na mimi bado ninaishi."[89]

Muawiyah alipoona kwamba lengo lake halitimii, alibadilisha mbinu na akasema, "Simulia sifa za Ali."

Adi akasema: "Kunradhi tafadhali."

Muawiyah akasema: "Hapana sikuachi hivi hivi."

Muawiyah alipong`ang`ania sana, Adi alianza kusoma shairi la kumsifu Ali (a.s.) kama ifuatavyo:

"Wallahi, Ali (a.s.) alikuwa muona mbali na jasiri sana. Alikuwa akizungumza kwa haki na uamuzi wa kuwajibika. Chemchemi za elimu na hekima zilitiririka kutoka kwake. Alichukia mvuto wa dunia hii. Yeye alivutiwa na giza la usiku na upweke. Alikuwa akilia kwa khofu ya Allah na kutafakari juu ya kila jambo. Alikuwa akitathmini matendo yake akiwa peke yake na kutubu kuhusu siku za nyuma yake. Alipokuwa karibu na sisi, alifanana kama sisi. Alikuwa anatupatia chochote tulichomuomba. Tulipomtembelea alitaka tuketi karibu naye na kamwe hakuketi mbali na sisi. Licha ya kuwa karibu sana naye lakini tulikuwa tunamheshimu sana hivyo kwamba tulikuwa hatuthubutu kusema mbele yake. Tulikuwa hatuthubutu kutazamana

---

89 *Safinatul Bihar*, Juz. 2, uk. 170

naye uso kwa uso kwa sababu ya ukuu wake. Alipotabasamu, meno yake yalimeremeta kama lulu. Aliheshimu ukarimu na ucha-Mungu. Aliawapenda wasiojiweza. Watu wenye nguvu kamwe hawakuogopa kwamba labda angewafanyia dhulma na wasio na uwezo hawakupoteza matumaini katika uadilifu wake.

"Ninaapa Wallahi, usiku moja nilimuona Ali (a.s.) amesimama kwenye pembe ya msikiti. Palikuwepo na ukimya kila mahali. Ndevu zake zililoa kwa machozi yake. Alikuwa anatetemeka na kugwaya kama mtu mwenye kusumbumbuliwa na jambo. Maneno yake bado yanagonga akili yangu: 'Ewe dunia! Kwa nini unanisakama? Nenda zako na ukamdanganye mtu mwingine. Mazingaombwe yako hayatakuwa na athari juu ya Ali (a.s.). Nimekutaliki mara tatu na hakuna uwezekano wa maafikiano sasa. Wewe (dunia) huna ladha na hutabiriki. Kwa masikitiko, mahitaji kwa ajili ya safari ni kidogo na safari ni ndefu na hakuna mtu wa kufuatana naye.'"[90]

Adi alisema yote haya na machozi yakaanza kutiririka kutoka kwenye macho ya Muawiyah. Alifuta machozi yake kwa mikono ya nguo aliyovaa na akasema: "Mwenyezi Mungu na amrehemu Ali (a.s.). Kwa kweli, alikuwa muadilifu kama ulivyomuelezea."[91]

Sasa hebu niambie, unajihisi vipi bila yeye kuwepo?

Adi akasema: "Ninajihisi kama vile mama ambaye mwanaye amechinjwa akiwa amempakata kwenye mapaja yake."

Muawiyah akauliza: "Je! Hutaweza kamwe kumsahau Ali?"

Adi akasema: "Hapana, lakini lihamu ya wakati inaweza kunifanya nisahau maumivu."

Shaykh Mufiid anaandika kwenye *Al-Irshad* kwamba kipindi cha Uimamu cha Amiri wa Waumini kilikuwa kwa miaka thelathini baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Katika kipindi hicho alishika hatamu ya kuendesha serikali kwa miaka mitano na miezi sita. Katika kipindi hiki kifupi pia alipigana na wanafiki. Aliuawa kishahidi mnamo siku ya Ijumaa alfajiri, tarehe 21 ya mwezi wa Ramadhani. Alikufa kishahidi kutokana na athari ya pigo la upanga wa Ibn Muljim Muradi.[92]

[90] *Safinatul Bihar*, Juz. 2, uk. 170.

[91] *Safinatul Bihar*, Juz. 2, uk. 170.

[92] *Kafi*, Juz. 7, uk. 52; *Mirat al-Uquul fi Sharh Kafi*, Juz. 23, uk. 88

Wosia mashuhuri wa Amiri wa Waumini umetajwa kwenye *al-Kafi* kwa kina. Wosia huu umeelekezwa kwa wanawe wa kiume na pia kwa binadamu wote hadi Siku ya Hukumu. Mwishoni mwa wosia huo imeandikwa kwamba Imam Ali (a.s.) alisema: "Allah na awalinde nyinyi Ahlul Bayt. Ninakukabidhini nyinyi nyote kwa Allah."

Imeandikwa kwenye *al-Kafi* kwamba Imam Ali (a.s.) aliendelea kurudia lile tamko la "Hapana mungu ila Mwenyezi Mungu," hadi alipokata roho kwenda kwenye Makazi ya kimbinguni.[93]

Rehema ya Allah Mwenyezi iwe juu yake na dhuria wake.[94]

---

[93] *al-Kafi*, Juz. 7, uk. 52; Mirat al-Uquul fi Sharh al-Kafi, Juz. 23, uk. 88
[94] *Biist Guftar*, uk. 67-71

# MAJILISI 10

Sura ya suala la Fadak kuhusiana na Bibi Zahra inashangaza na ngumu kufahamika. Kwa ujumla inatakiwa izingatiwe akilini kwamba Imam Ali (a.s.) na Bibi Zahra walikuwa wanandoa ambao kwamba hawakuwa na tamaa ya kujikusanyia mali. Imam Ali (a.s.) alikuwa amesema: "Nitapata maslahi gani kutokana na Fadak na rasilimali zingine ambapo nyumba halisi ya binadamu ni makaburi yao hapo baadaye." Kwa hiyo, Imam Ali (a.s.) hakuvutiwa kuhangaikia Fadak.[95]

Mtu ambaye tayari ameitaliki dunia atafanya nini na Fadak? Mbingu itafanya nini kwa mtu ambaye ameruka na kwenda upande mwingine? Mtu ambaye yuko mbali na hadaa na udanganyifu wa dunia ya maada na utajiri wake, ambao unafikiriwa na watu kuwa ni mafanikio ya maisha; wakati anapokuwa mkwasi sana, atafanya nini na Fadak?

## TABASAMU LENYE MAANA LA BIBI FATIMA

Hadithi ninayosimulia hapa ni jambo linalokubalika katika historia ya Uislamu na imesimuliwa na wapokezi wa Ahlus-Sunna. Wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa katika dakika zake za mwisho, binti yake mpendwa, Bibi Zahra alikuwa analia sana kuhusu hali ya baba yake. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimnong`oneza kitu kwenye masikio ya Bibi Zahra na akaanza kulia kwa sauti kubwa zaidi. Halafu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akanong`oneza kitu kwenye masikio ya Bibi Zahra na akatabasamu. Hili lilikuwa ni jambo la kushangaza sana! Baadaye Bibi Zahra aliulizwa kile Mtume alichomnong`oneza masikioni mwake. Akasema: "Mara ya kwanza, baba yangu alinifahamisha kwamba alikuwa anaondoka hapa duniani. Nililia kwa sauti kubwa kwa sababu ya uchungu wa kutenganishwa. Hata hivyo, aliponiambia kwamba: "Ewe binti yangu! Wewe utakuwa mtu wa kwanza kukutana na mimi baada ya mimi kufariki dunia, hapo nilitabasamu kwa furaha."[96]

[95] *Nahjul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 45, uk. 958.
[96] *Tarikh Kamil*, Juz. 3, uk. 323; *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 100; *Biharul Anwar*, Juz. 22, uk. 470.

# UJASIRI WA BIBI ZAHRA

Pia tunajua kwamba Bibi Zahra alikuwa akiugua na kuwa kitandani muda mwingi baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Bibi Zahra alikuwa anafahamu kwa uhakika kwamba taa ya uhai wake ingezimika baada ya muda si mrefu. Licha ya haya, madai yake ya umiliki wa Fadak yanaonekana kuwa kitu cha kushangaza. Jibu la swali hili linaloibuka akilini mwetu ni kwamba rasilimali ya Fadak haikuwa na thamani yoyote kwa Bibi Zahra lakini hiyo ilikuwa ni haki yake kisheria. Mtu anaponyang`anywa haki yake lazima aidai. Kwa hiyo, Bibi Zahra aliona ni muhimu na alikwenda kwenye msikiti wa Mtume ili kutetea haki yake. Alizungukwa na wanawake wa Bani Hashim na wanawake wengine waaminifu alipokuwa anakwenda msikitini.[97] Bibi Zahra alitoa hotuba mbele ya mtawala wa wakati huo, ambayo ilimtingisha mtawala huyo. Bibi Zahra alidai haki yake. Alishutumu madai ya upande wa upinzani na hakuwa na khofu hata kidogo. Kwa nini Bibi Zahra hakumuogopa mtawala wa wakati huo? Je, kitendo hiki kilikuwa kinyume na mafundisho ya Uislam? Je, kitendo hiki hakikufaa kufanywa na mwanamke? Je, ni kosa mwanamke kwenda msikitini namna hiyo na kuzungumza kuhusu mali ya kidunia mbele ya maelfu ya watu? Je, ni kosa mtu kutetea haki yake? Hapana, hapana kabisa. Haikuwa kosa kwa Bibi Zahra kutetea haki yake.

Bibi Zahra hakuwa na fungamano na ukwasi wa kidunia na aliuona kwamba ni kitu kisichokuwa na thamani, ambacho kiliishia kwenye utajiri na tamaa ya anasa ya mtu binafsi. Pia alikuwa anafahamu kwamba baada ya muda mfupi angetoweka kwenye Makazi haya ya muda. Mtu anapojua kwamba ataondoka hapa duniani baada ya muda mfupi, kwa kawaida, matamanio yake ya kidunia hukoma. Ukifikiriwa ukweli huu, msimamo wa Bibi Zahra ulikuwa ni kutetea haki katika hali ya aina yoyote ili kwamba jamii isije ikajiingiza kwenye tabia ya kupora haki za watu wengine. Ndiyo maana Bibi Zahra alijitokeza kwa ujasiri na kutetea haki yake ipasavyo.

Bibi Zahra alikwenda nyumbani kwa khalifa wa wakati huo na akapata barua ya ruhusa ya  kurudishiwa Fadak kutoka kwake. Hata hivyo, barua hiyo yenye idhini hiyo ilichukuliwa kwa nguvu kutoka kwa Bibi Zahra. Baada ya hapo, Bibi Zahra alikwenda msikitini akisindikizwa na Amiri wa

[97] *Biharul Anwar*, Juz. 9, uk. 216; Ibn Abil Hadid, *Sharh Nahjul Balaghah*, Juz. 16, uk. 211.

Waumini. Jambo lisilotajika lilitokea msikitini hapo na alilazimika kuwapa changamoto wanyang`anyi.

## UJASIRI WA BIBI ZAINAB

Utaona hali ile ile kama ukiangalia tabia ya Bibi Zainab. Endapo tabia njema inamlazimisha mwanamke kuwa muoga basi Bibi Zainab naye pia angekuwa muoga kama wanawake wengine. Kufuatana na maneno mashuhuri, Bibi Zainab alipaswa asitoke kwenye "gamba la uwanamke." Kitu gani kilimlazimisha Bibi Zainab kutoa hotuba kwenye lango la Kufa? Hivi mtu yeyote anaweza kulazimishwa kutoa hotuba? Basi ni kitu gani kilimlazimisha Bibi Zainab kuonyesha ujasiri wake na kumuita Ibn Ziyad majina kama hayo ndani ya baraza lake, jambo ambalo liliweka maisha yake na yale ya watu wengine wa familia yake hatarini?

Baraza la Yazid lilikuwa tukufu zaidi na umaarufu wake ulionekana kwa urahisi zaidi kwa sababu Ibn Ziyad alikuwa gavana na Yazid alikuwa khalifa. Pili, Ibn Ziyad alikuwa Kufa ambapo Yazid alikuwa Syria, ambayo ilikuwa jirani na Costantinople. Utawala ulipamba makasiri yote kwa ufanisi katika kujifanya kwenda sambamba na utukufu wa Uislamu. Imeandikwa kwenye vitabu vya historia kwamba "kasri ya kijani" hiyo ilikuwa kubwa sana hivyo kwamba baada ya kuingia kwenye lango, mtu alilazimika kupita kwenye idadi ya viwanja vya mabaraza, milango na makundi ya watumishi kadhaa ili kuweza kufika kwenye lango lingine. Baraza yake iliyopambwa, ilikuwa na viti vya kifalme meza za chakula na viti vizuri mno kwa ajili ya watu tajiri. Ilikuwa ni baraza adhimu sana lakini binti yake Ali (a.s.) mwenye ujasiri kama wa simba hakujali vitu hivyo na akasema: "Ewe Yazid! Wewe ni mtu wa hali ya chini sana na duni kwa maoni yangu kwamba niweze kuzungumza na wewe."[98]

Hivi mwanamke muoga anaweza kumfedhehesha Yazid mbele ya watumishi wa baraza? Hatari mbaya zaidi iliyokuwa inamkabili Bibi Zainab ilikuwa ni kupoteza uhai wake mikononi mwa mfalme yule dhalimu lakini hakuogopa kupoteza uhai wake hata kidogo. Hapakuwepo na hatari kwa heshima yake. Kwa kweli, heshima yake iliongezeka kwa sababu ya ujasiri wake.

[98] *Luhuuf*, Sayyid bin Tawuus, uk. 181.

Kwa hiyo tofauti hii inahusishwa na hali fulani maalum ambayo mwanamke anayo. Halafu jambo muhimu ni kwamba tofauti hii inahusishwa na tabia na si maadili au utu wa mtu. Hakuna tofauti kati ya mwanamume na mwanamke kuhusu utu wa kimaadili. Sote tunajua kwamba hata kama mwanamume anakabiliwa na hali kama ile ambapo anao wajibu wa kulinda amana ya jamii huo si muda wa kusamehe na kuonyesha ujasiri na wala hakuna nafasi ya kuonyesha kutojiweza na unyonge. Anatakiwa kubakia mwaminifu na kutenda kwa uangalifu. Lazima aonyeshe ujasiri ili kwamba mnyang`anyi asiruhusiwe kunyang`anya.[99]

"Na hapana uwezo wala nguvu isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu Aliye Mkuu na Muweza wa Yote."

[99] *Talim wa Tarbiyat dar Islam*, uk. 178-181.

# MAJILISI 11

## BIBI ZAHRA AMHUZUNIKIA BABA YAKE

## ENYI WAOMBOLEZAJI WA FATIMA ZAHRA!

Siku hizi zinahusishwa na kifo cha Bibi Zahra na zinahusishwa na nafsi yake tukufu. Kwa hiyo, nitasema maneno machache kuhusu mateso yake na kuhitimisha hotuba hii. Inasimuliwa kwamba baada ya kifo cha baba yake, Bibi Zahra kamwe hakuonekana bila kufunga kitambaa kwenye paji la uso wake. Alianza kukonda kila uchao. Alikuwa analia kila wakati kuhusu kifo cha kutia huruma cha baba yake.[100]

Maneno haya: 'nguzo zilibomolewa' yana kidokezi cha ajabu. Nguzo maana yake ni mhimili; kama vile nguzo za nyumba ambamo jengo husimama. Katika sayansi ya mwili wa binadamu, miguu na viungo vya mfupa wa uti wa mgongo ndio nguzo za mwili wa binadamu, kwa kutumia nguzo hizo mtu husimama. Wakati mwingine, katika umbile la kimwili nguzo huharibika. Mathalani, miguu ya mtu hukatwa au viungio vya uti wa mgongo wake huachana. Kwa hali ile, mtu hawezi kusimama. Vivyo hivyo, nafsi ya mtu huangukia kuwa mawindo ya uharibifu kwa jinsi ambayo huelekea kwamba nguzo zinazosaidia nafsi ya binadamu huharibika kabisa. Hali ya Bibi Zahra baada ya kifo cha baba yake inasemekana ilikuwa hivyo.

## ENYI WAOMBOLEZAJI!

Bibi Zahra na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walipendana sana. Ndiyo maana lazima utakuwa umesikia kwamba Bibi Zahra alikuwa na desturi ya kuwakumbatia sana wanawe,Imam Hasan na Imam Husain (a.s.) na kulia:

"Enyi vipenzi vyangu! Enyi nuru ya macho yangu! Baba yenu mwenye moyo wa upendo na huruma ambaye aliwapenda sana kuliko chochote amekwenda wapi? Alikuwa na tabia ya kutembea akiwa amewabebeni nyinyi mabegani mwake na kuwaweka kwenye mapaja yake na kupapasa vichwa vyenu kwa mapenzi mno![101]

"Kwa jina la Allah na kwa Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.)."

[100] *Biharul Anwar*, Juz. 43, uk. 181; *Baitul Ahzan*, uk. 238.

[101] Biharul Anwar, Juz. 43, uk. 181; Baitul Ahzan, uk. 238; Siiri dar Siirah-e-Nabawi, uk. 59-60.

# MAJILISI 12

## SIKU ZA UHAI WA FATIMA

Siku hizi zinahusishwa na Bibi Fatima (a.s.). Jaribu kufikiri ni kwa nini kuna thawabu nyingi sana katika kusimulia historia safi ya maisha na maadili ya Ahl Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).[102] Kuna thawabu nyingi sana kwa sababu waliumbwa katika umbo la binadamu, ambao ni mfano wa hali ya juu sana kwa ajili ya binadamu. Wao walikuwa ni mifano ya kuigwa. Walifanywa na Mwenyezi Mungu, muumba wa binadamu kama "mfano kamili."

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Ninafundishwa maadili kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Ali (a.s.) amefundishwa maadili na mimi."[103] Ali (a.s.) ni mfano bora wa mtu aliye kamili. Ni mtu bora sana kuhusu hotuba, kutembea na tabia. Pia Bibi Zahra alikuwa ni mfano bora wa mtu aliye kamili kwa wanadamu.

### WOSIA WA BIBI ZAHRA

Sasa Bibi Zahra alihisi kwamba alikuwa aondoke hapa duniani punde tu. Kwa mujibu wa riwaya, aliandika wosia katika faragha na akaweka chini ya mto. Yafaa ifahamike ni jinsi gani tabia ya mke wa mfano bora kwa mume wake inavyotakiwa iwe. Imam Ali (a.s.) alipokwenda karibu na kitanda cha Bibi Zahra, alionyesha kutaka kwake kuandika wosia. Imam Ali (a.s.) aliketi karibu naye na akakiweka kichwa chake kwenye paja lake. Bibi Sayyada akasema: "Ewe Abul Hasan! Ninataka kuandika wosia chache." Imam Ali (a.s.) akasema: "Nitasikiliza na kutii. Unaweza kusema unachotaka kusema."

Bibi Zahra alianza kwa upole kutoa utangulizi, ambao Imam Ali (a.s.) alipousikia aliguswa sana. Bibi Zahra alisema: "Ewe Ali! Kipindi chote nilichoishi nyumbani mwako niliishi kama kijakazi wako. Nilitumia muda ndani ya nyumba yako kwa uaminifu sana, nilikuwa katika hali hii ndani ya

102 Maneno yanayofuata baada ya tamko hili yamekosekana kwenye kanda.
103 *Biharul Anwar,* Juz. 16, uk. 231; *Mizanul Hikma*, Juz.1, uk. 78.

nyumba yako ambayo kwamba....” Imam Ali (a.s.) aliposikia maneno haya, macho yake yalijaa machozi. Alikikandamiza kichwa cha Bibi Zahra kifuani mwake kama vile anataka kuwasilisha ujumbe: “Kamwe sitaki uombe radhi namna hii” kwa sababu maneno ya Bibi Zahra yalikuwa yanamaanisha kwamba alikuwa anaomba msamaha kwa mapungufu yoyote katika huduma zake. Ambapo kitendo cha Imam Ali (a.s.) kilimaanisha tu kwamba: “Ewe Zahra! Sipendi wewe uzungumze namna hiyo kwa sababu maneno hayo yananiumiza.”[104]

## MAHUSIANO YA ADABU YA FATIMA NA ALI (A.S.)

Ninaliacha jambo hili hapa na ninawasilisha mpangilio mwingine wa matukio kwenu wasomaji. Kama mjuavyo Bibi Zahra aliwakasirikia watu waliomfanyia ukatili. Walipofahamu kwamba hali ya Bibi Zahra imekuwa mbaya, walipeleka ujumbe kwake wa kuomba ruhusa ya kumuona. Kwa hakika walitaka kuomba radhi na kumtaka asahau yale waliyomfanyia siku za nyuma, kwa kisingizio cha kumtembelea wakati wa kuumwa kwake. Bibi Zahra hakuwaruhusu kumtembelea yeye na akasema: Sifurahikiwi na wale watu walionidhuru na kumnyang`anya mume wangu haki yake. Sitaki waingie nyumbani kwangu na kukanyaga sakafu ya nyumba yangu.”

Hatimaye, walikwenda kwa Imam Ali (a.s.) na wakasema: “Ewe Abul Hasan! Tumemuomba binti ya Mtume aturuhusu tumtembelee wakati wa maradhi yake lakini hakuturuhusu. Kwa hiyo tumekuja kwako kuomba ruhusa kutoka kwako.” Sasa ona heshima ambayo Imam Ali (a.s.) aliyokuwa nayo kwa Bibi Zahra. Imam Ali (a.s.) hakwenda kwa Bibi Zahra na kumwambia wazi wazi: “Unaweza kunipa chochote nitakachokiomba kutoka kwako?” au “Hali ya mambo inataka hivi na hivi.....” Lakini kinyume chake Imam alisema: “Zahra (au binti ya Mtume). Hawa watu wawili wameomba upatanishi wangu.” Yaani ni kwamba, uamuzi ni wa kwako, ama uwaruhusu au hapana. Hata hivyo, angalia jinsi Bibi Sayyada alivyojibu. Alisema: “Ewe Ali! Hii ni nyumba yako, mimi ni mkeo na nisingepinga uamuzi wako.”[105]

---

[104] *Biharul Anwar*,Juz. 43, uk.191; *Baitul Ahzan*, uk. 253.

[105] *Biharul Anwar*, Juz. 28, uk. 303.

Imam Ali (a.s.) alimwambia Bibi Fatima kwamba fulani na fulani wapo mlangoni na walitaka kumsalimia na wanauliza kama wangeruhusiwa kuingia ndani. Bibi Fatima alijibu: “Hii ni nyumba yako na mimi ni mkeo. Ni

## KUKOSA UTULIVU KWA IMAM ALI (A.S.) KWA KUTENGANISHWA NA BIBI ZAHRA

Wanandoa hawa nyoyo zao zilikuwa zimefungwa pamoja kama vile usemi usemao: "Waswahili wa Pemba wajuana kwa vilemba," au "Ndege wafananao kwa manyoya huruka pamoja." Palikuwepo na mafungamano ya ajabu baina ya hawa watu wawili. Kwa hiyo, hivi Imam Ali (a.s.) hakuwa na haki ya kutamani afe baada ya kifo cha Bibi Zahra ambaye alikuwa mashuhuri kabisa hivyo kwamba hapakuwepo na mtu wa mbadala au mrithi wake?

Imam Ali (a.s.) mwenyewe anasema:

"Tulikuwa tukitumia siku za ujana wetu kwa furaha kama wanandoa wa njiwa. Hata hivyo, muda ulitutenganisha. Kwa hakika, muda huwatenganisha marafiki."[106]

Atafanyaje mtu ambaye ameharibikiwa kwa kumkosa msaidizi wake ambaye ni wa kipekee? Alipokuwa akitembelea kaburi tukufu la Bibi Zahra, alikuwa na tabia ya kumsalimia na kusimulia hisia zake kwake. Alikuwa na tabia ya kumwambia jambo halafu anatoa jibu yeye mwenyewe.

Imam Ali (a.s.) alikuwa akijiambia mwenyewe:

"Kwa nini nimesimama kwenye kaburi la mpendwa wangu na kumsalimia yeye ambapo sipati majibu ya salamu kutoka kwenye kaburi la mpendwa huyo? Wewe ni mpendwa wa aina gani! Hujibu salamu zangu. Je, umesahau urafiki wetu baada ya kuondoka duniani? Umemsahau Ali?"[107]

Halafu alikuwa akijisemea mwenyewe peke yake:

"Mpendwa wangu alisema: 'Ewe Ali! Nitakujibuje? Hujui ya kwamba Zahra wako amelala na kufunikwa chini ya udongo?"[108]

uamuzi wako kufanya utakavyo." Hadithi ya *Biharul Anwar*, Juz. 43, uk. 246 na *Baitul Ahzan*, uk. 246 ni kama ifuatavyo: "Hii ni nyumba yako na wanawake lazima wawatii waume zao. Nisingepinga uamuzi wako wowote. Unaweza kumruhusu yeyote unayetaka."

[106] *Diwan Imam Ali*, uk. 86.

[107] *Diwani Imam Ali*, uk. 89.

[108] *Ashnal ba Quran*, Juz. 7, uk. 56-58.

# MAJILISI 13

## ALI ALIMKUMBATIA BATUUL

Enyi wafuasi wa Ali na Batuul!

Mfululizo wa Majilisi unakwisha leo. Usiku wa leo ni usiku wa kipekee. Kwa hiyo ni muhimu kutoa maelezo ya majanga ya Bibi Fatima Zahra katika kipindi cha siku za Fatima. Lilikuwa ni jambo lisiloweza kuvumilika kwa Imam Ali (a.s.) kutenganishwa na Bibi Zahra. Hali ya Bibi Zahra ilizidi kuwa dhaifu. Alikuwa amelala kitandani pake na Imam Ali (a.s.) aliketi karibu yake. Bibi Zahra alianza mazungumzo akionyesha unyenyekevu, ambao ulimgusa sana Imam Ali (a.s.). Macho yake yalijaa machozi. Maneno ya Bibi Zahra yanaweza kufupishwa kama ifuatavyo:

"Ewe Ali! Urafiki wetu wa hapa duniani unakaribia hatima yake. Mimi ninaondoka hapa duniani. Nilijaribu kuwa mtiifu ndani ya nyumba yako kwa kadiri nilivyoweza na sikukupinga wewe katika jambo lako lolote..... (na maneno mengine kama hayo)" Maneno haya yalimgusa Ali sana hivyo kwamba haraka sana alimkumbatia Bibi Zahra. Kichwa cha Bibi Zahra kilikandamizwa kifuani mwa Imam Ali (a.s.) na Imam Ali (a.s.) akasema huku macho yake yakiwa yamejaa machozi:

"Ewe binti ya Mtume (s.a.w.w.)! Wewe ni bora zaidi kuliko maneno haya; sasa kwa nini unaonyesha hali ya kutojiweza sana?"[109]

Mapenzi yasiyokuwa na mpaka baina ya Ali na Zahra hayawezi kuelezeka kwa maneno. Kwa hiyo tunaweza kuelewa jinsi ambavyo ingekuwa vigumu kwa Ali kuvumilia upweke baada ya kifo cha Bibi Zahra. Kuhusu hili, ningependa kusimulia tu maneno ya Imam Ali (a.s.) yale aliyosema akiwa kwenye kaburi tukufu la Bibi Zahra. Maneno haya yameandikwa pia kwenye *Nahjul Balaghah*.

**Kwa nini Bibi Fatima alizikwa wakati wa giza la usiku?**

Bibi Zahra alikwisha andika wosia: "Ewe Ali! Unizike wakati wa giza la usiku baada ya kunikosha na kunivisha sanda. Sitaki wale watu walionidhu-

[109] *Biharul Anwar*, Juz. 43, uk. 191; *Baitul Ahzan*, uk. 253.

ru wahudhurie mazishi yangu." Wakati wote historia huwa na muelekeo wa kupotoshwa. Baadhi ya watu hufanya uhalifu na wakati huo huo hujaribu kuthibitisha kuwa hawana hatia kwa lengo la kutaka kupotosha historia. Maamun Rashid alifanya hivyo. Alimuua Imam Ali Ridha (a.s.) kishahidi, lakini wakati wa mazishi ya Imam alichukua kiganja kizima cha udongo mkononi mwake na akaweka kwenye kichwa chake. Kisha akalia macho ya mamba na kusoma shairi.[110] Kwa njia hii, historia ilipotoshwa na watu wengi hawakuamini kwamba Maamun wa ukoo wa Bani-Abbas alimuua Imam Ali Ridha (a.s.) kishahidi. Huu unaitwa upotoshaji wa historia.

Bibi Zahra alitaka kuokoa historia kutokana na upotoshwaji. Kwa hiyo, alisema: "Tafadhali unizike wakati wa giza la usiku," ili kwamba swali liweze kubakia katika historia daima kwamba kwa nini binti huyo pekee wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizikwa wakati wa usiku? Kwa nini kaburi lake halijulikani? Hii ilikuwa ndio sera ya Bibi Zahra ambayo kwa sababu yake, hata baada ya zaidi ya miaka elfu moja bado kuna swali lisilojibika katika historia:

## "KWA NINI BINTI MPENDWA WA MTUKUFU MTUME (A.S.) ALIZIKWA WAKATI WA GIZA LA USIKU? KWA NINI KABURI LAKE HALIJULIKANI?"[111]

Historia inauliza: Kwa nini binti wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizikwa katika usiku wa giza? Hivi kuhudhuria mazishi sio kitendo kilichokokotezwa? Sasa ni kwa nini kikundi kidogo tu cha watu ndio kilihudhuria swala ya mazishi ya huyo binti wa pekee wa Mtume (s.a.w.w.)? Kwa nini mahali pa kaburi la Bibi Zahra palifanywa kuwa siri? Kwa nini watu walikuwa hawajui mahali alipozikwa Bibi Zahra?

## "EWE ALI, BAADA YA MAZISHI, BAKIA NAMI KWA MUDA KIDOGO"

Baada ya Imam Ali (a.s.) kumzika Bibi Zahra kufuatana na wosia wake, ghafla akasikia sauti yake kutoka kwenye kaburi lake: "Ewe Ali! Tafadhali keti karibu na kaburi langu kwa muda kidogo na usiondoke kwa sababu

[110] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 491. (mifano ya aina hii inaonekana kwa wingi kwenye siasa za zama za leo). Rizwani

[111] *Baitul Ahzan*, uk. 266.

ninakuhitaji wewe sana katika nyakati hizi za hofu ya kaburini."

Imam Ali (a.s.) alifanya hasa kama alivyousia Bibi Zahra. Hebu fikiri Imam alilazimika kupita kwenye mpito wa aina gani wakati huo. Siwezi kueleza hali aliyokuwa nayo Imam kwa maneno kwa wakati huo jinsi alivyolazimika kumshusha Bibi Zahra ndani ya kaburi kwa mikono yake mwenyewe na jinsi alivyoweka udongo juu ya kaburi. Kitu kimoja tu ninachojua ni kwamba imeandikwa kwenye historia: "Aliposambaza udongo kwenye kaburi kwa mikono yake, huzuni yake ilizidi."[112] Imam Ali (a.s.) alianza kukung`uta vumbi kwenye nguo zake baada ya kutengeneza kaburi lake (Bibi Zahra). Hadi hapo, Imam alikuwa anashughulika na kazi na wakati mtu anapojishughulisha na kazi, mawazo yake yote huelekea kwenye kazi hiyo anayoifanya. Kwa hiyo, huzuni inakuwa imepungua kwa kiasi fulani. Hata hivyo, sasa wakati ulifika ambapo Imam Ali (a.s.) alitakiwa kuketi karibu ya kaburis la Bibi Zahra baada ya kumzika kufuatana na wosia wake na alihisi alikuwa anahitaji mtu ambaye angemwambia hisia zake.

## ALI ANAELEZEA HISIA ZAKE

Kama unavyojua, Imam Ali (a.s.) alikuwa akijihisi mpweke wakati mwingine. Alipokuwa hawezi kumwambia mtu yeyote hisia zake, alikuwa na desturi ya kuegemea ndani ya kisima na kusimulia hisia zake. Hata hivyo, leo hii moyo wake uliharibika kabisa kwa sababu ya kutenganishwa na Bibi Zahra. Imam hakumuona mwingine aliye bora zaidi ya mpendwa Mtume wa Allah wa kumwambia hisia zake. Hatimaye, Ali aligeuka na kuelekea upande lilipo kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) huku moyo wake ukiwa mzito na akisema:

"Rehema na amani juu yako, Ewe Mjumbe wa Allah, salamu hizi zinatoka kwangu na kwa mpendwa binti yako ambaye sasa amelala kwenye udongo mbele yako na baada ya muda si mrefu atakutana nawe. Ewe Mjumbe wa Allah! Binti yako mpendwa amepunguza kiwango cha uvumilivu na subira yangu.[113]

"Ewe Mjumbe wa Allah! Kama ukitaka kujua hali ya Ali; sikiliza. Subira ya Ali imepungua." Ndiyo maana Ali (a.s.) alisema:

---

[112] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 273; *Baitul Ahzan*, uk. 264

[113] *Nahjul Balaghah*, *Faizul Islam*, Hotuba ya 193, uk. 642; *Sharh Nahjul Balaghah*, Ibn Abil Hadid, Juz. 10, uk. 265.

"Baada ya muda mfupi binti yako atakujulisha jinsi umma ulivyoungana na kumtesa kikatili."[114]

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**"Na punde watajua waliodhulumu ni mgeuko gani watakaogeuka?"**
**[Sura Ash-Shu'araa 26 : 227]**

[114] *Nahjul Balaghah, Faizul Islam*, Hotuba ya 193; *Sharh Nahjul Balaghah*, Ibn Abil Hadid, Juz. 1, uk. 265. *Falsafa Akhlaq*, uk. 248, 250.

# MAJILISI 14

## MTINDO WA MAISHA RAHISI YA MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.)

Maisha rahisi ilikuwa ni mojawapo ya kanuni za misingi za Mtume (s.a.w.w.). Inasimuliwa kwamba alifuata kanuni hii hadi mwisho wa uhai wake.[115]

Imetajwa kwenye hadithi kwamba siku moja Umar bin Khattab aliingia nyumbani kwa Mtume na kuona kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa amewapa kisogo wake zake na alikuwa anasema: "Mko huru kuchukua talaka au ili kuweza kuishi maisha rahisi au mfanye subira katika wito wenu." Ilikuwa hivyo kwa sababu baadhi ya wakeze Mtume walimwambia: "Hatuwezi kuishi maisha rahisi kama haya. Sisi tunataka pia kuwa na mapambo na vito kama wanawake wengine; kwa hiyo tafadhali tupatie chochote kutoka kwenye ngawira ya vita."

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anawaambia: "Mimi ninaishi maisha rahisi sana. Kwa hiyo, kama mnataka, mimi nipo tayari kuwapeni talaka na pia nipo tayari kuwalipeni fedha (kitoka nyumba) kama ilivyoagizwa na Qur`ani tukufu. Ni sawa kama mnataka kuishi maisha rahisi, vinginevyo nipo tayari kuwapeni talaka."[116] Kutokana na haya, wake wote wa Mtume walijibu kwa pamoja: "Ewe Mtume wa Allah! Tupo tayari kuishi maisha ya kawaida." Tukio hili limesimuliwa kwa kina sana.[117] Vitabu vya Ahlus-Sunna pia vinasimulia hadithi hii.

Inasimuliwa kwamba pale ambapo Umar alipata kufahamu matatizo ya wakeze Mtume, alikwenda kuzungumza na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Anasema kwamba alipofika pale, alikuwepo mtu mmoja; Mhabeshi ambaye alikuwa amekaa nje akiwa amepewa agizo la kutomruhusu mtu yeyote

[115] *Irshadul Quluub*, Sura, 32, uk.155

[116] "Ewe Mtume! Waambie wake zako: Ikiwa mnapenda maisha ya dunia hii na uzuri wake basi njooni, nitakupeni matumizi na kukuacheni muacho mzuri. Na kama mnamtaka Mwenyezi Mungu na Mtume wake na nyumba ya Akhera, basi Mwenyezi Mungu amewaandalia wafanyao mema miongoni mwenu malipo makubwa." [33:28-29]

[117] *Al-Mizan fi Tafsiir al-Qur`ani*, Juz. 3, uk. 316

kumuona Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Umar alimwambia mlinzi amfahamishe Mtume kuhusu kuwasili kwake. Mlinzi alikwenda ndani na aliporudi akasema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakutoa jibu lolote." Baada ya hapo Umar alijaribu kuomba ruhusa mara mbili zaidi tena lakini hakuipata. Alipokwenda pale kwa mara ya tatu, alipata ruhusa ya kuingia. Umar alimuona Mtume (s.a.w.w.) amepumzika kwenye mkeka wa makuti ya mtende. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliposogea, alama za mkeka zilionekana kwenye mwili wake mtukufu. Umar alipoona aliguswa na msisimko na akasema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hivi kwa nini wafalme wa kidunia wamezungukwa na ukwasi na Mjumbe wa Allah yuko katika hali kama hii?"

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikasirika baada ya kusikia maneno ya Umar. Alisimama na kusema:

"Unasema nini? Ni upuuzi gani huu? Kwa msingi wa haya ambayo umeyaona unastaajabu kwa nini mimi sina mali? Kwa maoni yako hii ni namna ya kunyimwa kuhusu mimi na neema kuhusu wao. Wallahi, hata kama anasa zote hizi zikija kwa Waislamu, bado hazitakuwa jambo la kujivunia."[118]

Enyi waombolezaji! Mmeona ni rahisi kiasi gani mtindo wa maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ulivyokuwa! Alipofariki dunia, aliacha rasilimali gani hapa duniani? Baadaye, Imam Ali (a.s.) alipofariki dunia, aliacha rasilimali gani hapa duniani?

## URAHISI WA BIBI FATIMA

Kama tujuavyo kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alibakiwa hai na mtoto mmoja tu wa kike. Kwa kawaida, kila baba kufuatana na mapenzi yake ya ubaba na kufuatana na desturi zetu, hujaribu kuacha kitu fulani kwa ajili ya binti yake kabla hajafa. Mathalani, anaweza kununua nyumba kwa ajili ya binti yake ambapo anaweza kuishi kwa amani. Hata hivyo, historia inasema kwamba siku moja Mtukfu Mtume (s.a.w.w.) alimtembelea binti yake nyumbani kwake. Alimuona binti yake amevaa bangili ya madini ya fedha na nyumba yake ilikuwa na pazia lililopendeza. Licha ya kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anampenda sana binti yake, aliondoka bila kusema naye. Bibi Zahra alielewa kwamba baba yake hakuwa anapenda hata

118 *Sirat-e-Halabiya*, Juz. 3, uk. 316

utajiri wa kiasi hicho kwa ajili yake. Kwa nini? Kwa sababu hicho kilikuwa ni kipindi cha watu wa Suffa (jukwaa lililokuwa kwenye msikiti wa Mtume ambapo watu wasio na Makazi walijihifadhi hapo).[119]

Bibi Zahra kila wakati alikuwepo kwenye safu ya watu wakarimu. Alikuwa na tabia ya kuwapa wasiojiweza rasilimali yoyote ya kidunia aliyokuwa nayo. Mara alipoona kwamba baba yake ameondoka alivua ile bangili na lile pazia na akampelekea Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pamoja na ujumbe ufuatao:

"Ewe Mjumbe wa Allah! Hii ni zawadi kutoka kwa binti yako na unaweza kuitumia upendavyo." Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliposikia haya, uso wake ulichangamka kwa furaha na akasema: Ewe binti! Baba yako atolewe kafara kwa ajili yako."[120]

## GAUNI LA KUVAA USIKU WA HARUSI

Ilikuwa ni usiku wa harusi ya Bibi Zahra. Nguo moja tu ilinunuliwa kwa ajili ya kuvaa yeye usiku wa harusi. Hakuwa na nguo nyingine mpya zaidi ya hiyo.

Katika usiku wa harusi, muombaji alifika nyumbani kwake na akasema kwa sauti kubwa, "mimi hapa sina nguo. Kuna mtu yeyote anaweza kunipa nguo?" Hakuna mtu aliyeonekana kumsikiliza mtu huyo mwombaji. Hata hivyo, akiwa ameketi kitandani pake, Bibi Zahra aliona kwamba hakuna mtu aliyeonekana kumsikiliza mwombaji huyo, alisimama na akaenda sehemu ya faragha, akavua ile nguo ya harusi na akavaa nguo zingine za zamani. Halafu akampa yule mwombaji nguo yake ya usiku wa harusi. Wageni walipowasili na kuulizia kuhusu nguo yake mpya, Bibi Zahra alijibu kwamba alikwisha toa nguo hiyo sadaka katika njia ya Allah.[121] Fikiria kuhusu ukubwa na umuhimu wa kitendo hiki kwa mtazamo wa Bibi Zahra? Hiyo nguo mpya ilikuwa nini kwake? Kitu gani kilionekana kumpendeza zaidi kuliko ibada?

---

[119] Ni kwamba hicho kilikuwa kipindi cha ufukara uliopindukia.

[120] *Biharul Anwar*, Juz. 43, uk. 83

[121] *Nuzhatul Majalis*, Juz. 3, uk. 235

## SASA BASI, KWA NINI FATIMA ALIKWENDA KUDAI FADAK?

Kama Bibi Zahra alikwenda kudai Fadak kwenye mahakama ya ukhalifa ilikuwa hivyo kwa sababu katika Uislamu ni wajibu mtu kutetea haki yake. Vinginevyo, Fadak ilikuwa na thamani gani kwake? Hata hivyo, kama asingedai haki yake kuhusu Fadak ingekuwa ni dhulma juu yake mwenyewe. Angeweza kujitolea Fadak elfu moja kwa njia ya Allah lakini alikwenda kutafuta haki yake kwa ajili ya kutojidhulumu mwenyewe. Yaani ni kwamba, Bibi Zahra alichukulia kwamba Fadak ilikuwa muhimu kwa sababu ilikuwa ni haki yake na si kwa sababu ilikuwa kitu cha maana na rasilimali. Umuhimu wa Fadak kama mali ulikuwa ni kwamba angeweza kuwasaidia watu mafukara kutokana na mapato yake.

## NYAKATI ZA MWISHO ZA BIBI FATIMA

Ndiyo, hali ya Bibi Zahra katika usiku wa harusi yake ilikuwa kama ambavyo nimesimulia hivi punde. Hata hivyo, wakati wa kifo chake, hususani hasa alivaa nguo iliyo safi ili kwamba avute pumzi yake ya mwisho akiwa amevaa nguo hizi tu. Asma binti Umais anasema:

"Siku moja (zipo hadithi mbili kuhusu kifo cha Bibi Zahra. Kufuatana na hadithi moja, Bibi Zahra alifariki dunia siku 75 baada ya kifo cha Mtume na kufuatana na hadithi nyingine, alifariki baada ya siku 90 baada ya kifo cha Mtume) niliona hali ya Bibi Zahra ilikuwa nzuri tu kwa sababu alinyanyuka kutoka pale alipokuwa na halafu akaketi tena. Halafu akanyanyuka tena na akaenda kuoga josho kubwa (*Ghusl*) na akasema: 'Ewe Asma! Tafadhali niletee ile nguo yangu ya hivi na hivi"[122]

Asma anasema kwamba alifurahi alipoona yote hayo lakini maneno yaliyotamkwa na Bibi Zahra baadaye yaligueza furaha yake yote na kuwa huzu-

[122] Bibi Asma binti Umais hakuwa mtumishi. Alikuwa wifi yake Bibi Zahra yaani mke wa Mtukufu, Ja'far Tayyar. Baada ya kifo chake cha kishahidi, aliolewa na Abu Bakr na walimzaa mtu mwaminifu Muhammad bin Abu Bakr. Baada ya Abu Bakr, Imam Ali alimuoa Asma. Kwa hiyo, Muhammad bin Abu Bakr pia alijulikana kama mtoto wa Imam Ali (a.s.). Alilelewa na Imam Ali (a.s.). Kwa hiyo, alimpenda sana Imam Ali (a.s.) na hakujihusisha na lolote kuhusu baba yake. Lengo la kusimulia haya ni kuweka wazi kwamba Asma binti Umais alikuwa mwanamke mwenye hadhi ya juu. Alipoolewa na Abu Bakr, yeye alikuwa na imani juu ya ukhalifa wa Imam Ali (a.s.) tu. Alikuwa miongoni mwa wale waliokuwa wakimuunga mkono Imam Ali (a.s.) na aliipenda sana familia ya Imam na alikuwa na imani juu yao. Asma hakuipenda familia ya Abu Bakr kabisa. (Ustaadh Mutahhari).

ni. Bibi Zahra alisema: “Ewe Asma! Ninalala kuelekea Qibla. Usinisemeshe kwa muda kiasi fulani. Baada ya muda kidogo kupita uniite. Kama sitajibu; ujue kwamba dakika zangu za mwisho wa uhai wangu zimewadia.”

Baada ya hayo, matarajio yote ya Asma yalivurugika. Haukupita muda mrefu ambapo Asma alianza kulia kwa sauti kubwa na alitoka nje kumtafuta Ali. Alifika msikitini na akamuita Imam Ali (a.s.) na Imam Hasan (a.s.) na Imam Husain (a.s.) pia walifika.[123]

[123] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 270; *Biharul Anwar*, Juz. 43, uk. 186

# MAJILISI 15

## KUTUPIA MACHO HARAKA TABIA YA IMAM HASAN

Kwa kuwa leo ni siku ya kifo cha kishahidi cha Imam Hasan, ningependa kuzungumza kidogo kuhusu tabia yake. Imesimuliwa kwamba mara mbili[124] katika kipindi cha uhai wake, Imam Hasan (a.s.) aligawa mali yake yote katika sehemu mbili. Sehemu moja alibaki nayo na sehemu nyingine aligawa kwa watu fukara na njia zingine za misaada.[125]

Imam Hasan (a.s.) alikwenda Makkah Kuhiji kutokea Madina mara kadhaa kwa miguu. Hata kama alikuwa na kipando lakini hakukitumia. Alikuwa akichukulia kuwa kutembea kwa mguu ni toba na ni kitendo cha ibada kwake binafsi. Cheo cha Imam ni kikubwa sana hivyo kwamba hakuna haja ya kutaja sifa hizi. Hata hivyo, hapana shaka kwamba thawabu za kwenda Kuhiji ukiwa na mahitaji yote sio kubwa kama zile za kwenda Kuhiji kwa kutembea kwa mguu hata kwa mtu wa kawaida.

### UKATILI JUU YA IMAM HASAN (A.S.)

Imam Hasan Mujtaba (a.s.) alikuwa mtu wa ibada sana lakini maadui zake walimshutumu kupita kiasi, wakiwa ni Bani Umayyah na Bani Abbas ambao walikuwa wabaya zaidi. Wakati wa utawala wa kidhalimu wa Bani Abbas, Masayyid wa Imam Hasan (a.s.) waliasisi harakati kadhaa dhidi ya Bani Abbas. Hatimaye, watawala wa Bani Abbas na mawaziri wengine walianzisha propaganda kwa lengo la kuwazima Masayyid wa familia ya Imam Hasan (a.s.) kwa kumbambikiza shutuma za uwongo mhenga wao mtukufu (Imam Hasan). Walidai kwamba alioa mara kadhaa na alikuwa akifuja mali. Bani Abbas nao pia walimbambikiza shutuma za uwongo hivyo hivyo kwa

[124] Imeandikwa kwenye historia kwamba Imam Hasan Mujtaba (a.s.) alikwenda Makkah kuhiji akitembea kwa mguu mara ishirini. (umbali wa kutoka Madina hadi Makkah ni takriban km 435 - mfasiri). Alitoa mali yake yote sadaka mara mbili na alitoa nusu ya mali yake sadaka mara tatu. *Biharul Anwar*, Juz. 43, uk. 339 na 349

[125] *Biharul Anwar*, Juz. 43, uk. 331,358.

kuhusika na madhara mengine kama hayo. Hata hivyo, Imam Hasan (a.s.) alikuwa mcha Mungu mkubwa kabisa wa wakati wa uhai wake.

Kila wakati Imam Hasan Mujtaba (a.s.) alipokuwa anaswali machozi yalikuwa yakitiririka kutoka kwenye macho yake. Alipokuwa anasoma Qur`ani tukufu na akakutana na aya inayozungumzia adhabu za kimungu, alikuwa na tabia ya kuanguka chini na kuzimia.[126] Kwa kweli, alikuwa ni nakala halisi ya tabia ya baba yake Imam Ali (a.s.) al-Murtaza

Enyi waombolezaji wa Imam Hasan (a.s.)!

Lolote mlilolisikia kuhusu Amiri wa Waumini, ndivyo ilivyo kwa Imam Hasan (a.s.) bila ya kuongeza chumvi.

## UKATILI NA UHALIFU WA MUAWIYAH

Hadithi ya ukatili aliofanyiwa Imam Hasan (a.s.) wakati wa uhai wake na propaganda dhidi yake baada ya kifo chake cha kishahidi ni ndefu na ya kusikitisha.

Imam Hasan (a.s.) aliishi kwa kipindi cha takriban miaka kumi baada ya kifo cha mtukufu baba yake. Amiri wa Waumini aliuawa kishahidi mwaka wa 40 A.H. na Imam Hasan (a.s.) aliuawa kishahidi mwaka wa 49 A.H. Miaka hii tisa au kumi ilikuwa miaka ya uovu mkubwa wa utawala wa Muawiyah uliojaa kisirani. Imam Hasan (a.s.) alikandamizwa sana katika kipindi hiki. Muawiyah hakupoteza hata dakika moja katika harakati zake za kueneza propaganda za uwongo dhidi ya Imam Hasan (a.s.) kwa lengo la kumfedhehesha.

Mwanzoni mwa kipindi cha ukhalifa wa Bani Umayyah, picha halisi ya Muawiyah na Bani Umayyah ilikuwa haijadhihiri kwa umma. Hata hivyo, pazia lililofunika uovu wa Bani Umayyah liliondolewa mnamo siku za mwisho za utawala wa Muawiyah na kuanza kwa utawala wa Yazid na msimamo yao ilijulikana wazi. Mwanzoni, watu walidhani kwamba Muawiyah alikuwa 'mtu mwenye busara.'

Muawiyah alitaka mwanae amrithi katika nafasi ya ukhalifa. Kwa hiyo alianza kuondoa vipingamizi vyote kimoja baada kingine wakati wa uhai wake mwenyewe. Jambo hili halikulengwa kuishia kwa Imam Hasan (a.s.)

[126] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 422; *Biharul Anwar*, Juz. 43, uk.331.

peke yake. Kwa mujibu wa Muawiyah walikuwepo watu wengine ambao pia wangeweza kugombea ukhalifa. Wangeweza kuchaguliwa kushika nafasi ya ukhalifa. Kwa hiyo, aliendelea kuwaondoa kwa lengo la kumfagilia njia mwanae. Sa'd bin Abi Waqqas, baba yake na Umar bin Sa'd aliuawa na Muawiyah kwa kutumia sumu kwa sababu Sa'd alikuwa mmojawapo wa wale watu sita ambao Umar aliwateuwa kuwa katika kamati ya Shura. Kwa hiyo, ilikuwa ni kawaida kuwa mashuhuri miongoni mwa watu kwamba Sa'd anastahili kuwa khalifa.[127]

Hali kadhalika, Abdur Rahman, mtoto wa Khalid bin Walid pia aliuawa na Muawiyah kwa kutumia sumu kwa sababu baba yake alikuwa mtemi maarufu na angeweza kutangaza uongozi wake. Pia Muawiyah aliwaondoa baadhi ya watu wa Bani Umayyah kwenye njia yake, ambao alihofia kama wenye tamaa ya ukhalifa kwa hiyo kuwa kipingamizi.

## AMRI YA KUMLAANI IMAM ALI (A.S.) MBELE YA IMAM HASAN (A.S.)

Watu hawa waliondoshwa ili wasijekuwa wagombea wa ukhalifa. Hata hivyo, nia yake ilikuwa tofauti kuhusu Imam Hasan (a.s.). Alitaka kwamba yale mapenzi na imani ya watu juu ya Imam Hasan (a.s.) yatoweke kwenye nyoyo zao. Ingawaje alikuwa anatambua kwamba watu walikuwa na imani na Ahlul-Bayt, alitaka kumtesa Imam Hasan (a.s.) kiakili wakati akiwa hai. Kwa hiyo, alimwandikia barua gavana wa Madina na kumuagiza kumlaani baba yake, Imam Ali (a.s.) mbele yake kila Ijumaa, ndani ya msikiti wa Mtume.[128]

Tunasoma aya katika swala ya Ijumaa kwamba unapowadia muda wa swala ya Ijumaa, ni wajibu wa kila mtu kujiunga nayo. (Hivyo, Muawiyah na wafuasi wake walikuwa wanawalazimisha watu kuhudhuria swala hiyo kwa kunukuu ulazima wa aya hii). Mtu yeyote aliyepinga swala ya Ijumaa kwa kisingizio kwamba waongozaji wa swala hiyo walikuwa hawastahiki kuongoza swala ya Ijumaa, alishutumiwa kwa kuitwa kafiri. Wakati wowote kundi la wafuasi wa Muawiyah (lenye siasa kali) lilipomuona mtu kama

[127] *Mu'jam Rijalul Hadith*, Juz. 8, uk. 53; *Tanqihul Maqal,* Juz. 2, uk. 12
[128] *Sharh Nahjul Balaghah*, Ibn Abil Hadid, Juz. 4, uk. 56

huyo, walikuwa wakimuua. Kwa hiyo, Imam Hasan (a.s.) alikuwa akilazimishwa kuhudhuria Swala hiyo katika hali kama hiyo. Tayari nimekwisha kuzungumzia kuhusu wajibu wa Imam wa kuongoza swala kusimama kwenye mimbari karibu na kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye hotuba ya swala ya Ijumaa kwenye mhadhara wangu juu ya 'hotuba na mimbari.'[129] Wajibu huu ulibadilishwa kwa kumlaani Imam Ali (a.s.).[130] Hatimaye, Muawiyah aliamua kumuua mtoto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Imam Hasan (a.s.) na kwa sababu ya uamuzi huu, alitumia sumu kumuua Imam.

Imam hakulishwa sumu mara moja tu lakini alifanyiwa hivyo mara mbili au mara tatu.[131]

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**"Na punde watajua waliodhulumu ni mgeuko gani watakao geuka?"**
**[Sura Ash-Shu'araa 26 : 227]**

---

[129] Hotuba zote zipo kwenye *Sukhan* ya Ustaadh Mutahhari iliyochapishwa na Jame Taalimaat-e-Islami.
[130] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 450; *Al-Ghadiir*, Juz. 10, uk. 257
[131] Baada ya hili, sehemu fulani ya hotuba hii haikurekodiwa; *Ashnai ba Qur`ani*, Juz. 7, uk. 118, 120

# MAJILISI 16

## NDOTO YA SHAHIDI MUTAHHARI WAKATI WA KUWASILI KWA MUHARRAM

Enyi waombolezaji wa aliyedhulumiwa Karbala!

Siku hizi, sisi sote tunajiandaa kukaribisha Muharram. Husainiyyah zinapambwa kwa ajili ya kuadhimisha kumbukumbu ya huzuni ya kuondokewa na kipenzi cha macho ya Fatima. Ni sadifa ya ajabu, mwaka 1962, alipofariki dunia Aqa Burujardi, nilimuona kwenye ndoto yangu (Aqa Burujardi alifariki dunia mwezi wa Shawwal) lakini hali ya ndoto hiyo ilikuwa ya aina ambayo hata mimi nilishindwa kuitafsiri.

### "USIONDOKE KWENYE MIMBARI"

Siku hizo, Haji Ahmad Qummi alikuwa mashuhuri kwa kutoa tafsiri za kushangaza za ndoto. Wakati mwingine, hata Ayatullah Burujardi alikwenda kwake ili amtafsirie ndoto zake. Hivyo, nilimpigia simu na kumuomba anitafsirie ndoto yangu. Ni kweli kwamba hata mimi sikuweza kuelewa ni kitu gani kilikuwa maalum sana kwenye ndoto ile, ambacho kilinifanya nitafute tafsiri kutoka kwa mheshimiwa Qummi kwa kumpigia simu.(Siku hizo, nilisha acha kuhubiri kutoka kwenye mimbari. Aliniambia nisiondoke kwenye mimbari kabisa. Sijui aliitoa wapi tafsiri hii. Aliniambia nisiache huduma ya Imam Husain (a.s.). Nilifanya kama nilivyoambiwa na nilijaribu kutekeleza kwa vitendo kama nilivyoshauriwa kwenye tafsiri hiyo.

### HUDUMA YA MKUU WA MASHAHIDI

Kama ilivyo kawaida, jana yake nililala kwa muda mfupi baada ya swala ya Alfajiri. Katika ndoto niliona mkusanyiko mkubwa wa Majilisi, iliyohudhuriwa na wanazuoni ambao wote walikuwa wanangojea kuwasili kwa Aqa Burujardi. Baada ya muda kidogo, mgeni rasmi aliwasili. Watu wote waliokusanyika walisimama kumkaribisha kama ilivyokuwa ikifanyika wakati wa uhai wake. Nilipojaribu kunyanyuka ghafla joho langu lilijizonga kwenye mkono na mguuni mwangu. Nilijisogeza pembeni, nikarekebisha nguo zan-

gu na nikasimama. Wakati huo huo Aqa alifika pale nilipokuwa nimeketi. Haraka sana niliondoka hapo kama vile nilijua kwamba alikuwa anataka kuketi hapo. Halafu nikaona anakwenda kuketi kwenye kiti na ilionyesha kama vile hakutaka kuhadhiri na badala yake angekuwa anasoma majilisi. Mara tu alipoketi kwenye mimbari, akasema:

"Sisi wasomaji wa Majilisi (*Dhakireen*)!" Nilishangazwa sana katika ndoto yangu baada ya kusikia kauli hii. Nilifikiri: Kwa nini Aqa Burujardi alijiita msomaji wa Majilisi? (Ingawaje ninajua kwamba kuna wakati alikuwa akisoma Majilisi kwenye jiji la Burujard wakati wa mwezi wa Ramadhani alipokuwa mwanasheria mkuu. Hata hivyo, alikuwa mwanasheria mkuu na si mhadhiri).

Halafu nikaona kashida nyeupe kichwani mwake na nikazidi kushangaa kwa sababu kwa kawaida matukio hubadilika kwenye ndoto. Nilimuona ameketi kwenye mimbari kwenye jiji lingine lakini akiwa kama mwanasheria. Halafu nikamuona kwenye bustani iliyojaa mandhari ya kijani. Ghafla nikamuona ameketi karibu na maji yaliyokuwa yanatiririka kama vile alitaka kuchukua wudhu. Nilikumbuka kwenye ndoto yangu kwamba siku za nyuma nilikuwa mwanafunzi wake. Kwa hiyo, nilisogea mbele ili nibusu mikono yake. Nilipofika pale alipokuwa, niliona nusu ya uso wake umezama kwenye maji safi na yaliyotakasika na nusu ya uso ilikuwa nje. Alikuwa amefumba macho kama sufi aliyeko katika tafakuri. Ghafla alianza kulia kwa sauti kubwa kwa kasi ya mapigo ya moyo. Alitamka jina la mkuu wa mashahidi kwa sauti kubwa na kusema: 'Ewe Husain! Ewe Husain bin Ali! Ewe mwana wa Zahra.' Alikuwa akitaja jina lake kwa kupaza sauti na halafu akilia. Alikuwa akisimulia mabalaa ya Imam mwenyewe huku akilia. Na ni kulia kwa aina gani huko! Uliaji huu ulikuwa si wa namna kwamba athari yake ingeonekana dhahiri kutoka kwenye machozi yake. Badala yake alikuwa akilia bila kujali dunia iliyomzunguka. Alizama kwenye huzuni ya Imam Husain (a.s.) sana hivyo kwamba alikuwa mbali na dunia. Baada ya hapo niliamka kutoka usingizini. Nilikumbuka kwamba nilikuwa nimeona ndoto siku mbili au tatu kabla ya mwezi wa Muharram miaka michache iliyopita. Safari hii pia niliona ndoto kabla ya kuwadia kwa Muharram.[132]

Hakuna nguvu na uwezo isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu, Mkuu, Mwenye nguvu.

[132] Baada ya hili, sehemu ya hotuba haikurekodiwa; *Ashnai ba Qur`ani*, Juz. 6, uk. 259-261.

# MAJILISI 17

Msiba wa Ashura unaamsha sana hisia za huzuni na hali ya uaminifu kiasi kwamba kama tungekuwa na mshipa wa imani kwenye mioyo yetu, basi macho yetu yangefurika machozi tunaposikia jina la Husain aliyedhulumiwa. “Kwa hakika, mapenzi juu ya Imam Husain (a.s.) yamejificha ndani ya mioyo ya waumini.”[133]

(Labda huenda ndio maana Imam Husain alisema: “Mimi ni shahidi ambaye ataombolezwa.”)[134]

## IMAM SADIQ AOMBOLEZA KIFO CHA HUSAIN (A.S.)

Wakati wa siku za uwanafunzi wangu katika jiji la Mash'had, nilikuwa nimekariri shairi la mistari mitano la kuhuzunisha lililoandikwa na sahaba wa Imam Ja`far Sadiq (a.s.) kutoka kwenye *'Nafthat al-Masdur'* ya Shaykh Abbas Qummi.

Muhadithi Qummi anaandika kwamba Abu Haruun Makfuf ambaye alikaribia kuwa kipofu na kwa hiyo akapewa jina la '*Makfuf*' alikuwa mshairi mwenye uwezo wa kusoma shairi bila kujiandaa na alisoma beti za maombolezo ya Imam Husain (a.s.). Alikuwa akisema: “Siku moja nilikwenda kwa Imam Ja`far as-Sadiq (a.s.). Aliniomba nisome shairi dogo sana la maombolezo nililotunga kuhusu babu yake. Nikasema: Kama utakavyo. Imam Ja`far Sadiq (a.s.) aliwaambia wanawake wa nyumba yake wakusanyike nyuma ya pazia ili na wao waweze kusikia shairi hilo la maombolezo. Hatimaye, wanawake wote walikusanyika nyuma ya pazia.”

Makfuf alianza kusoma shairi hilo la maombolezo. Pia unaweza kujaribu kuelewa maana ya beti hizo na kupata somo kutoka humo. Hata hivyo shairi hilo lilikuwa na beti tano tu, kila mtu aliyekuwemo ndani ya nyumba ya Imam Ja`far Sadiq (a.s.) alikuwa analia kwa huzuni kwa sauti ya kupaza. Imam mwenyewe alikuwa analia kwa namna ambayo matone ya machozi yalikuwa yanadondoka kutoka kwenye macho yake na mabega yake yalikuwa yanatikisika. Sauti za kulia na kuomboleza zikawa kubwa sana ndani

[133] *Khasais al-Husainia*, uk. 48

[134] *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 649; *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 279

ya nyumba yake tukufu hivyo kwamba hatimaye Imam akasema basi imetosha.

Sikuweza kuona shairi la maombolezo linalolingana na hili. Abu Haruun Makfuf alisema:

## "EWE WIMBI LA UPEPO WA MAOMBOLEZO!

Unapopita Karbala, utufikishie ujumbe na salam zetu, na uiambie mifupa iliyotakaswa ya mwili wake safi kwamba mifupa hiyo itakuwa inamwagiliwa kwa machozi ya waombolezaji wa Husain mfululizo. Wataendelea kutoa machozi ili kuweza kuzima kiu yako. Siku moja ulinyimwa maji na Mawla Husain aliuawa kishahidi akiwa na kiu. Hata hivyo, sasa Shi'ah (wafuasi) wake wakati wote watajitolea machozi juu yake."

"Ewe upepo mwanana wa asubuhi!

"Unapopita karibu na kaburi la Husain, usiseme haya tu. Ngoja hapo kwa kitambo kiasi na ulie zaidi juu ya mateso yake. Kulia kwako kusiwe kama kwa mtu wa kawaida. Lia kama mama ambaye mwana wake wa pekee amefariki. Ndiyo, lia kama mama aliyehuzunishwa kwa kutenganishwa na mwanae wa pekee, kwani Imam Husain (a.s.) alikuwa safi na mama yake na baba yake wote walikuwa safi pia."[135]

Kwa Jina la Allah na kwa ajili ya Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.).

[135] *Nafthatul Masdur*, uk. 254; *Aghani*, Juz. 7, uk. 260; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 541; *Seeri dar Seerah-e-Nabawi*, uk. 172-175

# MAJILISI 18

## HOTUBA YA IMAM HUSAIN (A.S.) BAADA YA KUJITAYARISHA KWENDA KARBALA

Imam Husain (a.s.) alikuwa kama mtukufu baba yake katika nyanja zote. Katika ufasaha wa kuongea pia alikuwa kama baba yake ingawa yeye hakupata fursa ya kutosha kama alivyopata Imam Ali (a.s.) wakati wa kipindi chake dhahiri cha ukhalifa. Fursa ndogo aliyopata Imam Husain (a.s.) ni wakati alipokuwa njiani kutoka Makkah kwenda Karbala. Hapo ndipo johari za ufasaha wa kuongea ulijitokeza dhahiri katika siku nane za mwisho hapo Karbala. Hotuba nyingi za Imam Husain (a.s.) zilizopo ni zile alizotoa katika kipindi hiki. Mtindo wa kuongea wa Imam Husain (a.s.) ulifanana na ule wa baba yake na bahari ya dhati na hekima inaonekana ikibubujika kutoka kwenye hotuba hizo.

Imam Ali (a.s.) alikuwa amesema kwamba ulimi ni njia ya kujieleza kwa nafsi. Kama johari za hekima hazitoki kwenye ulimi, basi ulimi una kazi gani hasa? Na kama hekima imo ndani ya nafsi, ulimi hauwezi kuzuia kujitokeza kwake. Imam (a.s.) alisema: "Sisi Ahlul-Bayt ni mabingwa stadi wa ufasaha wa kuongea. Sisi ni watawala wa fani wa nchi ya uongeaji. Mizizi ya ufasaha imechimbiwa katika uwepo wetu na matawi yake hugawa vivuli kwetu sisi tu."[136]

Hotuba ya kwanza ya Imam Husain (a.s.) wakati anaondoka kutoka Makkah kwenda Karbala imejaa utukufu na ufasaha. Ndani ya hotuba hiyo kuna muongozo, ujasiri na umakini na imani katika kisichoonekana (*Ghaib*). Baada ya kutangaza uamuzi wa kusafiri kwenda Karbala, Imam (a.s.) aliwaambia watu kwamba yeyote ambaye alikuwa anaunga mkono fikira zake angeweza kuungana naye. Imam (a.s.) alisema:

"Kifo kimeacha alama juu ya uzao wa Adam kama vile alama inayowekwa kwenye shingo ya mwanamke kwa sababu ya kuvaa kidani. Kifo katika njia ya haki ni jambo la kujivunia. Ninayo shauku ya kukutana na wahenga

[136] *Nahjul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 224, uk. 72; *Nahjul Balaghah*, Subhi Salih, Hotuba ya 233

wangu kama vile Yakuub alivyokuwa na shauku ya kukutana na Yusuf." Imam (a.s.) aliendelea kusema:

"Yeyote anayetaka kukutana na Mwenyezi Mungu baada ya kuuawa kishahidi katika njia yetu awe tayari kufuatana na sisi. Tutaondoka hapa kesho asubuhi, Inshallah."[137]

Imam anasema: "Enyi watu! Yeyote miongoni mwenu ambaye anatamani kutoa kitu kidogo katika njia iliyo sahihi anapaswa kufikiria ni kitu gani cha kutoa. Njooni, ngojeni niwaonyeshe hilo ili kukomesha khofu iliyojificha ndani yenu, lazima ununue mshale ili uweze kuondoka kwenda kukutana na Mola Wako. Inshallah, pia mimi kesho asubuhi nitaondoka nikiwa na nia hiyo. Mwenyezi Mungu akipenda."

[137] *Luhuuf*, uk. 60; *Biharul Anwar*, Jz. 44, uk. 366; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 328

# MAJILISI 19

## KIFO CHA KISHAHIDI CHA MUSLIM BIN AQIIL

Mahujaji walikwishaingia Makkah mnamo tarehe 8, mwezi wa Dhilhajj wakiwa na shauku kamili na hamu. Mnamo siku hiyo hiyo mahujaji walipotarajiwa kuondoka kwenda Mina na Arafat, Imam Husain (a.s.) alikuwa anaondoka Makkah. Wakati huo alitoa hotuba maarufu sana, ambayo imesimuliwa na Sayyid bin Tawuus. Halafu Imam alipita kila hatua ya safari hadi alipofika karibu na mpaka wa Iraq. Hali ya mambo ilikuwaje huko Kufa? Kitu gani kilikuwa kinaendelea huko? Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anayejua vyema zaidi.

Wakati akiwa njiani Imam Husain (a.s.) alimuona mtu aliyekuwa anakuja kutokea Kufa na alikuwa anaelekea upande wa Imam. (Arabuni hapakuwepo na njia ya kuelekea upande moja tu, hivyo kwamba watu wanaokwenda pande zote mbili waliweza kupishana wakiwa karibu. Ilikuwa ni jangwa, na mtu anayetokea upande wa pili alikuwa anampisha mtu anayekwenda njia hiyo kwa mbali). Hatimaye, Imam alingoja kwa muda fulani. Alitaka kumpa ishara mtu anayetokea upande wa pili asimame ili aweze kuongea naye. Inasimuliwa kwamba mtu huyo naye pia alikuwa anamfahamu Imam Husain (a.s.) na alikuwa na taarifa mbaya kuhusu yeye. Mtu yule alifikiri kwamba kama angekutana na Imam Husain (a.s.) angemuuliza kuhusu habari za Kufa naye angepaswa kumweleza kuhusu habari hizo mbaya za Kufa. Mtu huyo hakutaka kumpa Imam habari mbaya za Kufa, kwa hiyo alibadili njia na kuelekea upande mwingine.

Kwa upande mwingine, watu wawili kutoka kabila la Bani Asad waliokuwepo Makkah kwa ajili ya Hijja; walikuwa na nia ya kumsaidia Imam. Hivyo, walimaliza taratibu za ibada ya Hijja na wakaondoka kwa mwendo wa kasi ili wamkute Imam (a.s.) humo njiani. Walipofika kituo kimoja kabla ya kituo alipokuwa Imam, walikutana na yule mtu aliyekuwa anatokea Kufa. Walis-

alimiana naye na kama ilivyokuwa desturi za Waarabu, walimuuliza yeye alikuwa wa kabila gani. Alijibu kwamba alikuwa wa kabila la Bani Asad. Walishangaa na wakasema na wao ni wa kabila la Bani Asad. Walimuuliza kuhusu baba yake na babu yake na mtu huyo alijibu maswali hadi wakafahamiana. Baada ya hapo wote walimuuliza yule mtu kuhusu habari za Kufa. Alijibu kwamba palikuwepo na habari za kuhuzunisha huko Kufa. Akasema, "Imam Husain (a.s.) anakwenda Karbala kutoka Makkah na aliniona mimi na akanisimamisha. Nilijua kwamba Imam angeniuliza habari za Kufa na sikutaka kumpa habari hizi mbaya. Kwa hiyo nilibadili njia yangu.." Halafu akawaeleza kila kitu kwa undani.

Watu hawa wawili waliendelea na safari yao kwa mwendo wa kasi zaidi hadi wakamkuta Imam katika kituo kilichofuata lakini hawakusema kitu chochote naye. Walingoja Imam asimame kwenye kituo kilichofuata. Baada ya kupishana na yule mtu aliyetoka Kufa, msafara wa Imam ulikuwa umekwishasafiri kwa muda wa siku moja na usiku mmoja kabla ya kufika kwenye kituo hicho. Imam (a.s.) alikuwa kwenye hema lake wakiwemo na baadhi ya masahaba wake. Watu hao wawili walimwendea Imam na wakasema kwa heshima kabisa:

"Ewe Aba Abdillah! Tunazo habari zinazokuhusu wewe. Unataka tukuambie mbele ya kila mtu au katika faragha?"

Imam akajibu: "Mimi huwa sifichi kitu kwa masahaba wangu. Semeni chochote kile mnachotaka kusema mbele ya kila mtu." Waliposikia hivi, wakasema:

"Ewe mwana wa Mjumbe wa Allah! Tulikutana na yule mtu ambaye wewe ulimsimamisha jana na hakukutana na wewe. Ni mtu wa kuaminika. Sisi tunamjua. Anatoka katika kabila letu tu. Tulipomuuliza kuhusu Kufa, alisema kwamba alipoondoka Kufa, Muslim bin Aqiil na Hani bin Urwah walikuwa wameuawa kishahidi. Miili yao ilifungwa kamba na kuburuzwa kwenye mitaa ya Kufa."

Imam Husain (a.s.) alipopata taarifa hiyo ya kusikitisha ya kuuawa kishahidi Muslim bin Aqiil, machozi yalianza kutoka machoni mwake lakini hakukawia kusoma aya ifuatayo:

مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ ۖ فَمِنْهُم مَّن قَضَىٰ نَحْبَهُ وَمِنْهُم مَّن يَنتَظِرُ ۖ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا

**"Miongoni mwa waumini wapo wanaume waliotimiza waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea; wala hawakubadilisha ahadi yao hata kidogo."** **[Sura Al-Ahzab 33 : 23]**

Katika tukio hili Imam Husain (a.s.) hakusema kwamba Muslim bin Aqiil na Hani bin Urwah wameuawa kishahidi na Kufa imetekwa na maadui. Tumeshindwa vita kwa hiyo ni vema turudie hapa hapa. Badala yake Imam alisema kitu, ambacho kilielekea kwenye lengo tofauti. Aya iliyotajwa hapo juu kwa dhahiri inahusiana na vita vya Ahzab, ambapo baadhi ya waumini walitimiza ahadi yao waliyowekeana na Allah na waliyatoa maisha yao katika njia iliyonyooka ambapo wengine walikuwa wanangojea zamu yao ya kujitoa mhanga. Imam Husain (a.s.) alisoma aya hii na akasema: "Muslim ametimiza wajibu wake na sasa ni zamu yetu."[138] Sasa lazima na sisi tutimize wajibu wetu. Hapa, kila sahaba alitoa maoni yake, ambayo yalionyesha hisia zao za ndani kabisa. Baadhi ya watu waliokutana na Imam (a.s.) njiani hawakuwa na kiwango cha utambuzi kama kilivyotakiwa na Imam Husain (a.s.). Hivyo, Imam alifadhaika na alijitenga nao. Walipotambua kwamba hawangepata kila kitu bila wao kushughulika baada ya kufika Kufa, walimwacha Imam, kama inavyotokea kwenye vita nyingi. Waliobaki na Imam ni Ahlul-Bayt na masahaba mahsusi na walikuwa wachache sana (Wale waliomwacha Imam walipoamka kutoka kwenye usingizi wao wa ujinga, waliondoka kwenye jeshi la Umar bin Saad na kujiunga na Imam Husain mmoja baada ya mwingine).

Wakati Imam Husain (a.s.) alipopata habari ya kifo cha kishahidi cha Muslim, masahaba wake hawakufika hata ishirini. Unaweza kukisia Imam Hu-

[138] Chochote kile kinachosimuliwa kuhusu Imam Husain (a.s.) katika historia ni maana ya aya ya 23 ya Surah Ahzab na si aya yenyewe. Imeandikwa kwamba hata pale Imam Husain (a.s.) alipoambiwa kuhusu kifo cha kishahidi cha Muslim alirudia **'innaa lillahi..'** mara chache. Baadhi ya wasimulizi wameandika kwamba Imam alisema: Allah na ampe wokovu Muslim ambaye alikwenda karibu na Mwenyezi Mungu, Pepo na Ridhwan. Ametimiza wajibu wake ambapo sisi bado hatujafanya hivyo."

*Biharul Anwar,* Juzuu. 44,Uk. 374; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain,* Uk. 349

Imesimuliwa pia kwamba Imam Husain (a.s.) alikariri aya ya 23 ya Surah Ahzab baada ya kupata habari ya kifo cha kishahidi cha Qais bin Musahhar Saidawi; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 363

sain (a.s.) na masahaba wake watiifu wangehisi vipi baada ya kusikia habari ya kifo cha kishahidi cha Muslim bin Aqiil na Hani bin Urwah. Mwandishi wa *Lisanul Ghaib* anasema kwamba baadhi ya waandishi wa historia wameandika kwamba kwa kuwa Imam Husain (a.s.) hakuwa akiwaficha kitu chochote masahaba wake, kwa hiyo, baada ya kupata habari ya kifo cha kishahidi cha Muslim, ikamlazimu aende kwenye nyumba ya wanawake ili awape habari hizo licha ya kuwepo kwa binamu yake wa kike na ndugu wengine kwa nyongeza ya ndugu zake wengine wadogo. Mungu anajua jinsi gani Imam aliyekuwa madhlumu alivyowasilisha kwao habari hiyo ya kuogofya!

## BINTI YAKE MUSLIM APEWA TAARIFA ZA SHAHADA YA MUSLIM

Mtukufu Imam (a.s.) aliingia kwenye hema na alipoketi alimuita mtoto wa kike mdogo wa Muslim. Binti huyo alipofika, Imam alimkalisha kwenye mapaja yake na akawa anapitisha mkono wake kichwani mwa binti kwa upendo mwingi. Binti huyu mdogo wa familia ya utume alikuwa na akili sana. Yeye alipoona tabia hii ya Imam isiyokuwa ya kawaida, aliuliza kwa hofu kabisa, "Ewe Aba Abdillah! Ewe mwana wa Mjumbe wa Allah! Baba yangu amekufa? Kiasi kwamba unanifariji sana….?"[139]

Imam (a.s.) aliguswa sana katika kusikia haya na akasema: "Binti! Mimi pia ni kama baba yako. Baada ya baba yako, nitakupa upendo kama baba." Baada ya Imam kusema hivi pakatokea zogo kwenye kambi ya Ahlul-Bayt.

## WATOTO WA AQIIL WAAHIDI UTII

Imam Husain (a.s.) alizungumza na watoto wa kiume wa Aqiil na akasema:

"Enyi wana wa Aqiil! Mmetoa mhanga wa Muslim. Muhanga huu unatosha kwa familia yote ya Aqiil. Kama mnataka mnaweza kurudi." Wote walitoa jibu kwa pamoja: "Ewe mwana wa Mjumbe wa Allah! Hatukumtoa Muslim kwa ajili ya kufa kishahidi. Tumeandamana na wewe hadi sasa na sasa basi pia tunataka kulipa kisasi kwa ajili ya Muslim, tunawezaje kukuacha wewe sasa? Haiwezekani kabisa, tutaandamana na wewe ili na sisi pia tukutane na hatima kama alivyofanya Muslim."[140]

---

[139] Baada ya haya, kuna baadhi ya maneno yamekosekana kwenye kanda.

[140] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 222; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 344

# MAJILISI 20

## CHEO CHA MKUU WA MASHAHIDI

Enyi waombolezaji wa Mkuu wa Mashahidi!

Mtukufu, Hamza aliitwa mkuu wa mashahidi kabla ya tukio la Karbala. Hata hivyo, baadaye cheo hiki alitunukiwa Imam Husain (a.s.). Ilikuwa kama vile kifo cha kishahidi cha Imam Husain (a.s.) kilifunika kifo cha kishahidi cha Mtukufu Hamza. Masahaba watiifu wa Imam Husain (a.s.) pia nao walikuwa kwa namna fulani kama hivyo kicheo kwa sababu walipewa umuhimu wa kwanza kuzidi mashahidi wote wa zamani. Imam Husain (a.s.) alisema mwenyewe: “Hakika, sijapata kuona masahaba watiifu na bora zaidi kuliko wangu.” Pia alisema: “Siwajui watu bora kuliko Ahlul-Bayt wangu.”[141] Imam Husain (a.s.) alikuwa huru kutoka upande wa marafiki zake na pia kutoka kwa maadui zake.

Imam mwenyewe alisema: “Tazameni (Enyi masahaba zangu watiifu)! Hawana jambo dhidi ya mtu yeyote isipokuwa mimi. Kwa hiari kabisa mimi ninawaruhusu muondoke kama mnataka.”

Baada ya hapo alisema: “Ondokeni zenu, mkitumia fursa ya giza la usiku.” Aliposema hivi, Mtukufu Imam aliinamisha kichwa chake ili kwamba masahaba wakiangalia, wasione aibu kutazamana ana kwa ana na Imam. Masharti ya masahaba wa Imam Husain (a.s.) hayakuwa kama yale ya masahaba wa Tariq ambao walichoma moto posho zao (na kubakisha posho ya siku moja tu) na meli zao; wala sharti lao halikuwa kama lile la mtu aliyelazimishwa kusimama mlangoni na rafiki yake, Imam Husain (a.s.) aliinamisha kichwa chake ili macho yake yasiwe na athari yenye nguvu mno kwa masahaba wake.[142]

[141] *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 395

[142] Ni dhahiri, maneno ya Ibn Abil Hadid: “Walipendelea kifo zaidi.” Yanafaa kwa masahaba hao. Kufuatana na Imam Ali, “Wenye vipando watashuka kwenye vipando vyao mahali hapa na sehemu hii itakuwa uwanja wa vita wa wale wenye kujitolea.” Wala si mashahidi wa zamani ama wa siku zijazo watakuwa bora kuwazidi hawa; *Biharul Anwar,*Juz. 41, uk. 295

## HADHI YA MASAHABA WA HUSAIN

Kama vile tu ambavyo masahaba wa Imam Husain (a.s.) walivyokuwa bora kuzidi masahaba wa Mtume ambao walipigana vita ya Badr na masahaba wa Imam Ali (a.s.) ambao walipigana katika vita ya Siffiin, kwa njia hiyo hiyo, jeshi la Umar bin Saad lilikuwa na moyo mgumu zaidi na baya zaidi kuliko jeshi la Abu Sufyan hapo Badr na jeshi la Muawiyah hapo Siffiin, kwa sababu jeshi la Umar bin Saad halikuwa linapigana kwa ajili ya 'imani' yao kama watu wa Badr; wala hawakuwa na suala lolote la ubishani kama ilivyokuwa kwa watu wa Siffiin ambao walitaka kulipa kisasi kuhusu kuuawa kwa Uthman. Walikuwa wakifanya jinai hili licha ya upinzani wa mara kwa mara kutoka kwenye dhamira zao. Hali yao ilikuwa kama usemi huu ufuatao: "Nyoyo zao zilimuunga mkono lakini mapanga yao yalikuwa dhidi yake."[143] Ni jambo la kushangaza kiasi gani kwamba jeshi la Umar bin Saad lilikuwa linalia lakini pia wakati huo huo lilimuua mjukuu wa Mtume. Ilikuwa ni kulia na wakati huo huo kupora hereni kutoka kwenye masikio ya watoto wasio na hatia wa Husain. Lilikuwa linakata kichwa cha Husain (a.s.) kwa sime ya ukandamizaji na wakati huo huo lilikuwa linatetemeka.[144]

Kwa Jina la Allah na kwa Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.)

[143] *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain,* uk. 370

[144] *Hamasa-e-Husaini,*Juz. 3, uk. 56-57

# MAJILISI 21

## NI BORA KUTAHINIWA

Kwenye Ziarat ya Imam Husain (a.s.) huwa tunasoma, "Ewe Aba Abdillah! Tunatamani tungekuwa na wewe hapo Karbala kukabiliana na batili na kutoa mhanga maisha yetu kama vile masahaba watiifu wa Imam walivyopata kufuzu kukubwa kupitia kifo cha kishahidi."[145] Sentensi hii imekuwa kitu cha kukariri tu na hatuzingatii maana yake. Tafakari kwa muda kiasi. Hivi madai yetu ni ya kweli? Hivi sisi ni watu wa aina ya kuweza kudai madai kama hayo kweli? (Hapana, hapana kabisa) Wengi wetu ni watu wa kusoma tu maneno ya Ziarat bila kuyapatia uzito.

### MASAHABA WALIO WATIIFU SANA

Imam Husain (a.s.) aliwasifu sana masahaba wake mnamo mkesha wa Ashura kwa kusema: "Sijapata kuona masahaba bora na watiifu kama wangu."

Mwanazuoni wa daraja la juu sana wa Shia wakati fulani alikuwa na mawazo kwamba huenda Imam Husain (a.s.) hakutoa kauli hii. Kwa mujibu wake yeye, masahaba wa Imam Husain hawakufanya tendo lolote la ajabu. Sasa kwa nini Imam aliweza kusema hivyo? Hata hivyo, maadui zake walionyesha ukatili mbaya sana. Imam Husain (a.s.) alikuwa ua la bustani ya utume. Alikuwa Imam wa wakati wake na aliyependwa sana na Ali na Batuul (Fatimah). Kwa hiyo, Mwislamu yeyote ambaye angeona Imam amezungukwa na mabalaa kama yale kwa hakika angejitokeza ili amsaidie. Hivyo, kulingana na mwanazuoni huyo, watu wale ambao hawakumsaidia Imam walikuwa viumbe wabaya kuliko viumbe wote lakini pia wale waliomsaidia Imam hawakufanya jambo lolote la ajabu.

Mwanazuoni huyo mkubwa anasema: Labda Mwenyezi Mungu alitaka mimi niondoke kwenye ujinga. Kwa hiyo, niliuona uwanja wa vita wa Karba-

[145] Kauli hii "*Yaa laitanii kuntu ma`akum fa-afuuza fauzan a`dhiimaa*" imo katika mojawapo ya Ziarat za Imam Husain. Ziarat maalum ya siku ya Arafah ina kauli hii: "*Yaa laitanii kuntu ma`akum fa-afuuza ma `akum fil h`inaani maa`sh shuhadaa-l was`s`aalih`iina wa h`asuna uulaa-ika rafiiqaa.*"

la kwenye ndoto yangu na nilikuwapo pale. Nilikuwa ninamwambia Imam, "Ewe mtoto wa Mtume! Mimi nimekuja kukusaidia wewe." Imam akasema: "Ngoja" Nilingoja hadi muda wa Swala ukawadia."

(Nimesoma kwenye vitabu vya Masaibu ya Karbala kwamba Said bin Abdullah Hanafi na masahaba wengine walisimama kama ngao ya kibinadamu mbele ya Imam aweze kuswali. Ni watu ambao walikuwa na shauku ya kweli. Ambapo viungo vya miili yao vilikuwa vinakatwa na kuanguka chini ardhini). Walikuwa wanafikiri:

**Uhai ambao nimeutoa mhanga nilipewa na Yeye tu**

**Ukweli ni kwamba, hatujalipa deni tunalodiwa**

Mwanazuoni huyo anasema kwamba Imam (a.s.) alimwambia kwenye ndoto yake: "Ninataka kuswali. Simama mbele yetu. Maadui wakitupa mishale, izuie na usiiruhusu ifike kwetu." Mwanazuoni akasema: "Kwa vyovyote vile." Alisimama mbele ya Imam ambapo Imam alianza kuswali. Anasema (mwanazuoni): "Niliuona mshale wa kutisha unakuja kumuelekea Imam. Mshale ulipofika karibu zaidi, niliinama bila hiari na mshale ukampiga mtukufu Imam. Nikasema: Ninaomba msamaha wa Allah na ninatubu Kwake. Hilo lilikuwa baya sana. Sitaruhusu litokee tena. Sasa nitazuia kila mshale kwa kifua changu. Ghafla, mshale mwingine ulikuja na kwa mara nyingine niliinama kuokoa maisha yangu. Mshale huu pia ulimuumiza mtukufu Imam. Halafu mshale wa tatu na wa nne ilikuja na yote ilimuumiza Imam tu kwa sababu kila mara nilikuwa najaribu kunusuru maisha yangu. Halafu ghafla macho yangu yaliangukia kwa Imam, na nilimuona kwamba alikuwa anatabasamu na kusema: "Sijapata kuona masahaba walio bora na watiifu zaidi kuliko wangu mimi."[146]

Kukaa nyumbani na kusoma "Natamani ningekuwa......" haiwi sababu ya mtu kufika kwenye daraja hilo. Inahitaji ujasiri wa kivitendo.[147] Pale wakati unapowadia, itajulikana kuwa ni nani atakayeweza kuyaweka maneno yake

[146] Imam Husain alisema katika mkesha wa Ashura: "Siwajui masahaba wowote walio bora na watiifu zaidi kuliko wangu na familia yoyote iliyo na uchamungu na bora zaidi ya Ahlul-Bayt wangu." *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk.395.

[147] Wakati Imam Husain alipoingia Karbala alisema, "Watu wamekuwa watumwa wa dunia na dini ipo kwenye ncha za ndimi zao tu. Wanatumikia dini pale tu ambapo maisha yao yamefarijika. Wakati wa mtihani unapowadia, watu wachache sana wa dini hubaki." *Tuhafful Uquul*, uk. 245

kivitendo. Masahaba wa Imam Husain (a.s.), hawakutoa ahadi tu, bali waliyaweka maneno yao kivitendo. Walikuwa wakisema:

"Kufa chini ya miguu yako,

hilo tu ndio shauku ya nyoyo zetu."

## HALI YA UJASIRI

Mazungumzo yangu bila kujitambua yakafika wakati wa Swala ya Adhuhuri ya Imam Husain (a.s.) na muda wa Swala yetu ya Adhuhuri pia umekaribia. Kama mjuavyo masahaba wengi wa Imam waliuawa kishahidi kabla ya Swala yenyewe ya Adhuhuri. Kwa hiyo, masahaba wachache tu na watu wa familia walikuwa hai hadi Adhuhuri ya Ashura.

Hatua ya kwanza ya kuuliwa kishahidi masahaba wa Husain ilikuwa ni kutupiana mishale kwa safu zilizosimama pande zote mbili. Upande wa Imam Husain (a.s.) ulikuwa na watu sabini na mbili tu lakini walikuwa jasiri sana. Walikuwa wachangamfu mno na ukweli ulikuwa ni kwamba hapakuwepo na wa kulingana nao kwa uchangamfu na ujasiri.

Imam Husain (a.s.) hakutaka kuonyesha hata dalili ndogo ya kudhani kwamba yeye angeshindwa. Aliligawa jeshi lake katika makundi matatu: kushoto, kulia na katikati. Zuhair bin Qayn aliongoza upande wa kulia, Habib bin Mudhahir aliongoza upande wa kushoto na mdogo wake, Abbas aliongoza sehemu muhimu (moyo) ya jeshi. Alipewa bendera ya jeshi na kwa sababu hiyo, cheo *Alamdar* (Mshika bendera) kikawa sehemu ya jina tukufu. Masahaba wa Imam waliomba ruhusa ya kuanza mapigano lakini Imam (a.s.) alisema:

"Hapana, sisi hatutashambulia hadi hapo adui atakapoanza uhasama."

## DINI NA DUNIA

Mwanzoni kabisa, Ibn Saad alianzisha mashambulizi yaliyocheleweshwa kwa sababu alitaka kushikilia imani ya dini na mambo ya kidunia kadhalika. Alikuwa anataka kupata ufalme wa Rayy kutoka kwa Ibn Ziyad na wakati huo huo akiepuka kupakaza mikono yake damu tukufu ya Imam Husain (a.s.). Kwa hiyo, kwa mfululizo alikuwa akiandika barua kwa Ibn Ziyad ak-

ipendekeza pawepo na mkataba wa amani baina yao na Imam Husain (a.s.) ili vita visianzwe. Ibn Ziyad alipotambua jambo hilo, aliandika barua ya kumuamuru akamilishe kazi aliyopewa au ampe ukamanda wa jeshi mtu mwingine ambaye amepewa wajibu huo kwa kusaidiana naye. Ibn Saad hakutaka dunia imponyoke mikononi mwake. Kwa hiyo, ulipofika wakati wa kuchagua baina ya dini na dunia, aliiaga dini akasema: "Nitapigana kwa lengo la kutimiza amri ya gavana."

## MWANZO WA VITA NA MATOKEO YAKE

Mnamo siku ya Ashura, katika jangwa la Karbala, Ibn Saad alifanya vitendo kadhaa vya kifisadi kwa sababu alitaka kuthibitisha kwamba yeye ni kamanda mtiifu wa Ibn Ziyad na kukanusha taarifa zilizopelekwa kwa Ibn Ziyad kwamba Umar bin Saad alikuwa anasitasita kuanza vita kwa sababu alikuwa anamtakia heri Husain. Hivyo, majeshi ya pande zote mbili yaliposimama na kuelekeana, Ibn Saad aliwaambia watupa mishale wake kuwa tayari. Wote walijitayarisha. Halafu akatupa mshale kuelekea kwenye jeshi la Imam huku akisema:[148]

"Enyi watu! Kuweni mashahidi kwa Amiri, Ibn Ziyad kwamba mimi nilikuwa mtu wa kwanza kutupa mshale kuelekea jeshi la Husain."

Kila ninapofika kwenye maelezo haya ya Ibn Saad, hukumbuka kauli ya rafiki yangu na rafiki yenu pia, watu wa Narmik,[149] marehemu Ibrahim Ayati, ambaye alikuwa mwanazuoni mashuhuri na msomaji wa Majilisi na aliyefariki dunia miaka kumi iliyopita, ambayo niliisikia kutoka kwake na labda pia kuisoma kwenye kitabu chake. Alikuwa akisema:

"Vita ya Karbala vilianza kwa mshale na vikaishia kwa mshale."

Vita vilianza kwa sababu ya mshale uliotupwa na Umar bin Saad; lakini unajua ni mshale upi uliomaliza vita hivyo? Mishale ilitupwa kutoka kushoto na kulia na yote ilikuwa inamlenga Imam (a.s.). Imam (a.s.) alikuwa anapigana mfululizo na kuwaua wale ambao wamehukumiwa kwenda motoni. Lakini (Imam) aliishiwa nguvu kwa sababu ya majeraha na uchovu wa vita.

[148] Ibn Saad alikuwa mtoto wa sahaba wa Mtukufu Mtume, Saad bin Abi Waqqas na ilitokea kwamba, mtu huyu alikuwa mtaalam wa kupiga mishale na alikuwa anajulikana sana katika bara Arabu yote. Hivyo, Ibn Saad alikuwa amesadia kwenye vita nyingi kupitia Ustadi wake. (Ustaadh (Mutahhari).

[149] Watu wanaozungumziwa hapa ni watu wa Msikiti ujulikanao kama Jame Masjid Narmik (Tehran) ambako ndipo shahidi Mutahhari alikuwa akisoma Majilisi hii.

Ghafla mtu akampiga jiwe usoni pake kikatili kabisa; na damu ikamwagika kwa wingi. Imam alichukua sehemu ya chini ya shati lake ili afute damu wakati mmojawapo wa mishale miwili ya ncha sita yenye sumu ulipotua kwenye kifua kitukufu cha Imam madhlumu, na jihadi ya Imam ikaishia hapo.

Sasa, madhalimu wakaona kwamba Husain alikuwa hasemi: "Hivi yupo yeyote....." badala yake akawa anaongea na Mwenyezi Mungu tu akisema:

"Kwa Jina la Allah na kwa Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) "

Kwa vyovyote iwavyo, nilikuwa ninasema kwamba mshale wa kwanza ulitupwa na Ibn Saad. Baada ya hapo, mishale ikaanza kumwagika kama mvua juu ya masahaba wa Imam Husain (a.s.). Ni ushujaa na ujasiri kiasi gani hawa masahaba wa Imam Husain (a.s.) walikuwa nao! Walipiga magoti na wakatupa mishale yote iliyokuwa kwenye mapodo yao mmoja baada ya mwingine kwa haraka haraka na wakawapeleka maadui wengi waliostahili kwenda jahanamu.

Baadhi ya wapiganaji wa jeshi dogo la Imam Husain (a.s.) waliuawa kishahidi kwa mishale hiyo ya maadui. Baada ya hapo, vita vya mtu na mtu vikaanza. Wakati wowote mtu kutoka upande wa Imam Husain (a.s.) akijitokeza kwenye uwanja wa vita, makafiri kadhaa walikuwa wakimkabili. Hata hivyo, moyo wa imani wa Imam Husain (a.s.) kila mara uliibuka mshindi. Hata mpiganaji mzee kutoka jeshi la Imam Husain (a.s.) alikuwa anaweza kuwapeleka maadui watano hadi kumi jahanamu.

## KIFO CHA KISHAHIDI CHA ABIS BIN ABI SHABIIB SHAKRI

Sahaba mmoja wa Imam Husain (a.s.), Abis bin Abi Shabiib Shakri alikuwa na hali ambayo moyo wake ulijaa 'shauku ya hisia za ki-Husain.' Alipoingia kwenye uwanja wa vita, alikariri shairi la vita (*Rajaz*)[150] kama ilivyokuwa desturi, na akawapa changamoto adui kwa pambano la mtu na mtu. Hata hivyo, hakuna aliyethubutu kujitokeza kutoka upande wa adui kuja kupambana na huyu sahaba wa Imam Husain (a.s.) mwenye moyo kama wa simba.

[150] Rajaz ya Abis ilikuwa *"ala rajulun? "ala rajulun*? yaani "hivi hakuna mtu miongoni mwenu ambaye anaweza kuja kupigana na mimi?"

Ilipokuwa kwamba licha ya wito uliorudiwa tena na tena hapana mtu aliyethubutu kujitokeza kupigana na Abis, akakasirika na akarudi kutoka kwenye uwanja wa vita. Akavua helmeti yake, deraya na viatu na akaenda kwenye uwanja wa mapambano akiwa hana viatu na akaita: "Njooni sasa angalau mpigane na Abis."[151]

Lakini hakuna aliyethubutu kujitokeza. Hatimaye jeshi la Umar bin Saad lilinywea kwenye woga na wakaanza kutupa mawe na vipande vya mapanga yaliyokatika kwa Abis na kwa njia hii walimuua kishahidi.

Ujasiri na uaminifu ulioonyeshwa na masahaba watiifu wa Imam Husain (a.s.) mnamo siku ya Ashura hauwezi kulinganishwa. Hali hiyo haikuwa kwa wanamume tu. Hata wanawake walikuwa nayo hali hii. Wameacha nyuma yao zile dalili ambazo katika historia ya binadamu zitabakia hadi mwisho wa dunia. Endapo dalili hizo zingeonekana kwenye historia ya watu wa Ulaya tungeona jinsi ambavyo wangenufaika nazo.[152]

---

[151] *Biharul Anwar*, Juz. 45. uk. 28; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 251

[152] Ni suala muhimu kabisa. Kipengele cha msingi cha muundo wa jumuiya huja kutokana na mambo kama hayo tu. Washairi, wanafikra na viongozi wa kisiasa ambao ndio wajenzi wa jumuiya, huwafanya watu kama hao mashujaa wa jumuiya na hubadili jumuiya yote.

Tunajua kwamba nguvu za kisiasa na kishetani zimebakia kwenye mamlaka tangu mwanzo lakini kufuatana na falsafa ya migongano, dhamira miongoni mwa watu huendelea kuwa imara kwa sababu ya migongano ya kijamii. Hivyo, watu wangeendelea kuelewa wahyi na Uislamu ungefunika dunia kwa sababu wenyewe unaendana na maumbile ya mwanadamu. Mathalani, kwa kawaida mwanadamu anapenda haki na anachukia dhuluma. Watu hupenda uhuru na wanachukia utumwa. Watu wanapenda uhuru wa kukusanyika, uhuru wa kufikiri, uhuru wa kufuata dini yoyote, uhuru wa kisiasa, uhuru wa kiuchumi na uhuru binafsi. Mafundisho ya Uislamu yanaongoa akili za watu duniani kote bila kuchukua jina la Mola wa Ulimwengu. Ndio sababu maadui wa Uislamu wanajaribu bila mafanikio kuzima taa hii.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mtu wa kwanza kupinga ubaguzi wa kimbari. Yeye aliamini kwamba watu weusi, weupe na binadamu wote ni sawa. Kiwango cha heshima ya mtu kinategemea na ucha Mungu wake na tabia yake njema. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alilikuwa amewafahamisha watu kupitia Qur`ani juu ya thawabu za kuwaachia watumwa huru. Hivyo, aliziamsha fikra za wanadamu, hali ambayo bado imo kwenye mabadiliko.

Marekani kusini na Ulaya zilisimama dhidi ya utumwa kwa zaidi ya karne moja na nusu iliyopita. Martin Luther King alipigania haki sawa za watu weusi nchini Marekani. Nelson Mandela alipambana kwa ajili ya uhuru wa Afrika ya Kusini. Juhudi zote hizi zilikuwa na msukumo wa mkono wa Uislamu usiotajika ndani yake kwa sababu Uisalmu hufundisha uhuru na usawa. Mafundisho ya Uislamu ni kwa zama zote, jamii na vizazi vyote. Mtukufu Mtume alisema: "Enyi watu! Wanawake wanazo haki juu yenu kama vile nyinyi mlivyo na haki juu yao." Uislamu hutetea haki za wanawake na hadhi yao. Kufuata Sunna na matendo ya Mtukufu Mtume kungeihakikishia "neema" dunia yote na wanadamu wote.

Tabia ya Imam Ali Murtaza (a.s.) ni ya mfano bora katika uwanja mpana wa historia kuhusu kuwafichua wanafiki, kupigana dhidi ya udikteta, kuwasaidia wanaokandamizwa, kuuchukulia utajiri wa jumuiya kuwa dhamana na kuwaongoza watu wanaounga mkono serikali ya jamhuri. Ipo tabia nyingine zaidi katika historia nayo ni ile ya Imam Husain (a.s.) aliyethubutu kukataa katakata kutoa kiapo cha utii kwa dikteta dhalimu.

## MAMA MWENYE KUJITOA MUHANGA WA ABDULLAH BIN UMAIR

Abdullah bin Umair alikuwepo Karbala akiwa na mama yake na mke wake. Alikuwa mtu jasiri sana na mwenye nguvu. Aliponuia kwenda kwenye uwanja wa vita, mke wake alimuuliza: "Mimi utanikabidhi kwa nani? Nini kitanitokea baada yako?" Hawa ni wanandoa ambao walioana sio muda mrefu uliopita. Mama yake Abdullah bin Umair aliposikia mazungumzo yao, alisema:

"Mwanangu! Usitilie maanani yale anayosema mkeo. Leo ni siku ya mtihani wako. Kama hukujitoa mhanga leo, nitajiona kama mimi sikukunyonyesha." Abdullah alipigana vita vikali sana na akauliwa kishahidi. Baadaye, mama yake Abdullah alitwaa nguzo ya hema na akawashambulia maadui fidhuli. Imam Husain (a.s.) alipoona ujasiri wa mwanamke huyu, akasema kwa kupaza sauti: "Mwenyezi Mungu akulipe thawabu! Rudi kwenye hema la wanawake na ukae huko. Jihadi sio wajibu kwa wanawake." Baada ya kusikia amri ya kiongozi wake aliinama kwa heshima na akarudi kwenye hema lake.

Kwa upande mwingine adui walimkata kichwa Abdullah na kukitupa upande alikokuwa mama yake na kusema: "Chukua hiki, muweke mwanao pamoja nawe." Mama alikiinua kichwa cha mwanae kijana, akakikandamiza kifuani mwake, akakibusu na akasema: "Hongera mwanangu, wewe ni jasiri sana. Sasa nimefurahishwa nawe na ninakubali kwamba nilikunyonyesha." Halafu akakitupa kichwa kilichokatwa kuelekea upande wa maadui na akasema: "Huwa hatuchukui kile tunachokitoa katika njia ya Mwenyezi Mungu."[153]

---

Aliwafundisha wapenda uhuru kwamba ni bora zaidi kufa kiheshima kuliko kuishi na fedheha. Midomo inapofungwa kwa sababu ya dhuluma, kimya huenea kila mahali na watu hukubali kutii udhalimu. Baada ya kifo cha Stalin, katibu mkuu wa chama cha kikomnisti, Khrushchev alikuwa akimkosoa Stalin kwenye mojawapo ya mikutano ya chama. Mmojawapo wa wanachama alitoa maoni yake, "Kwa nini ulinyamaza kimya mbele ya Stalin?" Khrushchev akasema,"Yeyote ambaye ametoa maoni haya asimame." Hata hivyo, hakuna aliyesimama. Khrushchev alicheka na akasema. "Kama ambavyo hapana yeyote miongoni mwenu anayethubutu kusema mbele yangu, mimi sikuthubutu kusema mbele ya Stalin.?"

Padri mmoja wa Kikristo anasema kwamba kama wangekuwa na Imam Husain (a.s.) badala ya Nabii Isa wangeweza kutawala dunia hii. Benard Shaw ametabiri, "Ulaya (na Marekani) watakubali Uislamu hapo baadaye." Litakapotokea hili, watu hawa wanaong`aa watakuwa minara ya mwanga mkubwa katika njia ya mwongozo kwa ajili ya Waislam.

[153] Tukio lilimesimuliwa na Ustadhi Mutahhari ni la Wahab bin Abdullah bin Habbab Kalbi. Hadithi ya aina hii hii imesimuliwa kuhusu Abdullah bin Umair Kalbi ambaye aliishi Kufa na alikwenda Karbala na mke wake Umme Wahab. Marehemu Allamah Sherani ameandika pembezoni mwa *Damaus Sujum*, uk. 147 kwamba

## MTOTO ANAYESTAHILI KUSIFIWA

Pia muda uliwadia ambapo Imam Husain (a.s.) aliona kwamba ni watu wachache tu ambao walikuwa wamebakia kwenda kwenye uwanja wa vita na walikuwa wanaomba ruhusa kutoka kwake. Wakati huo, mtoto wa miaka kumi na mbili alijitokeza kutoka kwenye mkusanyiko wa masahaba akiwa na upanga umening`inia kiunoni mwake. Alimwambia Imam Husain (a.s.), "Bwana wangu, Imam! Tafadhali nakuomba uniruhusu niende kwenye uwanja wa vita." – Baba yake mtoto huyu alikwishauawa kishahidi kwenye vita hivyo sio muda mrefu uliopita.

Imam akasema: "Huwezi kwenda. Wewe ni mdogo mno."

Mtoto akasema: "Maulana Imam! Tafadhali niruhusu niende."

Imam (a.s.) akasema: "Hapana, ninahofia mama yako ambaye sasa ni mjane atadhikika."

Baada ya kusikia haya, mtoto akasema: "Maulana Imam! Mama yangu ameniamuru niende nikajitoe mhanga juu yako. Alisema kwamba kama sikujitoa mhanga juu ya Imam hatakuwa radhi na mimi."

Mtoto huyu ambaye alikuwa anaomba rukhsa kutoka kwa Imam alikuwa na adabu nzuri sana, na alipata heshima hiyo, ambayo hapana mtu mwingine angepata, kwa sababu kila mpiganaji alijitambulisha alipofika kwenye uwanja wa vita kufuatana na desturi ya Waarabu, lakini mtoto huyu hakujitambulisha na haikuwezekana kurekodiwa mtoto huyo alikuwa nani.[154]

Waandishi wa Masaibu ya Karbala hawakuweza kumtambua mtoto huyu. Walichofanya ni kuandika tu haya yafuatayo: "Na mbele akajitokeza kijana ambaye baba yake alikuwa amekwisha kuuliwa katika mashambulizi ya awali."

---

tukio hili limethibitishwa kuwa la kweli kwa sababu ya kurudiwa kusimuliwa kwake na watu wawili. Wahab bin Abdullah Kalbi alikuwa bado kijana na mwanandoa mpya ambapo Abdullah bin Umair Kalbi alikuwa sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na alikuwa mtu mzima. (Rizwani)

*Luhuuf*, uk.105; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 17; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 651; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 435.

[154] Jina la mtoto huyu limetajwa kama Amr bin Junada Ansari kwenye *Maqtal-e-Muqarram.* Baba yake, Junada Ansari aliuawa kishahidi katika shambulio la kwanza.

Hivi huyu mtoto hakughani shairi hili la kivita?

“Enyi watu! Sikilizeni, mkuu wangu ni Husain na hii inatosha kwa utambulisho wangu.

“Mimi ni mmojawapo ambaye Husain ndiye bwana wake; ambaye ni bwana bora sana; ambaye ni furaha ya moyo wa Mtume ambaye alileta habari njema na akaonya.”[155]

[155] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 27; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk. 457.

# MAJILISI 22

## MSAFARA WA WATU WANAOJITOA MHANGA

Imam Husain (a.s.) aliuhutubia mkusanyiko wa mahujaji na wale waliotembelea Kaaba kabla hajaondoka Makkah na akasema: "Ni yule tu miongoni mwenu ambaye anataka kutoa muhanga maisha yake kwa ajili yangu na akutane na Mola Wake anapaswa kuandamana nami. Nitaondoka kesho asubuhi, Inshallah."[156] Kana kwamba mtukufu Imam alikuwa anawaambia watu kwamba wale wanaopenda ukwasi na mamlaka na wale wanaofikiri kuwa maisha yao ni muhimu wasifuatane naye kwa sababu msafara wao ni wa watu wanaojitoa mhanga tu.

Ndugu wa karibu wa Imam Husain (a.s.) walikuwepo pia miongoni mwa wale watu waliokuwa tayari kujitoa mhanga. Je! Kama Imam angewaacha ndugu zake Madina hivi kuna mtu yeyote ambaye angepinga? Hapana kabisa. Hata hivyo, hebu fikiria kama Imam Husain (a.s.) angewaacha ndugu zake na akauawa kishahidi peke yake hivi kifo chake cha kishahidi kingepata hadhi kama kilivyo hivi sasa? Hivi tukio la Karbala lingepata umuhimu kama lilivyopata sasa? Hapana kabisa.

Imam Husain (a.s.) alifanya jambo la ajabu hivyo kwamba alieleza maana ya kutoa kila kitu mhanga katika njia ya Allah. Imam alifanikisha kazi hii na alionyesha wazi kwamba hakuna kilichobaki kwa ajili ya kutolewa muhanga.

Ndugu wa Imam Husain (a.s.) hawakulazimishwa kufuatana naye lakini walikuwa na imani na fikra zilezile kama za Imam (a.s.).

### "YEYOTE AMBAYE HANA MOYO WA KUJITOA MHANGA ASIJE"

Kimsingi, Imam Husain (a.s.) alikwishaamua kwamba kwenye msafara wa watu wa kujitoa mhanga pasiwepo hata mtu mmoja mwenye dalili yoyote

[156] *Luhuuf*, uk. 61; *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 366; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 329.

ya "udhaifu" ndani mwake. Ndio maana Imam aliwatahini masahaba wake mara mbili au mara tatu wakati wa safari na aliwarudisha watu wachache wenye udhaifu kila alipowatahini. Kabla ya kuondoka Makkah, Imam (a.s.) alitangaza kwa sauti kuu: "Yeyote ambaye hana moyo wa kutoa mhanga maisha yake asifuatane na sisi." Licha ya kusikia tangazo lake la kuogofya, baadhi ya watu wenye nyoyo dhaifu walidhani kwamba ingewezekana kwamba baada ya kufika Kufa, wangefaidika kutokana na kitendo cha kuungana na Imam. Walifikiri kwamba pia wangepata kazi nzuri serikalini huko. Kwa hiyo, watu wenye nyoyo dhaifu pia walifuatana na Imam katika safari yake. Zaidi ya hayo, Waarabu wachache wanaoishi maisha ya kuhamahama pia walijiunga kwenye msafara wa Imam (a.s.).

## MASAHABA WA HUSAIN WATAHINIWA

Imam Husain (a.s.) aliwaambia masahaba wake wakati wa safari:

"Yeyote miongoni mwenu anayefikiri kwamba atapata kazi serikalini baada ya kufika huko anapaswa kufuta matarajio yake hayo na arudi nyumbani." Baada ya kusikia taarifa hii, watu wengi walirudi nyumbani.[157]

Baada ya hapo, Imam aliwapima masahaba wake kwa mara nyingine mnamo mkesha wa Ashura. Wanahistoria wote mashuhuri wanayo maoni mamoja kwamba hakuna sahaba hata mmoja aliyerudi wakati wa usiku huu. Mkono wa Kimungu ulikwisha waondosha wote wale waliokuwa waoga kutoka kwenye kundi la Imam Husain (a.s.). Mwandishi wa "*Nasikhut Tawarikh*" amefanya kosa kwa kuandika kwamba pale Imam Husain (a.s.) alipowaruhusu masahaba wake kurudi kama walipenda kwa kutumia fursa ya giza la usiku; baadhi ya masahaba walimuacha na wakaondoka. Hata hivyo, taarifa hii si sahihi kwa sababu haijathibitishwa na kitabu kingine chochote cha historia. Hakuna mwanahistoria ambaye amefanya kosa hili isipokuwa mwandishi wa "*Nasikhut Tawarikh*." Ni ukweli uliothibitika kwamba hakuna msaidizi yeyote miongoni mwa wasaidizi wa Imam Husain (a.s.) aliyeondoka mnamo siku ya Ashura. Hii inathibitisha kwamba hakuna sahaba wa Imam Husain (a.s.) aliyepungukiwa na kiwango cha juu kabisa cha imani na hakuna hata mmoja wao aliyekuwa na udhaifu wa imani.

Mafanikio makubwa kabisa ya harakati za Imam Husain (a.s.):

[157] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 223; *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 374; *Mausuat-e-Kalimat*, uk. 348.

Kama katika Siku ya Ashura hata kama sahaba au mtoto mmoja tu angeonyesha chembe ndogo sana ya woga na akajiunga na jeshi la adui lililo kubwa na lenye nguvu ili aweze kunusuru maisha yake hiyo ingekuwa dosari kwa upande wa Imam Husain (a.s.) na madhehebu ya Husain.

Kinyume chake, baadhi ya watu kutoka jeshi la adui ambao walikuwa salama salimini kutokana na hatari zote,walijiunga na Imam (a.s.), wakaacha anasa zote na wakathubutu kuingia kwenye ukanda wa hatari ambapo watu ambao walizungukwa na hatari hawakuziendea anasa.

Kama Imam Husain (a.s.) asingetangaza zile hatari na asingewatahini masahaba wake kabla, nusu ya masahaba wa Imam Husain (a.s.) wangeondoka na wangemshutumu Imam Husain (a.s.). Kwa sababu yeyote anayekimbia hakubali udhaifu wa imani yake lakini huwasilisha visingizio kadhaa ili aweze kuficha mapungufu yake na akasema: "Baada ya kufanya uchunguzi sahihi, nilimuunga mkono yeyote ambaye niliona alikuwa kwenye njia iliyonyooka......kama ningeona ridhaa ya ki-Mungu (ikipendelea kifo changu cha kishahidi) ningetoa mhanga maisha yangu. Hata hivyo, mambo hayakuwa hivyo. Tulidhani kwamba upande wa upinzani ulikuwa sahihi na tukajiunga nao." Watu kama hao huwasilisha mantiki potofu. Hata hivyo, jambo kama hilo halikuonekana kwenye msafara wa Husain na hayo ni mafanikio makubwa na suala la kujivunia kuhusu Vuguvugu la Husain.

## HURR, MFANO WA DHAMIRA ILIYOZINDUKA

Hapo Karbala, harakati za Imam Husain (a.s.) zilimvuta jemedari mkuu wa jeshi la adui, Hurr Yazid Riyahi na kwenda kuzielekea. Hurr hakuwa mtu wa kawaida. Baada ya Umar bin Saad, Yeye alikuwa mtu muhimu sana kwenye jeshi la Yazid. Mwanzoni, alifanywa kuwa kamanda. Alikuwa wa kwanza kupewa ukamanda wa kikosi cha askari wapanda farasi elfu moja na wakapelekwa kufunga njia ya Imam Husain (a.s.). Licha ya ukweli kwamba yeye alikuwa ndiye mtu wa kwanza kuchomoa upanga wake dhidi ya Imam Husain (a.s.) mnamo siku ya kwanza, alikuwa amejaa imani na moyo wa kutenda matendo mema. Hatimaye moyo huu huu ulimfanya asalimu amri mbele ya Imam Husain (a.s.) na kutubia kwa ajili ya kosa lake la mwanzo la kijinga. Kwa njia hii, Hurr alijiunga na kundi la 'watubiaji' ambalo kuhusu wao imo aya ndani ya Qur`ani:

التَّائِبُونَ الْعَابِدُونَ الْحَامِدُونَ السَّائِحُونَ الرَّاكِعُونَ السَّاجِدُونَ الْآمِرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَالنَّاهُونَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَالْحَافِظُونَ لِحُدُودِ اللَّهِ ۗ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ

**"Wanaotubia, wanaoabudu, wanaohangaika, wanaorukuu, wanaosujudu, wanaoamrisha mema na wanaokataza maovu na wanaohifadhi mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na wape bishara Waumini." (Sura At-Tawbah 9 : 112).**

## HURR ANATUBIA

Alipata umashuhuri kwa sababu ya uthubutu na ujasiri wake. Hili linathibitishwa na ukweli kwamba alipewa cheo cha ukamanda wa kikosi cha askari wapanda farasi elfu moja ambacho kilipelekwa kuwa kizuizi kwenye njia aliyokuwa anapita Imam Husain (a.s.).Lakini Imam Husain (a.s.) alibadili namna ya kufikiri ya mtu huyu.

Kama vile ambavyo moto unavyowaka katikati ya sufuria na kuchemsha maji na mvuke unaotengenezwa na hali hiyo, husababisha chombo chote kutetemeka, kwa njia hiyo hiyo mshumaa wa ukweli, ambao Imam Husain (a.s.) aliuwasha moyoni mwa Hurr, ulitetemesha uhai wake wote kabisa. (Hurr naye pia alijali maisha ya kidunia kama wewe na mimi. Pia naye alipenda utajiri, cheo kikubwa na usalama lakini " moto wa haki" ulikuwa unamshinikiza kuungana na Imam Husain (a.s.).

Mahitaji ya kidunia yalikuwa yanamshawishi Hurr. Hurr alikuwa amesimama kwenye njia panda na akifikiria kwamba kama angeungana na Husain angeuawa kishahidi katika kipindi cha saa moja baadaye na hangeweza kumuona mkewe na watoto wake tena. Serikali itataifisha rasilimali zake. Mke wake atakuwa mjane. Mawazo kama hayo yalikuwa yakimzuia asiondoke kuelekea kwa Imam.

Nguvu hizi mbili pinzani zilikuwa zinamshawishi Hurr. Ghafla mtu mmoja alimuona Hurr anatetemeka. Mtu yule alisogea mbele akauliza: "Ni nini hiki ninachokiona? Kwa nini mtu jasiri kama wewe anatetemeka?" Labda muulizaji huyu alidhani Hurr alikuwa anahofia maisha yake. Hurr akajibu: "Hapana siogopi kifo changu. Hujui ni mateso ya aina gani moyo wangu unayapitia. Sasa hivi, ninajikuta nimesimama katika njia panda ya jahanamu

na pepo; nikiwa huru kuchagua mojawapo ya hizi njia mbili. Naweza nikachukua Pepo, ambayo ni heshima njema na ninaweza kuchukua dunia hii, ambayo ni pato lakini ambalo linaweza kunipeleka jahanamu."

Hurr aliendelea kuwa katika hali hii ya vuta nikuvute ya ndani mwake kwa muda mrefu. Hatimaye alisikiliza ushauari wa dhamiri yake katika dakika za mwisho na akawa Hurr huru, kama isemavyo kauli ya Imam Husain (a.s.). Akiogopa kwamba adui angemzuia, aliondoka pole pole. Halafu alimtia chonjo farasi wake na upesi aliondoka kasi kwenda kwenye kambi ya Imam Husain (a.s.). Aliashiria kusimamisha vita kwa muda ili kwamba masahaba wa Imam Husain (a.s.) wasije wakamfikiria kuwa ni mshambuliaji.

## "JE, TOBA YANGU INAWEZA KUKUBALIWA?"

Inasimuliwa kwamba Hurr alipindua ngao yake ili kutoa ishara kwamba yeye hakuwa akienda kupigana ila alikuwa anakwenda kuomba usalama. Mtu wa kwanza aliyekuja mbele ya Hurr alikuwa Imam Husain (a.s.). Alikuwa amesimama nje ya kambi ya watu wa familia yake. Hurr alisogea karibu na akasema: "Amani iwe juu yako, Ewe Aba Abdillah!" na halafu akasema:

"Ewe Maulana! Mimi ni mkosaji mwenye dhambi, mimi nilikuwa mtu wa kwanza kufanya Jinai ya kufunga na kuzuia njia yako."

Halafu Hurr akamuomba Mwenyezi Mungu Muweza wa Yote:

"Ee Mola! Nisamehe dhambi zangu. Nilizitisha sana nyoyo za mawalii zako na kuwaogofya." (Ahlul-Bayt wa Imam Husain (a.s.) walipomuona Hurr kwenye njia yao kwa mara ya kwanza, alikuwa akifuatana na wapiganaji elfu moja wenye silaha ambao walifunga njia Imam. Kwa hiyo, ilikuwa ni jambo la kawaida wao kuhofia.)

"Ewe Maula! Nimefanya toba kwa ajili ya dhambi zangu. Weusi wa uchafu wa uso wangu hauwezi kuoshwa kwa kitu kingine cho chote isipokuwa kwa damu yangu. Nimekuja kwako kutubu baada ya kuomba ruhusa kutoka kwako. Hata hivyo, Imam wangu! Kwanza niambie kama toba yangu inaweza kukubaliwa?"

Sasa hebu iangalie tabia ya Imam Husein (a.s.). Yeye hakujali kuhusu jambo lake binafsi. Alijua kwamba hata kama Hurr ametubia kwa ajili ya vitendo vyake, mazingira yaliyopo sasa hayataweza kubadilika. Hata hivyo Imam hakujali mambo kwa ajili yake binafsi bali tu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hasa. Kwa hiyo yeye akajibu: "Kwa hakika toba yako itakubaliwa. Ni kwa vipi toba yako isikubaliwe? Je, mlango wa rehema za mbinguni umewahi kufungwa kamwe kwa ajili ya mtubiaji yeyote yule? Hasha lillahi, kamwe!

## KWA NINI HURR HAKUINGIA KWENYE HEMA LA IMAM?

Hurr alipojua kwamba toba yake imekubaliwa, alimtukuza Mwenyezi Mungu na akasema: Kiongozi wangu! Sasa kwa kuwa toba yangu imekubaliwa, nataka kujitoa mhanga juu yako. Nataka kutoa damu yangu katika njia yako."

Imam Husain (a.s.) akasema: "Ewe Hurr! Wewe ni mgeni wangu. Shuka kutoka kwenye ngamia wako. Kaa kwa muda na mimi ili tuweze kukuhudumia kwa kiasi fulani." (Sijui Imam Husain (a.s.) alitaka kumhudumia nini Hurr). Lakini Hurr aliendelea kuomba ruhusa kutoka kwa Imam ili kwamba asiwe na haja ya kuteremka kutoka kwenye farasi wake. Imam naye alisisitiza sana lakini Hurr hakushuka kutoka kwenye farasi wake.

Baadhi ya waandishi wa msiba wa Karbala wameeleza kwamba Hurr alitaka kukaa na Imam kwa muda kidogo lakini aliogopa kwamba kama angeketi naye, mmojawapo wa watoto wa Imam angetokeza na kusema: "Ni mtu huyu huyu ndiye aliyefunga njia yetu ile siku ya kwanza." Hurr alitaka kujiokoa kutoka kwenye mazingira hayo ya kuaibisha kwa kufuta uchafu wa uhalifu wake kwa wekundu wa damu yake. Hivyo, aliposisitiza mno, Imam alisema: "Ewe Hurr! Kama kweli unataka hivyo, unaweza kwenda."

## MAZUNGUMZO BAINA YA JESHI LA UMAR BIN SAAD NA HURR

Kwa kuwa mtu huyu jasiri naye pia alikuwa anatoka Kufa alizungumza na jeshi la Kufa akirejelea barua ambazo watu wa Kufa walimpelekea Imam na akasema: "Enyi watu! Kwa bahati nzuri mimi sikuwa katika watu wale waliomuita Imam kuja Kufa kwa kumwandikia barua. Hata hivyo, nyinyi

na wazee wenu mmemualika Imam aje hapa baada ya kumwandikia barua na pia mliahidi kumsaidia. Kwa hiyo, ninawaulizeni nyinyi watu, ni kwa msingi gani, kanuni na msimamo wa dini gani, mnamtendea mgeni wenu kwa namna isiyo ya kibinadamu kiasi hiki?"

Baada ya hapo, mtu huyo jasiri alisema kitu ambacho kinaonyesha kwamba kitendo hicho kilikuwa cha kifisadi sana na kilikuwa kinyume na Uislamu na maumbile. Ni kitendo hiki ndicho kilichomfanya mtu huyu jasiri kukasirika sana. Historia ya Uislamu inathibitisha kwamba ni makosa kumtendea hata adui wa Uislamu kwa namna kama hii. Kwamba ni kosa kumbughudhi mpinzani kwa kudhikisha maisha yake kwa kumzuia asipate maji. Imam Ali bin Abi Talib (a.s.) pia alishauriwa kumzuia Muawiyah na jeshi lake wasipate maji lakini Imam hakufanya hivyo.

Imam Husain (a.s.) alikata kiu ya Hurr na masahaba wake humo njiani pamoja na kwamba walikuwa maadui. Kwa hakika Hurr alikumbuka tukio hili. Alikuwa akifikiri ni nani ambaye wamemzuia asipate maji? Ni yeye ndiye aliyewaona kuwa wana kiu na kukata kiu yao hata kabla ya kuyaomba. Hurr alishangaa, "Jinsi gani Husain alivyo mkuu na mtukufu na jinsi sisi tulivyo waovu na duni hivi." Kwa hiyo, akasema: "Enyi watu wa Kufa! Hivi hamuoni haya kwamba maji yanayobubujika kwenye mto Furati yanapaswa kupatikana kwa kila kiumbe pamoja na binadamu, wanyama wa kufugwa, wanyama-pori lakini kwamba nyinyi mnamzuia mtoto wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu asipate huduma hiyo?"

## IMAM HUSAIN (A.S.) AMWENDEA HURR WAKATI WA MWISHO WA UHAI WAKE

Hatimaye, mtu huyu jasiri alipigana na akauawa kishahidi baada ya kushangiliwa kwa ujasiri wake. Imam Husain (a.s.) hakumuacha Hurr aondoke duniani bila ya yeye kumzawadia. Mkuu wa Mashahidi kwa haraka alifika pale alipokuwa Hurr na akakiweka kichwa chake kwenye paja lake lililobarikiwa na akasema: "Ni zuri lilioje hili Hurr, Hurr ar- Riyahi!"[158] Maana yake ni kwamba, ni jina la ajabu ya kipekee kiasi gani ambalo mama yake alimchagulia. Mama yake alimuita Hurr ('huru') mnamo siku ya kwanza, na

[158] Luhuuf, uk.103; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 13; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 437; *Maqtal-e-Husain, Muqarram,* uk. 236

Hurr kwa kweli alikuwa ni mtu huru hasa.

Imam Husain (a.s.) ni mtukufu jinsi gani! Alielezea wasiwasi wake kuhusu masahaba wake kadiri alivyoweza na akawashughulikia. Huku ndio 'Kuamrisha mema' na 'Kukataza Maovu' kwa uhalisi. Kila sahaba aliyetembelewa na Imam Husain (a.s.) katika wasaa wake wa mwisho alikuwa katika hali tofauti. Baadhi yao walikuwa hai Imam Husain (a.s.) alipowatembelea na waliweza hata kuzungumza na Kiongozi wao ambapo wengine walikwisha kufa kabla hata Imam hajawafikia pale mahali walipokuwa.

## UHAI WANGU NAUWE MUHANGA KWA AJILI YA ABBAS

Hapana sahaba katika wale waliotembelewa na Imam Husain (a.s.) alikuwa katika hali ya kuhurumiwa kama kaka mdogo wa Imam, Mtukufu Abul Fazl al-Abbas ambaye alikuwa anapendwa sana na Imam Husain (a.s.) na ambaye alikuwa mrithi wa ujasiri wa Haider-e-Karrar (Imam Ali). Imetajwa kwamba Imam Husain (a.s.) alimwambia Mtukufu Abbas: "Ewe Abbas! Mimi nitolewe kafara kwa ajili yako!" Kauli hii ni ya maana muhimu sana.[159]

Mtukufu Abbas alikuwa takriban miaka 23 nyuma ya umri na Imam Husain (a.s.). Imam Husain alikuwa na umri wa miaka 57 na Mtukufu Abbas alikuwa na umri wa miaka 34. Imam Husain (a.s.) alikuwa kama baba kwa Mtukufu Abbas ukilinganishwa umri wao na bado alisema: "Ewe Abbas mimi nitolewe kafara kwa ajili yako!"

## IMAM AUENDEA MWEZI WA BANI HASHIM

Imam Husain (a.s.) alikuwa anangojea karibu na hema. Ghafla akasikia mngurumo wa sauti ya Mtukufu Abbas. (Imerekodiwa kwamba uso wa Mtukufu Abbas ulikuwa unapendeza sana hivyo kwamba aliitwa Mwezi wa Bani Hashim.[160] Mtukufu Abbas alikuwa mrefu sana hivyo kwamba imeandikwa kwenye baadhi ya vitabu kwamba alikuwa akipanda farasi mwenye nguvu na alipoingiza miguu yake ndani ya kikuku cha farasi, vidole vyake

[159] *Irsahad*, Shakh Mufid, uk. 230; *Maqtal-e-Husain Muqarram*, uk. 210

[160] *Biharul Anwar*,Juz. 45, uk. 39; *Muntahaiul Amaal*, uk. 687

vya miguuni viligusa ardhi.[161]

Ningependa kutaja kauli ya Shaykh Muhammad Baqir Birjandi ambayo licha ya kwamba imekuzwa, inaonyesha kwamba Mtukufu Abbas alikuwa kijana mrefu. Alikuwa na sura ya kupendeza sana hivyo kwamba Imam Husain (a.s.) alikuwa akifurahia kumwangalia.

Imam Husain (a.s.) alipomfikia kijana huyu katika dakika zake za mwisho, aliona kwamba mikono yake yote ilikuwa imekatwa. Alipigwa kichwani kwa rungu la chuma na jicho lake lilitobolewa kwa mshale. Haikusemwa kimakosa kuhusu Imam Husein (a.s.) kwamba Mtukufu Abbas alipouawa kishahidi, ilionekana kwamba uso mtukufu wa Imam Husain (a.s.) pia ulisinyaa.[162]

Imam Husain (a.s.) yeye mwenyewe alisema: "Ndugu yangu Abbas! Baada ya kifo chako cha kishahidi mgongo wangu umevunjika na dhamira yangu thabiti imepungua."[163]

---

[161] *Biharul Anwar*, Juz. uk.39; *Al-Abbas Muqarram*, uk. 76

[162] *Qissa Karbala*, uk. 351; imesimuliwa kutoka kwenye *Zariat al-Najah*, uk. 125

[163] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 41

# MAJILISI 23

## IMAM HUSAIN (A.S.) ANAOMBA MUDA WA SIKU MOJA MNAMO MKESHA WA ASHURA

Mnamo '*Tasua*' yaani tarehe 9 ya Muharram wakati wa alasiri (mwishoni mwa wakati wa mchana), majeshi ya Umar bin Saad yalianza mashambulizi kama alivyoamuru Ibn Ziyad. Walitaka vita vianze siku hiyo. Imam Husain (a.s.) alimtuma kaka yake, Abbas kwao pamoja na ujumbe wa kuomba kuahirishwa kwa usiku ule mmoja tu.

Imam Husain (a.s.) alisema: "Ndugu yangu mpendwa! Waombe kuahirisha kwa usiku huu mmoja tu." Halafu ili kuondoa kutokueleweka kwamba alikuwa anatengeneza ucheleweshaji usio wa lazima, Imam Husain (a.s.) aliongeza akasema: "Ndugu yangu! Allah anajua vema zaidi jinsi ninavyopenda kumuomba Yeye. Ninataka kutumia usiku huu katika kuomba dua ili kwamba uweze kuwa ni usiku wa toba kwa ajili yetu."

### MKESHA WA ASHURA ULIKUWA KAMA ULE MKESHA WA MIRAJI KWA WAFUASI

Lakini wapi! Kama tunaweza tu kujua jinsi mkesha wa Ashura ulivyokuwa mkubwa! Hakika, ulikuwa usiku wa Miraji. Ulikuwa ni usiku uliojaa shangwe furaha na bashasha. Katika usiku huo, mashahidi wa Karbala walijitakasa sana. Mnamo usiku huo walipamba kila sehemu ya maisha yao. Hema ilikuwa ndio sehemu ya shughuli ya kupambia maisha yao.

Wote walikuwa ndani ya hema. Watu wawili tu ndio walikuwa nje, wakilinda hema hilo kwa zamu. Kwa dhahiri kabisa, mmojawapo alikuwa Burair Hamadani.[164] Huenda Buraira alifanya maskhara na masahaba wake ambao walimwambia kwamba usiku huo haukuwa usiku wa burudani. Burair akajibu: "Kimsingi, mimi sitokani na watu wachekeshaji lakini usiku wa leo ni usiku wa burudani kwa ajili yetu."

[164] Inasimuliwa kwamba Buraira alikuwa akizungumza kicheshi na Abdur Rahman Ansari. *Maqtal-e-Husain, Muqarram*, uk. 216

## MVUMO WA SAUTI ZA WAFUASI

Adui alipowaona wamejishughulisha sana na toba, unajua walisema nini? Walipopita karibu na kambi ya Imam Husain (a.s.) walisema: "Wanasikika kama mvumo wa nyuki kwenye sega la asali."[165] Sauti za Imam Husain (a.s.) na masahaba wake za kuomba maghfira, kuswali na kuomba dua zilikuwa za juu sana (hivyo kwamba palitokea ghasia katika safu za malaika).

Imam Husain (a.s.) alikwishasema:

"Nataka usiku wa leo kuwa usiku wa toba yetu na kuomba maghfira." Ningeweza kusema kwamba alitaka usiku huo kuwa usiku wa kupaa kwake (Miraji). Kauli hii ya Imam (a.s.) inastahili kufanyiwa tafakuri. Baada ya tamko hili, tunaweza kusema kwamba hakuna haja ya sisi kutubia? Hivi Imam alikuwa anahitaji kutubu na sisi tusihitaji kutubu? Imam Husain (a.s.) alitumia usiku wote wa Ashura katika kumtukuza na kumuabudu Mwenyezi Mungu na kuendelea kukagua hali ya watu wa familia yake. Ulikuwa pia ni usiku ambapo Imam Husain (a.s.) alitoa hotuba isiyosahaulika kwa masahaba wake.

## TOBA IMEKUBALIWA

Enyi waombolezaji!

"Hapa nitazungumzia kuhusu muombaji toba wa jangwa la Karbala na kuhitimisha mhadhara wangu kwa hilo. Mojawapo ya toba hapo Karbala alikuwa muhimu sana, nayo ilikuwa ni toba ya Hurr bin Yazid Riyahi.

Hurr alikuwa mtu jasiri kupindukia. Pale Ubaidullah Ibn Ziyad alipopeleka kikosi cha  kwanza cha jeshi lake dhidi ya Imam Husain (a.s.), alimfanya Hurr kuwa kamanda wa wapiganaji wapanda farasi elfu moja. Hurr huyu alikwisha wafanyia Ahlul-Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mateso na uovu. Nilikwisha sema katika mojawapo ya hotuba zangu kwamba mtu akifanya uhalifu mkubwa na kama dhamiri yake iko hai, kwa kweli humlazimisha kufanya marekebisho. Kwa hiyo, nyinyi wasikilizaji mnapaswa kukadiria athari ya dhamiri ya mtu ambaye alifanya uhalifu dhidi ya wale ambao roho zao zilikuwa katika daraja la juu kabisa.

[165] *Luhuuf*, uk. 94

## HURR ALIKUWA NA DHAMIRI ILIYO HAI

Msimuliaji anasema kwamba alimuona Hurr kwenye jeshi la Ibn Saad akitetemeka kwa hofu. Alikwenda mbele na akasema: "Ewe Hurr! Nilikuwa nikikuona wewe kuwa mtu jasiri sana. Kama ningeulizwa ni nani aliye jasiri sana hapa Kufa, nisingetamka jina la mtu mwingine isipokuwa jina lako. Lakini sasa hivi kwa nini unatetemeka sana?"

Hurr akajibu: "Umeelewa sivyo. Mimi sihofii uhai wangu katika vita hivi. Kwa kweli, nimejikuta ninasimama katika njia panda. Njia moja inaongoza kwenda Peponi na nyingine inaongoza kwenda Jahanamu. Ninashindwa kuamua nielekee wapi na nichague njia ipi." Hatimaye Hurr alichagua njia ya wokovu na akaanza kumsogeza kipando wake polepole kwenye njia hiyo. Alikwenda kwa namna ambayo hakuna mtu ambaye angetambua alikuwa anataka kufanya nini. Alipofika mahali ambapo alikuwa na uhakika kwamba hakuna mtu ambaye angeweza kuzuia njia yake, alimuongeza kasi farasi wake na akaenda shoti haraka sana kuelekea kambi ya Imam Husain (a.s.).

Inasimuliwa kwamba aligeuza ngao yake kuonyesha ishara kwamba yeye hakuwa akienda kule kupigana bali kujisalimisha. Alifika kwa mtukufu Imam (a.s.), akamsalimia na akasema: "Ewe mwana wa Mtume! Inawezekana toba ya mtenda dhambi huyu kukubaliwa?" Imam Husain (a.s.) akajibu: "Kwa nini isiwezekane? Kwa hakika toba yako itakubaliwa."[166]

## HURUMA NA UPOLE WA HUSAIN

Enyi waombolezaji! Tazameni huruma na upole wa mtoto mwenye huruma wa Imam mwenye huruma. Hakusema : "Hii ni toba ya aina gani? Sasa ni vipi umetuleta kwenye hatari ya aina hii, hivi umekuja kutubu?" Ilikuwa hivyo kwa sababu Imam (a.s.) hakuwa na fikra kama hiyo. Mara zote yeye amekuwa akiwaongoza watu. Kama jeshi la Ibn Saad lingetubu baada ya kuwaua vijana wake wote, basi na yeye pia angesema :"Ninakubali toba yenu wote." Kwa sababu Yazid alipomuomba Imam Sajjad (a.s.) baada ya msiba wa Karbala. "Hivi toba yangu itakubaliwa, kama nikitubu sasa?" Imam alijibu, "Ndio kama ukitubu kwa dhamiri safi, toba yako itakubaliwa." Hata hivyo, Yazid hakutubu wakati huo.[167]

[166] Luhuuf, uk. 103; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk 438

[167] Shaykh Saduuq (a.r.) amesimulia hadithi kutoka kwa Imam Ridha (a.s.) kupitia kwa vyanzo vya kuaminika vitatu kwenye *Uyun Akhbaar al-Ridha*, Juz. 2, uk. 47 kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kwamba

Hurr akasema, “Kiongozi wangu! Niruhusu niende kwenye uwanja wa vita na nijitoe mhanga juu yako.”

Imam akasema: “Hurr! Wewe ni mgeni wangu. Shuka kwenye farasi wako na uketi hapa na mimi kwa muda kiasi.” Hata hivyo, Hurr alisisitiza tena na tena kuomba amruhusu kwenda.

Hurr alikuwa anaona haya sana kuendelea kuwa hai. Kwa nini? Kwa sababu alikuwa akikumbuka kwamba ni yeye ndiye aliyewatishia vipenzi wa Mola kwa mara ya kwanza na aliwaogopesha dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).[168]

Kwa nini (Hurr) hakutaka kuketi karibu na Imam Husain (a.s.)? Kwa sababu aliogopa kwamba wakati ameketi karibu na Sayyid huyo, mtoto mdogo mwenye kiu angetokeza na kumuona, tukio ambalo lingemfanya yeye afe kwa soni.

---

Nabii Musa aliomba kwa Allah, Ee Mola! Ndugu yangu Haruna amekufa. Nakuomba umsamehe.” Hatimaye Allah aliteremsha wahyi unaosema: Ewe Musa! Ningekubali toba yako kwa ajili ya mtu yeyote kutoka mwanzo hadi mwisho isipokuwa ya wauaji wa Husain bin Ali (a.s.) kwa sababu nitalipiza kisasi kwao kwa ajili ya kifo cha kishahidi cha Husain.” Allamah Majlisi amesimulia hadithi kwenye *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 308 kwamba mtu mmoja kutoka Bani Israel alimuona Nabii Musa (a.s.) akiwa anakwenda mahali kwa haraka. Alionekana amesawajika, akitetemeka na macho yake yalikuwa dhaifu. Mtu yule alielewa kwamba alikuwa anakwenda kuomba dua. Mtu yule akauliza: “Ewe Mtume wa Allah! Mimi nimefanya dhambi kubwa. Nakuomba uniombee msamaha kwa Allah.” Hivyo, Nabii Musa (a.s.) alipokuwa anaomba msamaha kwa ajili yake na akasema: ”Ee Mola! Unajua ninachotaka kusema kwamba mja wako fulani ametenda dhambi na anaomba msamaha kutoka Kwako.” Allah akajibu: “Ningemsamehe yeyote anayeomba msamaha kutoka Kwangu isipokuwa wale wauwaji wa Husain.....” Imeandikwa kwenye *Damaatus Sakiba*, Juz. 5, uk. 194-195 kwamba Yazid bin Muawiyah alipokutana na Imam Sajjad (a.s.) alijaribu kumbambikiza Ibn Ziyad uhusikanaji na uhalifu wake wote na yeye mwenyewe akajitoa kabisa.

[168] *Luhuuf*, uk. 103; *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 235; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk.13; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 437; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 236

# MAJILISI 24

## ZUHAIR BIN QAYN

**Waombolezaji wa Imam anayedhulumiwa!**

Jana nilizungumzia kuhusu toba ya Hurr. Leo mtasikia kuhusu sahaba mwingine wa mtukufu Imam (a.s.), Zuhair bin Qayn kwa sababu yeye pia anafikiriwa kuwa miongoni mwa watu waliotubia. Hata hivyo, toba yake ilikuwa tofauti. Alikuwa anamuunga mkono Uthman bin Affan. Alikuwa miongoni mwa watu waliofikiri kwamba Imam Ali (a.s.) alihusika na mauaji ya Uthman. Kwa hiyo, yeye alikuwa hana fikra nzuri kuhusu Imam Ali (a.s.).

Wakati wowote Imam Husain (a.s.) alipokabiliana ana kwa ana na adui aliye kaidi, alikuwa akionyesha hali ya kujiamini ya jinsi ambayo hapana nguvu ambayo ingeweza kupunguza heshima yake; weka pembeni fursa ya kuinamisha kichwa chake chini. Mara nyingi Imam (a.s.) alikuwa katika hali kama hiyo pale ambapo ilikuwa muhimu kuwaongoza baadhi ya watu; katika hali kama hizo alikuwa hata hajali uzembe wa watu hao.

Zuhair alikuwa anarudi na msafara wake kutoka Makkah akielekea Iraq na Imam Husain (a.s.) pia alikuwa anasafiri kwenye njia ile ile kwenda Iraq. Zuhair alikuwa anajaribu kwa vyovyote vile kutokukutana uso kwa uso na Imam Husain (a.s.). Kila alipoona msafara wa Imam Husain (a.s.) unakaribia msafara wake, alikuwa akiuondoa msafara wake. Imam alijua kwamba Zuhair alikuwa anamkwepa kwa sababu alikuwa hafahamu ukweli wa mambo. Licha ya hili, Imam (a.s.) alitaka kumkumbusha yeye (Zuhair) kuhusu jambo fulani kwa sababu Allah Muweza wa Yote amesema: **(Basi kumbusha, hakika wewe ni mkumbushaji tu 88:21)** Imam (a.s.) alitaka kumuondoa Zuhair kwenye ujinga; hakutaka kumlazimisha. Pamoja na kwamba Zuhair hakuwa anamjali Imam, lakini Imam (a.s.) alitaka kumuongoza yeye kwa sababu moyo wake ulijaa nuru ya imani.

Zuhair alikuwa anajua kwamba Imam alikuwa mtoto wa kipenzi cha Allah Mwenyezi; na haki yake ilikuwa ipi kwa umma. Alikuwa akiogopa kwamba

kama angekutana na Imam, angeweza kutakiwa jambo ambalo asingeweza kulitimiza; na ingekuwa dosari kubwa.

Kwenye kituo kimoja, ingawa ilikuwa kinyume kabisa na matakwa yake, Zuhair alisimamisha msafara wake karibu na Imam. Imam Husain (a.s.) alikwisha simama hapo na kwa hiyo, misafara yote miwili ilisimama kwenye kisima kile kile. Imam (a.s.) alimtuma mjumbe kwenda kumuita Zuhair. Wakati huo Zuhair na masahaba wake walikuwa wanakula chakula ndani ya mojawapo ya mahema. Ghafla, pazia la hema lilinyanyuliwa na mtu akasema: "Ewe Zuhair! Husain anakuita."[169]

Zuhair aliposikia wito huu, uso wake ulisawajika na akajisemea kwa sauti ya mnong`ono, "Hili ndilo nililokuwa naliogopa." Masahaba wake pia walikuwa wanafahamu kuhusu hali yote.

Imaeandikwa kwenye vitabu kwamba Zuhair na masahaba wake waliacha kula kwa sababu Zuhair alikuwa anafahamu vema kuhusu hadhi ya Imam Husain (a.s.). Kwa hiyo, hakuweza ama kukataa wito huo wala kukubali mualiko huo kwa moyo mkunjufu. Alijua kwamba haingefaa kukataa mualiko wa Imam Husain (a.s.). Aliketi akiwa ameduwaa, kama usemi wa Kiarabu usemavyo, "Kana kwamba ndege alikuwa ametua kwenye kichwa chake. Kwa ufupi, mazingira yote yakawa ya kufadhaisha.[170]

## USHAURI WA MKE WA ZUHAIR

Mke wa Zuhair (Dalham binti Amr) alipotambua kwamba Imam Husain (a.s.) alituma mjumbe kumualika Zuhair aende kwake lakini Zuhair alikuwa hajatoa jibu, alijitokeza na akasema: "Ewe Zuhair! Kipenzi cha Fatimah anakuita na unakataa mualiko badala ya kuuchukulia mualiko huu kama heshima? Zuhair! Lazima uende kwake." Mwishowe, Zuhair alinyanyuka kwa kujikaza na alikwenda kukutana na Imam (a.s.). Wakati mwingine, wakumbushaji pia huonyesha athari zao kwa njia hii.

## MVUTO WA HARAKATI ZA HUSAIN

Sijui, yaani ni kwamba haikuandikwa kwenye kitabu chochote cha historia na huenda hakuna anayejua mazungumzo hayo yalihusu kitu gani na wali-

[169] Ewe Zuhair! Aba Abdullah al-Husain amenituma nije kukuita. *Luhuuf*, uk. 72.

[170] Tulikuwa tumeketi kimya kana kwamba tulikuwa na ndege waliotua vichwani mwetu na kwamba wangeruka kama tungetikisika. *Luhuuf*, uk. 72

hisi nini pale Zuhair alipokutana na Imam Husain (a.s.) kwa sababu uso wa Zuhair ulikuwa umesawajika alipokwenda kukutana na Imam na baada ya kukutana na Imam Zuhair alionekana na uso wa kung`aa na muonekano wa ujana.

Sijui jinsi gani Imam Husain (a.s.) alibadili fikra za Zuhair. Pia sijui Imam (a.s.) alimkumbusha kuhusu nini, lakini kwa hakika najua kwamba mapinduzi yalionekana ndani ya moyo wa Zuhair. Alibadilika kabisa. Watu waliona kwamba Zuhair hakuwa tena yule wa zamani. Aliporudi, aliamuru hema lake lihamishwe kutoka pale lilipokuwa na kupelekwa karibu na hema la Imam Husain (a.s.). "Sasa ningependa kuishi na kufa nikiwa na Aba Abdillah tu." Pia alianza kutengeneza wosia wa jinsi gani rasilimali yake ingetumika. Pia alitoa wosia kuhusu watoto wake wa kiume na wa kike. Aliamuru kwamba mke wake alipaswa apelekwe nyumbani kwa baba yake baada yake.

Zuhair alizungumza na akaaga kwa jinsi ambayo kila mtu alielewa kwamba hangerudi. Alipotoka ndani ya hema lake akiwa amejitayarisha kipiganaji, mke wake alishika sehemu ya mwisho ya joho lake na akasema huku akilia. "Zuhair! umechagua kufa kishahidi ukiwa na kipenzi cha Fatimah ili kwamba aweze kukuombea shifaa wewe katika Siku ya Hukumu. Usifanye namna ambayo itasababisha mimi na wewe tuwe tumetengana mnamo Siku ya Hukumu. Mimi ninakushikilia wewe tu nikiwa na matumaini kwamba utamuomba Bibi Zahra aniombee mnamo Siku ya Hukumu. Zuhair! Niahidi kwamba utaniombea kwa ajili ya shifaa yangu. Nataka uombezi wa Bibi Fatima kwa ajili yangu."[171]

Baada ya hapo, ni Zuhair huyu huyu ambaye anaonekana akiwa mistari ya mbele miongoni mwa safu za masahaba wa Husain (a.s.) na Imam alimpa ukamanda wa kikosi cha upande wa kulia. Hili linastajabisha kiasi gani!

## ZUHAIR SASA AWA JUU YA ORODHA YA MASAHABA WA IMAM HUSAIN (A.S.)

Zuhair alionyesha aina ya tabia hivyo kwamba pale Imam Husain (a.s.) alipoachwa peke yake mnamo siku ya Ashura na hakuna sahaba wa Imam

[171] Mke wa Zuhair alisema, "Mwenyezi Mungu ndiye msaidizi wako. Lolote litakalokutokea lina wema ndani yake. Ninatamani kwamba babu yake Husain atanikumbuka mimi pia wakati wa uombezi mnamo Siku ya Hukumu." *Luhuuf*, uk. 73; *Maqtal-e-Husain,* uk. 178; *Biharul Anwar*,Juz. 44, uk. 372

Husain (a.s.) aliyebaki, aliwaita masahaba wake na Zuhair alikuwa mmojawapo.

Imam aliyedhulumiwa alisema, "Enyi wapendwa wangu! Enyi mashujaa! Ewe Muslim bin Aqiil! Ewe Hani bin Urwah! Ewe Zuhair! Kwa nini mmelala? Amkeni mkalinde utakatifu wa Mtume wenu kutokana na wale wasaliti wasio na soni."[172]

Vita ilipokwisha, mke wa Zuhair alikuwa na wasiwasi. Alifikiria kwamba maiti za wengine zingevishwa sanda na ile ya Zuhair ingelala bila kuvishwa sanda. Baada ya kufikiria hivi, alimtuma mtumwa wake akiwa amemuamuru kumvisha sanda bwana wake. Mtumwa alipofika pale zilipokuwa maiti za mashahidi, aliona maiti zote hazikuvishwa sanda na aliona aibu sana. Mtumwa huyo hakuweza kustahimilia kuivisha sanda maiti ya Zuhair na akaondoka akimuacha bwana wake Husain akiwa hakuvishwa sanda.[173]

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**"Na punde watajua waliodhulumu ni mgeuko gani watakaogeuka?"[174]**

**[Sura Ash-Shu'araa 26 : 227]**

[172] Imam Husain alitazama pande zote na akaona kwamba masahaba wake wote wameuawa kishahidi. Kaka zake na watoto wake walikuwa wamelala chini ardhini wakiwa wametapakaa damu yao. Imam (a.s.) aliita kwa sauti ya juu, "Ewe Muslim bin Aqiil! Ewe Hani bin Urwah! Ewe Habib bin Mazahir na Ewe Zuhair bin Qayn! Enyi masahaba wangu wa kweli na jasiri! Enyi wale mliopigana sambamba na mimi! Enyi vijana waaminifu na mnaoheshimiwa! Amkeni kutoka usingizini ili muiokoe familia ya Mtukufu Mtume wenu kutokana na wale wasaliti katili." *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 484

[173] *Luhuuf*, uk. 71; *Maqtal-e-Husain*, uk. 177; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 342; *Tarikh-e-Ashura*, uk. 198 kilichochapishwa na Taalimaat-e-Islami, Pakistan

[174] **Sura Ash-Shu'araa [26:227].**

# MAJILISI 25

## KIFO CHA KISHAHIDI CHA JAUN BIN ABI MALIK

Enyi waombolezaji!

Imam Husain alifika na akawaona masahaba fulani wakiwa kwenye dakika zao za mwisho wa uhai wao au baada ya kufa kishahidi kwenye vita vya Karbala. Miongoni mwao, ni uhakika kuhusu masahaba wawili kwamba walikuwa watumwa walioachiwa huru. Walinunuliwa na baadaye wakakombolewa. Mmojawapo alikuwa mtumwa mwenye asili ya Kirumi na mwingine Jaun, wa asili ya Uhabeshi, ambaye aliachiwa huru na Mtukufu, Abu Dharr Ghaffari.

Ni dhahiri kwamba hakuondoka kwa Ahlul-Bayt hata baada ya kuachiwa huru na aliendelea kuhudumia familia ya Mtume.

Katika siku ya Ashura Jaun alikwenda kwa Imam Husain (a.s.) na akasema, “Bwana, tafadhali nakuomba uniruhusu na mimi pia kwenda kwenye uwanja wa vita.” Imam akasema: “Hapana, si wakati wako huu kuiacha dunia hii. Wewe unapaswa kuendelea kuwa hai baada ya vita hivi pia. Huduma yoyote uliyotoa kwa familia yetu inatosha. Sisi tuna radhi na wewe.” Jaun alisisitiza tena lakini Imam alikataa kuruhusu. Mwishowe, alianguka miguuni kwa Imam, akaibusu miguu yake na akasema, “Bwana! Usininyime mimi kifo cha kishahidi.” Baada ya hapo, Jaun alisema maneno ambayo yalimfanya Imam asimkataze tena.

### IMAM HUSAIN (A.S.) AMWENDEA MTUMWA WA KI-HABESHI

Jaun akasema: “Bwana! Ninajua kwa nini unanikataza. Ni hivyo kwa sababu mimi ni mtu duni hivyo kwamba sistahili heshima hii.Nitapataje daraja la kifo cha kishahidi na ngozi nyeusi, damu iliyo chafu na mwili unaonuka?”

Imam (a.s.) alijibu, "Hapana Jaun, si hivyo. Sababu ya kutokukuruhusu wewe sio hiyo uliyodhania wewe. Endapo kweli unataka kwenda, basi haya unaweza kwenda." Jaun alitabasamu sana baada ya kusikia hivyo. Alianza kurukaruka kwa furaha, alighani shairi la vita na akaondoka kwenda kwenye uwanja wa vita kwa furaha. Alipigana kwa ujasiri na akatoa maisha yake mhanga kwa ajili ya bwana wake.

Imam Husain (a.s.) alikuwa anafuatilia kwa kuangalia mapigano ya Jaun. Jaun alipoanguka kutoka kwenye farasi wake, kwa haraka Imam Husain (a.s.) alifika pale alipokuwa Jaun na akaketi karibu na kichwa chake. Akamuomba Mola: "Ee Mola! Ung`arishe uso wake hapa duniani na Akhera. Badilisha harufu ya mwili wake kuwa harufu nzuri na ya kuvutia na umfufue pamoja na watu watakatifu (Lazima ikumbukwe kwamba daraja la watu watakatifu ni la juu zaidi ya lile la watu wacha-Mungu).[175] "Ee Mola! Dumisha urafiki baina yake na dhuria wa Muhammad huko Akhera."[176]

## KIFO CHA KISHAHIDI CHA MTUMWA WA KIRUMI

Palikuwepo na mtumwa mwingine hapo Karbala, na alikuwa Mrumi naye pia aliuawa kishahidi akiwa kwenye kundi la Imam Husain (a.s.). Alipoanguka kutoka kwenye farasi wake na Imam Husain (a.s.) akafika karibu naye, kitu cha ajabu kilitokea.

Ama mtumwa huyu alikuwa amepoteza fahamu au macho yake yalijaa damu. Inasimuliwa kwamba Imam Husain (a.s.) alikiweka kichwa chake kwenye paja lake na akafuta damu kutoka kwenye uso wake na macho yake. Ghafla mtumwa huyu alipata fahamu. Aliutazama uso mtukufu wa Imam Husain (a.s.) na akatabasamu.

Imam (a.s.) aliweka shavu lake juu ya shavu la mtumwa huyo. Ni tendo hili la kihisia ambalo Imam alilitwaa na kulitumia kwa mtumwa huyu tu na mwanae, Ali Akbar. Tendo la kihisia kama hili hailijasimuliwa kuhusishwa na mwingine yeyote; yaani kwamba; "aliweka shavu lake juu ya shavu lake." Alipoona kitendo hiki cha upendo, mtumwa huyo alifurahi kupita kiasi. Yeye alitabasamu tu na akaendelea na safari kwenda kukutana na Mola Wake.[177]

[175] **Sura Mutaffifin 83:18**

[176] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 22; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 252; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 667

[177] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 30; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 669; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 457

"(Kiongozi wangu!) Kama ukija karibu na kichwa changu kama daktari sitaachilia ile hali ya ladha ya ugonjwa hata kama ni kubadilishana na dunia zote, hii na ya akhera.

Kichwa cha mtumwa kilikuwa kwenye paja la Imam pale ambapo roho yake ilipaa na kuondoka kwenye kizimba cha mwili."

# MAJILISI 26

## WANAWAKE WALIOMSAIDIA IMAM HUSAIN (A.S.)

Vipengele vyote vya Uislamu, viwe vya kimaumbile, kijamii au vinavyohusiana na imani ya Mungu mmoja tu, kutambua dini na hali ya kiimani au migogoro, vyote vinaonekana kukamilika. Kwenye msiba wa Karbala waliotoa mchango ni pamoja na mtoto mchanga anayenyonya na mtu mzima wa miaka sabini au themanini na wanawake. Mke wa Abdullah bin Umair Kalbi (Ummu Wahab) alikuwa mmojawapo wa wale watu wazima. Watu watatu walikwenda Karbala wakifuatana na wake zao na watoto wao kumsaidia Imam Husain (a.s.). Baada ya kuuliwa kishahidi kwa watu hawa watatu, familia zao zilibaki na familia ya Imam Husain (a.s.). Masahaba wengine hawakufuatana na wake na watoto wao. Watu watatu hawa ambao walifuatana na wake zao na watoto wao hadi Karbala walikuwa Muslim bin Awsaja, Abdullah bin Umair Kalbi na Junada bin Harth Ansari.

### NICHUKUE PAMOJA NAWE

Abdullah bin Umair alikuwa miongoni mwa masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alikuwa ameshiriki kwenye vita vya Kislamu. Inasemekana kwamba hakuwepo Kufa siku hizo. Alipopata habari za kuvurugika kwa mambo ya Kufa, kwamba kuna jeshi lililokuwa linatayarishwa kupigana dhidi ya Imam Husain (a.s.), alijiambia mwenyewe, "Wallahi, mimi nilipigana dhidi ya makafiri kwa miaka mingi kwa ajili ya Uislamu. Hata hivyo jihadi ile haiwezi kuwa sawa kwa daraja na jihadi hii ambapo ninapata fursa ya kuwalinda watu wa nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alifika nyumbani kwake na akamwambia mke wake kuhusu uamuzi wake. Mke wake akasema: "Mwenyezi Mungu na akulipe thawabu! Umefanya uamuzi mkubwa, lakini mimi ninaweka sharti kuhusu uamuzi wako huo." Aliuliza sharti hilo lilikuwa ni lipi. Mke wake akajibu: "Unapaswa unichukue twende wote." Kwa hiyo, akamchukua mke wake na mama yake vilevile. Hebu tazama mtu

kufanya kitendo kikubwa kama hiki! Wanawake hawa walikuwa mashuhuri kiasi gani!

Abdullah bin Umair alikuwa mpiganaji jasiri. Alipigana na watumwa wa Umar bin Sa'd na Ibn Ziyad ambao walikuwa wanatafuta mtu wa sawa na wao na walikuwa ni watu wenye nguvu sana. Yeye akawaua wote wawili na kuwapeleka Jahannam.

Imesimuliwa kwamba watumwa hao walipokuwa wanatafuta watu wa kulingana nao kijasiri, macho ya kuchagua ya Imam Husain (a.s.) yalitazama mwili na mikono ya Abdullah bin Umair na Imam akamteua yeye. Akasema: "Wewe ndiye mtu wa kupigana na hawa wawili." Kwa hiyo, alikwenda kwenye uwanja wa vita na akawa mshindani anayefaa kwa wote wawili.

Kwanza, mtumwa wa Umar bin Saad, aliyeitwa Yasar alijitokeza mbele. Abdullah bin Umair alimshinda kwa pigo moja tu. Hata hivyo, kabla ya hapo, mtu mmoja alimshambulia Umair kutokea upande wa nyuma. Masahaba wa Imam walipiga ukelele wa kumtahadharisha lakini kabla hajajiweka sawa, alishambuliwa vikali kwa upanga ambapo mkono wake ulikatwa sehemu ya kifundo. Hata hivyo, mtu huyu jasiri (Abdullah bin Umair) alimuua adui yake huyu kwa mkono wake mwingine.[178]

Yeye (Abdullah bin Umair) alikwenda kwa Imam Husain (a.s.) akiwa katika hali hiyo huku akighani shairi la vita na akamuuliza mama yake, "Ewe mama yangu, je umefurahi sasa?" Mama yake akajibu, "Nisingefurahishwa na wewe hadi hapo utakapojitoa mhanga kwa ajili ya kipenzi cha Fatimah."

Mkewe Abdullah alikuwepo pia. Alimkumbatia mumewe. Mama yake akasema: "Tahadhari, usijali kile anachosema mkeo. Huu sio muda wa kumsikiliza mkeo. Kama unataka mimi niwe radhi na wewe, huna njia nyingine kwa ajili yako, isipokuwa kufa kishahidi.

Mtu huyu wa miraba minne alikwenda kwenye uwanja wa vita tena na mwishowe aliuawa kishahidi. Maadui walimkata kichwa chake na kukitupa kuelekea upande wa mahema ya watu wa familia ya Husain (vichwa vilivyokatwa vya baadhi ya mashahidi vilitupwa kuelekea kwenye kambi ya Husain na kile cha Abdullah bin Umair kilikuwa kimojawapo).

[178] *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 433 (mada hiyo inahusishwa kwa sahaba wa Mtukufu Mtume, Abdullah bin Umair Kalbi hadi hapa. Baada ya hili, inahusishwa na Wahab bin Abdullah bin Habbab Kalbi ambaye alikuwa mdogo kwa umri.) – Rizwani.

Mama wa shahidi huyu ambaye alikuwa mkongwe alikiinua kichwa cha mwanawe, akakikandamiza kifuani mwake, akakibusu na akasema:

"Ewe kipenzi changu! Sasa nimekuridhia wewe. Umetimiza wajibu wako." Halafu akakitupa kichwa hicho kuelekea upande wa adui, akisema, "Huwa hatuchukui chochote kile ambacho tumekitoa katika njia ya Allah."

Baadaye, mama yake Abdullah bin Umair ambaye alikuwa anawapenda sana Ahlul-Bayt, aliinua nguzo ya hema na akawashambulia maadui waovu akisema:

**"Pamoja na kwamba mimi ni mwanamke kikongwe na aliye dhaifu nipo tayari kuilinda familia ya Fatimah almuradi bado zipo nguvu kwenye mifupa yangu iliyozeeka."[179]**

***Kwa jina la Allah na kwa Allahi na juu ya dini ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.).***

[179] Beti hizi hazikughaniwa na mama yake Abdullah bin Umair Kalbi. Badala yake zilitajwa na yule mama wa yule mtoto ambaye habari kuhusu yeye zimeandikwa kwamba alikuwa kijana ambaye baba yake aliuawa kwenye shambulio hilo. *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 28; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 458

# MAJILISI 27

## KIFO CHA KISHAHIDI CHA AMR BIN QARZA BIN KAAB ANSARI

Amr bin Qarza bin Kaab alitokana na kizazi cha ki-Ansari cha Madina. Alikuwepo Karbala pamoja na Imam Husain (a.s.) hadi alasiri ya siku ya Ashura. Huyu alikuwa miongoni mwa wale waliounda ngao ya binadamu watupu kwa lengo la kumlinda Imam Husain (a.s.) wakati alipokuwa anaswali swala ya Adhuhuri.

Amr aliizuia mishale kwa kifua chake huku Imam akiendela kuswali. Alipigwa mishale mingi sana hivyo kwamba alishindwa kuhimili maumivu ya majeraha na akanguka chini. Imam Husain (a.s.) alipokwenda kumuona baada ya Swala hiyo, alikuwa katika dakika zake za mwisho za uhai wake. Alikuwa akifikiria kama amekwisha timiza wajibu wake au hapana. Imam Husain (a.s.) alipofika karibu na kichwa chake, alimuuliza Imam kitu kimoja tu, "Ewe Aba Abdillah! Hivi nimetimiza haki yangu ya utiifu?"[180]

180 Imeandikwa kwenye *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 248, "Ewe mwana wa Mtume! Hivi nimetimiza wajibu wangu?"

# MAJILISI 28

## SHAHIDI KIJANA

Enyi waombolezaji!

Kwenye vita ya Karbala ambapo vijana na wazee, wote waliandika hadithi za ushujaa, watoto nao hawakukosekana. Inasimuliwa kwamba watoto tisa au kumi walijitoa mhanga kwa ajili ya kipenzi cha Fatimah kwenye vita hivi. Inasimuliwa kwamba mtoto mmoja ambaye baba yake aliuawa kishahidi muda mchache tu, alijitokeza mbele kwa shauku ya Jihadi.[181] (Hatujui mtoto huyo alikuwa nani au kwamba ni mtoto nani ).[182] Mtoto huyu aliibusu miguu ya Imam Husain kisha akasema: Bwana! "Tafadhali niruhusu niende kwenye uwanja wa vita." Imam alimtazama na akasema: "Hapana, hautakwenda. Kifo cha kishahidi cha baba yako kinatosha. Huenda mama yako hatafurahi kama ukienda."

Baada ya kusikia haya, mtoto alijibu: "Ewe Aba Abdallah! Ukweli ni kwamba upanga unaouona unaning`inia kiunoni mwangu unafungwa na mama yangu tu. Ameniambia niende kuyatoa maisha yangu mhanga, kama alivyofanya baba yangu, kwa ajili ya Imam ." Mtoto alisisitiza sana hivyo kwamba Imam Husain (a.s.) alimruhusu aende.

Kwa nini isiweze kujulikana kama alikuwa mtoto wa Muslim bin Awsaja au Harth bin Junada Ansari? Ni hawa watu wawili tu ndio waliochukua familia zao na kufuatana nazo huko Karbala. Ingawaje Abdullah bin Umair pia alifuatana na familia yake huko Karbala, ni ukweli unaojulikana kwamba mtoto huyu hakuwa wa kwake.

Mtoto huyu alipokwenda kwenye uwanja wa vita, tofauti na wengine ambao walijitambulisha kwa kutumia jina la baba yake au jina la babu yake na ambao walighani shairi la vita: "Mimi ni fulani mtoto wa fulani bin fulani," yeye alijitambulisha kwa njia tofauti kabisa. Kupitia njia hiyo aliyojitambul-

[181] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 27; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 253 na *Mausat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 457

[182] Muqarram ameandika kwamba mtoto huyo wa miaka kumi na moja alikuwa Amr. Baba yake alikuwa Junada Ansari ambaye aliuawa kishahidi katika shambulio la kwanza.

ishia alipata hadhi ya pekee. Alipofika kwenye uwanja wa vita alisema kwa sauti ya kupaza:

"Bwana wangu Husain; ni bwana mzuri alioje. Yeye ni kipenzi cha Mjumbe ambaye alikuwa Bashira (mtoa habari njema) na Nadhiira (muonyaji)."[183]

[183] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 27; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 253; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk.457

# MAJILISI 29

## UJUMBE WA HUSAIN ULIPENYA NA KUZIENEA NYOYO

"Enyi wapendwa!

Imeandikwa kwamba wafalme na watu wengi ambao walitaka kuwa mashuhuri walitengeneza kipande cha chuma na kuandika humo jina lake na mlolongo wa ukoo wake. Maandishi hayo yalijumuisha majina ya watu walioinama mbele yao ikiwa ni ishara ya utiifu kwao. Kwa nini ujumbe huu uliandikwa kwenye vipande vya chuma maelfu ya miaka iliyopita? Kitendo hicho kilifanywa ili majina yao yasisahaulike. Ishara hizi zilibaki zimezikwa chini ya tani nyingi za mchanga na hakuna mtu aliyekuwa anajua habari zao hadi hapo ambapo watafiti wa jeolojia wa Ulaya walizifukua. Chochote kilichoondolewa hakina umuhimu. Hakuna chochote mahsusi kuhusu kitu hicho. Vivyo hivyo, hapana mtu anayejali ujumbe ulioandikwa kwenye vitabu. Watu hawafikirii kuwa ujumbe huo una umuhimu na hawavutiwi nao kwa sababu ujumbe huu umeandikwa kwenye vipande vya chuma na mawe na si kwenye nyoyo. Imam Husain (a.s.) hakuandika ujumbe wake kwenye mawe. Badala yake chochote alichosema kilitiririka kwenye mawimbi ya hewa, kikafika kwenye masikio ya wanadamu na kikaandikwa kwenye nyoyo zao kwa namna ambayo si rahisi kufutika. Kama mshairi Josh amesema:

'Mwanadamu naazindukane angalau'

Kila umma utatangaza, Husain ni wetu:

Imam (a.s.) mwenyewe alikuwa anatambua vyema juu ya jambao hili. Aliutabiri wakati ujao kwa usahihi kabisa kwamba baada ya siku hii Husain huyu hatauawa tena. Jina lake halitaweza kufutika kwa vyovyote vile mtu atakavyojaribu kulifuta na Husain ataishi milele. Tafadhali tafakari kuhusu hili. Inawezekana hili kuwa ni sadifa tu? Hapana, sivyo kabisa!

# WITO WA IMAM HUSAIN (A.S.) KWA AJILI YA MSAADA

Imam Husain (a.s.) alitoa wito kwa ajilil ya msaada mwishoni mwa dakika za siku ya Ashura. Hivi Imam Husain (a.s.) naye pia alikuwa anahitaji msaidizi wakati huo? Je, Imam Husain (a.s.) alihitaji wasaidizi ambao wangejitokeza kisha wauawe? Hapana, Imam Husain (a.s.) hakuhitaji msaidizi kumlinda yeye kutokana na maadui.

Imam Husain (a.s.) hakutaka kuwa hai baada ya Shahada za masahaba wake, ndugu zake na watoto wake kupatikana. Hata hivyo, Imam Husain (a.s.) alitaka msaidizi ambaye angeuawa kishahidi. Kwa hiyo, alitoa wito: "Hivi kuna yeyote wa kunisaidia?"[184] Sauti ya Imam Husain (a.s.) ilisikika kwenye kambi yake na wanawake wakaanza kulia kwa sauti kubwa.[185] Imam Husain (a.s.) alimtuma Mtukufu, Abbas na mtu mmoja kutoka Ahlul-Bayt waende kuwaliwaza hao wanawake. Walikwenda na wakawafariji wanawake.[186]

Kifo cha Kishahidi cha Mtoto Mchanga:

Halafu Imam mwenyewe alirudi akaenda kwenye kambi ya watu wa familia yake. Wakati huo huo Bibi Zainab alimwendea Imam Husain (a.s.) akiwa amembeba mtoto mchanga. Imam Husain alimchukua mtoto huyo lakini hakuuliza: "Ewe dada! Kwa nini umetoka nje na mtoto huyu katika hali ya hatari ambapo mishale inafuatana kama mvua kwa mfululizo kutoka pande zote?" Alimchukua mtoto huyo mikononi mwake. Mshale ulikuja kutoka kwa adui na ukapasua ile shingo laini ya mtoto. Imam Husain (a.s.) alifanya nini baada ya hilo? Majibizo yake yanashangaza kwa kiasi gani! Mtoto huyo mchanga alipouawa mikononi mwa baba yake, Imam (a.s.) alichukua

[184] Kauli hii mashuhuri "*Hal min nas'irin yans'una*" imesimuliwa kwa namna mbalimbali kwenye vitabu vya historia kama: "Hivi kuna yeyote wa kuulinda utukufu wa Mtukufu Mtume? Hivi kuna mfuasi wa imani ya Mungu Mmoja (*Tawhiid*) ambaye anamuogopa Mwenyezi Mungu katika jambo letu? Kuna mtu yeyote wa kujibu miito yetu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu? Yupo mtu yeyote anayetafuta ukweli ili atusaidie? Hivi kuna mtu yeyote wa kulinda utukufu wa Mtukufu Mtume (usidhuriwe)? Kuna mtu yeyote wa kusikia wito wetu kwa ajili ya Allah Mwenye-Enzi? Kuna msaidizi yeyote wa kuwasaidia dhuria watukufu (a.s.)? (*Firhang-e-Ashura*, uk. 271)

[185] *Luhuuf*, uk. 116

[186] Imam Husain (a.s.) alipomtuma Mtukufu Abbas na Mtukufu Ali Akbar kuwaliwaza wanawake, alikuwa amesimama akiwa na upanga wake na alikuwa anajitambulisha kwa sauti ya kupaza kabla ya vita mnamo siku ya Ashura. – *Luhuuf*, uk. 87; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*,uk. 427.

damu hiyo kiganjani mwake na akaitupa juu angani huku akisema: "Ewe anga! Angalia ukatili huu na uwe shahidi."[187]

## IMAM HUSAIN (A.S.) ALIJIPAKA DAMU HIYO USONI MWAKE

Imam Husain (a.s.) alikosa nguvu katika dakika za mwisho wa uhai wake kwa sababu ya majeraha na alianguka chini. Kuna wakati alikuwa ananyanyuka na kutembea hatua chache akisaidiwa na mikono yake halafu anaanguka tena. Ikatokea akapigwa mshale kwenye shingo yake. Mara moja alichukua damu yake na akajipaka usoni mwake na akasema: "Mimi nataka kukutana na Mola wangu nikiwa katika hali hii tu."

Hadithi hii ya Karbala yenye kuvunja moyo iliupatia ujumbe wake uhai wa milele, ujumbe ambao utaendelea kuwepo wakati wote wa kuwepo kwa dunia.

## ALASIRI YA TAREHE TISA YA MUHARRAM

Wakati adui aliposhambulia mnamo alasiri ya tarehe tisa ya Muharram, Imam Husain (a.s.) alimtuma kaka yake Mtukufu Abbas akasema: "Ninataka kumuomba Mwenyezi Mungu usiku huu wa leo, kuswali, kusoma dua na kuomba msamaha. (Ewe ndugu yangu!) Wazuie mpaka kesho asubuhi kwa vyovyote vile. Kesho kwa hakika tutapigana nao." Baada ya mazungumzo, jeshi la Ibn Saad liliahirisha vita. Imam Husain (a.s.) alifanya mambo muhimu katika huo mkesha wa Ashura, ambayo yameandikwa katika historia.

## MKESHA WA ASHURA

Kwanza kabisa, Imam Husain (a.s.) aliamuru kila mpiganaji anoe mkuki na upanga wake. Jaun ambaye alikuwa mtaalam wa kunoa silaha, alishughulika akinoa silaha za masahaba. Imam Husain (a.s.) alimwendea kuangalia kazi yake na akazikagua silaha hizo.

[187] Luhuuf, uk. 117; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 476

Pili, Imam Husain (a.s.) aliagiza mahema yakaribiane. Mahema yalisogezwa na kukaribiana sana hivyo kwamba kigingi cha hema moja kiliingia kwenye hema lingine na nafasi baina ya mahema haikutosha hata kupita mtu. Halafu Imam akaagiza mahema yapangwe kwa namna ambayo kambi ionekane kama umbo la mwezi mwandamo. Handaki lilichimbwa nyuma ya mahema kwa usiku moja, ambalo lilikuwa pana sana hivyo kwamba farasi hangeweza kuvuka. Kwa hiyo, hapakuwepo na njia ya adui kufanya mashambulizi kutokea upande wa nyuma. Pia aliagiza kwamba majani Makavu na kuni vikusanywe na kukoka moto kwenye handaki lote wakati wa asubuhi ya siku ya Ashura na kuhakikisha kwamba adui hawezi kushambulia kutokea upande wa nyuma.

Imam Husain (a.s.) aliwakusanya masahaba kwenye hema kwa mara ya mwisho usiku huo kwa kumalizia hoja. Kwanza, alimshukuru kila mmoja kwa namna ya ufasaha kabisa. Halafu akazungumza na watu wa familia yake na masahaba. "Hakuna watu wa nyumba katika dunia hii ambao ni bora kuliko watu wa nyumba yangu na hakuna masahaba walio bora hapa duniani kuliko hawa wa kwangu."

Aliendelea: "Wote mnajua kwamba adui hatafuti kitu kingine chochote isipokuwa uhai wangu. Lengo pekee la adui ni mimi. Wakinipata mimi hawatamtaka mwingine kutoka miongoni mwenu. Kwa hiyo, wote nyinyi ondokeni hapa wakati wa giza la usiku huu.

Kila mmoja alisema, "Ewe Aba Abdillah! Tunawezaje kufanya hivi?" Mtu wa kwanza kusema hivi alikuwa kaka yake Imam wa daraja la juu, Mtukufu Abbas bin Ali.

Katika tukio hili kwa mara nyingine tunasikia tena kauli ambazo kwa kweli ni za kihistoria na zinadokeza uwasilishaji bora na ufafanuzi bora wa mzugumzaji. Kila mtu huzungumza kufuatana na namna anavyofikiri. Mtu mmoja akasema, " Maula Imam! kama nikiuawa na mwili wangu ukachomwa moto na majivu yakatupwa hewani na ikafanyika namna hii mara sabini, basi hata hivyo mimi sitakuacha wewe. Maisha yetu duni hayana thamani ya kutolewa muhanga kwa ajili yako." Sahaba mwingine akasema: "Hata kama nitauawa mara elfu moja, nisingekuacha wewe."[188]

[188] *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 393; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain,* uk. 400

## UAMINIFU WA MUHAMMAD BIN BASHIR HADHRAMI

Kabla ya kusahau, Muhammad bin Bashir Hadhrami, ambaye alikuwa sahaba wa Imam (a.s.), alipata habari huko Karbala kwamba mtoto wa kiume ametekwa vitani. Hakujua mwanae atapatwa na masaibu gani? Akasema: "Siwezi kuvumilia mimi kubaki hai ambapo mwanangu amepatwa na haya."

Imam Husain (a.s.) alipopata habari ya balaa lililompata sahaba wake, alimuita na akamshukuru. Imam (a.s.) alimsifu na akasema: Mwanao wa kiume amechukuliwa mateka na ni muhimu mtu amchukulie dhamana kutoka kwenye makucha ya adui. Viko vitu vichache hapa, ambavyo vinaweza kuuzwa ili fedha ipatikane. Chukua vitu hivi umdhamini mwanao kwa fedha utakayopata baada ya kuuza vitu hivi." Muhammad bin Bashir akasema: "Kama mimi nikikuacha wewe kwa sababu hii, wanyama-pori waje kunitafuna nikiwa hai. Acha mwanangu abakie kuwa mfungwa. Hivi mwanangu ni kipenzi zaidi kuliko wewe?"[189]

## MTUKUFU QASIM BIN HASAN

Usiku ule, ambapo Imam Husain (a.s.) alipoimaliza hoja bayana na kuwafanya kila mtu atangaze uaminifu wake kwa pamoja kwa uwazi wa dhahiri, kila mtu akasema: "Hatutakuacha wewe hata kwa gharama yoyote ile." Imam akasema: "Hali ya mambo iko mbele yenu. Lazima mlitambue vema kwamba sisi sote tutauawa kishahidi." Kila mtu akasema: "Taarifa hii ni sababu ya kutufanya sisi tufurahi. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia fursa hii."

## USHINDI HUU SI KWA SABABU YA NGUVU MUSULI HAIPATIKANI TU MPAKA MWENYEZI MUNGU AIJAALIE

Mtoto ambaye umri wake haukuwa zaidi ya miaka kumi na tatu, aliketi kwenye kona ya hema. Alikuwa na shaka kama jina lake lilikuwepo kwenye orodha ya wale ambao wangeuawa kishahidi. Imam (a.s.) alikwishasema

[189] *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 393; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 403

kwamba wote wale waliokusanyika pale wangeuawa kishahidi kesho yake. Hata hivyo, mtoto huyo alikuwa bado mdogo na maelezo ya Imam (a.s.) yangeweza kuwa kwa ajili ya watu wazima tu. Kwa hiyo, mtoto huyo alimuuliza Imam, "Ewe ami yangu! Hivi jina langu limo kwenye orodha ya wale watakaouawa kishahidi kesho?"

Imeandikwa kwamba Imam (a.s.) alilia sana aliposikia swali hili. Hakumjibu Qasim. Imam (a.s.) akasema: "Mwanangu! Tafadhali jibu swali langu kwanza. Halafu nitajibu swali lako. Niambie, kwa maoni yako kifo ni nini?"

Qasim akasema: "Ewe ami yangu! Kwangu mimi kifo ni kitamu kuliko asali. Ukisema kwamba kesho nitauawa kishahidi, hiyo itakuwa ni habari kubwa kwangu." Imam (a.s.) akasema: "Ndio mwanangu lakini ni baada tu ya kukabiliwa na balaa kubwa." Qasim akasema: "Sifa zote ni zake Allah! Msiba mkubwa utatokea."

Enyi waombolezaji wa yule aliyedhulimiwa Karbala!

Shikeni nyoyo zenu na mtafakari. Kufuatana na maneno ya Imam Husain (a.s.) matukio mengi ya kupasua nyoyo yalikuwa yatokee siku inayofuata. Mtoto huyu wa umri wa miaka kumi na tatu Qasim anamuona Imam baada ya kuuawa kishahidi Mtukufu Ali Akbar, mwili wake ulikuwa bado haujawa mkubwa vya kutosha kwamba silaha kama hizo zining`inie humo. Mavazi ya kivita yalikuwa yametengezwa kwa ajili ya watu wazima tu na hata helimeti hazingeenea kwenye vichwa vya watoto. Mtoto huyu akaomba, "Mpendwa ami yangu! Sasa ni zamu yangu kwenda. Tafadhali niruhusu." Ikumbukwe kwamba hakuna mpiganaji aliyekwenda kwenye uwanja wa vita bila ya ruhusa ya Imam katika siku ya Ashura. Kila mmoja alikuwa anamsalimia kwanza, "Amani iwe kwako, Ewe Aba Abdillah!" Halafu alikuwa akisema, "Bwana! Tafadhali niruhusu."

Imam Husain (a.s.) hakumpa ruhusa Qasim kwa urahisi; badala yake alianza kulia alipomuona Qasim. Qasim na Imam Husain (a.s.) walikumbatiana na wote wakalia. Imeandikwa kwamba Qasim alianza kubusu mikono na miguu ya Imam Husain (a.s.).[190] Hivi sio inafaa kwamba historia inapaswa kuzingatia tukio hili na kutoa uamuzi kwa njia nzuri zaidi kuhusu msiba wa Karbala? Mtoto huyo alikuwa anasisitiza lakini Imam Husain (a.s.) hakumruhusu. Hata ingawa Imam Husain (a.s.) alitaka kumruhusu lakini ulimi wake haukumruhusu kutoa ruhusa. Halafu akiwa amenyoosha mikono yake akasema:

[190] Inasimuliwa kwenye riwaya za Karbala: "Mtoto alibusu mikono na miguu ya Imam hadi akapewa ruhusa."

"Ewe mabaki ya kaka yangu! Njoo, ngoja nikukumbatie na nikwuage." Qasim akamkumbatia Husain (a.s.) na ami akamshikilia mpawe katika kumkumbatia huko. Imeandikwa: Baada ya hapo wawili hao walilia sana hadi wakapoteza fahamu. (Masahaba na Ahlul-Bayt wa Imam Husain (a.s.) walikuwa wanalitazama tukio hili la kusikitisha). Halafu wakatengana na Qasim kwa haraka akapanda farasi na akaelekea kwenye uwanja wa vita.

## "MIMI NI MTOTO WA HASAN"

Msimulizi kutoka jeshi la Umar bin Saad anasimulia kwamba ghafla akamuona mtoto mdogo akiwa amepanda farasi akielekea walipokuwa. Alivaa kilemba badala ya helimeti, alivaa viatu vya mikogo vya kawaida badala ya vyenye vigwe vinavyovaliwa vitani. "Alionekana kama kipande cha mwezi"-ni kwamba alikuwa na sura ya kupendeza mno. Halafu msimuliaji anasema: "Qasim alipokuwa anaingia kwenye uwanja wa vita niliona machozi yalikuwa yanatiririka kutoka kwenye macho yake."

Kufuatana na desturi za Waarabu, kila mpiganaji alitakiwa kujitambulisha baada ya kuingia kwenye uwanja wa vita. Kila mtu alishangaa na hakuna mtu aliyejua mtoto huyu alikuwa ni nani. Mtoto huyu aliwasili kwenye uwanja wa vita na kutangaza kwa sauti ya kubwa.

"Enyi watu! Kama hamnijui; mimi ni mtoto wa Hasan, mjukuu wa Mtume Mustafa. Na huyu ni Husain ambaye mmezingira na hamkumpa hata kutu moja la maji kutoka kwenye maji yanayotiririka ya mto Furati."

## KICHWA CHA QASIM KWENYE MAPAJA YA AMI YAKE

Qasim alipokwenda kwenye uwanja wa vita, Imam Husain (a.s.) alikuwa ameshika hatamu za farasi wake akiwa amejiweka tayari kwa lolote. Ilionekana kama vile alikuwa anangoja kitimiza mojawapo ya majukumu yake. Sijui Imam Husain (a.s.) alikuwa katika hali gani. Imam Husain (a.s.) alingojea. Labda alikuwa anangoja wito wa Qasim. Ghafla Qasim akaita, "Ewe ami yangu! Nisaidie!" Msimulizi anasema kwamba hakuweza kuelewa ni kasi ya kiasi gani Imam Husain (a.s.) alipanda farasi na kushambulia jeshi. Kwa

mujibu wa msimulizi, Imam (a.s.) alikwenda kwenye uwanja wa vita kama muwindaji mwepesi. Watu waliokuwepo kwenye uwanja wa vita wanasimulia kwamba Qasim alianguka chini kutoka kwenye farasi wake na takriban farasi mia mbili walimzunguka. Mtu mmoja alitaka kumkata kichwa chake. Mara walipomuona Imam Husain (a.s.) anaingia kwenye uwanja wa vita, waliingiwa na mhamaniko mkubwa, wakaanza kukimbia hapa na pale. Katika purukushani hii, mtu aliyetaka kuja kumkata shingo Qasim alipondwa chini ya kwato za farasi. Wapiganaji wa jeshi la adui waliogopeshwa sana hivyo kwamba kwa ubinafsi wao walimponda mpiganaji mwenzao akiwa hai ili wajiokoe wenyewe. Palikuwepo na kundi kubwa. Farasi walikimbia kwa kasi na hakuna kilichokuwa kinaonekana kutokana na vumbi lililotimka hapo. Kama vile anavyosema Firdausi,

"Katika upana wa jangwa hilo, kwato za farasi ziligawa dunia katika sehemu sita na mbingu katika sehemu nane."

Hakuna aliyejua nini kilikuwa kinatokea. Mara baada ya vumbi kutulia,watu walikiona kichwa cha Qasim kwenye mapaja ya ami yake.[191]

## "......USISIMULIE SEHEMU HII YA MATESO YA QASIM"

(Kamwe sitasahau kile ambacho msemaji mashuhuri na fasaha hapa Qum, marehemu Aqa Ishraqi alikuwa akisema: "Wakati fulani mbele ya Ayatullah Haeri kwenye mojawapo ya majilisi nilisimulia majanga sawasawa kabisa kama ambavyo yameandikwa kwenye vitabu vya historia na maelezo ya masaibu ya Karbala bila kubadili hata neno moja. Baada ya kusikia haya, Ayatullah huyo alilia sana hadi akapoteza fahamu. Baadaye, aliniambia: Endapo utaniona mimi miongoni mwa wasikilizaji usisimulie sehemu hiyo ya mateso kwani siwezi kustahimilia kuisikiliza.)

Sasa hali ya Qasim ilikuwa ya kutikisa miguu yake kutokana na maumivu makali wakati wa dakika za mwisho za uhai wake. Wakati huo, watu walim-

[191] Wasemaji wanaosema kwamba mwili mwembamba wa Qasim ulipondwa na kwato za Farasi wanaombwa kurejelea kwenye vitabu vya Msiba wa Karbala na historia ya Karbala (Rizwani)

sikia Imam Husain (a.s.) anasema, "Wallahi! Ni hali ya kutovumilika kiasi gani kwa ami yako kwamba umemuita akusaidie lakini alipofika hapo ulipo akawa hawezi kutoa msaada wowote kwako."[192]

"Hapana nguvu na Uwezo isipokuwa kupitia kwa Allah Aliyeko Juu na Muweza wa Yote."

[192] *Irshad*, Shakhy Mufid, uk. 239; Luhuuf, uk. 114; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 34; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 464; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 680; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk.264

# MAJILISI 30

## ABDULLAH IBN HASAN

Enyi waombolezaji!

Leo ningependa kusimulia mateso ya mmojawapo wa watoto wa kiume wa Imam Hasan (a.s.). Abdullah alikuwa ni kaka yake Qasim. (Imam Hasan aliuawa kwa sumu miaka kumi kabla ya tukio la Karbala. Inasimuliwa kwamba mtoto huyu alikuwa na umri wa miaka kumi. Labda, mtoto huyu alizaliwa baada ya kuuawa kishahidi Imam Hasan (a.s.). Vyovyote vile iwavyo, yeye alikuwa hamkumbuki baba yake. Alilelewa katika nyumba ya Imam Husain (a.s.) ambaye alikuwa ami yake na mlezi wake.)

Imam Husain (a.s.) alimkabidhi mtoto huyo (ambaye jina lake aliitwa Abdullah) kwa shangazi yake, Bibi Zainab ambaye alikuwa mtunza watoto mahsusi. Abdullah bin Hasan alikuwa mmojawapo wa wale watoto ambao walikuwa wakijaribu tena na tena kwenda kwenye uwanja wa vita lakini walizuiwa kwa namna fulani.

### WALLAHI, MIMI SITAMUACHA AMI YANGU

Sijui ni kwa vipi mtoto huyu wa miaka kumi aliweza kutoka nje ya hema na kufika mahali ambapo Imam Husain (a.s.) alianguka wakati anapigana. Mtoto huyu alipotoka nje ya hema, Bibi Zainab alimkimbilia ili amrudishe, hata hivyo, aliweza kumponyoka na akakimbia huku akisema, "Wallahi, sitamwacha Baba yangu mdogo peke yake."

Mtoto huyu mara alifika pale alipokuwa amelala Imam Husain (a.s.), akikaribia kuuawa, na akajitupa juu ya mwili wa baba yake mdogo. Imam Husain (a.s.) alipomshika mikononi mwake mtoto alianza kumsemesha. Wakati huo huo mshambuliaji alijitokeza kutaka kumshambulia Imam. Mtoto alimlaani mshambuliji huyo na akasema: "Je! Umekuja kumwaga damu ya baba yangu mdogo? Wallahi, sitakuruhusu ufanye hivyo." Mara mshambuliaji alipochomoa upanga wake ili amkate kichwa Aba Abdillah al-Husain,

mtoto huyu alimkinga kwa mikono yake ambayo ilikatwa kwa upanga na ikawa inaning`inia toka kwenye ngozi. Sasa mtoto akaanza kulia, "Ewe ami yangu! Hebu ona huyu mtu aliyelaaniwa alivyonifanya!"[193]

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**".....Na punde watajua waliodhulumu ni mgeuko gani watakaogeuka?"**

**(Sura Ash-Shu'araa 26 : 227)**

[193] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 241; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 53; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 507

# MAJILISI 31

## 'KUAMRISHA MEMA' NA 'KUKATAZA MAOVU' – MISINGI YA HARAKATI ZA HUSEIN

Kutoka kwenye kila sura, Jihadi ya Imam Husain ndani ya Karbala ni kioo cha muujiza, ujasiri, uaminifu, na usahihi wake mwenyewe. Pia Imam Husain (a.s.) alikuwa muangalifu kuhusu '*Kuamrisha mema na kukataza maovu.*' Kwa hiyo Imam alisema: "Enyi watu! Hivi hamuoni kwamba haki inapuuzwa. Haki haifuatwi na hakuna anayekatazwa kutokana na batili. Badala yake uongo unafanywa kuwa desturi. Hivi hamuoni kwamba matendo mema yamepuuzwa na sumu ya matendo maovu inaingizwa kwenye damu ya binadamu? Katika hali kama hii, mtu muaminifu angependelea kifo zaidi ya maisha kama haya."[194] Kwa kweli hili linapaswa kutokea. Muumini anapaswa atamani kukutana na Allah katika hali kama hii na aepukane na dunia hii. Kulingana na chanzo kingine, Imam (a.s.) akasema, "Kwa kweli, ninakifikiria kifo kuwa kama neema katika hali kama hii na ninafikiria kuwa ni fedheha kubaki hai na kubughudhiwa na adui."[195]

Ndugu zangu wapendwa!

Fikirini, mwanadamu anayetaka kuishi na watu dhalimu na waonevu anakuwa na hisia za aina gani? Ni maisha ambapo alikuwa anaona watu madhalimu na waonevu kila mahali. Imam Husain (a.s.) anasema, "Hivi ninapaswa kuishi nao halafu niwe mfuasi wao? Hapana, maisha kama hayo si maisha kwa ajili yangu. Hayo ni kifo. Ni chanzo cha fedheha. Katika hali kama hiyo mimi ninatamani kifo kwa sababu itakuwa ni heshima kwangu."

## MTOTO ANAYE NYONYA ATENGANA NA IMAM HUSAIN (A.S.)

Imam Husain (a.s.) aliingia ndani ya hema mnamo siku ya Ashura na akamwambia Bibi Zainab, "Ewe dada! Niletee huyo mtoto anayenyonya ili

[194] *Tarikh Tabari*, Juz. 4, uk.305; *Biharul Anwar,* Juz. 44, uk. 381
[195] *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 381

nimuage."[196] Pamoja na kwamba mama wa mtoto huyo alikuwepo Karbala, lakini Imam Husain (a.s.) alimuomba dada yake ili kuashiria kwamba Zainab alikuwa ndiye kiongozi wa msafara baada yake. Bibi Zainab alikwenda ndani na akamchukua mtoto kutoka kwa wifi yake, akampeleka mtoto huyo kwa kaka yake. Imam Husain (a.s.) akamtazama mtoto huyo dhaifu mara moja; mtoto huyo alionekana kama ua lililonyauka kwa sababu alikuwa hajanyonyeshwa kwa siku chache zilizopita. Mama yake alikaukiwa maziwa kwa sababu ya njaa na kiu.

Imam Husain alimchukua mtoto kutoka kwa dada yake. Wakati Imam aliponuia kumbusu na kumpa mtoto mapenzi ya ubaba, kamanda alimwambia mmoja wa wapiganaji wake, "Tazama, shabaha nzuri iliyoje umeipata pale!" Mpiganaji akauliza ni shabaha gani aliyokuwa anaizungumzia. Kamanda alimuonyesha mtoto aliyekuwa mikononi mwa Imam Husain (a.s.).

Mtoto alikuwa mikononi mwa Imam na mshale ukatupwa kutoka upande wa adui. Mtoto alifurukuta kama kuku aliyechinjwa na akafa lakini tutasema nini kuhusu subira ya Husain (a.s.)?

Hivi midomo yetu inaweza kusifu subira na uvumilivu wake?

## ALISIFIWA NA MTUME NA ALI. (GHALIB)

Uthabiti wake haukuyumba. Alichukua damu ya kiumbe huyo asiye na hatia kwenye mkono wake uliokunjwa kama kikombe, akatazama mbinguni na akasema "Ee Mola! Unaangalia umwagaji damu huu dhalimu. Hii ni kwa ajili ya radhi Yako Wewe na kwa hiyo sio jambo llisilovumilika kwa Husain."[197]

[196] Kwenye baadhi ya vitabu vya masaibu ya Karbala maneno ya Imam Husain (a.s.) kwa Bibi Zainab yameandikwa kama ifutavyo: "Mlete mwanangu mchanga nimuage." Luhuuf, uk. 117; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 693.

[197] Luhuuf, uk. 117; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 477. Na *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 381

# MAJILISI 32

## MIHEMKO NA HISIA ZA HARAKATI ZA HUSAIN

Wapendwa marafiki zangu!

Tunawapenda watoto wetu. Je, ni kwamba Imam Husain (a.s.) hakuwapenda watoto wake? Kwa kweli, aliwapenda zaidi ya tunavyowapenda watoto wetu.

Nabii Ibrahim (a.s.) hakuwa na mapenzi pungufu kwa mwanae Isma'il kuliko tunavyowapenda watoto wetu sisi. Alikuwa anampenda mwanae kupita kiasi. Sababu ni kwamba yeye alikuwa ni mtu bora kuliko sisi. Imam Husain (a.s.) pia aliwapenda watoto wake kutuzidi sisi lakini alimpenda Mwenyezi Mungu kuzidi vitu vingine vyote na hakuruhusu mtu mwingine amtangulie katika hilo.

Imeandikwa kwamba familia yote ya Imam Husain (a.s.) ilifuatana naye katika safari yake ya kwenda Karbala. Ni ukweli kwamba kama mtu anasafiri na watoto wake huhisi kuwajibika na huwa na wasiwasi kuhusu kitu gani kitawatokea baada yake.

### KUTAMBULIWA KWA ALI AKBAR

Inasimuliwa kwamba Imam Husain (a.s.) alisinzia wakati wa safari. Baada ya muda aliamka na kufungua macho yake na akasoma "Kwa hakika sisi ni waja wa Allah na Kwake tutarejea." Kila mtu alianza kumuuliza mwingine ni kwa nini Imam Husain (a.s.) alikariri maneno hayo? Walifikiri labda kuna suala jipya limejitokeza. Imam Husain (a.s.) alimpenda sana mwanae Ali Akbar na mara nyingi alionyesha mapenzi yake kwake kwa sababu alikuwa anafanana na Mtume. Babu yake Imam Husain (a.s.). (Unaweza kufikiria baba anakuwa katika hali ya mpito wa aina gani pale ambapo mwanae kama huyo anazungukwa na hatari tele). Mtukufu, Ali Akbar anatokeza mbele na kuuliza: "Ewe baba! Kwa nini ulikariri aya ya marejeo?" Imam akajibu:

“Niliisikia sauti ya mtu asiyeonekana katika ndoto yangu akisema: “Msafara huu unaongozwa na kifo. Baada ya kusikia sauti hiyo, nilielewa kwamba hatima yetu ni kifo. Tunaelekea kwenye hatima ya uhakika ya kifo chetu.”[198] Hapa mazungumzo yakawa yamefanana na yale ya Nabii Isma’il na Nabii Ibrahim.[199]

Mtukufu Ali Akbar alimuuliza Imam Husain (a.s.), “Hivi tupo katika njia aliyonyooka?” Imam akasema: “Ewe mwanangu! kwa nini unauliza? Kitu kimoja tu ni kwamba tunakwenda kule ambako makusudio yetu yanatupeleka. Kama kwenda kwetu tunaelekea kwenye kifo au uhai si jambo la kujali. “Mtukufu Ali Akbar akasema: Hilo ni sawa lakini je, tupo kwenye njia iliyo sahihi au hapana?” Imam Husain (a.s.) akafurahi baada ya kusikia hilo. Uso wake ukachangamka kwa furaha. Inaweza kuonekana kutoka kwenye dua ile ambayo alikariri wakati huo. Imam akasema, “Ewe mwanangu! Mimi sina kitu chochote cha kumzawadia mtoto muwajibikaji kama wewe katika muda huu. Hata hivyo, naomba Mwenyezi Mungu akulipe chochote kile unachostahili kwa niaba yangu.”[200]

## KIFO CHA KISHAHIDI CHA ALI AKBAR

Enyi waombolezaji!

Fikiria mandhari ilivyokuwa ambapo Ali Akbar aliporudi kutoka kwenye uwanja wa vita mnamo alasiri ya siku ya Ashura baada ya kukabiliana na maadui kijasiri mno. Mdomo wake ulikauka sana hivyo kwamba hangeweza

[198] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 226

[199] Wakati Nabii Ibrahim alipokuwa amemwambia Isma’il kwamba alikuwa anaota ndoto mara kwa mara na kwamba alifikiri huo ulikuwa ni wahayi wa Mwenyezi Mungu. Alisema kwamba aliamriwa na Allah kwamba alipaswa kumchinja Nabii Isma’il (ingawa Nabii Ibrahim alikuwa hajui falsafa ya kafara hilo, alikuwa na uhakika kwamba hiyo ilikuwa ni amri ya Allah na ni ridhaa ya Mwenyezi Mungu). Mtoto angesema nini wakati huo? Je! Alimwambia baba yake kwamba hiyo ilikuwa ni ndoto tu na kwamba mtu akiota ndoto ya kifo basi anapata maisha marefu kwa hiyo na yeye ataishi maisha marefu? Hapana, mtoto akasema: **“Ewe baba! Tenda unavyoamrishwa, utanikuta mimi, Inshallah katika wanao subiri.”(Surah Saffat 37:102).** Nabii Ibrahim alipomchinja Nabii Isma’il, alipokea wahayi, **“.....Basi wote wawili walipojisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji. Tulimwita, Ewe Ibarahim! Umekwisha timiliza ndoto....”** yaani Ewe Ibrahim! Hatukutaka umchinje mwanao. Hilo halikuwa kusudio letu kabisa kwa sababu kusingekuwa na manufaa ndani yake. Kusudio halisi ilikuwa ni kuona jinsi wewe baba na mwana mlivyo watiifu kwa Allah. Lengo halisi ilikuwa ni kupima utayari wenu katika kumtii Allah. Mmethibitisha utiifu wenu. Baba alikuwa tayari kumtoa kafara mwanae na mtoto alikuwa tayari kutolewa kafara na Sisi hatutaki kitu kingine chochote zaidi ya hicho. Kwa hiyo, usimchinje mwanao.

[200] Imeandikwa kwenye *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 226 kama ifuatavyo: “Naomba Mwenyezi Mungu akupe thawabu nzuri sana ambazo mtoto anaweza kupata kwa (ajili ya tabia yake kwa) baba yake.”

kupigana zaidi ya hapo. Wakati mtoto huyu shujaa wa Husain mwenye moyo wa simba alipofika kwa baba yake, akasema, “Ewe baba! Mimi ninakufa kwa kiu. Uzito wa mavazi ya kivita unasababisha wasiwasi. Tafadhali, ninaweza kupata maji?”[201] (Kama vile alikuwa akimaanisha kwamba kama angepata maji angeweza kuwasukuma maadui kurudi nyuma zaidi). Jibu la Imam Husain (a.s.) kwa mwanae mpendwa lilikuwa, “Kipenzi changu! Ninao uhakika kwamba baada ya muda si mrefu utapata daraja la kifo cha kishahidi, punde tu utatoshelezwa na mpaji wa maji ya Kauthar.”

[201] *Luhuuf*, uk. 113; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 461

# MAJILISI 33

## KUAGA KWA VIJANA WA BANI HASHIM

Wakusanyaji wa maelezo ya msiba wa Karbala wameandika kwamba mnamo siku ya Ashura shauku ya masahaba wa Husain (a.s.) ilionekana wazi. Almuradi wasaidizi wa Imam Husain (a.s.) walikuwa bado hai hawakumruhusu yeyote kutoka kwenye familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenda kwenye uwanja wa vita. Masahaba hao walikuwa wakisema, "Bwana! Tafadhali turuhusu sisi kwanza ili tutimize wajibu wetu. Baada ya sisi kuuawa kishahidi, ni juu yako kuamua nini kifanyike."

Ahlul-Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walikuwa wanangoja zamu zao. Baada ya muda mfupi tu sahaba wa mwisho wa Imam Husain (a.s.) alipouawa kishahidi na halafu wimbi la shauku likasambaa miongoni mwa vijana wa ukoo wa Hashim. Wote walisimama kila mmoja kwenye sehemu yake. Imeandikwa kwamba walianza kuagana wao kwa wao.[202] Walikumbatiana na kubusiana wao kwa wao.

### ALI AKBAR, MWENYE KUFANANA SANA NA MTUKUFU MTUME (S.A.W.W.)

Mtukufu Ali Akbar, yule kijana mdogo wa Imam Husain (a.s.) alikuwa wa kwanza kupewa ruhusa ya kwenda kwenye uwanja wa vita. Alikuwa ni kijana yule ambaye Imam Husain (a.s.) alikwishashuhudia kwamba alikuwa ni nakala halisi hasa ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa upande wa sura, tabia, namna ya uzungumzaji na adabu. Alifanana sana na Mtume (s.a.w.w.). Ali Akbar alipozungumza ilionekana kama vile Mtukufu Mtume alikuwa anazungumza. Alifanana sana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hivyo kwamba Imam Husain (a.s.) alikuwa akisema: "Ee Mwenyezi Mungu! Unajua kwamba wakati wowote ninapotaka kumuona mtukufu babu yangu, huwa ninamtazama kijana huyu."

[202] *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 255; *Nafasul Mahmuum*, uk. 312; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 32.

## KUONDOKA KWA ALI AKBAR KWENDA KUPAMBANA

Ali Akbar alimwendea mtukufu baba yake na akasema, "Ewe baba! Tafadhali niruhusu niende kwenye jihadi." Imeandikwa kuhusu idadi ya masahaba, hususan vijana, kwamba walipokuwa wanakuja kuomba ruhusa, Imam alikuwa akichelewa kutoa ruhusa kwa kutoa udhuru fulani kama ambavyo huwenda umeshasikia kuhusu tukio la Qasim. Hata hivyo, Ali Akbar alipoomba ruhusa, Imam aliinamisha kichwa chake na mwanae kijana akaondoka kwenda kwenye uwanja wa vita.

Imeandikwa kwamba Imam Husain (a.s.) alimtazama kijana huyo huku akiwa amefinya kidogo macho yake halafu akamtazama kwa huzuni sana.[203] Halafu Ali Akbar akamsogeza farasi wake na kuelekea kwenye uwanja wa vita na Imam Husain (a.s.) alimfuata hatua chache na akasema, "Ee Mwenyezi Mungu! Tafadhali shuhudia kwamba kijana anayekwenda kwa waonevu wale, ni nakala halisi ya sura ya  Mtume Wako."

## APIZO LA IMAM HUSAIN (A.S.)

Halafu Imam alimwambia kitu Umar bin Saad kwa sauti kubwa sana ambayo yeye angeweza kuihimili, "Ewe Ibn Saad! Namuomba Allah akatishe uzao wako kwa sababu umekatisha kizazi changu kwa kumuua kishahidi mwanangu huyu."[204]

Miaka miwili au mitatu tu baada ya apizo hili, Mukhtar alimuua Umar bin Saad. Wakati mtoto wa Umar bin Saad alipokwenda kwa Mukhtar ili amchukulie dhamana baba yake, kichwa cha Umar bin Saad kiliwasilishwa kwa Mukhtar hapo mahakamani kikiwa kimefunikwa nguo. Mtoto huyo wa Umar bin Saad aliyekwenda kumdhamini baba yake aliulizwa. "Unamfahamu mtu huyu?" Alisogea mbele akafunua nguo ile na kukuta kichwa kile kilikuwa cha baba yake. Alipoona hivyo, alijaribu kutoroka lakini Mukhtar aliamuru: "Naye pia mpelekeni kwa baba yake."[205]

---

[203] Luhuuf, uk. 113; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 460.

[204] Luhuuf, uk. 113; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 460

[205] *Damaus Sujum*, uk. 365.

# KIU YA ALI AKBAR

Wanahistoria wana kauli moja kwamba Mtukufu Ali Akbar alipigana kijasiri na kisha akarudi kwa baba yake. Hiki ni kitendawili cha kihistoria lengo lake lilivyokuwa na ni kwa nini Ali Akbar alirudi kwa baba yake?

Alirudi na akasema, "Ewe baba! Ninakufa kwa kiu. Kama nikipata maji kidogo ningepata uhai mpya na ningeweza kwenda kupigana." Maneno haya yalimgusa sana baba yake. Imam akasema: "Ndio, Ewe mwanangu! Angalia na uone kwamba mdomo wangu ni mkavu kuliko wa kwako lakini ninakuahidi kwamba baada ya muda si mrefu babu yangu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) atakutosheleza (kwa kinywaji cha Kauthar)" Baada ya kusikia hayo, Ali Akbar alikwenda kwenye uwanja wa vita tena kwa ajili ya Jihadi.

Hamid bin Muslim ambaye anaitwa msimuliaji katika istilahi alikuwepo Karbala kama mwandishi wa habari. Hakushiriki katika vita lakini amesimulia matukio kadhaa. Anasema kwamba mtu mmoja alikuwa amesimama karibu naye. Wakati wote Mtukufu Ali Akbar alipokuwa akifanya mashambulizi, watu walimkimbia. Alipoona hivyo mtu huyo alikasirika kwa sababu alikuwa mtu jasiri. Alimwambia mwandishi huyo, "Wallahi! kama akipita karibu yangu kwa kweli nitaumiza moyo wa baba yake vibaya sana. Hamid akamuuliza mtu huyo: "Wewe una uadui gani na kijana huyu? Kwa vyovyote vile watu wale watamuua kishahidi." Mtu huyo akasema: "Hapana." Mara tu Mtukufu Ali Akbar akapita karibu ya mtu huyo, mtu huyo akamshambulia kwa kumchoma mkuki vibaya sana hivyo kwamba hakuweza kujidhibiti na akaning`inia kwenye shingo ya farasi wake na akapiga kelele akiomba msaada. "Ewe baba! Babu, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) amekuja kunichukua."[206]

Waandishi wa masaibu ya Karbala wametoa maelezo ya kustaajabisha kuhusu tukio hilo:

" Farasi alimpitisha katikati ya jeshi la maadui na wakampiga kwa mapanga na kuukatakata mwili wake dhaifu na kuwa vipade vipande."[207]

[206] Biharul Anwar, Juz. 45, uk. 44; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk. 462; Maqtal-e-Husain, Muqarram, uk. 259

[207] Biharul Anwar, Juz. 45, uk. 44; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk. 462; Maqtal-e-Husain, Muqarram, uk. 259

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**“.....Na punde watajua waliodhulumu ni mgeuko gani watakaogeuka?”**
**(Sura Ash-Shu’araa 26 : 227)**[208]

[208] **Sura Ash- Shu’araa [26:227]**

# MAJILISI 34

## MIHEMUKO YA BINADAMU WALIOK AMILIKA

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mwanadamu mkamilifu na Imam Ali (a.s.) pia alikuwa mwanadamu mkamilifu. Imam Hasan (a.s.) naye alikuwa mtu mkamilifu. Pia Imam Husain (a.s.) pia alikuwa mwanadamu mkamilifu na Bibi Zahra pia alikuwa mwanadamu mkamilifu. Maana yake ni kwamba wote hawa walikuwa na sifa za binadamu. Na kwamba pia walikuwa na kiwango cha ukamilifu ambacho ni zaidi hata ya kile cha malaika. Kwa maneno mengine, wao pia walikuwa wakihisi njaa kama binadamu wengine na walikuwa wanakula chakula. Pia walikuwa wanahisi kiu na walikuwa wanakunywa maji. Walikuwa wakihisi usingizi na walikuwa wanapumzika. Pia walikuwa wanawapenda watoto wao. Pia walikuwa wanahisi tamaa ya jimai. Na hiyo ndio sababu ya wao kuweza kuwa viongozi. Kama isingekuwa hivyo hawangeweza kuwa viongozi.

Kama Imam Husain (a.s.) asingekuwa na hisia za kibinadamu na akawa hakuteseka kama baba anavyoteseka kwa sababu ya majanga yaliyompata mwanae alipokatwa vipande vipande isingeleta tofauti na kumtazama mtoto akikatwa vipande vipande au jiwe linalo pondwa na kugawika vipande vipande. Ugumu wa moyo wa aina hii si jambo maarufu. Kama ningekuwa mtu wa aina hiyo hata mimi ningeweza kufanya hivyo.

Lakini ukweli ni kwamba hali kihisia na ubinadamu aliyokuwa nayo Imam ina nguvu zaidi ikilinganishwa na vile tulivyo sisi. Na Imam yupo juu zaidi kuliko hata malaika katika hali ya ukamilifu wa mwanadamu. Ilikuwa kwenye msingi huu ambapo Husain alifanywa Imam kwa sababu alikuwa na sifa na tabia zote za kibinadamu (katika daraja la ukamilifu). Wakati mwanae kijana alimjia baba yake kuomba ruhusa ya kwenda kwenye uwanja wa vita, moyo wake pia uliumia sana kwa sababu Imam alimpenda mwanae mara nyingi zaidi kuliko vile sisi tunavyowapenda watoto wetu. Ni suala tofauti kwamba inapokuja kwenye kutafuta radhi ya Allah Mwenyezi, Imam alizuia shauku na hisia zote.

## HAIBA KUBWA YA ALI AKBAR

Ali Akbar alikwenda kwa Imam Husain (a.s.) na akasema: "Ewe baba! Tafadhali nakuomba uniruhusu." Imam Husain (a.s.) akasema, "Nenda mwanangu, nenda."[209] Hapa waandishi wa historia wamewasilisha nukta nzuri sana. Wameandika kwamba Imam Husain (a.s.) alimtazama mwanae kwa jicho la kukata tamaa na huzuni. Kama mtu ambaye amepoteza matumaini ya uhai wa huyo mtu mwingine.

Athari za kisaikolojia na kiroho kwa mwanadamu ni mambo ya kawaida. Kama mtu akisikia habari njema, uso wake huchangamka na macho yanafunguka kabisa. Hata hivyo, kama mtu ameketi karibu na mpendwa wake na anao uhakika kwamba mtu huyo atakufa wakati mfupi ujao, wakati wowote anapomtupia jicho yule mtu anayekufa macho yake huwa mazito. Macho yake yanaonekana kama vile anasinzia kwa sababu moyo wake haupendi amuone mpendwa wake anakata roho. Kwa upande mwingine, kama mtoto amepata heshima au anafunga ndoa, baba yake atamtazama kwa macho yaliyo wazi kabisa. Inasemekana kwamba Imam (a.s.) alipomtazama Mtukufu Ali Akbar, vigubiko vya macho yake viliinama. Ali Akbar alipoondoka, ilikuwa ni nguvu ya mvuto wa ujana wa mtoto wake ndio iliyomlazimisha Imam Husain (a.s.) kufuata nyuma. (Kana kwamba alikuwa anasema, "Mwanangu! Sio wewe unayekwenda. Ni uhai wa huyu baba ndio unaokwenda.")

"Mambo mengi mbalimbali husemwa kuhusu roho inayotoka kwenye mwili lakini nimeona kwa macho yangu mwenyewe uhai wangu ukitolewa kwenye mwili wangu."

Ali Akbar alipokuwa anasonga mbele Imam Husain (a.s.) alikuwa anafuata akiwa kiasi fulani cha umbali nyuma. Halafu akaita kwa sauti ya kupaza:

"Ewe Umar bin Saad! Ninamuomba Mwenyezi Mungu akatishe uzao wako kama ulivyokatisha uzao wangu."[210]

[209] Luhuuf, uk.113; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk. 260

[210] Luhuuf, uk. 113; *Mausuat-e-Kalimat, al-Imam al-Husain*, uk. 260

# MAJILISI 35

## MWEZI WA BANI HASHIM - MFANO HALISI WA MUHANGA

Hapangekuwepo na mfano bora zaidi wa kujitoa mhanga kuliko wa Mwezi wa Bani Hashim, Mtukufu Abbas. Ninawasilisha kwenu mfano wa kujitoa mhanga kutoka kwenye Uislamu wa siku za mwanzo ambapo palikuwepo na mashujaa si mmoja bali wengi tu. Mtu mmoja anasimulia: "Nilikuwa ninapita karibu na wapiganaji waliojeruhiwa kwenye mojawapo ya vita. Nilimuona mtu aliyekuwa amejeruhiwa akiwa amelala chini akivuta pumzi zake za mwisho. Nilijua kwamba damu nyingi sana ikitoka mwilini humsababishia mtu kiu kali sana. Kwa hiyo, mtu huyo aliyejeruhiwa aliponitazama na kusema kitu, kwa haraka nilifikiri kwamba alikuwa anaomba maji. Nilichota maji kwenye gilasi lakini kabla sijampa alinielekeza kwa kidole kwamba ndugu yake alikuwa katika hali kama ile ya kwake na akaniomba nimpe maji hayo yeye huyo kwanza. Nilipokwenda kwa mtu huyo naye alinielekeza kwa kidole mtu mwingine mwenye kiu na kunitaka nimpelekee maji hayo yeye kwanza. Nilikwenda karibu na mtu huyo (wasimulizi wengine wameandika idadi ya watu waliojeruhiwa kuwa ni watatu na wengine wameandika kuwa ni kumi). Kabla sijafika alipokuwa majeruhi wa mwisho, akakata roho. Halafu nikarudi kwa majeruhi wa pili kutoka mwisho naye akawa amekata roho. Vivyo hivyo, nilipofika kwa majeruhi wa kwanza, naye alikwisha kata roho." Kwa hiyo, msimulizi hakuweza kumpa maji yeyote katika majeruhi hao kwa sababu kila alipompa maji majeruhi, alimuomba ampe mwenzake kwanza. Kitendo hiki kinaitwa muhanga, ambacho ni dhihirisho bora sana la mapenzi ya kiroho. Je, umepata kushangaa kwa nini Sura Hal Ata iliteremshwa? Imo ndani yake aya hii:

وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا
إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ

**"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, maskini, na yatima, na mateka. Hakika tunawalisha kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu tu. Hututaki kwenu malipo wala shukrani."[211]**

[211] **Surah Insan [76:8-9]**

(Kwa kweli Sura hii iliteremshwa ili ifundishe umuhimu wa kujitolea mhanga).

Imekuwa ni wajibu wa msiba wa Karbala kupamba na kuwasilisha moyo wa kibinadamu na Kislamu wa kujitoa mhanga. Inaelekea kama vile wajibu wa kufanya hisia hizi kuwa kamilifu alipewa Mtukufu Abbas.

Enyi wapendwa!

Abbas alishambulia kwa nguvu sana na akawarudisha nyuma wanajeshi elfu nne waliokuwa wanalinda mto Furati. Sasa mto wa Furati ukawa chini ya miliki ya Abbas. Abbas alikwenda hadi kwenye kina kirefu ndani ya mto hadi maji yakafika kwenye tumbo la farasi na akajaza maji kwenye kiriba bila kushuka kwenye farasi. Baada ya kujaza maji kwenye kiriba, alichota maji kwenye mkono wake alioukunja mithili ya kikombe na kuusogeza hadi kwenye mdomo wake. Maadui walikuwa wakitazama kutoka umbali fulani. Wanasema kwamba walimuona anachukua maji kwenye mkono wake alioukunja mithili ya kikombe na halafu akayatupilia mbali; lakini hakuna anayejua kwa nini Mtukufu Abbas alifanya hivyo. Inasimuliwa kwamba lazima atakuwa amekumbuka kwamba Husain alikuwa na kiu.[212] Inawezekana alifikiria kwamba Husain (a.s.) angesema: "Ewe Abbas! Haipendezi Husain anabaki na kiu kule kambini na wewe unakunywa maji. Lakini fikira hii ya Abbas iliandikwa lini? Ilikuja kujulikana kutoka kwenye mistari ya mashairi yaliyoghaniwa na Mtukufu Abul Fazl al-Abbas[213] alipotoka nje ya mto. Alighani shairi la kivita, ambapo kwa sababu ya hilo ikawa ndio watu wakajua kwa nini hakunywa maji hayo.

Abbas alijiambia mwenyewe akasema, "Ewe nafsi ya Abbas! Kitu gani kitabaki katika maisha baada ya Husain? Unataka kunywa maji na uendelee kuwa hai? Unataka kunywa maji ya baridi na kumuacha bwana Husain abaki na kiu huko kambini? Wallahi, hii sio adabu ya mtumwa. Hii si desturi kutoka kwa ndugu. Hii sio desturi ya kawaida ya wafuasi wa Imam. Huu si mtindo wa utiifu. Kwa kweli, Mtukufu Abbas, alikuwa mfano wa utii wa kuigwa.

"Hapana nguvu na uwezo isipokuwa kwake Allah Mwenyezi Aliyeko Juu na Muweza wa Yote."

---

[212] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 41; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 472; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 688 una maneno: Halafu akakumbuka kiu ya Husain na Ahlul-Bayt wake.

[213] *Yanabiul Mawaddah*, Juz. 2, uk. 408; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk.41; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 268

# MAJILISI 36

## UTIIFU WA ABBAS

Shimr bin Dhiljaushan alikuwa anaondoka Kufa kuelekea Karbala, mtu mmoja ndani ya baraza la Ibn Ziyad akasema, "Baadhi ya ndugu zangu upande wa mama wamefuatana na Husain bin Ali. Kwa hiyo, ninataka uandike barua ya kuwasamehe. Mwishowe, Ibn Ziyad aliandika barua kuhusu watu hao.

Kabila la Shimr pia lilikuwa na nasaba ya mbali na kabila la Ummul Banin. Hivyo, alipata barua pia ya msamaha kutoka kwa Ibn Ziyad na akawasili Karbala akiwa na barua hii mnamo alasiri, tarehe tisa ya Muharram.

Wakati mtu huyu mwenye kutia kinyaa alipofika karibu na kambi ya Imam Husain alisema kwa sauti ya kupaza, "Wapo wapi watoto wa dada yangu?"[214] Mtukufu Abbas alikuwa ameketi karibu na Imam Husain (a.s.) akiwa na kaka zake. Hapana yeyote aliyejibu. Halafu Imam Husain (a.s.) akasema, "Mpe jibu hata kama yeye ni mkosaji."

Imam Husain (a.s.) alipotoa ruhusa, wote walijibu, "Unajaribu kusema nini?" Akasema, "Nimeleta habari njema kwenu. Nimeleta barua ya msamaha wenu kutoka kwa Gavana, Ubaidullah Ibn Ziyad. Mko huru. Mkiondoka na kwenda zenu sasa, maisha yenu yatakuwa yameokolewa."

Wote walijibu kwa pamoja, "Tunamuomba Mwenyezi Mungu akulaani wewe, Amir wako na barua yako ya msamaha ambayo umeleta. Hivi tumwache Imam wetu na ndugu yetu kwa sababu tu ya kuokoa maisha yetu?"

### USHUJAA WA MTUKUFU, ABBAS

Mtu wa kwanza kutangaza kumuunga mkono Imam Husain (a.s.) mnamo mkesha wa siku ya Ashura alikuwa ni ndugu yake, Mtukufu Abbas. Hata kama yote yale yaliyotajwa kuhusu yeye kwa kukuzwa yatapuuzwa, inajulikana sana katika historia kwamba Mtukufu Abbas alikuwa na tabia njema

[214] *Luhuuf*, uk. 88; *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk.391; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 389.

sana; alikuwa jasiri, kijana mrefu na sura ya kupendeza. Alikuwa amejipatia lakabu ya 'mwezi wa Bani Hashim.' Sasa huu ni ukweli ambao hauna shaka ndani yake na pia haukutiwa chumvi. Bila ya shaka yoyote, alikuwa mrithi wa ujasiri wa Ali (a.s).[215]

Pia ni ukweli kwamba Imam Ali (a.s.) alimwambia kaka yake Aqiil, "Nitafutie mke ambaye anatoka kwenye nasaba ya mwanamume jasiri"[216] na Aqiil alimchagua Ummul Banin. Alithibitisha sawa kabisa kama alivyokuwa anataka Imam Ali (a.s.). Imam alitamani kwamba mke huyo azae mtoto mwanamume aliyejasiri.[217] Yote yaliyosimuliwa hadi hapa ni ukweli na matamanio ya Imam Ali (a.s.) yalitimia katika umbile la Mtukufu Abbas.

## MWEZI WA BANI HASHIM NA USAWA

Kufuatana na riwaya moja au mbili, Mtukufu, Abbas alikwenda kwa Imam Husain (a.s.) mnamo siku ya Ashura na akaomba, "Mpendwa kaka! Tafadhali niruhusu niende kwenye Jihadi. Kifua changu sasa kinadhikika. Ninahisi kukabwa roho. Siwezi kujidhibiti zaidi ya hapa. Ninataka kujitoa mhanga kwa ajili yako haraka iwezekanavyo." Nani anayejua ni uhitaji kiasi gani aliokuwa nao Imam Husain (a.s.) aliposema, "Ndugu yangu! Nenda kama unataka, lakini fanya mpango wa maji kwa ajili ya watoto." Imam (a.s.) anajua sababu hiyo vizuri zaidi. Mtukufu, Abbas tayari alikwishapokea cheo cha (*Saqqa-e-Haram*) 'mbeba-maji wa nyumba tukufu' kwa sababu mara kadhaa siku za nyuma nyakati za usiku aliweza kupenya katikati ya safu za maadui na kuchota maji na kuyapeleka kambini kwa ajili ya watoto.[Ndio maana pia anaitwa '*Ghaazi*' (mshindi)].

Tangu tarehe 7 ya Muharram, adui alikata huduma ya maji kwa dhuria wa Mtume ambao walikuwa wakikariri kalima yake. Kwa vyovyote vile, katika kumjibu Imam Husain (a.s.) Mtukufu Abbas alisema: "Amri yako imekubalika."

Sasa angalia jinsi mandhari hii inavyoshangaza. Ni ujasiri ulioje! Ni ushujaa gani huu! Ni ubinadamu ulioje huu! Ni heshima kubwa kiasi gani hii! Ni utambuzi mkubwa kiasi gani wa dini na kujitoa mhanga!

[215] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 687; *Al-Abbas*, Muqarram, uk. 81; *Damaus Sujum*, uk. 176

[216] *Absarul Ain*, uk. 126; *Damaus Sujum*, uk. 176

[217] *Absarul Ain*, uk. 26

Simba wa simba wa Mwenyezi Mungu alishambulia jeshi kubwa peke yake na akawafukuza wanajeshi elfu nne ambao walikuwa wanalinda mto. (Baada ya kuwafukuza) aliingia mtoni. (Pia imeandikwa kwenye vitabu kwamba) kwanza alijaza kiriba chake cha maji na kukining`iniza begani kwake wakati yupo juu ya farasi. Uso wa maji ya mto uligusa tumbo la farasi. Alikuwa anahisi kiu. Kulikuwa na joto kali sana. Ameingia mtoni baada ya kupigana vita. Alichota maji kwenye mkono wake alioukunja mithili ya kikombe na kuyaelekeza mdomoni kwake. Maadui walikuwa wanatazama wakiwa mbali kwamba baada ya muda mfupi alimwaga maji hayo kwenye mto Furati na akatoka nje ya mto akiwa bado anayo kiu. Hapana mtu aliyeelewa kwa nini hakunywa maji. Hata hivyo, alipotoka nje ya mto na akaghani shairi lifuatalo la kivita, ndipo watu wakajua kwa nini hakunywa maji:

**"Ewe nafsi ya Abbas! Sitaki ubakie hai baada ya kufariki Husain. Husain anajitayarisha kunywa kikombe cha mauti huku akiwa na kiu na wewe unataka kunywa maji ya baridi kidogo? Ujanadume wa aina gani huu? Hii ni aina gani ya upendo na huba? Hivi Husain ni Imam wako au hapana? Wewe sio mfuasi wa Imam Husain? Hivi wewe siye yule mtiifu wa Husain? Wallahi, dini yangu hainiruhusu kufanya hivi wala utiifu wangu hauwezi kuvumilia kuona kwamba Husain anabaki na kiu na mimi ninywe maji."**[218]

## ABBAS, MWANGALIZI WA KAMBI YA IMAM HUSAIN (A.S.)

Wakati Abbas aliporudi kutoka kule mtoni, alibadili njia yake. Alikwenda mtoni kwa kufuata njia iliyonyooka lakini sasa wakati wa kurudi alipita mahali penye miti na chemchem kwa sababu alikuwa amebeba kitu cha thamani. Alikuwa anajaribu kadiri awezavyo kufikisha maji hayo kambini kwa vyovyote vile na asingeachia mwanya wa hatari ya mshale ambao ungeweza kutoboa kiriba cha maji na kuacha maji yote yapotee. Abbas alikuwa anasonga mbele kwa uangalifu mkubwa lakini ghafla jambo lilitokea na akalia kwa sauti ya kupaza:

[218] *Yanabiul Mawaddah*, Juz. 2, uk. 408

"Wallahi, Hata kama umeukata mkono wangu wa kulia, nitaweza kuendelea kusaidia dini yangu na Imam wa kweli ambaye ni mjukuu wa mtume safi na wa kuaminika."[219]

Baada ya muda kidogo, alibadili shairi lake la kivita kama ifuatavyo:

**"Ewe nafsi ya Abbas! Usiwaogope Makafiri. Furahi kwani ipo rehema ya Mwenyezi Mungu Muweza wa Yote na ukaribu na Utume wa Kweli kwa ajili yako. Kipi cha kukufanya uwe na wasiwasi hata kama maadui wamekata mkono wangu wa kushoto pia kwa sababu ya woga wao?"[220]**

Kwenye shairi hili la kivita, Mtukufu Abbas alisema kwamba mkono wake wa kushoto ulikatwa pia. Imeandikwa kwamba mbeba-maji huyu alijaribu kwa kila njia kuokoa kiriba hicho cha maji. Alikizungusha kiriba kwa ustadi mkubwa kwa mbele yake na kuinama juu yake ili kukizuia kisitobolewe. Ulimi wangu hauna uwezo wa kuelezea tukio hili la kuhuzunisha. Mandhari hii ni ya kusisimua sana na inamfanya mtu kulia machozi ya damu.

Kwa kawaida, mateso ya Mtukufu Abbas husimuliwa mnamo mkesha wa tarehe Tisa.

## NAUHA YA UMMUL BANIN NDANI YA BAQII

Hebu ngoja pia niseme kwamba mama yake Mtukufu Abbas, Bibi Ummul Banin alikuwa hai wakati wa msiba wa Karbala. Hata hivyo, yeye alikuwa Madina. Alipopata habari kwamba wanawe wote wanne wameuawa kishahidi huko Karbala, akawa na kawaida ya kwenda Jannatul Baqii na kulia. Imesimuliwa kwamba kilio chake kilikuwa cha kuhuzunisha sana kwamba yeyote aliyepita karibu naye hapo na kusikia kilio hicho naye pia alilia. Hata Marwan bin Hakam, adui mkubwa wa Ahlul-Bayt mwenye moyo mgumu kama jiwe naye alikuwa akitokwa na machozi machoni mwake. Wakati mwingine Bibi Ummul Banin alikuwa anawakumbuka watoto wake wote na kulia machozi na wakati mwingine alimkumbuka mwanae mkubwa na kulia.

Mtukufu Abbas alikuwa ndiye mkubwa kwa umri na alikuwa bora kuzidi

---

[219] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 40; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 688; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 169

[220] *Biharil Anwar*, Juz. 45, uk. 40; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 688

wenzake kuhusu ukamilifu wa kiroho na kimaumbile. Nitawasomea mojawapo ya nauha ya maombolezo mawili ya bibi huyu, ambayo ninaweza kuikumbuka. Nauha hii lilighaniwa na mama mwenye uchungu. (Kwa kawaida, Waarabu husoma nauha za kuhuzunisha sana).

"Ewe jicho lenye kutazama lililokuwa likiangalia matukio ya Karbala! Nisimulie mimi yale mandhari ambapo Abbas wangu jasiri, na kabla yake, watoto wake (watatu) jasiri wenye nyoyo za simba walivyoshambulia jeshi lile lenye woga. Hivi ni kweli kwamba baada ya mikono ya mwanangu kukatwa, dhalimu mmoja akampiga kichwani kwa rungu la chuma?"

"Oh! Simba wangu jasiri, Abbas, alipigwa kichwani kwa rungu la chuma."

"Ewe Abbas wangu! Ewe kipenzi changu! Ninajua kwamba kama mikono yako yote ingekuwa sawasawa, adui mwenye woga asingeweza kubaki mbele yako. Adui mchafu alithubutu kufanya hivyo kwa sababu tu mikono yako ilikuwa imekatwa."[221]

**Kwa Jina la Mwenyezi Mungu na Kwake Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.)**

[221] *Matahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 689

# MAJILISI 37

## VITENDO VIOVU VYA DHALIMU YAZID

Leo ni mkesha wa mwezi Tisa. Kwa hiyo, ninapaswa kusimulia mateso ya mpiganaji yule wa njia iliyonyooka ambaye ni mashuhuri kabisa katika kutimiza wajibu wa kuamrisha mema na kukataza maovu. Nina nia ya kuzungumza kuhusu Mtukufu Abbas, ambaye Imam amedhihirisha kuridhika kwake kupita kiasi kwake.

Wakati tukio la Karbala lilipotokea, hapakuwepo na njia za mawasiliano kama hizi tulizonazo leo. Habari za Syria zilikuwa zikiwasili Kufa na Madina baada ya muda mrefu. Wakati mwingine, watu walikuwa hawapati hata habari za tukio fulani. Ushahidi mzuri kabisa wa jambo hili ni tukio hili la Karbala. Imam Husain (a.s.) alikataa kutoa kiapo cha utii kwa Yazid na akaondoka Madina na kwenda Makkah. Baada ya hapo, matukio mengi yalitokea na Imam Husain (a.s.) akauawa kishahidi. Watu wa Madina walipopata habari hizi, waliamka kutoka kwenye usingizi mzito, wakafikicha macho yao na kuuliza, "Hivi Imam kweli ameuawa kishahidi? Kwa nini ameuawa kishahidi?" Waliamua kwenda Syria ili wakajue sababu hasa. Watu saba au nane walikwenda Syria kwa madhumuni haya. Baada ya kuuliza kwa muda fulani walikutana na khalifa na wakarudi baada ya kuona hali yote ilivyokuwa. Watu wa Madina walipouliza kuhusu jambo halisi hasa, wakasema, "Tafadhali msiulize hilo. Muda wote tuliobakia Syria, tuliogopa kwamba mawe yangeanguka kutoka mbinguni na tungeangamizwa.[222] (Watu wanakana ukweli wa kauli hii ya Imam Husain (a.s.): "Ninasema kwa heri kwa Uislamu huu nikiwa mbali, ambamo mtawala mchafu, Yazid anawakatili watu kwa mateso Makali."). Walipoulizwa zaidi, wakasema, "Tunarudi baada ya kukutana na mtu ambaye anakunywa mvinyo waziwazi, anacheza na mbwa, anafuga nyani kama wanyama wa nyumbani na anafanya dhambi zote wazi wazi. (Abdullah bin Hanzala Ghasilul Malaika, alikuwa akisema kwamba Yazid hakumuacha hata mama yake). Alizini hata na wanawake ambao ni haramu kwake.[223] Ndio kusema kwamba watu wale walihakikisha

[222] *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 326; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 285.
[223] *Tarikh Khulafa*, Suyut, uk. 205.

kwamba utabiri wa Imam Husain (a.s.) ulikuwa wa kweli kabisa kwa sababu Imam Husain (a.s.) alikuwa anatambua mambo haya siku nyingi kabla.

## UFALME WA BANI UMAYYAH WATIKISWA

Mnamo siku ya Ashura, Imam Husain (a.s.) alisema, "Najua kwamba watu hawa wataniua mimi lakini wao pia wataangamizwa si muda mrefu kuanzia sasa baada ya kifo changu cha kishahidi. Si tu dhuria wa Sufyan lakini Bani Umayyah wote watashindwa," na ilitokea kwa njia hii tu. Baadaye Bani Abbas walikamata ufalme kutoka kwa Bani Umayyah na wakatawala kwa miaka mia tano iliyofuata. Kwa hiyo, inaweza kusemwa kwamba ufalme wa Bani Umayyah ulitikiswa kabisa baada ya tukio la Karbala.

## ATHARI ZA HARAKATI ZA HUSAIN ZAENEA NDANI YA NYUMBA YA ADUI

Ni uzito gani wa matokeo unaweza kuwa mkubwa zaidi wa tukio la Karbala kuliko ukweli kwamba lilisababisha tofauti miongoni mwa Bani Umayyah na kulipatia tukio hilo nguvu ya kiroho na kimaadili? Hebu tuchukue mfano wa Ibn Ziyad ambaye alikuwa mashuhuri kwa ugumu wa moyo wake. Kaka yake Uthman bin Ziyad alimwambia:

"Ninatamani kwamba dhuria wote wa Ziyad wakumbwe na masikini, huzuni na mabalaa lakini wasipate kashifa na fedheha kwa sababu ya uhalifu huu."[224]

Mama yake Ibn Ziyad, Marjana alikuwa mwanamke mchafu kimaadili. Hata hivyo, wakati mwanae alipofanya uhalifu huu, akasema:

"Ewe mwanangu! Sasa ndio umefanya nini? Kumbuka kwamba hutaweza kunusa hata ile harufu ya Pepo."[225]

Marwan bin Hakam, mtu aliyekuwa muovu daima, alikuwa na ndugu yake aliyeitwa Yahya bin Hakam. Inasimuliwa kwamba alisimama kutoka pale alipokuwa ameketi kwenye baraza la Yazid na akamlaani Yazid akasema, "Ulaaniwe Yazid! Dhuria wa Sumaiyya (watoto wa mama yake Ziyad) na

[224] *Damaus Sujun*, uk. 230
[225] *Damaus Sujun*, uk. 372

mabinti wa Sumaiyya wanastahili kuheshimiwa kwa maoni yako, lakini unawafanyia dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) uovu huu na unawafanya wasimame namna hii kwenye baraza lililojaa watazamaji?"[226] Ndio, sauti ya Husain ilikuwa inasikika kutoka majumbani mwao wenyewe!

Wapendwa wasikilizaji wangu!

Inawezekana mliwahi kusikia tukio la mke wa Yazid, Hinda. Alitoka nje ya nyumba yake na akaenda kwenye baraza na kumlaani sana Yazid hivyo kwamba akakanusha kuhusika na kumuua Husain na akakiri kwamba hakupendezwa na tukio hili na kwamba kitendo hicho kilifanywa na Ubaidullah Ibn Ziyad.[227]

## MTOTO WA YAZID AJITENGA NA BABA YAKE

Utabiri wa mwisho wa Imam Husain (a.s.) ulikuwa kwamba Yazid angefariki dunia baada ya muda mfupi. Hatimaye, Yazid alitawala kwa miaka miwili au mitatu takriban na akaelekea jahannam mwishowe. Mwanae, Muawiyah bin Yazid alikuwa ndiye mrithi mstahiki. Na Muawiyah bin Abi Sufyan alikwisha jaribu kila njia kwa hali yoyote ile kuandaa mazingira haya. Alipanda kwenye mimbari siku arobaini baada ya kifo cha Yazid na akasema:

"Enyi watu! Babu yangu Muawiyah alipigana na Ali bin Abi Talib (a.s.) ingawaje hakuwa kwenye njia iliyonyooka. Badala yake Ali alikuwa kwenye njia iliyonyooka. Halafu akaja baba yangu, Yazid akapigana na Husain bin Ali ingawaje baba yangu huyu hakuwa kwenye njia iliyonyooka. Kwa hiyo ninamlaumu baba yangu na ninataka kuwajulisheni kwamba ninajifikiria mimi mwenyewe kwamba ninastahili kwa ukhalifa huu. Sitaki kujiingiza kwenye dhambi kama baba yangu na babu. Hivyo, ninaacha nafasi ya ukhalifa."[228] Alipokwisha kusema hivi, alishuka kutoka kwenye mimbari.

Hivyo, inaweza kusemwa kwamba haya yalikuwa ni matokeo ya nguvu ya damu ya Husain na nguvu ya haki ambayo iliwaathiri marafiki na maadui.

[226] *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 354
[227] *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 355
[228] *Hayatul Haiwan al-Kubra*,Juz. 1, uk. 16

## MASHAHIDI WALIONEA WIVU DARAJA LA ABBAS:

Imam Ja`far Sadiq (a.s.) amesema, "Mwenyezi Mungu na amhurumie ami yangu, Abbas. Alikabiliana na majanga akiwa katika tabasamu na utulivu. Ami yangu Abbas analo daraja karibu ya Mwenyezi Mungu, ambalo linaonewa wivu na mashahidi wote."[229] Wallahi! Kiwango kama hicho cha ujasiri, nia safi na utiifu kama huo! tunavitazama kama matendo ya mfano wa kuigwa. Kamwe hatujachunguza moyo wa msukumo wa Mtukufu, Abbas kwamba tunaweza kukadiria umuhimu wake.

## BARUA YA MSAMAHA KWA WATOTO WA UMMUL BANIN

Mtukufu, Abbas alikuwa ameketi ndani ya hema na Imam Husain (a.s.) mnamo mkesha wa Ashura. Ghafla, kamanda mmoja wa jeshi la adui akaita, "Waleteni Abbas bin Ali na ndugu zake kwangu." Mtukufu Abbas alisikia sauti hiyo lakini akaipuuza na akaendelea kuketi na Imam kwa heshima kabisa. Imam alipoona hivyo akasema, "Unapaswa kujibu hata kama ni muovu."

Mtukufu Abbas alitoka nje ya hema na kumuona Shimr bin Dhiljaushan amesimama hapo. Alikuwa ndugu wa mbali wa mama yake Abbas na alikuwa na uhusiano na kabila lake.

Imesimuliwa kwamba kabla yeye hajaondoka Kufa, alikuwa amechukua barua ya msamaha kwa Mtukufu Abbas na ndugu zake. Alidhani kwamba alikuwa amefanya kazi nzuri sana kwa manufaa ya ndugu zake. Alipomwambia Mtukufu Abbas kuhusu barua ya msamaha, Mtukufu Abbas alimkaripia kwa kusema:

"Mwenyezi Mungu akulaani wewe na yule aliyekupa barua hii ya msamaha! Unafikiri mimi ni mtu gani? Unanifikiriaje mimi? Unadhani mimi nitamuacha Imam na ndugu yangu, Husain bin Ali, peke yake, ili niokoe maisha yangu na kufuatana na wewe? Mama yetu aliyetunyonyesha na kutulea hakutufundisha hivi."[230]

---

[229] *Safinatul Bihar,* Juz. 2, uk. 155 na *Al-Abbas*, Muqarram, uk. 69 (Hadith hii imesimuliwa kutoka kwa Imam Zainul Abidiin na sio kutoka kwa Imam Ja`far Sadiq (a.s.) *Nafasul Mahmoom*, uk. 204.

[230] *Luhuuf*, uk. 88; *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 391; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 389

## MASHAIRI YA KUHUZUNISHA YA UMMUL BANIN

Imam Ali (a.s.) alikuwa na watoto wa kiume wanne aliozaa na Ummul Banin. Waandishi wa historia wameandika kwamba Imam Ali (a.s.) alimpa kaka yake Aqiil ombi maalum kumtafutia yeye mke[231] ambaye angetokea kwenye dhuria ya walio majasiri ambao wamerithi ushujaa" ili anizalie mtoto jasiri."[232]

Ingawaje haipatikani katika historia kwamba Imam Ali (a.s.) alieleza lengo lake, watu wanaojua tabiri za Imam (a.s.) na kuziamini wanasema kwamba Imam Ali (a.s.) alijua kuhusu hayo tangu mwanzo. Aqiil alimchagua Ummul Banin na akamwambia Ali (a.s.). "Huyu ndiye mwanamke kama anayetakiwa na wewe." Alizaa watoto wanne na miongoni mwao akiwemo Mtukufu Abul Fazl al-Abbas ambaye alikuwa ndiye mkubwa. Watoto hao wote wanne waliuawa kishahidi hapo Karbala wakiwa upande wa Imam Husain (a.s.). Zamu ya Bani Hashim ilipofika ya kwenda kwenye uwanja wa vita, Mtukufu Abbas aliwaambia ndugu zake, "Enyi ndugu zangu! Nataka nyinyi wote mwende kwenye uwanja wa vita kabla yangu kwa sababu nataka kuteseka kwa jeraha la kifo cha kishahidi cha ndugu zangu." Wao wakajibu, "Tutafanya kama unavyoagiza." Hivyo, wote watatu walikwenda kwenye uwanja wa vita na kuuawa kishahidi.[233] Baada ya hapo, Mtukufu Abul Fazl al-Abbas aliondoka kwenda kupigana.

Wakati Ummul Banin alipopata habari kwamba watoto wake wote wanne walikufa kishahidi huko Karbala pamoja na Imam Husain (a.s.), alianza kuomboleza kwa ajili yao. Akawa na mazoea ya kwenda Jannatul Baqii au kuketi kwenye barabara iendayo Iraq na kuwakumbuka na kuwaomboleza wanawe. Wanawake wengine walikusanyika karibu naye walipomuona akilia kwa huzuni kubwa mno.

Marwan bin Hakam, gavana wa Madina na adui mkubwa sana wa Ahlul-Bayt pia alikuwa na mazoea ya kulia kila anapokuwa akisikia mashairi ya bibi huyo kila alipopita karibu na Jannatul Baqi. Mojawapo ya mashairi hayo ni kama ifuatavyo:

[231] *Absarul Ain*, uk. 62; *Damaus Sujum*, uk. 176

[232] *Absarul Ain*, uk. 62

[233] Majina ya ndugu zake Mtukufu Abbas yalikuwa: Uthman, Ja`far na Abdullah. *Malimul Madrasatain*, Juz. 3, uk. 160

"Enyi mabibi! Sasa msiniite Ummul Banin. Mama wa watoto wanamume huitwa Ummul Banin, mama wa watoto mashujaa. Mnaponiita mimi kwa jina hili, huwakumbuka watoto wangu jasiri na moyo wangu umevunjika-vunjika. Ndio, ni kweli nilikuwa naitwa Ummul Banin wakati fulani, lakini sasa sibakii tena kuwa yule 'mama wa watoto wa kiume."[234]

Kwenye shairi maalum kwa ajili ya Mtukufu Abbas anasema:

"Ewe jicho lenye kutazama lililokuwa likiangalia matukio ya Karbala! Nisimulie mimi yale mandhari ambapo Abbas wangu jasiri, na kabla yake, watoto wake (watatu) jasiri wenye nyoyo za simba walivyoshambulia jeshi lile lenye woga. Hivi ni kweli kwamba baada ya mikono ya mwanangu kukatwa, dhalimu mmoja akampiga kichwani kwa rungu la chuma?"

"Oh! Simba wangu jasiri, Abbas, alipigwa kichwani kwa rungu la chuma."

"Ewe Abbas wangu! Ewe kipenzi changu! Ninajua kwamba kama mikono yako yote ingekuwa sawasawa, adui mwenye woga asingeweza kubaki mbele yako. Adui mchafu alithubutu kufanya hivyo kwa sababu tu mikono yako ilikuwa imekatwa."[235]

**Kwa Jina la Mwenyezi Mungu na Kwake Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.)**

---

[234] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 689

[235] *Matahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 689

# MAJILISI: 38

## ASHURA, SIKU YA MASHAHIDI

Kwa nini tumekusanyika hapa leo? Huu ni usiku gani? Leo ni usiku wa mashahidi. Katika dunia yetu ya leo ni desturi ya kawaida kuadhimisha siku fulani kila mwaka kuonyesha moyo wa utii na heshima. Kwa mfano, tunasherehekea Siku ya Mama, Siku ya Walimu na Siku ya Kazi. Hata hivyo, kamwe hatujaona jamii yoyote ikiadhimisha Siku ya Mashahidi. Ingawaje umma wa Kiislamu huadhimisha siku ya Ashura kama Siku ya Mashahidi, kwa njia hii, usiku wa leo ni usiku wa mashahidi.

### MANTIKI YA KIFO CHA KISHAHIDI

Kwenye mojawapo ya hotuba zangu nimesema kwamba mantiki ya kufa kishahidi msingi wake umo kwenye "Mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu" kwa upande moja na kwa upande mwingine ni muongozo wa jamii. Kama shaksia ya mwana mageuzi na Sufii (*Gnostic*) zikikusanyika na kuwa ndani ya mtu mmoja, basi mtu huyo ataitwa 'Shahidi'. Mmojawao anaweza kuwa Muslim bin Awsaja, mwingine Habib bin Mudhahir, mwingine wao akiwa Zuhair bin Qayn...kwa sababu daraja za mashahidi wote si sawa na kuna viwango tofauti ndani yake.

### MKESHA WA ASHURA

Imam Husain (a.s.) alikwisha shuhudia kwa ajili ya "mashahidi wa Ashura" usiku uliopita, jambo ambalo linaonyesha daraja la mashahidi hao. Mashahidi wanaonekana wanang`aa kwa uchangamfu miongoni mwa watu waadilifu na wanaoheshimiwa ambapo masahaba wa Husain wanaonekana wakimeremeta zaidi miongoni mwa mashahidi wote.

Unajua Imam Husain (a.s.) alisema nini? Alisema nini kuhusu masahaba wake? Wale ambao walikuwa hawafai kufa kishahidi walimuacha Imam Husain (a.s.) wakati wa safari ya kwenda Karbala na wale waliokuwa wanafaa

kupata heshima hiyo waliendelea kuwa na Imam hadi mwisho. Hata hivyo, Imam Husain (a.s.) aliwatahini kwa mara ya mwisho. Safari hii hakuna hata mmoja aliyeondoka baada ya kutahiniwa.

## VIRIBA VYA MAJI VITUPU

Imam alifanya nini katika mkesha wa Ashura? Wale ambao wameandika "Aliwakusanya masahaba wake karibu na hema la maji," wanasema kwamba palikuwepo na hema moja kama hilo kwenye kambi ya Imam Husein (a.s.) ambalo lilikuwa na viriba vitupu vya maji.[236] Viriba vya maji viliwekwa ndani ya hema hilo tangu siku ya kwanza na liliitwa hema la maji. Imam (a.s.) aliwakusanya masahaba na wasaidizi wake ndani ya hema hilo katika mkesha wa siku ya Ashura. Hata hivyo, sijui ni kwa nini alifanya hivyo. Huenda aliwakusanya kwa sababu hapakuwepo na viriba vyenye maji ndani ya hema hilo usiku huo.

Hata kama tukichukulia maelezo mengine kwamba: "Aliwakusanya masahaba wake vile usiku ulipoingia," basi hiyo pia inaendana na simulizi iliyopita.[237]

## HOTUBA YA IMAM HUSAIN (A.S.) KATIKA MKESHA WA ASHURA

Imam Husain (a.s.) aliwakusanya masahaba wake waaminifu ndani ya hema moja na akatoa hotuba yenye lugha fasaha. Kwa kweli, hotuba hii ilikuwa ni matokeo ya matukio yaliyotokea mnamo nyakati za Alasiri ya tarehe Tisa.

Muda ulioongezwa na adui ungekwisha jua linapochomoza kesho yake ambayo ni siku ya Ashura. Kwa hiyo, Imam aliwakusanya masahaba wake ili awape taarifa kuhusu hali ya mambo na kuwatahini kwa mara ya mwisho. Imam Zainul Abidiin (a.s.) anasimulia kwamba Imam Husain (a.s.) alikuwa amewakusanya masahaba wake ndani ya hema, ambalo lilikuwa karibu na hema lake. Baba yake alimtukuza Mwenyezi Mungu na akasema, "Ninamtukuza Mwenyezi Mungu na kumshukuru Yeye wakati wa neema na wakati wa shida. Ewe Allah! Ninakushukuru kwamba Wewe ulitupatia sisi utume, ukatufundisha Qur`ani Tukufu na kutufanya tuielewe dini."[238]

---

[236] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 625; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 395

[237] Baadhi ya maneno ya Ustaadh Mutahhari hayakujumuishwa hapa ili kuepuka kurudia maneno kwa sababu falsafa ya kifo cha kishahidi cha Ustaadh Shahiid tayari kimechapishwa na *Jam'e Talimaat-e-Islami*, Pakistan.

[238] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 625; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 395

Mtu anayefuata njia ya haki na ukweli, hata akiwa katika mazingira na hali yoyote ile, kwake yeye mambo yatakuwa sawa tu. Mtu mkweli hutambua vema wajibu wake katika hali yoyote ile na lolote litakalotokea njiani kumkabili, kwake yeye sio baya.

## JIBU LA IMAM HUSAIN (A.S.) KWA FARAZDAQ

Imam Husain (a.s.) alipokuwa anaelekea Karbala alitamka kauli katika kumjibu mshairi mashuhuri, Farazdaq, jibu ambalo linastahili kuzingatiwa. Wakati Farazdaq alipomuambia Imam (a.s.) kuhusu mazingira mabaya ya Iraq, Imam akasema:

"Endapo ikitokea hali ya mambo kutupendelea sisi tutamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hiyo na kutaka msaada Wake katika kumshukuru, na endapo mambo yatakuwa dhidi yetu; hata hivyo pia hatutakuwa wenye hasara kwa sababu nia zetu ni njema na dhamira safi. Lengo letu si lolote isipokuwa uadilifu unaotokana na uchaji Mungu. Kwa hiyo, lolote litakalotokea katika njia hii ni jema wala si hasara. Sisi tunamshukuru Mwenyezi Mungu katika hali yoyote ile nzuri au mbaya."[239]

"Nilikuwa ni mja wake mwenye kushukuru wakati wa raha na vilevile hata katika siku za matatizo." Hivyo, Imam (a.s.) alitaka kusema, "Nimeona siku za furaha na amani katika maisha yangu kama siku zile nilizokuwa ninaketi kwenye mapaja ya Mtume (s.a.w.w.) au nikipanda kwenye mabega yake. Nimekuwa katika mpito wa nyakati hizo nilipokuwa mmojawapo wa watoto waliopendwa sana katika ulimwengu wa Kiislamu. Nilimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku zile na pia kwa siku hii ya leo ambapo nimezungukwa na mabalaa. Siyachukulii mazingira haya kuwa ni mabaya kwangu. Badala yake ninayachukulia kuwa ni mazuri. Ee Mola! Tunakushukuru kwa kutupatia heshima ya utume katika familia yetu na kwamba ulitunawirisha kwa elimu ya Qur`ani. Ni sisi tu tulio na utambuzi kamili wa Qur`ani Tukufu. Ee Mola! Tunakushukuru Wewe kwa kutupatia utambuzi na uelewa wa dini na kutuwezesha sisi kufika kwenye vina vyake ili kwamba tuweze kuelewa roho yake na kiini cha ndani zaidi, ambavyo ndiyo ukweli halisi.

[239] *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 336

## USHUHUDA WA IMAM HUSAIN (A.S.) KUHUSU MASAHABA NA WATU WA NYUMBA YAKE

Unajua Imam alisema nini baada ya hapo? Baada ya hapo, Imam Husain (a.s.) alishahidilia kwa ajili ya masahaba na Ahlul-Bayt wake na akasema, "Hakika, sijaona masahaba watiifu na bora zaidi ya masahaba wangu."[240]

Katika maneno yake Imam (a.s.) alitaka kusema, "Enyi masahaba wangu, nyinyi ni bora sana kuliko masahaba wa babu yangu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wale ambao waliuawa kishahidi. Nyinyi ni bora kuliko masahaba wa baba yangu, Ali al-Murtaza na bora kuliko masahaba waliouawa kishahidi kwenye vita vya Jamal, Siffiin na Nahrawan, kwa sababu mazingira mnayokabiliana nayo ni tofauti kabisa na yale waliyokabiliana nayo."

Halafu Imam (a.s.) alishuhudia kwa niaba ya Ahlul-Bayt wake na akasema: "Pia sijapata kuona watu wa nyumba walio bora na wakamilifu hasa katika kutimiza haki za undugu wa damu, zaidi ya watu wa nyumba yangu. Haijapata kutokea watu wa nyumba ya mtu mwingine kuwa na cheo na hadhi kama watu wa nyumba yangu." Hivyo, Imam (a.s.) alithibitisha hadhi ya masahaba na watu wa nyumba yake watiifu na wakati huohuo akawashukuru pia.

## YEYOTE ANAYETAKA KUONDOKA YUKO HURU KUFANYA HIVYO

Baada ya hapo, Imam alitupa jicho kwenye mkusanyiko ule na akasema: "Enyi watu! Ninataka kuwapeni taarifa nyinyi wote kwamba adui hamtaki mtu yeyote isipokuwa mimi. Wanachotaka tu ni Husain kutoa kiapo cha utii kwao na mimi kamwe sitafanya hivyo. Ni mimi tu ambaye wananifikiria kuwa kikwazo kwenye njia yao. Kama wakinipata mimi, basi hawatakudhuruni nyinyi. Kwa hiyo, mimi ninakuondoleeni mzigo wa kiapo cha utiifu kwenye shingo zenu. Sasa nyinyi hamna shinikizo kutoka ama kwa adui wala upande wangu mimi. Mpo huru. Mnaweza kwenda popote mnapotaka kwa furaha kabisa."

Baada ya hapo, Imam (a.s.) alisisitiza kwa masahaba wake kwamba kila mmojawao ashike mkono wa mtoto kutoka familia yake mwenyewe na

240 *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 231; Luhuuf, uk. 90; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 395

kuondoka kwenye tatizo hili. Hapa ndipo wakati ambapo daraja na heshima ya masahaba wa Imam Husain (a.s.) linapoweza kueleweka. Hawakushinikizwa na adui wakati ule ambapo tungeweza kusema kwamba walikuwa wameangukia kwenye mtego wa fumbato la maadui. Na Imam Husain (a.s.) pia naye akawaacha wawe huru kutokana na wajibu wa kiapo cha utii kutoka kwao.

## FURAHA YA IMAM HUSAIN (A.S.) ILIONGEZEKA MARA DUFU

Furaha ya Imam Husain (a.s.) iliongezeka zaidi kwenye mkesha wa Ashura na siku ya Ashura. Sababu ya kwanza ya kumfanya Imam awe na furaha ni kwamba masahaba wote pamoja na watoto wadogo na hata wazee walimzunguka. Pili, Imam (a.s.) hakuona hata chembe ya unyonge miongoni mwa masahaba wake. Hapakuwepo na yeyote miongoni mwa masahaba wa Imam Husain (a.s.) mnamo siku ya Ashura ambaye angejiondoa katika kundi lake au kujiunga na jeshi la adui. Kinyume chake, Imam (a.s.) aliwavutia watu wengi kutoka kwenye kambi ya adui kupitia imani yake yenye mvuto kama wa sumaku. Hurr alikuwa mmojawapo wa watu hao. Imeandikwa kwamba takribani watu thelathini walijiunga na Imam Husain (a.s.) katika mkesha wa Ashura na hali hii ilizidisha furaha ya Imam Husain (a.s.).

## MASAHABA WAONYESHA UTIIFU WAO

Baada ya kusikia maneno ya Imam Husain (a.s.), kila mtu alijibu mmoja baada ya mwingine wakisema, "Bwana! Hivi unasema kwamba sisi tuondoke tukuache wewe peke yako? Hapana, Wallahi! Maisha haya hayatoshelezi kuwa mhanga kwa ajili yako. Kutolewa muhanga kwa ajili yako mara moja tu si chochote chenye uzito wa kutosha." Mwingine akasema, "Mimi ningependa kuuawa mara elfu moja mfululizo na kuhuishwa mara elfu moja ili niweze kujitoa mhanga kwa ajili yako kila ninapokuwa hai."

Mtu wa kwanza kuanza mazungumzo na kudhihirisha fikira hii alikuwa Bwana Abbas. Baada yake, masahaba wengine walirudia maneno yake au walisema kwa kufuata mkondo mmoja. Huu ulikuwa ndio mtihani wa

mwisho ambao masahaba na watu wa familia ya Mtume (saww) ilibidi waupitie.

Walipotangaza dhamira na uungaji mkono wao, Imam Husain (a.s.) pia alianza kuyafichua matukio ambayo yangejitokeza kesho yake na akasema: "Ningependa kuwapeni habari nyinyi wote kwamba wote nyinyi mtauawa kishahidi kesho." Baada ya kusikia haya, wote walisema, "Shukurani ziende kwa Mwenyezi Mungu, Mola wa Walimwengu, kwamba kesho tutatoa mhanga maisha yetu kwa ajili ya mwana kipenzi cha Fatima."[241]

## KWA NINI IMAM HUSAIN (A.S.) ALIWARUHUSU MASAHABA KUBAKIA?

Hapa kuna nukta inayofaa kuzingatiwa. Kama mantiki ya kufa kishahidi haieleweki watu wangesema kwamba kama Imam Husain (a.s.) alikuwa anakwenda kuuawa kishahidi kwa vyovyote vile kulikuwa na sababu gani ya kubakia na masahaba wake? Isipokuwa kwamba na wao watauawa kishahidi katika mchakato huo. Kwa nini hata hivyo Imam Husain (a.s.) aliwaruhusu masahaba wake kubaki naye? Kwa nini hakuwalazimisha kuondoka? Kwa nini hakusema, "Adui hana ugomvi wowote na nyinyi na hakuna hata chembe ya faida kubakia kwenu nyinyi na mimi. Kama mkikaa na mimi hapa hakutakuwepo na athari yoyote isipokuwa na nyinyi mtauawa kishahidi. Kwa hiyo, mnapaswa kuondoka. Ni wajibu wenu kuondoka na kinyume cha sharia nyinyi kubaki hapa."

Endapo mtu kama vile sisi angekuwa katika nafasi ya Imam Husain (a.s.), angeketi kwenye kiti cha mwanasheria na, angechukua kalamu na kuandika: "Ninatoa hukumu kwamba ni kinyume cha sheria kwa masahaba kukaa hapa na ni wajibu kwa wao kuondoka na kwenda zao. Kama mkiendelea kubakia hapa, safari yenu itahesabiwa kuwa ni safari ya dhambi na itakuwa ni wajibu kwenu kuswali swala kamili badala ya swala ya safari." Hata hivyo, Imam Husain (a.s.) hakufanya hivyo. Badala yake aliwaambia masahaba na Ahlul-Bayt wake kuwa tayari kufa kishahidi. Hii inathibitisha kwamba mantiki ya kifo cha kishahidi ni mantiki tofauti.

[241] *Luhuuf*, uk. 91; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 400; *Muntahaiul Amaal*,Juz. 1, uk. 626.

## KIFO CHA MFIADINI (SHAHIDI) KINATIA UHAI KWENYE JAMII

Wakati mwingine, baadhi ya watu huuawa kishahidi ili kuweza kuamsha moyo wa Jihadi ndani ya jamii iliyolala au kutoa kafara ili kuipatia nuru ya imani au uhai mpya. Hali kama hiyo ndio iliyokuwepo Karbala.

Kufa kishahidi si tu ni kwa ajili ya kumshinda adui. Inajumuisha kuamsha moyo wa Jihadi. Kama masahaba na Ahlul-Bayt wa Husain wasingeuawa kishahidi katika siku hiyo, dunia ya moyo wa kufa kishahidi ingewezaje kukaliwa na watu?

Ingawaje msingi wa ufiadini (Shahada) ni ile nafsi yenye kuheshimiwa ya Imam Husain (a.s.), masahaba waliongeza uzuri wa kifo chake cha kishahidi. Kama wasingeuawa basi na Shahada ya Imam Husain (a.s.) isingepata na ukuu na umaarufu ambao inao hadi Siku ya Hukumu. Watu wataendelea kuja na kutafuta msukumo na moyo mpya kutoka humo kwenye kivuli ambamo wanaweza kutembea pia.[242]

Marafiki! Kwa ajili ya maji ya Furati

Kwa ajili ya kiu ya dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

Kwa ajili ya uzima ndani ya damu ya Shabbir

Kwa ajili ya Ujana wa Akbar

Chukua msaada kutoka misukumo ya nyoyo inayoongezeka

Ndiyo, shikilia, shikilia kwa Husain

Uzuri wa dunia hii ni kwa sababu ya Mapambano

Kila sekunde iwe Badr na kila pumzi iwe ni Hunain

Songa mbele katika kutafuta kuikamata magharibi

Nyoyo zenu lazima ziongoke na ndimi zenu lazima zitamke: "Yaa Husain!"

Wewe ni Haidari; pasua kifua cha Ibilisi

Ng`oa mlango wa Khaiber hii mpya

[242] *Qiyam O Inqilab-e-Mahdi az Deedgah Falsafa-e-Tarikh*, uk. 124-134

Uchunguzi wa vita lazima uendelee kama ifuatavyo
Kila shambulizi lazima liwe kamili na kila pigo liwe la kutetemesha
Jeshi dhalimu linajaribu kutoroka
Ewe damu! Kuwa moto zaidi! Ewe pigo la moyo! Piga haraka zaidi!
Shetani wa dhulma anatetemeka. Na asifanikiwe kupata kimbilio!
Zimwi la fitina linatetemeka. Na lisifanikiwe kupata kimbilio!
Hakuna nafasi ya ucheleweshaji, Enyi watu jasiri!
Umri unaita,"Songa mbele! Songa mbele!"
Ujana unatoa mshindo; songa mbele
Nguruma kama radi na nyesha baada ya radi
Ndiyo, ngurumeni kama simba aliye jeruhiwa, Enyi marafiki!
Toa sauti, sauti ya mgongano wa Zulfiqar, Enyi marafiki
Enyi wabebaji wa moto unaowaka! Songeni mbele
Enyi washindi wa dhoruba nzito! Songeni mbele
Enyi ulio na nguvu mlizopewa na Mwenyezi Mungu! Songeni mbele
Choma huo upanga kwa nguvu kwenye kifua cha Shimr wa leo
Ndiyo, mtupe Yazid ndani ya Jahannam, mtupe.

[Hii ni tungo ya kishairi wa Josh Malihabadi]

# MAJILISI 39

## TAREHE TISA YA IMAM HUSAIN (A.S.)

Enyi waombolezaji!

Tarehe Tisa ya Muharram ni siku ya majuto kwa Ahlul-Bayt. Imam Ja`far Sadiq (a.s.) amesema, "Babu yangu, Imam Husain (a.s.) alizungukwa kutoka pande zote mnamo tarehe 9 ya Muharram,"[243] Batalioni zilikuwa zinaingia moja baada ya nyingine hapo Karbala kumsaidia Umar bin Saad. Hata hivyo, hapakuwepo na yeyote wa kuwasaidia Ahlul-Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Wakati wa Alasiri (mwishoni mwa mchana) wa tarehe 9 Muharram, mtu aliyelaaniwa tangu mwanzo hadi mwisho aitwaye Shimr bin Dhiljaushan, aliwasili Karbala na akamkabidhi barua Umar bin Saad. Shimr alitarajia kwamba Umar bin Saad angesema, "Sitapigana na Husain." Hapo basi angemuua Umar bin Saad kama alivyoagizwa na Ibn Ziyad na yeye kuchukua madaraka ya kuongoza jeshi. Hata hivyo, Ibn Saad aliingalia barua na kusema: "Nadhani barua yangu ilimuathiri Ibn Ziyad lakini kwa sababu ya wewe kuwepo pale haukumruhusu kubadili mawazo yake." Shimr akauliza, "Nia yako ni ipi sasa?" Umar bin Saad akasema, "Wallahi, nitapigana kwa namna ambayo kichwa na mikono vitakatwa na kuruka hewani." Shimr akauliza, "Nifanye nini sasa?"

Umar bin Saad alijua pia kwamba Shimr alikuwa na cheo kikubwa karibu na Ubaidullah Ibn Ziyad kwa sababu wote wawili walikuwa wa aina moja. Wale wenye mioyo migumu zaidi wapo karibu zaidi na kila mmojawao. Umar bin Saad akasema, "Wewe ongoza kikosi cha askari wa miguu." Amri ya Ibn Ziyad ilikuwa kali sana. Ilikuwa imeandikwa: "Lazima muanze kumnyanyasa na kumsumbua Husain mara kwa mara baada ya kupokea barua yangu. Husain anapaswa kupewa masharti mawili – atoe kiapo cha utii au apigane. Hakuna chaguo jingine."[244]

[243] *Kafi*, Juz. 147; *Wasailush-Shia*, Juz. 7, uk. 339; *Miratul Uquul*, Juz. 16, uk. 362; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 624.

[244] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 229

## KITU GANI KILITOKEA MNAMO ALASIRI YA TAREHE TISA?

Inasimuliwa kwamba jua lilikwishaanza kuzama mnamo tarehe 9 ya Muharram. Imam Husain (a.s.) alikuwa ameketi kupumzika huku akiwa ameegemeza mikono na kichwa chake kwenye magoti yake nje ya hema. Alikuwa anahisi kusinzia. Wakati huo huo Umar bin Saad alisoma barua iliyotoka kwa Ibn Ziyad na akaita kwa sauti kubwa ya kujiamini hasa; "Enyi jeshi la Allah! Pandeni farasi wenu kwani ninakupeni habari njema za Peponi."[245] (Kauli hii ilitumiwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa anawahutubia masahaba wake kwenye mojawapo ya vita. Angalia uongo wa Umar bin Saad). Imaendikwa kwamba jeshi dhalimu lenye wapiganaji elfu thelathini lilikuwa limezigira Imam kutoka pande zote. Jeshi la Umar bin Saad liliamshwa na wito wa Umar bin Saad kama bahari inavyokuwa kali wakati wa dhoruba. Ghafla, uwanja wote wa vita ulijaa kelele za kwato, miito ya watu na sauti za migongano ya silaha.

## HALI YA BIBI ZAINAB MNAMO MKESHA WA ASHURA

Bibi Zainab alikuwa shughulini akimhudumia Imam Sajjad (a.s.) kwenye mojawapo ya mahema. Mara aliposikia kelele hizo, alikimbia kwenda kwa Imam Husain (a.s.), akamtikisa bega lake na akasema, "Ewe kaka! Unazisikia sauti hizo? Hebu angalia kuna nini huko nje?" Imam Husain (a.s.) alinyanyua kichwa chake kutoka kwenye magoti yake na kujibu bila kulijali hilo jeshi, "Ewe dada yangu! Nilikwisha lala usingizi. Nilimuona babu yangu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye ndoto yangu sasa hivi. Alikuwa anasema: "Ewe Husain! Utakuja kwetu hivi karibuni."[246] Ni Mwenyezi Mungu peke Yake ndiye anayejua Bibi Zainab alikuwa katika hali gani baada ya kusikia maneno haya.

Ndiyo, bila shaka, leo ni mkesha wa Ashura. Huu ni usiku ambao kwamba kama tukiangalia kwa karibu zaidi hali ya mashahidi wa Karbala na moyo wa Jihadi ndani mwao inaweza kutengeneza vurumai katika mioyo yetu kwa upande moja na tutajihisi kuumia sana. Kwa upande mwingine, tut-

[245] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 230; *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 391

[246] *Malimul Madrasatain*, Juz. 3, uk. 109

azama kwenye bahari ya huzuni. Ni dhahiri kwamba mkesha wa Ashura ulikuwa wenye huzuni zaidi kwa Bibi Zainab kuliko usiku mwingine wowote kwa sababu shaksia ya kiroho ya Bibi Zainab ilipata nguvu zaidi mnamo siku hiyo ya Ashura. Iliendelea kuwa na nguvu zaidi jinsi matukio yalivyokuwa yanakuja na kupita.

Mabalaa mawili yalimhuzunisha Bibi Zainab mnamo mkesha wa Ashura na alifadhaika sana. Balaa moja lilitokea wakati wa Alasiri ya tarehe 9 Muharram na lingine lilitokea mnamo mkesha wa Ashura. Imam Husain (a.s.) alianza kufanya matayarisho ndani ya mkesha wa Ashura na aliwaamuru masahaba wake kunoa silaha zao.

Jaun, mtumwa aliyeachiwa huru na Bwana Abu Dhar Giffari alikuwa stadi wa kunoa silaha. Aliketi kwenye hema la peke yake na akaanza kunoa silaha za masahaba wengine. Imam Husain (a.s.) alikwenda kuangalia kazi ya Juan. Imam Sajjad (a.s.) alikuwa anapumzika kwenye hema linalofuatia kwa sababu ya maradhi yake na shangazi yake Bibi Zainab alikuwa anamtunza. Mahema haya mawili yalikuwa karibu sana kwa sababu kufuatana na maagizo ya Imam Husain (a.s.), mahema yalisogezwa na kuwa karibu zaidi hivyo kwamba mambo za hema lingine ziliingia ndani ya hema lililo jirani. Tutaeleza baadaye kwa nini ilifanyika hivyo.

Tukio hili linasimuliwa na Imam Sajjad (a.s.). Yeye anasema, "Shangazi yangu alikuwa ananihudumia wakati baba yangu alipoingia ndani ya hema ambamo silaha zilikuwa zinanolewa ili kumkagua Jaun anavyofanya kazi. Ghafla, nilimsikia baba yangu ananong`ona maneno yafuatayo ambayo aliyarudia mara mbili au mara tatu:

**"Ewe Wakati, aibu kwako kama rafiki! Pale siku inapokucha na machwe ya jua.**

**Ni masahaba au watafutaji wangapi watakuwa maiti!**

**Wakati hautatoshelezwa na chochote mbadala kile.**

**Jambo hili litabakia na Yule Muweza Mwenye nguvu."**[247]

[247] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 232; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 1 "Jambo hili litabakia na Yule Mwenye Uwezo,na kila kiumbe hai kitalazimika kupita njia niliyopita mimi."

Kwenye beti hizi, Imam Husain (a.s.) alionyesha uasi wa dunia hii. Alikuwa na maana kwamba wakati mwingine dunia hutabasamu kama rafiki mwenye huruma na watu hupumbaa na kuanza kufikiri kwamba dunia itabaki kuwa hivyo wakati wote. Hata hivyo, dunia hugeuzia mbali macho yake na inakuwa yenye kukosa huruma. Maisha huwa si matamu tena kama asali na huwa machungu. Marafiki wa kuaminika humuacha mtu peke yake na baadhi huwa maadui wachungu. Hakuna mtu ajuae nini kitatokea kesho. Heshima, mamlaka, afya na kadhalika ni vitu vya kupita. Hivi yupo mtu ambaye hakukutana na kushindwa katika maisha? Hivi yupo mtu yeyote ambaye hakulazimika kustahamili majanga?

Imam (a.s.) anajisemea peke yake kwamba vijana wengi watauawa kishahidi kesho yake.

Imam Sajjad (a.s.) anasema kwamba alielewa lengo la baba yake mtukufu. Alikuwa anatoa taarifa kuhusu kifo chake mwenyewe. Bibi Zainab pia alisikia beti hizi lakini kimya chenye maana kiliendelea baina yetu. Imam Sajjad (a.s.) alikuwa anasongwa na pumzi lakini alidumisha utulivu wake. Moyo wa Bibi Zainab pia ulijaa huzuni lakini hakulia kwa sababu Imam Sajjad (a.s.) alikuwa mgonjwa. Wote wawili walidhibiti machozi yao hadi Bibi Zainab aliposhindwa kuendelea kuvumilia na akaangua kilio kwa sababu alikuwa mwanamke na kimaumbile wanawake wana mioyo ya huruma. Akasema (Bibi Zainab), "Nisingepaswa kuishi na kuiona siku hii." Alikwenda kwa Imam Husain (a.s.) na kusema, "Ndiyo, Ewe kaka! Ningepaswa kufa kabla ya kuona siku hii. Wewe ni kumbukumbu ya wale ambao watakwenda na wewe ni tegemeo letu." Imam (a.s.) alimliwaza akasema, "Ewe dada! Vumilia vinginevyo shetani ataipora subira kutoka kwako."[248] Unasema nini? Kitu gani kinakufanya uwe na huzuni? Kifo ni haki. Babu yangu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa bora kuliko mimi. Baba yangu Ali, Mama Fatima na kaka Hasan walikuwa bora kuliko mimi, lakini wote wamekwenda zao. Mimi pia ninakwenda; lakini Ewe dada yangu! Kumbuka kwamba wewe utapaswa kuongoza msafara huu baada yangu. Utafuatana na msafara huu. Utalazimika kuwaangalia wanangu."

Bibi Zainab alijibu kwa sauti yenye mawimbi:

"Kaka yangu! Mazingira yote haya yalivyo ni mazuri lakini wakati wowote ilipotokea mmoja kati ya wale waliotajwa hapo juu kufariki dunia, wengine walikuwepo pamoja na mimi. Moyo wangu uliendelea kuwa na furaha

[248] *Irshad*, uk. 232; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 403 na *Malimul Madrasatain*, Juz. 3, uk. 114

kukuona wewe baada ya kaka yangu Hasan alipoiaga dunia. Ikiwa na wewe pia unaondoka na kumwacha Zainab peke yake, kitu gani kitakachobakia hapa duniani kwa ajili ya Zainab?"

## KWA NINI IMAM ALIOMBA KUAHIRISHWA KUANZA VITA?

Baada ya kueleza ndoto yake wakati wa Alasiri ya tarehe Tisa kwa Bibi Zainab, Imam Husain (a.s.) alimuita Mtukufu Abbas na kusema, "Ndugu yangu Abbas! Wachukue watu kadhaa na haraka uende nao na uulize kama kuna habari mpya. Kama wanadhamiria kupigana na sisi, waambie kwamba kuanza vita wakati jua linachomoza ni kinyume na kanuni za vita (kwa kawaida, Waarabu walikuwa wakianza vita asubuhi na kurudi kwenye kambi zao wakati jua linapozama). Kwa hakika kuna kitu kipya." Mtukufu, Abul Fazl al-Abbas alifuatana na masahaba kadhaa waandamizi ikiwa ni pamoja na Zuhair bin Qayn na Habib Ibn Mudhahir na wakaenda kwenye jeshi la adui na kusema, "Nimetumwa na kaka yangu kutaka kujua sababu ya shambulio hili la ghafla." Umar bin Saad akasema, "Amiri Ubaidullah Ibn Ziyad ameamuru kwamba kaka yako anapaswa kutoa kiapo cha utii bila masharti ili tusije tukapigana."[249] Mtukufu Abbas akasema, "Usiwe na haraka. Siwezi kusema lolote lile langu mimi sasa. Nitakwenda kwa Abu Abdillah na kupata majibu."

Mtukufu Abbas alirudi na akamueleza jambo hilo Imam Husain (a.s.) ambaye alisema, "Sitatoa kiapo cha utii kwa gharama yoyote ile na nitapigana nao hadi tone la mwisho la damu linabakia mwilini mwangu. Nenda kwao na kama inawezekana, vita iahirishwe hadi kesho asubuhi."[250] Imam Husain (a.s.) hakutaka wao wafikirie kwamba anataka kuishi kwa usiku mmoja zaidi na kwa hiyo, akasema: "Mwenyezi Mungu ndiye anayejua vema zaidi kwamba ninataka muda wa usiku mmoja zaidi kwa sababu ninataka kuzungumza na Mwenyezi Mungu wakati wa usiku wangu wa mwisho wa maisha yangu. Ninataka kuutumia usiku huu katika kuomba dua, kuswali na kusoma Qur`ani."[251]

Mtukufu Abbas aliwasilisha jibu la Imam kwa wale watu. Wao hawakuwa tayari kuahirisha vita hivyo lakini baadaye, tofauti zilijitokeza miongoni

[249] *Malimul Madrasatain*, Juz. 3. uk. 109

[250] *Malimul Madrasatain*, Juz. 3, uk. 110

[251] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 230; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 264; *Malimul Madrasatain*, Juz. 3, uk. 115

mwao. Baadhi yao waliwaambia wenzao, "Wote nyinyi ni watu msio na aibu. Hata kama tungekuwa tunapigana na Makafiri tungekubali kuahirisha vita nanyi hamko tayari kuwapa muda dhuria wa Mtume?" Umar bin Saad alilazimika kusitisha mabishano hayo miongoni mwa maofisa wake. Akasema, "Basi sasa inatosha, vita vitaanza kesho asubuhi."[252]

Usiku huu ulikuwa usiku uliong`ara kipekee kwa Imam Husain (a.s.). Aliutumia akiwa katika shauku kubwa. Watu ambao wametafsiri usiku huu kuwa kama usiku wa Miraji kwa Imam Husain (a.s.) wako sahihi kabisa. Alitoa hotuba yenye fasaha kwa masahaba na Ahlul-Bayt wake wakati wa usiku huo. Kila mmoja alimuaga Imam wakati wa usiku huu na masahaba nao wakamuaga. Imam (a.s.) alisema:

"Enyi masahaba wangu na Enyi Ahlul-Bayt wangu sijui masahaba wowote na Ahlul-Bayt wowote wale bora kuliko wangu. Ninawashukuruni wote. Hata hivyo, nyinyi wote mnapaswa kutambua ukweli. Adui anatafuta damu yangu tu. Hawataki chochote isipokuwa uhai wangu. Ninabatilisha kiapo cha utii kilichotolewa na nyinyi wote. Sasa wote mpo huru. Yeyote anayetaka kwenda anaweza kuondoka. Yeyote miongoni mwenu anayetaka kwenda anapaswa kuchukua na kufuatana na mtu mmoja kutoka miongoni mwa Ahlul-Bayt wangu, kama ikiwezekana." Hata hivyo, hakuna hata sahaba mmoja wa Imam Husain (a.s.) aliyeondoka. Mkono wa Mungu ulikwisha waondosha waoga kutoka kwenye msafara wa Imam (a.s.).

Imeandikwa kwamba wote walijibu kwa pamoja, "Inawezekanaje kwamba sisi tuondoke tukuache peke yako? Mwenyezi Mungu na asiilete siku hiyo ambapo wewe utauawa kishahidi na sisi tuachwe tukiwa hai." Inasimuliwa kwamba Mtukufu Abu Fazl Abbas alikuwa wa kwanza kutoa jibu hili Muslim bin Awsaja alisimama na kusema, "Endapo tunarudi nyuma na kuacha kukusaidia wewe na kukuacha wewe peke yako, tutatoa majibu gani kwa Mwenyezi Mungu? Wallahi, siwezi kukuacha wewe peke yako kwa gharama yoyote ile. Nitachoma na kusukuma mkuki wangu kwenye kifua cha adui yako na nitaendelea kukidhi kiu ya upanga wangu kwa damu yao kwa kadiri muda utakavyoruhusu. Endapo hapatakuwepo na silaha iliyobakia nitawavurumishia mawe kama mvua. Ninaapa Wallahi, sitakuacha wewe ili aone kwamba nimetimiza wajibu wangu kwa mjukuu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yeye akiwa hayupo. Endapo mtu ataniua na halafu akanihuisha tena na akanichoma kwenye moto na apulize majivu yangu hewani na arud-

[252] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 625

ie mlolongo huu mara sabini hapo pia sintasita kwa wasiwasi kukusaidia wewe na kuendelea kuyatoa maisha yangu kwa ajili yako. Sasa ninaelewa kwamba nitauawa mara moja tu na kuwa na furaha daima milele."

Baada ya Muslim bin Awsaja, Zuhair bin Qayn alinyanyuka na kusema, "Ninatamani niuawe na kuhuishwa tena na mlolongo huu uendelee mara sabini lakini wewe na Ahlul-Bayt wako mbakie kuwa salama."

"Wengine pia walitoa mawazo yenye ghera kama hayo. Imam aliwaombea wawe na afya njema na akarudi kwenye hema lake." Maelezo ya 'Qausain' yamechukuliwa kutoka kwenye kitabu cha Dkt. Ibrahim Ayati kiitwacho *'History of Ashura'* kilichochapishwa na Jame Taaliaat-e-Islami.

## UTAMBUZI WA QASIM

Ili tuweze kuhuisha upya muambatano wetu na Muhammad na watu wa nyumba ya Muhammad, usiku wa leo tutasimulia mateso ya yatima wa Imam Hasan(a.s.) Qasim. Kwa kawaida mateso haya husimuliwa kwenye mkesha wa Ashura. Wakati kila mtu alipokwisha kutoa kiapo cha utii kwa Imam, Imam (a.s.) alibadili mtindo wake wa hotuba na akaanza kufichua siri. Imam (a.s.) alisema, "Ninataka kuwataarifuni nyinyi wote kwamba wote mtauawa kishahidi kesho. Hakuna yeyote kati nyinyi mliokusanyika kwenye hema hili atayebaki hai." Kila mtu alitamka kwa kuguta, "Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia heshima ya kufa kishahidi."

(Rafiki mmoja amekumbusha kwamba Ayatullah Aqa Hakim na Ayatullah Allamah Mujahid Amini, mwandishi wa "*Ghadiir*" wanaumwa na wanatibiwa nje ya nchi; kwa hiyo waumini wote wanamume kwa wanawake wawaombee. Ni wajibu wetu kuwaombea viongozi wetu kwa ajili ya kupata nafuu, hususan hivi, "Ewe Mola! Kwa ajili ya Husain bin Ali na kwa ajili ya roho safi ya Qasim, wape afya njema waliotajwa hapo juu na wengine wote ambao wanaugua.)

Mtoto mwenye umri wa miaka kumi na tatu alikuwepo pia kwenye hema hilo. Imam Husain (a.s.) alipotangaza kwamba kila mtu aliyeko ndani ya hema angeuawa kishahidi kesho yake, mtoto huyu alifikiri, "Labda maelezo haya ya Imam (a.s.) yanawahusu watu wazima tu na watoto wadogo kama mimi hawamo." Kwa kawaida mtoto yeyote mwenye umri kama huu angefikiria namna hiyo. Mtoto huyu alinyanyua kichwa kwa huzuni na akauli-

za "Ewe ami yangu! Hivi mimi nimejumuishwa katika wale watakaouawa kishahidi kesho?" Imam alimuangalia mtoto huyo kwa huzuni na kusema, "Ewe mwanangu! Jibu swali langu kwanza ndipo na mimi nitajibu swali lako." Mtoto akasema, "Ewe ami yangu! Tafadhali uliza." Imam akasema, "Mwanangu! Kifo kina ladha gani?" Mtoto alijibu haraka, "Ewe baba mdogo! Kifo kama hicho ni kitamu kwangu kuliko asali." (Mtoto ameweka bayana kwamba sababu iliyomfanya amuulize baba yake mdogo ni kwamba alihofia kwamba angeachwa nje ya heshima hii.) Imam akasema, "Ndiyo, mwanangu! Na wewe pia utauawa kesho. Hata hivyo, utapaswa uvumilie janga kubwa kabla ya hapo." Imam hakueleza janga hilo atakalo kabiliana nalo wakati huo lakini watu walikuja kutambua kwamba tukio hilo ni lipi katika siku ya Ashura.[253]

## "EWE AMI YANGU! NISAIDIE

Qasim aliondoka kwenda kwenye uwanja wa vita. Alikuwa mdogo mno hivyo kwamba hakuna vazi la kivita au helmeti ambalo lilimuenea. Halafu pia, mjukuu huyu wa simba wa Mwenyezi Mungu alipata ushindi wa heshima kuu kwa ajili ya ujasiri wake. Ghafla alishambuliwa kwa pigo la upanga kichwani mwake, hali ambayo ilisababisha ashindwe kukaa sawa juu ya farasi wake na akanguka chini. Imam Husain (a.s.) alikuwa amesimama karibu na hema lake akiwa ameshikilia hatamu za farasi wake akiwa tayari kuondoka katika sekunde yoyote. Ghafla, wito ulisikika "Ewe ami yangu! "Ewe ami yangu! Tafadhali nisaidie."

Inasimuliwa kwamba Imam Husain (a.s.) aliondoka kuelekea kwa Qasim kwa kasi kama mwewe anavyokwenda kwenye windo lake. Hakuna mtu ambaye angeweza kuelewa Imam alifika kwa Qasim kwa kasi ya jinsi gani. Imeandikwa kwamba baada ya Qasim kuanguka chini, alizungukwa na wapiganaji takriban mia mbili wenye farasi wa jeshi la adui. Mmojawao alisonga mbele kutaka kumkata kichwa chake. Ghafla, maadui wakagundua kwamba Husain alikuwa anawashambulia. Baada ya kuona hali hiyo, maadui walianza kukimbia huko na huko kama kundi la mbwa mwitu linavyokimbia linapomuona simba. Yule mtu aliyelaaniwa ambaye alishuka kwenye farasi kutaka kumkata kichwa Qasim alipondwa hadi kufa na kusafirishwa jahanam na kwato za farasi waliowabeba wapiganaji

253 *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 402

wenzake. Palitimka vumbi jingi sana kila mahali hivyo kwamba haikuwa rahisi mtu kuelewa nini kilikuwa kinaendelea. Marafiki na maadui wote walitazama wakiwa mbali. Vumbi lilipotulia, watu waliona kichwa cha Qasim kikiwa kwenye mapaja ya Imam Husain (a.s.). Watu wamlisikia Imam Husain (a.s.) anasema kwa sauti ya juu, "Mpendwa wangu! Ni jinsi gani lisivyovumilika kwa ami yako kwamba ulimuita akusaidie lakini alipofika pale ulipokuwa hakuweza kufanya lolote la kukusaidia wewe."[254]

Enyi waombolezaji!

Inasimuliwa kwamba kichwa cha Qasim kilikuwa kwenye mapaja ya Imam na Qasim alikuwa na wakati mgumu. Halafu, Qasim alikoroma na akaondoka kuelekea kwenye maskani ya mbinguni.[255] Watu walimuona Imam Husain (a.s.) akiubeba mwili wa Qasim mikononi mwake akielekea kambini. Ni tukio la ajabu iliyoje na majuto yaliyoje! Wakati Qasim alipotaka kwenda kwenye uwanja wa vita, Imam Husain (a.s.) aliona vigumu kumruhusu. Halafu kabla ya kutoa ruhusa, wote wawili, baba na mpwawe walilia, wakiwa wamekumbatiana sana hivyo kwamba walipoteza fahamu. Hata hivyo, mandhari hiyo ni tofauti hivi sasa. Baba alionekana amemkumbatia mwanae sio muda mrefu uliopita lakini sasa watu wanamuona Imam huyo anaukumbatia mwili wa mpwawe aliyeuawa kishahidi na mikono ya Qasim ilikuwa inajipweteka, kwa sababu hapakuwepo na uhai kwenye mwili wake.

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**".....Na punde watajua waliodhulumu ni mgeuko gani watakaogeuka?" (Sura Ash-Shu'araa 26 : 227)**

---

[254] Ustadhi Shahidi Mutahhari anasema kwamba palikuwepo na msemaji mashuhuri wa Qum. Alisimulia majanga haya wakati marehemu Ayatullah Haji Shaykh Abdul Karim Haeri alikuwepo. (Alikuwa mtu muadilifu sana. Nimekuja kujua kutoka kwenye vyanzo vingi kwamba alikuwa amejumuishwa miongoni mwa wale waliokuwa na mapenzi yasiyo na ukomo kwa Ahlul-Bayt. Sikuweza kukutana naye kwa sababu nilifika Qum miezi kumi baada ya kifo chake. Hata hivyo, watu ambao walimuona wanasema kwamba mwanachuoni huyu alikuwa na mazoea ya macho yake kujaa machozi kila aliposikia jina la Husain.) Alikuwa akilia sana na kukipiga makofi kichwa chake hadi anapoteza fahamu. Baadaye, alimuomba msemaji asiendelee kusimulia mabalaa hayo wakati yeye akiwepo kwa sababu hawezi kujizuia baada ya kuyasikia.

[255] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 239; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 680; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 463

# MAJILISI 40

## IMAM HUSAIN (A.S.) NI MHAMIAJI (*MUHAJIR*) NA PIA NI MPIGANAJI (*MUJAHID*)

Kutokana na fikira ya mantiki ya Ki-Qur`ani, Imam Husain (a.s.) ni Muhajiri na pia Mujahidi. Alihama kutoka kwenye mji wake na nchi yake kama Nabii Musa. Nchi ya Nabii Musa ilikuwa Misri. Aliiacha na akaondoka kwenda Madayn.[256] Hata hivyo, Nabii Musa alikuwa Muhajiri tu na sio Mujahidi.

Nabii Ibrahim pia alikuwa Muhajiri kwani aliondoka nchini mwake, Babeli.[257]

Hata hivyo, Imam Husain (a.s.) ni wa pekee; kwani alikuwa Muhajiri na pia Mujahidi. Wakati wa siku za mwanzo wa Uislamu, baadhi ya watu walikuwa Muhajirina lakini hawakuwa wapiganaji watukufu kwa sababu amri ya Jihadi ilikuwa haijalazimishwa kwao. Kwa hiyo, wao walikuwa Muhajirina tu. Baadaye, amri ya Jihadi ikalazimishwa na wapiganaji Watukufu wakatokeza pia kutoka miongoni mwa Muhajirina.

Hata hivyo, Husain ni wa kipekee; kwani alikuwa Muhajiri na Mujahidi vilevile. Wakati wa siku za mwanzo za Uislam, baadhi ya watu walikuwa Muhajirina lakini hawakuwa wapiganaji wa vita tukufu kwa sababu amri ya Jihadi ilikuwa bado haijalazimishwa juu yao. Hivyo walikuwa ni Muhajirina tu. Baadae, amri ya Jihadi iliwekwa na wapiganaji watukufu walitoka humo humo kwenye Muhajirina.

Hata hivyo, Husein (a.s.) ndiye pekee tu ambaye alikuwa Muhajir na Mujahid kuanzia ile siku ya kwanza.[258]

---

[256] Basi akatoka, naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Akasema: Mola wangu Mlezi! Niokoe na watu madhalimu. Na alipoelekea upande wa Madyana alisema. Asaa Mola wangu Mlezi akaniongoa njia iliyo sawa. Qur`ani Tukufu Sura ya Qas`as [28:21-22]

[257] Qur`ani Tukufu [Sura ya 99].

[258] "Na mwenye kuhama katika njia ya Mwenyezi Mungu atapata pengi pa kukimbilia na wasaa. Na anayetoka nyumbani kwake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kisha yakamfika mauti, basi umethibiti ujira wake kwa Mwenyezi Mungu…." Qur`ani Tukufu Sura ya Nisa [4;100]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimshauri Imam Husain (a.s.) kwenye ndoto yake, "Ewe mwanangu! Heshima ya pekee iliyohifadhiwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili yako haiwezi kupatikana bila kufa Shahidi."[259]

Imam Husain (a.s.) aliishi kama mhamiaji kwa takriban siku 23 hadi 24 yaani tangu tarehe 8 Zilhajj alipoondoka Makkah hadi alipofika Karbala mnamo tarehe 2 Muharram na halafu kuanzia hapo alipowasili Karbala hadi Siku ya Ashura.

## KIFO CHA KISHAHIDI NI TAJI LA KUJIVUNIA KWETU SISI

Imam Husain (a.s.) alitoa hotuba mashuhuri siku alipoondoka Makkah. Imam alizungumzia kuhusu Hijira na pia Jihadi kwenye hotuba hiyo na akasema:

"Enyi watu! Kifo kimeacha alama kwa dhuria wa Adam kama vile kidani kinavyoacha alama kwenye shingo ya mwanamwali. Ninayo shauku ya kukutana na wahenga wangu kama Ya'kub alivyokuwa katika kukutana na Yusuf. Kifo ni jambo la uhakika kwa binadamu. Hakuna mtu atakayesamehewa kutokana na kifo. Sihofii kifo. Kuuawa Shahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu ni taji la kujivunia juu ya kichwa cha mtu. Kifo ni pambo lenye thamani ndogo (kishaufu) la paji la uso kwa shahidi kama ilivyo kwa kidani kinachovaliwa na mwanamwali. Enyi watu! Ninaona huko mbele kwamba wanyama-pori wanapasua mnofu wangu baina ya Karbala na Nawawis. Furaha ya Ahlul-Bayt, imo kwenye radhi ya Mwenyezi Mungu. Chochote kile anachokipenda Mwenyezi Mungu pia kinapendwa na sisi.[260] Kama anaridhishwa na usalama wetu, na sisi tunaridhia usalama na kama anafurahishwa na maradhi yetu na sisi tutayapenda maradhi. Kama Anataka sisi tunyamaze kimya, tutanyamaza na kama anatutaka sisi tuongee, basi tutaongea. Kama anatutaka sisi tupumzike, tutapumzika na kama anatutaka sisi twende, basi tutakwenda kama mawimbi."

Imam alihitimisha hotuba yake baada ya kutangaza nia yake ya kuhama:

"Yeyote anayetaka kujitoa mhanga katika njia ya Allah kama sisi, yeyote anayetaka kuunganisha sauti yake na sauti yetu, yeyote anayetaka kuhama katika njia ya Allah na kukutana na Mola Wake anapaswa kufuatana na sisi. Inshallah, nitaondoka kesho."[261]

[259] *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 313; na **Suratun-Nisa [4:100]**

[260] Biharul Anwar, Juz. 44, uk. 366; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk. 328

[261] *Luhuuf*, uk. 60; *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 366; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 328

## NI WALE TU WALIO SAFI NDIYO WALIBAKI

Wakati Imam Husain (a.s.) alipoondoka Makkah, alifuatana na idadi kubwa ya watu. Mwanzoni watu wengi walifikiri kwamba Husain bin Ali alikuwa anatia chuku hotuba yake na palikuwepo na uwezekano kwamba ingekuwepo amani kila mahali siku za usoni. Watu wengi waliungana naye njiani lakini Imam Husain (a.s.) hakutaka kufuatana na watu waroho. Alikuwa akichuja masahaba wake kwa kupitia maneno yake wakati wa safari ili kwamba wale watu ambao hawafai kujumuishwa naye kwenye vita watengwe.. Baada ya mchujo wa mara kadhaa, yeyote aliyepita mtihani wa usafi kufuatana na kiwango alibaki kama sahaba mtiifu wa Imam na wengine walimuacha .

## WALIKUWA TAJI LA MASHAHIDI WOTE

Sasa basi, masahaba waliobaki na Imam Husain (a.s.) ni wale tu ambao kuhusu wao Imam alikwisha kushahidilia kwamba alikuwa hajapata kuona masahaba bora na watiifu zaidi kuliko wale. Kwa hiyo, endapo ulinganifu unafanywa baina ya masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ndani ya Badr na masahaba wa Imam (a.s.) ndani ya Karbala, masahaba wa Imam Husain ndani ya Karbala watasemekana kuwa taji la mashahidi wote.

Imam Husain (a.s.) alitoa ruhusa kwa masahaba wake mnamo mkesha wa Ashura na alifuta kiapo cha utii wao kwake. Kwa hiyo, aliweka wazi kwamba adui alitaka kumwaga damu yake tu na hakuwa na lolote kuhusu masahaba. Wakati huo, wote walisema, "Tumechagua kufa kishahidi katika njia yako tu. Uhai hauna maana yoyote ukilinganishwa na kujitoa mhanga kwa ajili yako. Tunatamani tungepata uhai mara elfu moja na mara zote hizo tungejitoa mhanga kwa ajili yako." Mtu wa kwanza kusema hivyo alikuwa ni ndugu yake Imam, Mtukufu Abbas.[262]

Ni furaha ya jinsi gani Imam Husain (a.s.) alikuwa nayo alipoona kwamba alikuwa amefuatana na masahaba ambao walikuwa wanakubaliana na lengo lake. Aliposikia hayo, Imam Husain (a.s.) aliwaambia, "Sasa kwa kuwa mmefanya uamuzi, ninawaarifu kuhusu matukio yatakayotokea kesho. Kwa hakika vita vitapiganwa kesho na hapana hata mmoja wetu atakayebakia hai."[263]

---

[262] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 231; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 626

[263] Allamah Majlisi anasema kwamba Imam Husain (a.s.) aliwafanya wazione nafasi zao ndani ya Pepo. Kwa hiyo, waliona Makasiri yao na bustani zao na neema za Mola Wao ndani ya Pepo. *Muntahaiul Amaal*, Juz, 1,

## HESHIMA KWA MASAHABA WA HUSAIN (A.S.)

Imam alitoa heshima kama hiyo kwa masahaba wake mnamo siku ya Ashura, kwamba iweze kukumbukwa katika historia daima milele. Hizo zilikuwa dakika za mwisho na kila mtu aliuawa kishahidi. Hakuna aliyebaki isipokuwa Imam Sajjad (a.s.) ambaye alikuwa amelala kitandani kwenye hema lake kwa sababu ya maradhi yake. Imam Husain (a.s.) alikuwa amesimama peke yake akiwa amezungukwa na maadui. Imam alitazama kushoto kwake na kulia kwake lakini hakuona kitu isipokuwa masahaba wake waliouawa kishahidi. Alipoona hali hiyo, Imam alitamka kauli ambayo kusudio lake lilikuwa, "Sioni mwili wowote kati ya iliyolala ardhini ulio hai." Halafu Imam akasema:

"Wote wale waliozikwa ndani ya ardhi na wale wanaolala juu ya ardhi hii wapo hai." Halafu Imam akaita akitaka msaada (*Istighatha*). Imam aliomba msaada. Nani alikuwa hai kumpa Imam msaada? Ni watu gani hao ambao walikuwa hai? Hao watu ni ile miili iliyokuwa imelala juu ya ardhi ikiwa maiti? Imam (a.s.) aliwaita masahaba wake kwa sauti ya kupaza akiwatolea heshima kuu. "Enyi watu wangu watiifu na jasiri! Enyi watu wangu watiifu na mashujaa! Amkeni kutoka usingizini. Amkeni! Songeni mbele! Hawa watu waovu wanataka kushambulia utakatifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Watu hawa wasio na aibu wanataka kuja kupora mahema ya dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)."[264] Halafu akasema: "Nendeni mkalale! Nendeni mkalale. Najua kwamba vichwa vyenu vimekatwa na kutenganishwa na miili yenu."[265]

uk. 626

[264] *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 484 "Enyi mashahidi! Amkeni. Amkeni kutoka usingizini na mkawafukuze hawa wapenda fitina kutoka kwenye utakatifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)"

[265] *Guftar Hai Maanawi*, uk. 250-255.

# MAJILISI 41

## UMASHUHURI WA ROHO YA IMAM HUSAIN (A.S.).

Kauli nyingi sana za Imam Husain hazikuweza kutufikia. Hali ya mambo ya wakati huo ndiyo sababu kubwa zilizo sababisha hili. Tunayo hazina kubwa ya hotuba na semi za Amiri wa Waumini. Hususan, hotuba zilizotolewa na Imam Ali (a.s.) wakati alipokuwa khalifa ni utajiri wa thamani kubwa. Hata hivyo, Imam Hasan (a.s.) na Imam Husain (a.s.) iliwabidi wakabiliane na vikwazo kutoka kwa watawala wa wakati wao. Hususan, katika kipindi cha Imam Husain (a.s.), Muawiyah aliwatishia sana watu hivyo kwamba hapana mtu aliyethubutu kwenda kwa Imam Husain (a.s.). Hata kama mtu alisikia jambo kutoka kwa Imam Husain (a.s.) hakuthubutu kulinukuu kwa wengine.

Hata hivyo, ingawaje hakuna kauli nyingi za Imam Husain (a.s.), nimeona sifa fulani kwenye semi za Imam Husain (a.s.) wakati wa utafiti wangu ambazo maana ya maneno ya Imam Husain (a.s.) si tu yasiyolinganishika bali kimsingi yanaakisi muungano wa roho na umashuhuri wa Imam Husain (a.s.). Kila sentensi ya Imam imejaa johari za umashuhuri.

### SEMI ZA IMAM HUSAIN (A.S.) KATIKA NYAKATI ZAKE ZA MWISHO

Kauli moja ni ile ambayo Imam alisema wakati wa mwisho wa uhai wake, Imam (a.s.) alionyesha johari ya ujasiri kwenye uwanja wa vita na akaanguka chini akiwa amejeruhiwa. Mwili huo mtukufu tayari ulikuwa umekwishapoteza damu nyingi. Roho ya Imam ilikuwa na nguvu sana lakini mwili wake ulikwishadhoofika sana. Alikuwa hana nguvu za kumwezesha kusimama. Aliweza tu kunyanyuka kwa kutumia magoti yake akiwa ameegemea upanga wake. Imam (a.s.) hakuwa hata na nguvu za kuweza kuzizuia zile hatua ovu zilizokuwa zinaelekea kwenye kambi yake tukufu.

Hatimaye, Imam (a.s.) alisimama kwa kujikaza kwa taabu sana na akasema kwa sauti ya juu, "Enyi wafuasi wa Abu Sufyan! Enyi wale ambao wameuza nyoyo zao! Laana iwe juu yenu! Hata kama hamna dini na hamuogopi Siku ya Hukumu, mnapaswa kuona haya kama watu walio huru wa dunia hii."

"Ninajua kwamba hamna imani yoyote ile juu ya Mwenyezi Mungu na Siku ya Hukumu lakini angalau mngetoa njia ya uheshimikaji kwenye nyoyo zenu. Mtu anayeheshimika, ambaye hutoa harufu ya heshima kutoka mwilini mwake, huwa hafanyi kama mnavyofanya nyinyi." Waonevu wale waliuliza, "Ewe mtoto wa Fatima! Unasema nini? Tumefanya nini dhidi ya uhuru?" Imam alijibu:

"Mimi ninapigana na nyinyi na mnapaswa kunikabili mimi. Kwa nini sasa mnataka kuwashambulia wanawake?"[266]

## VIASHIRIO VYA UJASIRI KWENYE HOTUBA ZA HUSAIN (A.S.)

Tukitazama kwa haraka hotuba za Imam Husain (a.s.) tangu hotuba ya kwanza, ambayo alihutubia Makkah hadi ile aliyotoa wakati wa safari, tunaona maneno ya Imam Husain (a.s.) yamejaa heshima na umashuhuri.

Imam (a.s.) alitoa hotuba wakati anaondoka Makkah na alisema, "Kifo kimeacha alama kwenye dhuria wa Adam kama alama ya kidani kwenye shingo ya mwanamwali." Pia alisema, "Yeyote anayetaka kujitoa mhanga katika njia ya Allah kama sisi, yeyote anayetaka kuunganisha sauti yake na sauti yetu, yeyote anayetaka kuhama kwa ajili ya Allah na akutane na Mola Wake anapaswa kufuatana na sisi. Mola akipenda nitaondoka kesho."[267] Imam (a.s.) alitaka kusema, "Kimsingi roho yangu haipendi kuona mazingira yaliyojaa uharibifu, nibakie kuwa hai na kuwa sehemu yake. Ninapendelea kifo kwa ajili yangu mimi kama ustawi wangu katika hali kama hiyo. Mimi kufuzu kwangu kumo katika kutobaki kuwa hai miongoni mwenu. Kufuatana na vile nionavyo mimi, kuishi na wakandamizaji ni kifo cha moyo na fedheha ya maisha."[268]

[266] *Biharul Anwar*, Juz. 45,uk. 51; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 503.
[267] *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 366; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 328.
[268] *Luhuuf*, uk. 79

Watu wengi walikutana na Imam (a.s.) na kuongea naye wakati wa safari. Wengi wao walikuwa watu wasiojali na walijaribu kuwakiuka wenzao. Mtu mmoja alimwambia Imam, "Bwana! Nyakati si nzuri. Kwa nini unajitupa ndani ya makucha ya kifo?"[269] Pale ambapo mtu kama huyo alijaribu kuzuia Imam (a.s.), yeye alisema, "Jibu langu ni kama lile la msaidizi anayepigana ubavuni mwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambalo alimpa binamu yake ambaye alikuwa anajaribu kumzuia asiende vitani." Halafu Imam (a.s.) alinukuu beti za msaidizi huyo kama ifuatavyo:

"Mimi ninakwenda. Kifo si sababu ya fedheha kwa mtu ambaye ana nia ya kupigana katika njia ya haki kama Mwislamu. Jihadi sio sababu ya utovu wa heshima kwa sababu hiki ni kifo ambacho humfanya mtu akutane na waadilifu. Ni heshima mtu kuyatoa mhanga maisha yake akiwa anapigana na maadui wa njia iliyonyooka. Ama nitabaki hai katika vita hii au nitakufa. Endapo nitabaki hai hakuna uwezekano wa kufedheheka na kama nikifa sitakuwa na wasiwasi."[270]

"Ni fedheha ya kutosha kwako kwamba upo hai na una hali ya kushindwa kunakodhalilisha juu yako. Mimi, Husain (ambaye nimenyonyeshwa na Fatima Zahra), kamwe sitavumilia hili. Ninaweza kukatwa kichwa kwa ajili ya maisha ya heshima lakini maisha ambamo mimi nitalazimika kuinama chini hayana maana kwangu."

Wakati wa safari hiyo, Imam (a.s.) alizungumza na mmojawapo wa masahaba wake kwamba yeye (Husain) alipendelea maisha ya umashuhuri, heshima na hadhi zaidi ya maisha ya fedheha na akasema, "Je huoni? Hivi macho yako hayafunguki? Hivi huwezi kuona kwamba njia iliyonyooka haifuatwi? Hivi huwezi kuona kwamba uharibifu na upotoshaji mbaya umeenea kila mahali na hakuna mtu wa kukataza hili? Katika mazingira kama haya, ni wajibu wa muumini kutamani kifo."[271]

Imam husain (a.s.) alirithi kuheshimika na uaminifu kutoka kwa baba yake. Wakati Imam Ali (a.s.) alipopata taarifa kwamba majeshi ya Muawiyah yamezidi kufanya unyang`anyi katika jiji la Anbar na kwamba wamepokonya hereni za mwanamke kafiri, Imam (a.s.) alisema, "Wallahi, kama Mwis-

[269] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 238; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 358.

[270] Imam Husain (a.s.) alighani beti hizi katika kumjibu Hurr ambaye alikuwa anasikitika kwa kuyaweka maisha yake hatarini.

[271] Tarikh Tabari, Juz. 4, uk. 305; Biharul Anwar, Juz. 44. uk. 381; Muntahaiul Amaal,Juz. 1, uk. 213; Maqtal–e-Husain, Muqarram, uk. 194; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk. 356.

lamu akisikia habari hizi na akafa kwa sababu ya kusikitika na kukasirika, mimi sitamlaumu."[272]

Njoo, hebu twende kwenye siku ya Ashura sasa. Taa ya uhai wa Imam Husain (a.s.) ilikuwa inakaribia kuzimika. Maneno yake, yalikuwa bado yanafurahisha. Imam Husain (a.s.) bado alikuwa anazungumzia kuhusu heshima na ujasiri. Hapa pia, kiini cha mazungumzo ya Imam (a.s.) kilikuwa tabia na mafundisho ya Kislamu. Mjumbe wa Ibn Ziyad alipokuja kwa Imam (a.s.) pamoja na ujumbe, Imam (a.s.) alimwambia, "Mwambie bwana wako kwamba sitatoa mkono wangu kushika mkono wako kwa fedheha. Haiwezekani mimi kujitetea kama mtumwa na kuomba msamaha kama niliyeangukia katika mawindo ya kutoelewana."[273]

Hata hivyo upo utukufu zaidi kwenye maneno ya Imam (a.s.) ambayo yalisemwa wakati anapigana pambano lake la mwisho. Masahaba wake wote na ndugu zake wote walikwisha kuuawa kishahidi. Imam (a.s.) aliweza kumuona mwanae mdogo ambaye aliuawa kishahidi. Mikono ya kaka yake ilikatwa na alijua kwamba adui angeshambulia kambi yake baada ya muda mfupi na kuwachukuwa watu wake kama mateka. Halafu pia, alikuwa anatamka kauli mbiu kwa sauti kubwa katika pambano lake kuhusu uongozi wake. Hata hivyo, kauli mbiu hizo hazikuwa za kuwataka wengine wamtii yeye. Hakuwa anawaomba wengine kumchukulia yeye kuwa mkubwa wao na wamfuate. Maana ya kauli mbiu ya Imam (a.s.) ilikuwa kwamba yeye alikuwa kiongozi mkamilifu na kwamba uongozi wake haukumruhusu yeye kumwangukia mtu duni.

"Kifo ni bora zaidi kuliko maisha ya kuvunjiwa heshima. Wakati wote kifo ni bora zaidi na kinapendwa zaidi kuliko fedheha na aibu. Kushindwa kwa dhahiri hapa duniani ni bora kuliko kuingia moto wa jahannam.[274]

Hii ndiyo maana ya umashuhuri wa nafsi. Hii ndiyo tofauti baina ya mtu tajiri na mtu mnyoofu. Ndiyo, watu watukufu wanaweza kuwa wakwasi lakini matajiri wote sio watukufu. Kila mzee sio mtukufu. Ndiyo maana tunaposimama mbele ya mtu mkubwa ambaye anaheshimiwa na kutukuzwa

[272] *Nahjul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba ya 27, uk. 85; *Nahjul Balaghah*, Subhi Salih, Hotuba ya 27; *Sharh Nahjul Balaghah*, Ibn Abil Hadid, Juz. 2, uk. 74.

[273] Ipo tofauti ndogo baina ya maelezo yaliyomo ndani ya *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 191 na *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 7

[274] *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 192; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 499.

tunapaswa kusema: 'Ninashahidilia kwamba ulisimamisha Swala, na ukatoa Zaka na uliamrisha mema na kukataza mabaya.'[275]

Kama tukisimama mbele ya Nadir Shah tutasema nini? Ni dhahiri, tutamsifu na kusema kwamba tunashahidilia kwamba ulikwenda India na ukaiharibu na ukatuletea sisi almasi za Kohinoor kutoka huko.

Hata hivyo, tunaposimama mbele ya Imam Husain (a.s.) tunasema, "Tunashahidilia ulisimamisha swala, ulitoa zaka na ulitimiza wajibu wa kuamrisha mema na kukataza mabaya. Uliimarisha uhusiano baina ya mja na Mola Wake kupitia Swala. Ulipambana katika njia ya Allah badala ya njia ya dunia hii na ukwasi wake. Wewe hukuwa katika wale wenye fursa ambaye anatamani rasilimali au kulipa kisasi au uovu au ukwasi. Wewe ulikuwa yule mwenye fursa ambaye alifanya jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Ulisahau matamanio yako ya kidunia na ukajifinyanga mwenyewe ndani ya tanuri lako mwenyewe. Athari zake zilikomesha umbali baina ya mja na Mola Wake. Ninashahidilia kwamba umetimiza wajibu wako wa kutekeleza jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu kama inavyostahili kufanywa."[276] "Ulitekeleza jihadi lakini haikuwa kwa matamanio ya ubinafsi na kupata mali au umashuhuri; ilikuwa kwa ajili ya haki na ukweli."

---

[275] *Mafaatihul Jinaan*, Ziarat Waritha

[276] *Mafaatihul Jinaan*, Ziarat Waritha

# MAJILISI 42

## SWALA - NGUZO YA DINI

Imetamkwa ndani ya Qur`ani Tukufu kwamba baadhi ya hao ambao wataingizwa kwenye adhabu ya jahannam wataulizana wao kwa wao, "Kitu gani kimekuleta hapa?" Watapata jibu, "Hatukusimamisha Swala na hatukuwalisha mafukara. Pia tulikuwa na mazoea ya kuwasikia Makafiri wakisema maneno dhidi ya dini kwenye mikusanyiko au hata sisi tulikuwa tukizungumza kama hivyo."[277] Hii inathibitisha umuhimu wa Swala katika dini. Kwa nini Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kwamba Swala ni nguzo ya hema la dini? Ni hivyo kwa sababu kama Swala inasaliwa kwa usahihi mambo mengine yote yatarekebishwa.

Imam (a.s.) alisema kwenye wosia wake wa mwisho, ambao unaanza na maneno, "Allah, Allah!" na ambao wewe unausikia mara kadhaa, "Allah, Allah! Usiache Swala katika wakati wowote ule kwa sababu hii ni nguzo ya dini yako."[278]

### SWALA YA MWISHO YA IMAM HUSAIN (A.S.)

Unajua kwamba umwagaji damu ulianza baada ya Adhuhuri ya Ashura. Hadi Adhuhuri, Imam Husein (a.s.), masahaba wengi na vijana wa Bani Hashim walikuwa hai.[279] Ni masahaba thelathini tu wa Imam Husain (a.s.) waliokuwa wameuawa kishahidi kwa kupigwa mishale kabla ya Adhuhuri na wengine walikuwa hai hadi Adhuhuri. Wakati sahaba alipoona kwamba ilikuwa wakati wa Swala Adhuhuri, alimuomba Imam,[280] "Bwana! Wakati wa Swala umewadia na tunataka kuswali Swala yetu ya jamaa ya mwisho nyuma yako."

Imam Husain (a.s.) alitazama mbinguni na akathibitisha kwamba wakati huo ulikuwa wakati wa Sala. Halafu akasema, "Umekumbuka Swala.

[277] **Sura ya Muddathir (74:42-45)**
[278] *Nahjul Balaghah*, Faizul Islam, Hotuba 47, uk. 968
[279] Majina ya watu waliouawa kishahidi katika shambulio la kwanza yametajwa ndani ya *Absarul Ain*.
[280] Jina la sahaba huyo ni Abu Thamama Amr bin Abdullah Saeed. *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 656

Mwenyezi Mungu akuweke miongoni mwa wale wanaoswali." Au alisema: "Umemkumbuka Allah. Allah akuweke miongoni mwa wale wanaosali."[281] Imam anamuombea mtu ambaye uhai wake umo kwenye fumbata la kifo ili ajumuishwe miongoni mwa wale wanaoswali. Kwa hiyo, ona ni daraja gani muumini wa kweli analo karibu na Mwenyezi Mungu?

Bila shaka sisi huwa tunasimamisha Swala. Hata hivyo, pia huwa tunaswali Swala wakati vita inaendelea. Swala hii inaitwa "swala ya hofu" katika sheria za Kislamu. Swala ya hofu ni sawa na Swala ya safari, ambayo huwa na rakaa mbili badala ya nne. Kwa hiyo, hata kama mtu yuko kwenye ardhi ya nyumbani kwake na anakuwa katika mazingira ya vita inamlazimu mtu huyu kuswali Swala ya rakaa mbili. Ni vigumu kuswali Swala yote wakati wa vita na kwa hiyo, Swala ya hofu inatakiwa kuswaliwa hapo kufuatana na sharia ya Kislamu. Sasa kama masahaba wote wanasimama kwenye Swala ya jamaa ulinzi wao unaweza kuvurugwa. Kwa hiyo, nusu ya wapiganaji wanaendelea kuweka ulinzi dhidi ya mashambulizi ya adui na nusu nyingine wanaswali Swala ya rakaa moja ya jamaa nyuma ya Imam na rakaa moja kila mtu anaswali peke yake na kumalizia swala yao. Imam anangojea ama akiwa amekaa au amesimama baada ya rakaa ya kwanza ili waweze kuchukua nafasi zao za ulinzi na nusu nyingine ya wapiganaji wanaungana naye katika Sala ya jamaa. Nusu ya wapiganaji wengine wataswali Swala ya rakaa moja katika jamaa na rakaa moja kila mmoja peke yake.

Imam Husain (a.s.) pia aliswali namna hii lakini hali ya mambo ilikuwa tofauti wakati huo. Imam hakuwa mbali na maadui zake. Kwa hiyo, masahaba waliokuwa wanamlinda walisimama karibu sana naye lakini maadui wasiokuwa na aibu hawakuwapa nafasi ya kuswali kwa amani. Maadui walianza kutupa mishale wakati Imam Husain (a.s.) alikuwa anaswali. Pia walikuwa wanadhihaki kwa maneno. Waliolaaniwa hawa walikuwa wanasema, "Ewe Husain! Usiswali. Swala yako haina manufaa. Umemsaliti mtawala wa wakati huu, Yazid na kwa hiyo, Swala yako haina manufaa."[282]

## SAID BIN ABDULLAH - SHAHIDI WA SWALA

Sahaba mmoja au wawili wa Imam Husain (a.s.) waliiweka miili yao kuwa ngao ya Imam Husain (a.s.) ili waweze kuzuia mishale ya maadui iliyo-

[281] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 21; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*,uk. 444

[282] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 21

lengwa kwa Imam (a.s.), ili ifikie kwenye miili yao na kumruhusu Imam kukamilisha Swala yake. Masahaba hawa wawili walipoanguka chini wakiwa wamejeruhiwa, ndiyo muda ambapo Imam Husain (a.s.) alikuwa amekamilisha Swala yake. Mmojawao alikuwa Said bin Abdullah Hanafi. Wakati Imam alipofika karibu yake, tayari alikuwa katika sekunde zake za mwisho. Mara Imam (a.s.) alipochukua kichwa chake na kukiweka kwenye paja lake, Said aliuliza swali la kushangaza, alisema, "Ewe Aba Abdillah! Je! Nilitimiza haki ya utiifu?"[283] Maana yake ni kwamba, alikuwa anafikiri kwamba haki ya Husain (a.s.) ni kubwa mno hivyo kwamba muhanga wa namna hiyo usingetosha. Kwa namna hii, ndivyo ilivyokuwa swala ya Imam Husain (a.s.) ndani ya jangwa la Karbala.

## IMAM HUSAIN (A.S.) ANARUKUU NA KUSUJUDU KWA MARA YA MWISHO

Imam Husain (a.s.) alitamka Takbira (*Allaahu Akbar*) na pia *Sub-h`aanallaah* (Utukufu ni Wake Allah) ndani ya Swala hii. Alirukuu, na akasujudu.[284] Hata hivyo, aliswali Swala moja zaidi baada ya saa mbili au tatu, ambapo alirukuu namna tofauti, akasujudu kwa namna tofauti na kusoma maneno kwa namna tofauti. Imam alirukuu alipopigwa mshale kwenye kifua chake kitukufu. Halafu alilazimika kuinama chini na kutoa mshale kutokea mgongoni kwake. Halafu unajua jinsi Imam (a.s.) alivyosujudu kwa mara ya mwisho? Hakuweka paji lake la uso juu ya ardhi kwa sababu alipotua kutoka kwenye mgongo wa farasi, shavu lake la kulia liligusa ardhi yenye joto ya Karbala na alikuwa anatamka:

**"Kwa jina la Allah na kwa Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)"**

[283] *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 244
[284] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 698

# MAJILISI 43

## MANENO YA IMAM HUSAIN (A.S.) WAKATI ANAONDOKA KWA MARA YA MWISHO

Kama mtu akichunguza maneno ya Imam Husain (a.s.) wakati alipokuwa anaondoka kwa mara ya mwisho kutoka kwenye mahema ya Ahlul-Bayt wake huzama kwenye bahari ya mastaajabu. Anaanza kufikiri, "Ewe Mwenyezi Mungu! Hivi Husain alikuwa na imani na utulivu gani? Alipata kutoka wapi imani hii na utulivu huu na hisia na shauku za hali ya juu kama hizi?

Imeandikwa kwenye vitabu kwamba wakati Imam Husain (a.s.) alipokwenda kuaga kwa mara ya pili, aliwaambia Ahlul-Bayt wake, "Kuweni tayari kuvumilia matatizo na mjue kwamba Mwenyezi Mungu ndiye msaidizi wenu na tegemeo lenu. Mwenyezi Mungu atawaokoa kutoka kwenye fitina ya maadui na mwisho wenu utakuwa mzuri. Mwenyezi Mungu atawaingiza maadui zenu kwenye aina nyingi za mateso na mtalipwa neema na heshima nyingi kwa ajili ya matatizo mtakayoyavumilia. Tahadharini na kutamka hata neno moja la kulalamika na msiseme jambo lolote ambalo linaweza kushusha hadhi yenu."[285]

Imam Husain (a.s.) alikuwa anawashauri Ahlul-Bayt wake kuwa wavumilivu kwa sababu ya kujiamini kwake katika ushindi wake, ambao chanzo chake ni aya hii ya Qur`ani:

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا

**"....na anayemcha Mwenyezi Mungu, Yeye humtengenezea njia ya kutokea."** **[Sura At-Talaq 65 : 2]**

Kujiamini huku kwa Imam (a.s.) kulitokana na Qur`ani Tukufu hususan aya hii. Ni aina kama hiyo ya imani na utulivu, ambayo aliipata Nabii Yusuf (a.s.) wakati ule alipofaulu kwa sababu ya ucha-Mungu wake na alikuwa na furaha na kuridhishwa sana kwa hilo. Alikuwa anasema:

---

[285] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 698; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 491

إِنَّهُ مَنْ يَتَّقِ وَيَصْبِرْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ

**"....Hakika mwenye takua na akasubiri basi Mwenyezi Mungu haupotezi ujira wa wafanyao mazuri." [Sura Yusuf 12 : 90]**

Hata hivyo, umaarufu wa Imam Husain (a.s.) upo kwenye ukweli kwamba aliweza kuona mwisho wa jambo na matokeo yake kabla ya jambo hilo halijaisha na kabla ya watu hawajafikia uamuzi wa mwisho.

## ZAINAB AL-KUBRA AZUNGUMZA KWENYE BARAZA YA YAZID

Maneno ya Imam Husain (a.s.) yaliandikwa kwenye nyoyo za Ahlul-Bayt. Waliyahimili majanga yote lakini hawakuacha uvumilivu na ucha Mungu wakati wowote ule. Hatimaye, matokeo yalikuwa ni yale yale kama alivyo hakikisha Imam Husain (a.s.) na kama ilivyothibitishwa na Mwenyezi Mungu ndani ya Qur`ani. Tumeona kwamba baada ya siku chache, Bibi Zainab al-Kubra aliyarudia maneno ya Imam Husain (a.s.) kwa utulivu ndani ya baraza ya Yazid. Roho ya Karbala ilikwaruza uso wa ufalme ndani ya jangwa na sasa ilikuwa inaupiga makofi wazi wazi.

Binti yake Ali alisema, "Ewe Yazid! (Umejichimbia kaburi lako mwenyewe). Unaweza kufanya uovu wowote unaotaka kufanya na kutujaribu sisi kadiri utakavyoweza. Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, kamwe hutaweza kufuta upendo wetu, ambao umejikita kwenye nyoyo za watu. Wahyi, ambao una uhai katika familia yetu, hauwezi kuwekwa kwenye usingizi wa kifo na wewe. Hakuna chochote hapa duniani isipokuwa fedheha juu yako."286

**Kwa jina la Allah na kwa Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)**

[286] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 135

# MAJILISI 44

## MTUME WA MWENYEZI MUNGU (S.A.W.W.) ALIMLILIA KHADIJA

Mwenyezi Mungu na apishie mbali, uhusuiano baina ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Bibi Khadija haukujengwa juu ya msingi wa matamanio duni ya kinyama na anasa. Kwa hiyo hoja kama hizo hazina maana. Bibi Khadija alikuwa na miaka kumi na tano zaidi ya Mtume (s.a.w.w.). Kwa hiyo, alipofariki dunia, Mtume alikuwa na desturi ya kumheshimu sana wakati wowote lilipotajwa jina lake. Mara nyingi alikuwa na mazoea ya kutoa machozi machoni mwake, hali ambayo Aisha alishindwa kuivumilia.[287] Kwa kuwa Aisha alikuwa mdogo na alikuwa anajivunia ujana wake, wakati fulani alimwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) "Mwanamke mzee sio mtu wa muhimu kama unavyomfikiria Bibi Khadija." Mtukutu Mtume (s.a.w.w.) akajibu, "Unasema nini? Khadija alikuwa tofauti kabisa."[288]

### WOSIA WA BIBI KHADIJA KWA ASMA

Wanawake walikuwa wamekusanyika nyuma ya chumba ambamo maharusi wapya Imam Ali (a.s.) na Bibi Zahra walikuwamo mnamo usiku wao wa harusi kama inavyotokea pia sehemu nyingi vijijini leo hii. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliamuru kwamba hapana mtu yeyote alikuwa na haki ya kukaa nyuma ya chumba hicho na kwamba wanawake walipaswa kuondoka mahali hapo.

Baada ya muda, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipita karibu na sehemu hiyo na akamuona Asma binti Umais ameketi karibu na chumba hicho. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema, "Hivi sikusema kwamba hakuna ruhusa ya mtu kukaa hapa. Kwa nini umekaa hapa?" Asma akasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Bibi Khadija aliniusia mimi: 'Nina wasiwasi sana kuhusu binti yangu kwa sababu ni mdogo. Nadhani atanihitaji mimi katika usiku wa harusi yake

[287] *Biharul Anwar*, Juz. 16, uk. 1-81

[288] *Seerat-e-Halabiya*, Juz. 3, uk. 313; *Kohlul Basar*, uk. 70

kwa sababu yapo mazingira fulani ambapo binti humhitaji mama yake usiku huo. Hivyo, ni wosia wangu kwako kwamba umwangalie Fatima katika usiku wa harusi yake.'"

Asma anasema kwamba macho ya Mtume (s.a.w.w.) yalijaa machozi aliposikia jina la Khadija. Alimwambia, "Kaa hapa tu." Akasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Nitakaa hapa tu, ili kwamba kama Zahra akiita na kuhitaji kitu niweze kumtimizia mahitaji yake."[289]

## MAPENZI YA IMAM HUSAIN (A.S.) KWA BIBI RABAB NA SAKINA

Bibi Rabab[290] alikuwa mmojawapo wa wakeze Imam Husain (a.s.). Ni bibi huyu tu ndiye aliyekuwepo Karbala. Alikuwa mama wa Sakina. Imam Husain (a.s.) alikuwa anajivunia sana utiifu wa mke huyu hivyo kwamba alikuwa na desturi ya kunukuu beti zifuatazo kwa heshima yake:

"Ninaapa kwa rafiki ambaye ni mpendwa kuliko uhai. Ninapenda kuishi ndani ya nyumba ambamo Rabab na Sakina wamo. Ninawapenda sana wote hawa wawili. Huhisi kutumia utajiri wangu wote juu yao na hapana yeyote anayepaswa kunizuia kufanya hivi."[291]

Uliona jinsi uhusiano wa watu wa haki ulivyo? Ni kuhusu wake za watu kama hawa ambao Qur`ani Tukufu inasema:

ادْخُلُوا الْجَنَّةَ أَنْتُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ تُحْبَرُونَ

**"Ingieni katika Bustani (Pepo), nyinyi na wake zenu katika hali ya kufurahishwa." (Sura Az-Zukhruf 43 : 70)**

---

[289] *Biharul Anwar*, Juz. 43, uk. 138

[290] Mama yake Imam Zainul Abidiin, Bibi Shaharbanu alikwishafariki dunia wakati wa kujifungua kwake. Mama yake Ali Akbar, Bibi Laila naye pia hakuwepo Karbala. Haijulikani kama aliondoka na msafara pale Madina au hapana. Hata hivyo, ni hakika kwamba hakuwepo Karbala (Ustaadh Mutahhari)

Ni Rabab binti Imrul Qais Kalbi tu miongoni mwa wakeze Imam Husain (a.s.) ndiye aliyefuatana naye hadi Karbala. Rejea *Tarikh Ashura*, uk. 199 cha Dkt. Ibrahim Ayati, kilichochapishwa na Jame Taalimaat-e-Islam.

[291] *Damaus Sujum*, uk. 311; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain,* uk. 825

## RABAB ANAMUOMBOLEZA IMAM HUSAIN (A.S.)

Bibi Rabab hakuketi kwenye kivuli wala kula chakula kizuri kwa kipindi kirefu. Alikuwa na kawaida ya kulia mara nyingi. Alipoulizwa kwa nini alikuwa hakai kwenye kivuli, alikuwa na mazoea ya kusema, "Nilipoona mwili wa mume wangu umelala kwenye jua kali[292] (Ustadhi Mutahhari), niliapa kutokaa kamwe kivulini."

Palikuwepo na fungamano halisi baina ya bibi huyu na Imam Husain (a.s.) hivyo kwamba akawa ushahidi wa aya:

ادْخُلُوا الْجَنَّةَ أَنْتُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ تُحْبَرُونَ

**"Ingieni katika Bustani (Pepo), nyinyi na wake zenu katika hali ya kufurahishwa."** **(Sura Az-Zukhruf 43 : 70)**

## "BINTI YANGU SAKINA, TAFADHALI USIUFANYE MOYO WANGU KUZIDI KUTESEKA"

Kama ilivyo dhahiri kutoka kwenye aya zilitajwa hapo juu, Imam Husain (a.s.) alimpenda Sakina sana. Mapenzi haya yalikuwa ya pande mbili. Sakina pia alimpenda sana baba yake. Historia inathibitisha kwamba mapenzi ya Sakina yalikuwa mtihani mkubwa kwa Imam Husain (a.s.). Huyu alikuwa binti mpendwa wa Imam Husain (a.s.) na hakuweza kuishi bila kuwa naye hata kwa muda mfupi. Wakati Imam Husain (a.s.) alipokwenda kuaga na Sakina akaanza kulia, Imam akasema:

"Sakina, mpendwa wangu! Usilie sasa. Utalia sana baada yangu. Usimwage machozi almuradi nikingali hai. Zuia machozi yako yatakayodondoka baada yangu. Ewe kipenzi adhimu cha baba yako! Hivi hujui kwamba moyo wangu unajaa huzuni ninapoona machozi yako? Kwa hiyo usiufanye moyo wangu kuzidi kuteseka."[293]

[292] *Muntahaiul Amaal*,Juz. 1, uk. 819

[293] Kwenye baadhi ya vitabu vya historia "*daa`ani*" imebadiliswa kwa "*dahaani*".

"Bila shaka, ni juu yako wewe kulia kadiri uwezanyo baada ya roho yangu kuondoka kwenye mwili wangu. Hata hivyo, Ewe binti yangu! Almuradi baba yako yu hai, moyo unadhikika unapoona machozi yako.[294] Kwa hiyo, unayo haki kabisa ya kulia baada yangu."[295]

[294] Kwenye baadhi ya vitabu vya historia "*taa-tiinahu*" imeandikwa kama "*taa-tiinanii*" badala yake.

[295] *Damaus Sujum*, uk. 184; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 491

# MAJILISI 45

## FEDHEHA HAIVUMILIKI

Mashairi yaliyoghaniwa na Imam Husain (a.s.) mnamo siku ya Ashura yalikuwa ya namna tofauti. Baadhi yake yalitungwa na Imam Husain (a.s.) na baadhi yalitungwa na watu wengine na kughaniwa na Imam Husain (a.s.). Kwa mfano, beti zilizotungwa na Farwa bin Musaik ambazo zilijazwa shauku na ari.

Hapa, ni baadhi ya beti zilizotungwa na Imam Husain (a.s.):

**"Kifo ni bora zaidi kuliko kuishi na fedheha. Kifo wakati wote ni bora na chenye kupendwa zaidi kuliko fedheha na aibu. Kushindwa kwa dhahiri hapa duniani ni bora zaidi kuliko kuingia jahannam"[296]**

Kauli mbiu hii ya Imam Husain (a.s.) inapaswa kuitwa kauli mbiu ya uhuru, kauli mbiu ya heshima na kauli mbiu ya uaminifu. Maana yake ni: 'Ni bora zaidi kwa Mwislamu wa kweli kufa badala ya kuishi maisha ya fedheha.'

Dunia inapaswa kujua kwa nini Imam Husain (a.s.) alikuwa tayari kumwaga kila tone la damu yake na damu ya vijana wake. Ni kwa sababu Imam Husain (a.s.) alilelewa kwenye paja la utume. Ni hivyo kwa sababu damu ya Ali ilikuwa inatiririka kwenye mishipa yake. Ni hivyo kwa sababu alinyonyeshwa na Fatimah Zahra (a.s.).[297]

Pale ambapo kwa dhahiri matumaini yote yalipotea mnamo siku ya Ashura, Imam alitoa hotuba iliyojaa ghera na shauku. Ilionekana kama vile ulimi wa Imam Husain (a.s.) ulikuwa unatoa ndimi za moto mkali usiovumilika. Je maneno haya yanaweza kuwa ni mzaha? Imam (a.s.) alisema, "Enyi watu! Tazameni mwana haramu huyu (Ibn Ziyad) anavyothubutu kunilazimisha mimi kukubali mojawapo ya masharti mawili –fedheha au kifo. Nenda umwambie bwana wako kwamba fedheha haiwezi kuvumillika kwa Husain."[298]

[296] Biharul Anwar, Juz. 44, uk. 192; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk. 499

[297] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk.19 na 83; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 423.

[298] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 83; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 425

Damu ilikuwa inatiririka kwenye upanga wa Ibn Ziyad. Baba yake dhalimu aliwakandamiza sana watu wa Kufa miaka ishirini iliyopita hivyo kwamba walipojua kwamba Ibn Ziyad ameteuliwa kuwa gavana wa Kufa, walijificha majumbani mwao kwa sababu walijua kwamba yeye pia alikuwa na moyo mgumu kama baba yake na angefanya uharibifu mkubwa kwao.[299]

Huyu Ibn Ziyad alipokuja kama gavana wa Kufa, watu waliacha kumuunga mkono Muslim bin Aqiil kwa sababu ya heshima iliyochanganyikana na woga waliokuwa nao kwa baba yake Ziyad.

## MTU ALIYELELEWA KWENYE MAPAJA YA FATIMAH HAWEZI KUVUMILIA FEDHEHA

Imam Husain (a.s.) aliwahutubia watu wa Kufa akasema, "Hivi nyinyi mnajua mtawala wenu ameweka mbele yangu masharti mangapi? Amenitaka mimi ama kukubali fedheha au kuchomoa upanga. Nendeni mkamwambie mtawala wenu kwamba Husain anasema kwamba fedheha iko maili nyingi mbali na yeye. Hatutaweka silaha zetu chini na tukubali kushindwa (Ustadhi Mutahhari analia). Mwenyezi Mungu anamtaka Husain kuwa hivyo lakini nyinyi hamjui."

"Mtu mwana haramu huyo hajui mimi nimelelewa kwenye paja la nani. Mimi nililelewa kwenye paja la utume na kukuzwa kwenye paja la Ali. Nilinyonyeshwa ziwa la binti yake Mtume (s.a.) Fatimah Zahra (Shahidi Mutahhari anaendelea kulia). Hivi mtu aliyenyonyeshwa na Zahra anaweza kukubali fedheha ya Ibn Ziyad? Fedheha iko maili nyingi mbali na mimi."

Kauli mbiu za Imam Husain mnamo siku ya Ashura zilikuwa za aina hii tu. Kwa hiyo, ninawaomba ndugu zangu ambao hutengeneza kauli mbiu kwa ajili ya marafiki zao kwamba wangefikiria kama kauli mbiu zao zinaendana na zile za Imam Husain (a.s.) au hapana?

[299] Ziyad aliwakamata Shi'ah wa Kufa na Basra. Aliwakata mikono na miguu yao na kuwachoma vyuma vya moto kwenye macho yao na kuwaning`iniza mlangoni (*Nahjul Balaghah*, Ibn Abil Hadid, Juz. 11, uk. 44; *Al-Futuh*, Juz. 4, uk. 320) Muovu huyu ndiye mwanzilishi wa desturi ya kufunga mikono na miguu na kuua katika Uislamu. Alimzika Abdur Rahman bin Hissan akiwa hai kwa ajili ya kumpenda Ali (a.s.) kama ilivyosimuliwa na Ibn Khaldun na Ibn Athir; *Shifa as-Suduur*, Juz. 1, uk. 315

## KIU YA IMAM HUSAIN MNAMO SIKU YA ASHURA

Kiu ya Imam Husain (a.s.), Ahlul-Bayt wake na masahaba wake halikuwa jambo la masihara. Hali ya hewa ilikuwa joto sana wakati huo (Ashura ilikuwa katika siku za mwisho za mwezi wa Juni na ni kipindi cha joto sana huko Iraq, ambako pia hata majira ya kipupwe huwa joto). Hapakuwepo hata tone la maji kwa ajili ya dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa mfululizo wa siku tatu. Ni kweli kwamba damu nyingi inapopotea mwilini, damu mpya inahitajika kuzalishwa na kiu huongezeka.

Mwenyezi Mungu ameuumba mwili wa binadamu kwa namna kwamba wakati wowote unapohisi kuhitaji kitu, unajieleza. Kwa hiyo, watu waliojeruhiwa huhisi kiu kwa sababu wamepoteza damu nyingi. Mwili hujaribu kuzalisha damu zaidi katika hali hiyo na huhitaji maji. Alipojeruhiwa Imam alihisi kiu sana hivyo kwamba alipotazama juu angani, palikuwepo na giza mbele ya macho yake.[300] Hili si jambo jepesi, ni jambo la kweli. Nimetafiti kwa ukamilifu vitabu vya msiba wa Karbala lakini sikuweza kuona maneno haya yanayohusishwa na Imam Husain (a.s.) ambapo alisema, "Nipeni maji kidogo"[301] kwa sababu hadhi ya Imam Husain (a.s.) ni ya daraja la juu sana kuliko kuomba maji kutoka kwa watu hao. Ndiyo, nimeona imeandikwa mahali fulani kwamba Imam Husain (a.s.) alikuwa anatafuta maji wakati anapigana.[302] Muktadha unaonyesha kwamba Imam Husain (a.s.) alikuwa akifika kwenye maji huku akipigana karibu na mto Furati. Hata hivyo, kamwe hakuomba maji kutoka kwao.

## MASHAIRI YA *NAUHA* NA *MATAM*

Umaarufu wa Imam Husain (a.s.) uko tafauti kabisa na sisi watu. Beti za Imam Husain (a.s.) nazo pia zilikuwa tofauti kabisa. Tunapoomboleza na kusoma Nauha, tunapaswa kujaribu kulandanisha Nauha zetu na zile za Imam Husain (a.s.). Kusoma Nauha na mashairi ni kitendo mashuhuri. Maimam Watukufu walikuwa na desturi ya kuwaalika washairi kusoma mateso yaliyotungwa kishairi ndani ya majilisi ya Imam Husain (a.s.). Washairi wa-

[300] *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 245 imeandikwa: "...alipotazama juu angani, ilikuwa kama moshi..."

[301] *Biharul Anwar*, Juz, 45, uk. 351; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*. uk. 500a

[302] *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 495

likuwa na kawaida ya kufika na kughani mashairi na Maimam watukufu walikuwa wakilia sana na kutoa machozi na kuomboleza kwa huzuni.[303]

Ninaunga mkono *Nauha*, kupiga kifua (*matam*) na kupiga mkufu (*zanjir*)[304] lakini kwa sharti kwamba beti zinazoghaniwa hazipaswi kutungwa na yeyote. Badala yake zinapaswa kuwa ni beti za Husain. Mathalani, inaposemwa, "Ewe Akbar wangu mdogo, Ewe Asghar wangu mdogo" hili sio shairi la Husain. Shairi la Husain linapaswa kuwa la aina hii: "Hivi hamuoni kwamba haki haifuatwi na njia ya uwongo haizuiwi? Katika hali kama hii, muumini anasonga mbele kwenda kuuawa kishahidi katika njia ya Allah."[305] Imam hakusema 'Husain ni mmoja' au 'Imam ni mmoja….' Alisema, 'muumini ni yule anayependa kukutana na Mola wake kuliko kuishi maisha kama haya.'

Kauli mbiu ya Husain ni: "Mimi ninakiona kifo ni kufuzu na kuishi na wakandamizaji ni fedheha."[306] Kila neno la Imam Husain (a.s.) linafaa kuandikwa kwa herufi za dhahabu na kusambazwa duniani kote ili kwamba dunia ipate kujua siri iliyoko nyuma ya vita vyake. Si rahisi sana kusema tu, "Kifo ni heshima kwangu mimi na kuishi na wakandamizaji ni fedheha."

"Ninaona aibu kuishi maisha kama mtumwa badala ya kuwa kiongozi."

Kauli mbiu za Imam Husain (a.s.) zinatia uhai katika maisha.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ

**"Enyi mlioamini! Mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapowaita kwenye lile litakalowapa uhai."** **(Sura Al-Anfal 8 : 24)**

Imam Husain (a.s.) ni mrekebishaji. Neno hili lilitumiwa na Imam kwa ajili yake mwenyewe. Imam alisema, "Madhumuni ya vita vyangu wala si kukandamiza ama kuasi au kuwa na msingi wa ubinafsi. Sina nia ya kueneza uharibifu au kumdhulumu yeyote yule. Ninatoka tu kurekebisha Ummah wa babu yangu na nitafuata njia ya wahenga wangu."[307]

---

303 *Damaus Sujum*, uk. 295; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 111.

304 Ustaadh Mutahhari anazungumzia *matam* ile na mkufu, jambo ambalo hufanywa Iran. Nyembe hazikuambatishwa kwenye mikufu hiyo. Mikufu hii haipigwi kwenye mgongo ulio wazi badala yake inapigwa kwenye mgongo ambapo mhusika amevaa shati au koti na damu hitiririki kwa sababu hiyo. (Ridhwani)

305 *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 381; *Munatahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 613

306 *Luhuuf*, uk. 79; *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 381

307 *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 329; *Mausuat –e-Kalimat al-Imam al-Husain,* uk.291

Imam alitamka hili kwenye barua aliyomwandikia kaka yake, Muhammad bin Hanafiyyah, ambayo pia ilikuwa wosia wake. Muhammad bin Hanafiyyah alipata changamoto ya kimwili.[308] Mikono yake ilipooza. Hakuwa na nguvu za kufuatana na Imam kwenye safari yake. Kwa hiyo, Imam (a.s.) alimkabidhi wosia huu ili kwamba dunia ipate kujua lengo la harakati zake.

Husain (a.s.) anasema, "Enyi watu wa dunia! Mimi si kama wengine. Mapinduzi yangu si kwa sababu ninataka kufika kwenye cheo kikubwa au kukusanya utajiri wa rasilimali. Mimi ninataka tu dunia kujua ukweli kwamba msimamo wangu ni kurekebisha Ummah. Mimi ndiye mrekebishaji wa Ummah wa babu yangu (Imam aliiandika barua hii akiwa Madina). Ninataka kutimiza wajibu wa kuamrisha mema na kukataza maovu. Lengo langu ni kutia nguvu mpya kwenye Sunnah ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambayo imekufa. Sunnah ya Ali Murtaza (a.s.) nayo pia imekufa na ninataka kuihuisha upya."

## FALSAFA YA KUIHUISHA ASHURA

Sasa tunajua kwa nini Maimam watukufu walisisitiza kwamba tunaichukulia Ashura kama madhehebu na kwa nini humo kuna malipo makubwa sana kwa waombolezaji. Hivi malipo ya waombolezaji ni sawa na yale matendo mazuri wanayofanya watu kwa ajili ya wazazi wao ambao ni marehemu? Hapana, sivyo kwa sababu vifo vyetu havina umuhimu kama huo. Ni hivyo kwa sababu vifo vyetu havina mantiki au lengo. Hivyo, Maimam watukufu walisisitiza kwamba tunapaswa kuihuisha Ashura ili kwamba si tu anakumbukwa Imam Husain (a.s.) bali pia madhehebu yake yanakumbukwa daima milele.

Ukamilifu wa madhehebu haya ni Imam Husain (a.s.). Imam Husain (a.s.) yu hai katika muundo wa fikira. Ingawaje Imam Husain (a.s.) hayupo dhahiri miongoni mwetu, bado nguvu ya tabia yake ipo hai. Kila mwaka Muharram unapoanza, sauti za ujumbe huu wa Imam Husain (a.s.) husikika kila mahali hewani; "Hivi hamuoni kwamba haki haitiliwi maanani na batili kufanywa kuwa desturi. Katika mazingira kama haya, muumini anapaswa

[308] Imeandikwa kwenye *Tanqihul Maqal*, Juz. 3, uk. 112 kwamba Allamah Hilli alimjibu Muhanna bin Sunan kwamba Muhammad bin Hanafiyyah asingeweza kumsaidia Imam Husain kwa sababu alikuwa mgonjwa ambapo maneno ya Ibn Numa Hilli ya pembeni mwa *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 135 ni kama yafuatayo: "Muhammad bin Hanafiyyah alikuwa na jeraha ambalo lilimfanya asiweze kufuatana na Imam Husain (a.s.)

kutamani kukutana na Mola Wake." Inasikika kila mahali ili kwamba ghera ya Shi'ah inatiwa nguvu zaidi na wanaanza kuunga mkono ukweli na kuhimiza watu kutenda mema na kusahihisha maovu yote yanayoonekana miongoni mwa Waislamu.

## ASHURA NI SIKU YA KUHUISHA MAISHA

Kama mtu anauliza, "Mnataka kuwapa watu ujumbe gani kwa kuita,Yaa Husain, Yaa Husain na kupiga vifua vyenu na vichwa vyenu? Ni muhimu kujibu hilo kwamba, "Tunataka kuufanya ujumbe wa bwana wetu uwafikie watu. Tunaazimia kuhuisha maisha ya kiroho kila mwaka. "

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ

**"Enyi mlioamini! Mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapowaita kwenye lile litakalowapa uhai."** **(Sura Al-Anfal 8 : 24)**

Tunapaswa kujibu kwamba Ashura ni siku ya kuhuisha maisha ya muumini. Tunajiosha sisi na nafsi zetu kwenye Kauthar ya Imam Husain (a.s.) katika siku hii na kutakasa nafsi zetu. Tunajifunza misingi ya Uislamu kwa wazi katika siku hii kwa sababu hatutaki kujiweka mbali na kuamurisha mema na kujiepusha na maovu au kufa kishahidi au kujitoa mhanga katika njia ya haki. Tunataka kufanya hisia hizi zisisahaulike kupitia Ashura. Falsafa ya Ashura si kwamba tufanye dhambi kwanza halafu ndiyo tuombe msamaha kupitia Imam Husain (a.s.). Tutapata wokovu hapo tu wakati ambapo nafsi zetu zinaambatana na nafsi tukufu ya Imam Husain (a.s.). Toba maana yake ni kwamba mtu hapaswi kufanya dhambi baada ya kuomba msamaha kwa ajili ya dhambi hiyo hata kama kwa kukosea.

## ISHARA ZA KUAMBATANA NA ROHO YA IMAM HUSAIN (A.S.)

Dhambi za mtu hazisamehewi kwa kusema tu 'dhambi zangu zimesamehewa' baada ya kuhudhuria Majilisi ya Imam Husain (a.s.). Dhambi husamehewa pale tu ambapo nafsi ya mtu inapoambatana na nafsi ya Imam Husain

(a.s.). Dhambi zetu kwa hakika husamehewa wakati huo lakini sharti ni kwamba tusirudie kufanya dhambi hiyo tena.

Hata hivyo, kama ukitenda dhambi na kuhudhuria Majilisi ya Imam Husain na halafu baada ya hapo unajishughulisha na kutenda dhambi tena, inaonyesha kwamba nafsi yako haijaambatana na nafsi ya Imam Husain (a.s.).

## KAULI MBIU YA HUSAIN (A.S.)

Kauli mbiu za Imam Husain (a.s.) ni kauli mbiu za kuhuisha Uislamu. Ni kauli mbiu ya ki-Husain ndiyo sababu ya utajiri wa hazina ya Mwislamu inapewa kundi moja maalum tu? Kwa nini halali inakatazwa na haramu inaruhusiwa? Kwa nini jamii inagawanyika? Kwa watu masikini wanahusika kwenye matatizo na hawapati cha kutosha kuua njaa yao ambapo wengine wamejaa sana hivyo kwamba hawawezi kuondoka pale walipo?

Imam Husain (a.s.) alitoa hotuba mashuhuri kwa jeshi la wapiganaji elfu moja la Hurr wakati wa safari yake ambamo alisimulia hadithi[309] ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akasema kwamba kama kipindi kama hicho kinakuja ambapo hazina ya Waisalmu inatumika kwa namna kwamba kilicho halalishwa na Mwenyezi Mungu kinakatazwa na kile kilichoharamishwa na Mwenyezi Mungu kinaruhusiwa na Waislamu wananyamaza kimya; basi ni haki yake Mwenyezi Mungu kuwapeleka Waislamu hawa mahali ambapo madhalimu wamepangiwa kwenda. Imam alisema kwamba alikuwa na wajibu muhimu[310] katika mazingira kama hayo na ni mwangalifu kwa hilo. Haya ni madhehebu ya Imam Husain (a.s.). Hii ni roho ya kauli mbiu ya Imam Husain (a.s.). Huu ni ukweli uliomo ndani ya kauli mbiu ya Ashura. Kwa hiyo, kauli mbiu zinazotolewa kwenye mikusanyiko yetu. Husainiyah zetu

[309] Enyi watu! Mtukufu Mtume amesema, "Kama mtu anamuona mkandamizaji anaruhusu lolote lile ambalo limeharamishwa na Mwenyezi Mungu na anavunja ahadi iliyofanywa kwa Allah na kwenda kinyume na Sunnah za Mtukufu Mtume na akawa na uadui na Allah na mtu huyo hampingi mkandamizaji huyo pamoja na kwamba anayo mikono na ulimi, Mwenyezi Mungu atamweka mtu huyo jahannam pamoja na huyo mkandamizaji.

Wanamfuata Shetani na kumuasi Mola Mwenye Kurehemu. Wanaeneza uharibifu kwa wazi. Wamevuka mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu. Wanatumia hazina ya Waislamu kinyume cha sheria. Wanakataza yale ambayo Mwenyezi Mungu amehalalisha na wanaruhusu yale ambayo Mwenyezi Mungu ameharamisha. Katika hali kama hiyo, mimi ninawajibika zaidi kuliko wengine kusimama dhidi yake.' (*Tarikh Tabari*, Juz. 5, matukio ya mwaka wa 61 A.H.)

[310] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 68; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 183 ambapo kwenye *Tarikh Tabari*, Juz. 4. uk. 266 imetajwa lakini kuna tofauti ndogo.

na maandamano lazima ziwe madhubuti. Zinapaswa kuwaamsha watu na si kuwafanya watu walale. Mtu anayeanzisha kauli mbiu zisizo na maana ni kwamba atatupeleka mbali na Imam Husain (a.s.).

## KUMLILIA IMAM HUSAIN (A.S.)

Moyo unapaswa kujazwa sana na huzuni ya Shabbir:

Kwamba macho yangu yanabaki yamepakwa rangi ya

Moyo wangu. (Ghalib)

Kumlilia Imam Husain (a.s.) kuna malipo makubwa lakini kwa sharti kwamba Imam Husain (a.s.) yuko hai mioyoni mwetu. Imesimuliwa kwamba mapenzi kwa Imam Husain (a.s.) yamejificha kwenye nyoyo za waumini.[311]

Kama mtu anayo imani moyoni mwa mtu haiwezekani kwamba mtu huyo awe hana mapenzi na Imam Husain (a.s.) kwa sababu Imam Husain (a.s.) ni imani iliyowakilishwa.

Kauli mbiu zilizoanzishwa na masahaba wa Imam Husain (a.s.) nazo pia zinashangaza. Masaibu ya Karbala yalitokea kwa namna ambayo watu walilazimishwa kufikiri kwamba mkono wa Mwenyezi Mungu umeiweka sura au picha hii kwa namna ambayo kamwe haitafutika kwenye fikira za watu. Ni ajabu iliyoje kwamba Imam Husain (a.s.) anajitambulisha yeye mwenyewe kama ifuatavyo:

"Mimi ni Husain bin Ali. Sitatupa upanga kwa gharama yoyote ile. Nitawasaidia Ahlul-Bayt wangu na kubakia madhubuti juu ya dini ya mtume wetu."[312]

Mashairi ya Imam Husain (a.s.) ni ya msisitizo ulio tofauti. Aliposimama kwenye uwanja wa vita alighani beti nzito kama ifuatavyo:

"Mimi ni mtoto wa Ali, ambaye anatoka kwenye ukoo safi wa Hashim na inatosha kwa fahari yangu kwamba damu ya Ali inatiririka kwenye mishipa yangu."[313]

---

[311] *Khasaisul Husainia*, uk. 48

[312] Muntahaiul Amaal, Juz. 1, uk. 695; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk. 499.

[313] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 49; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 694; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 498.

Kama asemavyo Josh Malihabadi:

"Ambaye mishipani mwake hutiririka moto wa Badr na Hunain.

Mpiganaji huyo jasiri anaitwa Husain."

## USHUJAA WA IMAM HUSAIN (A.S.)

Ushujaa na utulivu wa Imam Husain (a.s.) huonyesha kwamba alikuwa ameacha kila kitu pembeni. Alionyesha ujasiri ambao Waarabu wote walio jasiri walishangazwa. Msimulizi kutoka upande wa adui anasema: "Ninaapa kwa Allah Mwenyezi, sijapata kuona mtu ambaye amepitia mateso mengi mno ya majanga kwamba watu wote wa familia yake, watoto na masahaba wanauawa mbele yake na anabakia mtulivu?"[314]

"Ninaapa kwa Allah Mwenyezi, ninashangaa kwamba ni ujasiri ulioje aliokuwa nao! Alikuwa na nguvu za aina gani hivyo kwamba utulivu wake haukuathirika hata baada ya kuvunjwa moyo pale ambapo wapendwa wake walikatwa vipande vipande mbele yake! Moyo jasiri wa aina hiyo hauwezi kuonekana popote hata kama utatafuta na kusaka kila mahali."

## ROHO YA ALI NDANI YA MWILI WA HUSAIN

Imam Husain (a.s.) aliteuwa sehemu fulani kuwa ndiyo kituo chake mnamo siku ya Ashura. Alikuwa na kawaida ya kufika mahali hapo, kusimama na kuwahutubia adui na halafu kurejea kwenye kambi yake. Ni jambo ambalo limeandikwa na wanahistoria wote kwamba hapana mtu aliyethubutu kupigana na Imam Husain (a.s.) kwenye mapigano ya mtu kwa mtu. Yeyote aliyefika mbele ya Imam Husain (a.s.) hakurudi akiwa na kichwa chake mwilini mwake. Mwanzoni watu wachache walijitokeza mbele kwa mapambano ya ana kwa ana na wote walisafirishwa kwenda Jahannam. Baada ya kuona hivi, Umar bin Saad alisema kwa sauti ya kupaza, "Mnafanya nini? Moyo wa baba yake, Ali, unagonga ndani ya kifua chake. Lazima mjue mnapigana na nani."[315] Baada ya hapo, mapambano ya ana kwa ana yalisitishwa na wale waovu walianza kutupa mawe na

[314] *Luhuuf*, uk. 119; *Tarikh Tabari*,Juz. 44, uk. 245; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 695

[315] "Huyu ni mtoto wa Ali ambaye ameua Waarabu wengi jasiri. Mshambulieni kutoka kila upande." *Muntahaiul Amaal*,Juz. 1, uk. 697; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 275

mishale kutoka kila upande. Hebu fikiria! Jeshi la watu elfu thelathini lilimzingira mtu mmoja peke yake kutoka pande zote na kuanza kutupa mishale na mawe kwa kumlenga yeye!

## HISIA ZA HESHIMA ZA U-HUSAINI

Imam Husain (a.s.) alipolishambulia jeshi hili, wapiganaji wake walianza kukimbia kama kundi la mbwa mwitu linapomkimbia simba. Imam Husain (a.s.) hakuwakimbiza sana kwa sababu hakutaka kwenda mbali na kambi yake. Hadhi yake haikumruhusu kwamba heshima ya watu wa nyumba yake ishambuliwe wakati yeye bado yu hai.

## KAULI MBIU YA KUMPWEKESHA MUNGU

Ndiyo maana alikuwa akiwashambulia adui, akiwafukuza na kuwapeleka mbali na kurudi kwenye kituo chake. Kituo hicho kilikuwa katika umbali ambapo sauti yake iliweza kusikika kwa urahisi kwenye kambi yake. Pamoja na kwamba watu wa familia yake hawakuweza kumwona lakini walikuwa wanamsikia yeye kwa urahisi. Hivyo, Imam Husain (a.s.) alikuwa na kawaida ya kukariri: **"Hapana nguvu na uwezo isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu Aliye Juu na Muweza wa Yote,"** kwa sauti ya kupaza ili kwamba Bibi Zainab apate kutulia, Sakina awe na uhakika na watoto wake wabaki na matumaini kwamba atarudi kwao akiwa hai. Kila alipofika kwenye kituo chake, alikuwa na tabia ya kupitisha ulimi wake kwenye midomo yake mikavu na kusoma: "Hapana mwenye nguvu na uwezo isipokuwa Allah Aliye Juu na Muweza wa Yote."[316] Husain alitaka kuonyesha kwamba uwezo aliopewa ulitoka kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa upande mmoja Imam alikuwa anaanzisha kauli mbiu ya kumpwekesha Mungu mmoja na kwa upande mwingine alikuwa anamjulisha Bibi Zainab kwamba alikuwa bado yu hai. Aliwaelekeza watu wa nyumba yake kwamba hapana ruhusa mwanamke kutoka nje ya hema almuradi bado yu hai.

[316] Muntahaiul Amaal, Juz. 1, uk. 295; Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain, uk. 496

## IMAM HUSAIN (A.S.) ANAAGA

Imam Husain (a.s.) alikwenda kuaga mara mbili kambini kwake. Aliaga mara moja kabla ya kwenda na halafu akarudi alipofaulu kufika kwenye mto Furati. Mara tu Imam Husain (a.s.) alipoingia mtoni, mtu akaita kwa sauti ya kupaza, "Ewe Husain! Unakunywa maji hapo na huku adui anaelekea kambini kwako." Aliposikia hili, Imam (a.s.) alirudi kutoka mto Furati na akaenda kambini kwake na akawaaga watu wa nyumba yake kwa mara nyingine.[317]

Wakati huo Imam (a.s.) alitoa tamko la kuwaelimisha watu wa familia yake: "Enyi watu wa familia yangu! Kuweni watulivu. Msiwawasike. Angalieni, mtachukuliwa mateka baada yangu lakini msisahau wajibu wenu wa kidini wakati mpo gerezani. Msitamke neno lolote ambalo linaweza kuwapunguzia malipo ya thawabu zenu. Pia mkumbuke kwamba hili ni shambulio la mwisho la adui. Linaweza kuwa ni sababu ya kufedheheka na kuangamia kwa adui. Kuweni watulivu, kwani Mwenyezi Mungu atawapeni wokovu kutokana na fitna ya watu wale madhalimu na atawaweka mbali na fedheha. Baada ya hayo, kuna kunyanyuliwa daraja kwa ajili yenu."[318] Haya ni maneno muhimu ya Imam Husain (a.s.), "Enyi watu wa familia yangu!! Kwa hakika ninyi mtachukuliwa mateka lakini Mwenyezi Mungu hatawaacheni mkafedheheshwa; yaani jela si fedheha kwenu; badala yake ni sababu ya heshimia na fahari."

Ndiyo maana pale ambapo watu wa Kufa walipotoa mkate kama sadaka kwa watoto wa mateka wenye njaa,[319] Bibi Zainab aliwazuia wasichukue mikate hiyo. Pamoja na kwamba wao walikuwa wafungwa, lakini hawakukubali fedheha. Kama simba amefungiwa kwenye tundu muda wote lakini bado yeye ni simba na kama mbweha yu huru; hata hivyo yeye ni mbweha tu. Hivyo, Imam Husain (a.s.) alipokwenda kwenye kambi yake kwa mara ya pili, watu wa familia yake walifurahi, Imam Husain (a.s.) alimuaga kila mmojawao na akatoka nje ya hema lakini watu wa nyumba yake hawakutoka nje kufuatana na amri yake.

[317] *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 276

[318] *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 491

[319] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 728

## MAZUNGUMZO YA SAKINA NA DHULJANAH

Baada ya muda fulani farasi wa Imam Husian (a.s.) aitwaye Dhuljanah alianza kutoa mlio mkali na watu wa nyumba ya Imam Husain (a.s.) wakadhani kwamba labda alikuwa anarudi kuaga kwa mara ya tatu (Shahidi Mutahhari hapa analia). Hata hivyo, walipotoka nje walikuta Dhuljana amesimama bila mpandaji wake (Shahidi Mutahhari analia zaidi). Kila mmoja alimzunguka Dhuljanah na kuanza kuzungumza naye. Sakina akasema, "Ewe Dhuljanah! Mimi ninakuuliza tu kwamba hivi kuna mtu yeyote aliyempa maji baba yangu au wamemuua akiwa na kiu yake?"[320] (Shahidi Mutahhari analia kwa sauti kubwa zaidi).

## NAUHA YA IMAM WA ZAMA ZETU (A.T.F.S.)

Mojawapo ya matukio ya Karbala kwa hakika huvunja moyo wa Imam wa zama Zetu. Imam wa zama zetu anasema:

"Dhuljanah alirudi kambini akilia kwa sauti kubwa. Wanawake walipomuona Dhuljanah bila ya mpandaji wake na matandiko yake yananing`inia, walitoka kwenye mahema yao na nywele zimefumuka na huku wanajipiga nyusoni."[321]

## IMAM WA ZAMA ANAGHANI *NAUHA*

"Ewe babu yangu mtukufu! Watu wa nyumba yako hawakutoka nje ya mahema yao kama ulivyowaamuru. Hata hivyo, walipomuona Dhuljanah bila mpandaji wake, walifumua nywele zao na kukimbia kuelekea uwanja wa vita. (Shahidi Mutahhari analia).

Miito ya 'Ewe Husain' na 'Ewe Muhammad' ilisikika kila mahali.

[320] *Masaib al-Masuumiin*, uk. 320
[321] *Damaus Sujum*, uk. 200; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk.706

# MAJILISI 46

## MASHINDANO BAINA YA SIFA ZA KI-HUSAIN SIKU YA ASHURA

Leo ni siku ya Ashura, ni siku ya Mi'raj kwa ajili ya Imam Husain (a.s.). Ni muhimu kwetu sisi leo kujaribu kupata msukumo kutoka kwenye moyo, heshima, umadhubuti, ujasiri na fikira angavu kutoka kwa Imam Husain (a.s.). Kama kuna chembe ndogo tu ya hisia ya ubinadamu ndani mwetu, basi inaweza kutuamsha.

Mwandishi mmoja mashuhuri, Abbas Mahmuud Aqqad anasema kwamba mnamo siku ya Ashura ilionekana kama vile sifa za Imam Husain (a.s.) zilikuwa zinashindana zenyewe kwa zenyewe, yaani kila sifa ya Imam Husain (a.s.) ilitaka kutangulia mbele ya zingine. Subira yake ilitaka kuwa bora zaidi ya sifa zingine. Uaminifu wake ulitaka kuwa bora zaidi. Ujasiri wake ulitaka kushinda sifa zingine zote.

Mshairi mmoja kwa uhodari kabisa amesema:

**Barabara ya uhai inanukia hadi leo**

**Ni ubora ulioje wa shaksia yenye manufaa ya Husain**

**Kwenye ukurasa wa mahaba na orodha ya maadili**

**Hata leo hii muhuri wa kanuni za Husain unang`aa.**

### UTULIVU WA IMAM HUSAIN (A.S.)

Siwezi kufanya hata maelezo kidogo kuhusu subira ya Imam Husain (a.s.) kwa sababu mimi ni mdogo mno nikilinganishwa nayo. Halafu pia ningethubutu kusema kwamba sifa ya Imam Husain (a.s.) ambayo ilikuwa inaonekana wazi zaidi ilikuwa ni nguvu ya moyo wake, utulivu wake, uimara wake. Sio jambo ambalo limesimuliwa na mimi peke yangu lakini hili lilitambulika mnamo siku ya Ashura. Ni maelezo ya msimulizi kutoka upande wa

adui ambayo yana maana sana. Yeye anasema, "Ninaapa kwa jina la Allah kwamba nimeshangazwa. Alikuwa na moyo wa aina gani huo! Alikuwa na nguvu ya aina gani hivyo kwamba utulivu wake haukuathiriwa hata pale alipovunjwa moyo baada ya wapendwa wake kukatwa vipande vipande mbele yake! Nguvu ya moyo wake haiwezi kuonekana popote hata kama ukifanya msako wa kina. Hili kwa kweli linastaajabisha."

## MAPINDUZI YA IMAM HUSAIN (A.S.) YALICHOCHEA MAPINDUZI MENGINE

Sio jambo la kawaida; inashangaza sana. Kila mara nilikuwa ninashangaa kwamba Imam Husain (a.s.) alikuwa anasonga mbele mnamo siku ya Ashura kwa namna ambayo kama vile alikuwa anatembea kuelekea kwenye mustakabali angavu wa siku za usoni baada ya kuona kwa macho yake ishara za kufuzu kwa mapinduzi yake.

Hakuwa na shaka kwamba ushindi ulikuwa unamwelekea yeye baada ya kuuawa kishahidi. Hakuwa na shaka kwamba siku ya Ashura ilikuwa ndiyo siku ya mwisho ya kupanda mazao. Kwa hiyo, asiwe na kinyongo kwa lolote alilokuwa anakabiliana nalo, kwa sababu matunda yake yangeonekana baada ya muda mfupi. Kwa hiyo, matunda ya mapinduzi yake yalianza kuonekana tangu ile siku ya Ashura. Hatimaye, tuliona kwamba usaliti na maasi dhidi ya Bani Umayyah yalianza mara tu baada ya kifo cha kishahidi cha Imam Husain (a.s.).

## SHAMBULIO LA KWANZA DHIDI YA UTAWALA WA UMAYYAH

Wa kwanza kupasua pazia kutoka kwenye uso wa fitina wa Bani Umayyah alikuwa mwanamke kutoka kwenye jeshi la Makafiri. Mwanamke huyu alitoa mchango muhimu katika kuelimisha muonekano wa kweli wa balaa hili. Mnamo nyakati za Alasiri, mwanamke huyo alipoona kwamba jeshi la Yazid lilikuwa linajitayarisha kushambulia kambi ya Imam Husain (a.s.), alikwenda mbio kwenye kambi ya Imam Husain (a.s.) alikuja huku akikimbia na akachukuwa nguzo ya hema mkononi mwake na akasimama

mbele ya mahema na kuyalinda. Mwanamke huyu alitoka katika kabila la Bakr bin Wail. Akaita kwa sauti ya kupaza, "Enyi dhuria wa Bakr bin Wail! Je bado mngali hai? Njooni mnisaidie kwa sababu watu hawa wanataka kuchukua hata nguo za wanawake wa familia ya Mtume (s.a.w.w.)"[322] Kupitia maneno yake machache, mwanamke huyu alionyesha dhahiri uduni mbaya wa adui.

## HISIA YA HESHIMA YA IMAM HUSAIN (A.S.)

Kwa maoni yangu, wakati ule Imam Husain (a.s.) alipowaaga watu wa familia yake ulikuwa wa huzuni mno. Hapakuwepo mtu yeyote aliyekuwa hai isipokuwa yeye. Tukio hili la kuondoka lilikuwa la kufadhaisha kweli lakini sababu ya Imam Husain (a.s.) kwenda kuaga kwa mara ya pili ni ya dhahiri kabisa. Imesimuliwa kwamba wakati Imam Husain (a.s.) alipokuwa anashambulia maadui kwa ukali kabisa na kuwarudisha nyuma majeshi ya Makafiri na yeye akaufikia mto Furati, adui akapata hofu kwamba kama Husain akinywa maji atapata nguvu upya. Hatimaye, mtu akaita kwa sauti ya kupaza, "Ewe Husain! Unakunywa maji ambapo jeshi linashambulia kambi yako." Aliposikia maneno haya, Imam mwadhamu kwa haraka sana aliondoka hapo mtoni.[323] Sijui kama maneno ya mtu huyo yalikuwa ya kweli au hapana au jeshi la Makafiri lilikuwa linajiandaa kushambulia kambi au hapana. Hata hivyo, ninajua kwamba Imam (a.s.) kufumba na kufumbua alifika kambini kwake. Kambi ilikuwa haikushambuliwa wakati Imam Husain (a.s.) alipofika hapo. Imam alitumia fursa hii kwa kuwakusanya wanawake na watoto kwa mara nyingine tena.

## BISHARA NJEMA ZA IMAM HUSAIN (A.S.) KWA WANAFAMILIA WAKE

Huu ni wakati ambapo utukufu wa nafsi ya Imam Husain (a.s.) unajionyesha. Kwanza alisema, "Enyi wanafamilia wangu! Jitayarisheni kuhimili ukatili." Ilikuwa kana kwamba aliwataka watu wa familia yake kuwa tayari kiakili kukabiliana na jambo hili. Hakusema la ziada. Hata hivyo, maara hapo akasema, "Enyi wanafamilia wangu! Mnapaswa kuwa na imani kwamba

[322] *Munatahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 710
[323] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 51

Mwenyezi Mungu atawalindeni nyinyi na kuwapeni ukombozi kutokana na fitina ya waeneza fitina. Atakurudisheni kwenye sehemu takatifu ya babu yenu kwa heshima kabisa. Baada ya hapo, fedheha ya adui yenu itaanza. Mnapaswa kuwa na uhakika kwamba Mwenyezi Mungu atamfanya adui yenu kuingia kwenye aina mbalimbali za adhabu hapa duiani."[324] Ilikuwa kama vile Imam alikuwa anaangalia hali ya siku za usoni kwa macho yake mwenyewe.

## IMAM HUSAIN NI DHIHIRISHO LA HALI YA HESHIMA TUKUFU

Imam Husain (a.s.) aliteua sehemu mnamo siku ya Ashura kama kituo wakati wa mapambano. Alikuwa akifanya mashambulizi kutokea hapo. Kwanza alipigana pambano la mtu na mtu. Maadui walikuja mmoja mmoja kwa makundi lakini Imam (a.s.) hakumuacha hata mmoja na kichwa chake. Mashambulizi ya Imam yalikuwa ya namna kwamba adui alirudi nyuma. Baada ya kuona hali hiyo, Umar bin Saad alisema kwa sauti ya kupaza, "Mnafanya nini sasa? Moyo wa Ali unagonga ndani ya kifua chake. Huyu ni mtoto wa yule mtu ambaye upanga wake uliangamiza fahari ya Waarabu mashujaa kabisa." Kwa namna hii Umar bin Saad kwa kweli alikuwa anajaribu kuwasha upya chuki ya Makabila ya Waarabu dhidi ya Imam Husain (a.s.). Hatimaye wapiganaji waliuliza, "Sasa tufanye nini?" Akajibu, "Hii si njia ya sawa. Kama mkienda mmoja mmoja hivyo, hakuna atakayebaki hai. Mnapaswa kumshambulia kutoka kila upande."

Maadui walikuwa wakikimbia kila mara Imam alipofanya mashambulizi, lakini wakati wote wa mapambano alihakikisha kwamba hakwenda mbali ya kambi yake. Hali ya heshima yake haikuruhusu kwamba mtu yeyote angethubutu kwenda karibu na kambi yake almuradi akingali hai. Aliwaamuru watu wa familia yake wasitoke nje ya mahema yao wakati yeye bado yu hai.

Kama umesikia mahali fulani kwamba watu wa familia ya Imam (a.s.) walikuwa wanatoka nje ya mahema yao na kusema kwa sauti: "tuna kiu" na kurudia mara nyingi; huo ni uwongo kabisa.[325]

[324] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 698; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 491

[325] Kadhalika, ipo hadithi ambayo inasimuliwa kwa umashuhuri sana kuhusu "kutomtii Allah," ambamo humo malaika Fitrus alipoteza mbawa zake. Malaika huyu alijisugua kwenye susu ya Imam Husain (a.s.) wakati alipozaliwa. Kama matokeo ya baraka za kuwepo kwa Imam (a.s), alirudishiwa mbawa zake. Kwa upande mwingine, Qur`ani Tukufu inasema: يَخَافُونَ رَبَّهُمْ مِنْ فَوْقِهِمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ "Wanamhofia Mola Wao aliye juu yao na wanafanya

Walitoka kwenye mahema yao mara moja tu, pale Dhuljanah aliporudi bila mpandaji wake. Yeyote aliyetoka nje wakati huo hakuweza kujua kitu gani kilikuwa kinatokea. Waliposikia Dhuljanah analia, walidhani kwamba Imam alirudi kuja kuwaaga kwa mara ya tatu.

## DHULJANAH WA IMAM HUSAIN (A.S.)

Inasimuliwa kwamba farasi wa Imam Husain (a.s.) aitwaye Dhuljanah alikuwa amefundishwa vema. Si tu Dhuljanah wa Imam (a.s.) lakini pia farasi wa maadui nao walifundishwa vema hivyo kwamba wakati wapandaji wao walianguka chini walikuwa wakitambua haraka sana. Hivyo, Dhuljanah alipoona kwamba Imam Husain (a.s.) ameanguka na alikuwa hawezi kunyanyuka kutoka pale alipokuwa, farasi huyo aliloanisha manyoya ya shingo yake na damu tukufu ya Imam Husain (a.s.) na akakimbia shoti kuelekea kambini[326] kuwaarifu watu wa familia ya Imam kwamba yeye ameuawa.

Kwa upande mwingine, watu wa familia walidhani kwamba Imam alirudi kuja kuwaaga kwa mara ya tatu. Hivyo basi, walitoka nje ya mahema yao. Hata hivyo, walipoyaona mazingira halisi, walianza kulia na kuomboleza wakimzunguka Dhuljanah pande zote. Imam alikuwa hajawaruhusu kutoka nje kabla ya hapo. Imam alikuwa ameteua kituo kwa ajili ya mapambano ambapo sauti yake ingesikika huko kambini kutokea hapo. Kwa njia hii, Imam (a.s.) alihakikisha kwamba matumaini yao yanakuwa hai.

---

wanayoamriwa." (Sura An-Nahl 16:50). بَلْ عِبَادٌ مُكْرَمُونَ Maana yake: hao ni waja waliotukuzwa (Sura Al-Anbiyaa 21:26). عَلَيْهَا مَلَائِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ لَا يَعْصُونَ اللَّهَ Tarjuma yake; "...wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamwasi Mwenyezi Mungu....." (Sura At-Tahrim 66:6) Allamah Sayyid Muhammad Tabatabai, mwandishi wa Tafsiir al-Mizan alijibu mojawapo ya maswali akasema kwamba tukio la Fitrus haliendani na aya za Qur`ani. Pia Qur`ani Tukufu inasema:

مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِلَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَرُسُلِهِ وَجِبْرِيلَ وَمِيكَالَ فَإِنَّ اللَّهَ عَدُوٌّ لِلْكَافِرِينَ

**Tarjuma: "Anayemfanyia uadui Mwenyezi Mungu na Malaika Wake na Mitume Wake na Jibril na Mikail, basi Mwenyezi Mungu ni adui kwa makafiri." (Sura Al-Baqarah 2:98).**

وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ

**"....lakini wema ni wa anayemwamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na Malaika, na Kitabu na Manabii;" (Sura Al-Baqarah 2:177). Aya zote hizi zinathibitisha kunyanyuliwa kwa hadhi ya malaika. (Ridhwaani)**

**Muntahaiul Amaal, Juz. 1, uk. 705**

[326] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 705

Wakati Imam alipokuwa anarudi kwenye kituo chake kila baada ya kumshambulia adui, alikuwa akisoma kwa sauti: “Hapana nguvu na uwezo isipokuwa kutoka kwa Allah, aliye juu na Mwenye nguvu,” (sijui kama sauti hiyo inaweza kuitwa sauti ya kupaza kwa sababu koo lake lilikwishakuwa kavu mno kwa sababu ya kiu kali; katika hali hiyo, Imam angewezaje kusema kwa sauti ya kupaza?) Alikuwa akikusanya nguvu zake zote na kusema: “Hapana nguvu na uwezo isipokuwa kutoka kwa Allah, aliye juu na Mwenye nguvu,” yaani; “Ewe Mola! Nguvu yoyote ile ya kiroho na kimaumbile aliyonayo Husain inatoka Kwako tu.” Watu wa familia yake walikuwa na kawaida ya kufurahi wanaposikia sauti hii kwa sababu walipata uhakika kwamba bwana wao alikuwa hai bado, na hii iliweka matumaini yao kuwa hai. Kwa upande mwingine, kila pale maadui waliposhambulia, walijaribu kumzingira Imam katika mduara mdogo zaidi. Maadui hao wa dini walikuwa wakimtupia Imam mishale na kumpiga mawe ambapo Imam aliwashambulia na kuwarudisha nyuma.

## MSHALE WENYE SUMU WACHOMA MOYO WA IMAM HUSAIN (A.S.)

Lazima utakuwa umesikia jinsi Ibn Saad alivyaonza vita mnamo siku ya Ashura. Pia lazima utakuwa umesikia kwamba Imam Husain (a.s.) hakuruhusu upande wake kuanza mashambulizi. Desturi hii ilifuatwa bila kukosa pale ambapo jeshi pinzani kwa dhahiri lilikuwa la Waislamu. Imam Ali (a.s.) aliifuata desturi hii hasa hasa. Huwa akisema, “Kamwe sitaanza mimi vita. Wao ndiyo waanze kupigana. Sisi tutawajibu baadaye.”

Pia Imam Husain (a.s.) hakuanza vita. Badala yake Umar bin Saad alitaka apewe upinde na mishale yake kwa kutafuta kumfurahisha Ubaidullah Ibn Ziyad. Baba yake Umar bin Saad alikuwa Sa’d bin Abi Waqqas, mtu aliyekuwa mashuhuri kwa kutupa mishale wakati wa siku za mwanzo wa Uislamu. Yeye (Umar) aliweka mshale kwenye upinde wake, akalenga kambi ya Husain na akasema kwa sauti ya kupaza: “Enyi watu! Kuweni mashahidi kwa Amiri Ibn Ziyad kwamba mimi nilikuwa wa kwanza kupiga kambi ya Husain kuanza mapambano.” Vita vya Ashura vilianza kwa mshale na vilikwisha kwa mshale. Ule mshale wenye sumu, ambao ndiyo ulihitimisha mapamabano, ulipiga moyo mtukufu wa Imam Husain

(a.s.). Mshale huo ulichoma kifua cha Imam kutokea upande wa mbele na kutokezea upande wa nyuma.[327] Kwa hiyo, Imam hakuweza kuuchomoa kutoka upande wa mbele. Imeandikwa kwamba Imam (a.s.) aliuchomoa mshale huo kutokea upande wa mgongo wake. Baada ya kupigwa mshale huu, Imam Husain (a.s.) hakuweza kujiweka sawa sawa kwenye mgongo wa farasi na kwa hiyo akaanguka chini. Hakuwa na nguvu za kutosha za kumwezesha kusimama.

## ABDULLAH BIN HASAN ALIJITOA MHANGA KWA AJILI YA AMI YAKE

Inasimuliwa kwamba baadhi ya watoto wa Imam Hasan (a.s.) walifuatana na Imam Husain (a.s.) kwenye safari ya Karbala. Mmojawao alikuwa ni Qasim. Pia mtoto mdogo kabisa wa Imam Hasan (a.s.), Abdullah, naye alikuwepo Karbala; huyu alikuwa na umri wa miaka kumi tu. Wakati Imam Hasan (a.s.) anauawa kishahidi mtoto huyu alikuwa na umri wa miezi michache tu. Imam Husain (a.s.) alimlea mtoto huyu. Imam Husain (a.s.) alikuwa anawapenda sana wapwa zake hawa. Labda alikuwa anawapenda watoto hawa zaidi ya watoto aliowazaa yeye kwani hawa walikuwa mayatima. Pia Abdullah alikuwa anampenda sana Imam Husain (a.s.). Imam Husain (a.s.) alimkabidhi Abdullah kwa dada yake, Zainab mnamo siku ya Ashura na alimuomba amtunze kwa uangalifu maalum kabisa. Bibi Zainab alikuwa anawahudumia watoto wakati wote kwa mfululizo. Ghafla, Abdullah alitoka nje ya hema. Bibi Zainab alimkimbilia ili amkamate lakini mtoto huyo akasema, "Ninaapa kwa jina la Allah, mimi sitamwacha ami yangu peke yake."[328] Aliposema hivi, mtoto huyu alikimbia kuelekea kwenye uwanja wa vita na akajitupa kwenye kufua cha Imam Husain (a.s.) ambapo Imam mwenyewe alikuwa katika hali mbaya. Wakati huo, mkandamizaji alitokeza akiwa na upanga tayari kumkata kichwa Imam. Mtu huyo aliponyanyua tu upanga wake, Abdullah alipiga ukelele, "Ewe mwanaharamu! Unataka kumuua ami yangu?"[329]

Mara tu mkandamizaji huyo alipomshambulia Imam (a.s.) kwa upanga wake, mtoto huyo aliweka mikono yake kama ngao ya kumkinga Imam la-

---

[327] *Biharul Anwar*, Juz. 55, uk. 53

[328] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 241; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 53

[329] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 241; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 53. Kwenye taarifa moja imeandikwa: '*Yabnal lakhnaa-*' na kwenye toleo lingine imeandikwa kama: '*Wailaka yabnal khabithati ataqtulu a`mmee*' - (Rizwani)

kini matokeo yake mikono hiyo ilikatwa. Mtoto alianza kulia, "Ewe ami yangu! Angalia wakandamizaji hawa walivyofanya mikono yangu."[330]

"Ninashahidilia kwamba uliamrisha mema na ulikataza maovu na ukafanya jihadi kwa ajili ya Allah kama inavyostahili kufanywa hadi ukaifikia yakini."

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**"...na punde watajua waliodhulumu ni mgeuko gani watakakao geuka?"**
**(Sura Ash-Shu'araa 26 : 227)**

330 *Mafaatiihul Jinaan*, Ziarat Mutliqa Imam Husain

# MAJILISI 47

## MANENO YA MWISHO YA IMAM HUSAIN (A.S.)

Almuradi palikuwepo na uhai ndani ya mwili wa Imam Husain (a.s.) mnamo siku ya Ashura, vita vikali vilipiganwa na vichwa vya wapiganaji wa Yazid vilikuwa vinaruka hewani. Hadi kufika Alasiri Imam alikuwa amechoka kwa sababu ya majeraha. Alianza kuhisi kizunguzungu akiwa juu ya farasi wake. Mtu mmoja alitupa mshale uliopakwa sumu ambao ulitua kwenye kufua cha Imam na akaanguka chini mara moja. Alisema nini wakati huo? Je! Alikubali fedheha kwa kutoa kiapo cha utii? Je! Alionyesha kuhitaji kitu chochote wakati huo? Hapana, hapana kabisa.

Baada ya kuonyesha johari za ujasiri katika mapambano, alielekea kwenye Qibla ambacho kamwe alikuwa hajakipa mgongo na akasema, "Ee Mola! Ninakubaliana na uamuzi wako. Ninatii amri yako. Hapana Mola isipokuwa Wewe. Ewe kimbilio la wale wasio na hifadhi!"[331]

Hii inaitwa ndio Jihadi ya kweli katika njia ya Allah na huu ndio ukamilifu halisi wa binadamu.

[331] *Maqtal–e-Husain*, Muqarram, uk. 283; imeandikwa kwenye *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 510 kama: "Mimi ni imara katika mtihani wako. Ee Mola! Hapana Mola ila Wewe. Ee msaidizi wa wale wanaotaka msaada! Hapana mola isipokuwa Wewe kwa ajili yangu. Wala hapana mungu yeyote isipokuwa Wewe."

# MAJILISI 48

## KIFO CHA MTU JASIRI

Kauli za Imam Husain (a.s.) zimejaa maadili ya heshima, staha na usharifu. Sababu ya kwa nini hali hii imeonekana zaidi katika kauli zake ikilinganishwa na zile za maasumini wengine ni kwamba msiba wa Karbala ulitokea ili nafsi takatifu ya Imam Husain (a.s.) iweze kuakisi vipengele vyake kwa uzuri zaidi.

Inasimuliwa kwamba mkuu wa mashahidi alipokuwa anaelekea Karbala, alikutana na watu wengi sana humo njiani ambao walimshauri kwa njia mbalimbali dhidi ya kuendelea na safari yake na walimuarifu kuhusu hatari kuhusu maisha yake. Hatimaye, Imam naye pia aliwajibu kwa namna mbali mbali na aliweka wazi lengo lake kwamba kwa hakika angeendelea na safari yake.

Pale mmojawao alipomwambia Imam (a.s.) kwamba mazingira yalikuwa mabaya na isingefaa yeye kuendelea na safari, Imam alijibu, "Majibu yangu ni kama yale ya sahaba wa Mtume aliyompa mtu ambaye alikuwa anamzuia asiende kushiriki katika Jihadi" Baada ya hapo, mkuu wa mashahidi alinukuu beti zifuatazo:

Kwa hakika nitakwenda. Kifo si sababu ya fedheha kwa mtu jasiri (ambaye nia yake ni kufanya Jihadi kama Mwislamu wa kweli). Kama mtu anapigana katika njia ya haki na akauawa, basi kifo kama hicho sio sababu ya aibu kwa sababu amepita kwenye njia ya waja waadilifu wa Mwenyezi Mungu. Kuwaunga mkono waja waadilifu, kutembea nao na kuungana nao hakufai kulaumiwa. Kumpinga mtu muovu ni chanzo cha fahari."

Baada ya hapo Imam (a.s.) akasema:

"Ninakwenda. Kifo sio chanzo cha fedheha kwa mtu ambaye anayo nia ya kupigana katika njia ya haki kama Mwislamu. Jihadi sio sababu ya kuwa fidhuli kwa sababu kifo hiki ni cha namna ambayo humfanya mhusika kukutana na watu wema. Ni heshima kwa mtu kujitoa mhanga uhai wake wakati anapigana na maadui wa njia iliyonyooka. Ama nitabaki kuwa hai katika

vita hii au nitakufa. Kama nitaendelea kubaki hai hakuna nafasi ya kufedheheshwa na kama nikifa nitakuwa sina wasiwasi."[332]

"Ama nitabaki hai au nitauawa Shahidi. Hakuna uwezekano wa chaguo la tatu. Njia niliyochagua ina malipo ya thawabu pande zote mbili. Kama nikibaki hai haitakuwa ni sababu ya aibu kwa sababu nimekikumbatia kifo. Kama nikiuawa, basi pia sitajuta. Maisha yasiyo na hofu ya kifo ni maisha ambayo sio sababu ya fedheha. Kama nikiuawa kifo changu hakitakuwa dhihaka hata kidogo." (Mistari mingine inazungumzia jambo lile lile lililotajwa kwenye mistari miwili ya kwanza.) "Ni fedheha tosha kwako kwamba unaishi na una hali ya kushindwa kunakofedhehesha. Mimi siwezi kuvumilia hili."

## "MFUNGWA WA DUNIA HII HATAMBUI YALIYOKO DUNIA ZINGINE"

Zipo beti nyingine chache, ambazo ama zimetungwa na Imam Husain (a.s.) au na baba yake mtukufu, Amirul-Mu'minina, (a.s.), ambazo zimesimuliwa kutoka kwenye Makusanyo ya Amirul Mu'miniin (a.s.). Kuhusu hayo pia imesimuliwa kwamba beti hizi pia zilighaniwa na Imam Husain (a.s.).[333]

"Dunia inaonekana kuwa nzuri sana kwamba mwanadamu anapendezwa nayo, lakini dunia ya Akhera ni bora zaidi na kubwa zaidi kuliko dunia hii. Mfungwa wa dunia hii hatambui dunia zingine."

"Kama mtu ataacha utajiri wake wote kabla ya kuondoka hapa duniani, je sio vyema zaidi kwamba awasaidie wengine kwa utajiri huo almuradi bado yu hai?"

"Kama kifo ni wajibu wa kila mtu, inaleta tofauti gani iwapo mtu anafia kitandani pake au kwenye uwanja wa vita au kwa sababu ya homa? Lakini itakuwa ni uzuri ulioje kwa mtu kufa kifo kizuri! Kuuawa Shahidi kwa upanga katika njia ya Allah sio tu ni vizuri lakini pia ni bora zaidi kwa mwanadamu."[334]

---

[332] Imam Husain (a.s.) alikariri beti hizi akimjibu Hurr ambaye alikuwa anasikitika kwa kuhatarisha maisha ya Imam.

[333] *Diwan Imam Ali*, uk. 312

[334] *Tarikh Ibn Asakir*, uk. 123; *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 374

## HISIA ZA KUVUNJWA VIPANDE VIPANDE KATIKA NJIA YA ALLAH

Unapaswa kukadiria hali ya kiroho na hisia ya furaha kwa mtu ambaye ameghani beti hizo hapo juu. Nina uhakika ni mtu mmoja tu ndiye atakaye kujia katika kumbukumbu zako ambaye alijisalimisha kwenye Makazi kama hayo ambapo atapambwa zaidi na zaidi.

Imam Husain (a.s.) alifurahi sana katika kuona kwamba damu yake, iliyokuwa imepangiwa itiririke juu ya ardhi ilikuwa inatiririka katika njia ya Mwenyezi Mungu, paji la uso wake likiwa limepasuliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu na mishale inapiga kifua chake katika njia ya Allah!

Inasimuliwa kwamba mwili wa Imam Husain (a.s) ulikuwa na majeraha elfu moja, mia tisa na hamsini na moja (Majeraha 1951).

Kama unaweza kuona furaha ya kuvunjwa vipande vipande katika njia ya Mwenyezi Mungu, majeraha yaliyomo kwenye kifua cha Imam Husain (a.s.) yangeonekana kama medali, ambazo zinaongeza heshima yake.

## NYANDA ZA CHINI ZA UFIADINI

Wakati wa mwisho wa uhai wake, Imam Husain (a.s.) alilala kwenye ardhi iliyoinama. Hakuwa na nguvu za kumwezesha kusimama. Mahali ambapo Imam Husain (a.s.) aliuliwa Shahidi palikuwepo na namna ya mwinamo. Mahali hapo pakaitwa "Nyanda za chini za ufiadini." Kama Imam Husain (a.s.) angekuwa mbali kidogo na sehemu hii watu wa familia yake wasingeweza kumuona. Mwili wa Imam Husain (a.s.) ulikuwa na majeraha mengi sana na damu nyingi ilikuwa imetoka mwilini mwake wakati wa mwisho wa uhai wake hivyo kwamba hakuweza kuvumilia kiu yake na uwezo wake wa kuona mbali ulififia. Pamoja na kuwa katika hali hii, maadui hawakuthubutu kuwashambulia watu wa familia yake. Walidhani kwamba Imam Husain (a.s.) angewatega kwa kujifanya hivyo. Maadui walikuwa na uhakika kwamba Imam angewashambulia kwa ukali kabisa almuradi bado angali na uhai mwilini mwake.

Mamluki mmoja alijitokeza mbele na kutaka kukata kichwa cha Imam (a.s.) lakini hakuthubutu kumkaribia. Wasimulizi wa tukio hili wanasema kwamba Imam Husain (a.s.) alikuwa mtu mwenye adhama kuu. Alikuwa

mwadhama wa Mwenyezi Mungu. Imam asingeweza kuvumilia kuona kambi yake inashambuliwa wakati akiwa na uhai mwilini mwake.

Hivyo, maadui walipodhani kwamba Husain (a.s.) amekosa uhai, walisonga kuelekea kwenye kambi yake. Imam alipoihisi hatua yao hii, yeye alikusanya nguvu zake zote na akasimama akiwa ameegemea upanga wake na akasema kwa sauti ya kupaza akiwashutumu maadui zake:

"Enyi wafuasi wa dhuria wa Abu Sufyan! Enyi mliouza dhamira zenu kwa kizazi cha Abu Sufyan! Mimi ninapigana na nyinyi na lazima ninyi mpigane na mimi tu. Wale wanawake na watoto wamefanya madhara gani kwenu nyinyi? Kama hamumtambui Mwenyezi Mungu, kama hamuogopi Akhera, kitu gani kimejiri kwenye heshima yenu na uungwana wenu wa kibinadamu? [335]

[335] *Luhuuf*, uk. 120; na *Falsafa Akhlaq*, uk. 160-161

# MAJILISI 49

## FURAHA YA IMAM HUSAIN (A.S.) WAKATI WA SHAHADA YAKE

Imesimuliwa kwamba mara baada ya Imam (a.s.) kukamilisha Swala yake ya Alfajiri akiwa na masahaba wake mnamo siku ya Ashura,[336] aliwaambia masahaba wake:

"Enyi masahaba jasiri! Jiandaeni kwa kifo. Kumbukeni kwamba kifo ni daraja, ambalo litawachukua kutoka katika dunia hii na kuwapeleka kwenye dunia nyingine. Daraja hili litawachukua kutoka kwenye dunia hii ya maovu na kuwapeleka kwenye dunia ya juu sana, yenye uadilifu na huruma."[337]

Hii ilikuwa sehemu ya hotuba ya Imam. Sasa tuangalie vitendo vyake katika suala hili.

Nukta nitakayoitaja hapa haikusemwa na Imam Husain (a.s.). Imeandikwa na wasimulizi. Hilal bin Nafi'i, afisa mawasiliano wa Umar Ibn Saad, ameelezea tukio hili. Anasema kwamba alishangazwa na dhamira ya Husain bin Ali. Muda wa kifo chake cha kishahidi ulipokaribia na mabalaa yake kuongezeka, uso wake ulizidi kunga`ra zaidi kama mtu anayekaribia muda wake wa mkutano. Yule aliyelaaniwa kuanzia mwanzo hadi mwisho ambaye alikuja kumkata kichwa, alikuwa amehofishwa na utukufu wa mng`aro wa uso wa Imam hivyo kwamba hakuweza kusogeza upanga wake. Anasema, "Nilipofika pale alipokuwa Husain bin Ali na kutazama uso wake, nilipotea kwenye mnga`ro wa mwanga uliokuwa unamulika kutoka usoni mwake na niliogopa sana hivyo kwamba niliacha nia ya kumuua."[338]

[336] Imesimuliwa kutoka kwa Imam Sajjad (a.s) kwenye *Mani al-Akhbaar*, uk. 288 kwamba mazungumzo haya yalifanyika wakati Imam Husain (a.s.) na masahaba wake wakikabiliwa na hali ngumu. Isipokuwa Imam Husain (a.s.) na masahaba wake wateule ambao imani yao madhubuti haikuwa na mfano wa kulinganisha, wengine wote nyuso zao zilisawajika na waliogopa. Halafu Imam Husain (a.s.) aliamsha kujiamini kwao na imani yao kwa maneno haya.

[337] *Maani al-Akhbaar*, uk. 288

[338] *Luhuuf*, uk. 128; *Mausuat-e-Kalimat al-Imam al-Husain*, uk. 513

## KULINDA KAMBI HADI DAKIKA ZA MWISHO

Inasimuliwa kwamba Imam Husain (a.s.) alichagua sehemu kwa ajili ya mapambano yake ambapo ni karibu sana na kambi yake. Kulikuwepo na sababu mbili za kufanya hivyo. Kwanza, alijua kwamba adui alikuwa muoga sana na asingekumbuka kwamba alikuwa na uadui na Husain tu, na kwamba asingeacha kuwadhuru wanawake na watoto pale kambini. Pili, hakutaka mtu yeyote kugusa mahema yake wakati bado yu hai na neva zake zikigonga. Hatimaye, wakati wa vita, kama adui walimkimbia hakuwafukuza kwenda nao mbali na alirudi mahali pale kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote anayeshambulia kambi yake.

## "MTU YEYOTE ASITOKE NJE YA MAHEMA WAKATI NINGALI HAI"

Alitaka kwamba wanafamilia wake wataarifiwe kwamba alikuwa hai bado. Kwa hiyo, aliteuwa sehemu kama kituo cha kati ambapo sauti yake ingesikika kwa urahisi kambini kwake. Alikuwa na akishambulia adui na kurudi kwenye kituo hicho na kukariri kwa sauti ya kupaza: "Hapana nguvu na uwezo isipokuwa kutoka kwa Allah, Aliye juu, Mwenye nguvu." Waliposikia sauti hii ya Imam Husain (a.s.), wanawake walikuwa wakishusha pumzi ya maliwazo kwamba mkuu wao alikuwa bado yu hai.

Imam (a.s.) aliamuru watu wa familia yake kwamba hapana ruhusa kwa mwanamke kutoka nje ya mahema almuradi bado akingali hai. Ni lazima usiamini kwamba mwanamke yeyote alitoka nje ya mahema wakati Imam alikuwa bado hai kama inavyosimuliwa sana. Kamwe haikutokea hivyo. Hiyo ilikuwa ni amri ya Imam kwamba si ruhusa kwa mwanamke yeyote kutoka nje ya mahema almuradi Imam bado yu hai. Imam (a.s.) aliwaambia pia watu wa familia yake, "Angalieni, hampaswi kutamka neno lolote, ambalo linaweza kupunguza malipo ya thawabu zenu. Kuweni wavumilivu. Mwisho wenu ni mzuri sana. Mtalindwa kutokana na fitina ya wapenda fitina. Baada ya muda si mrefu Mwenyezi Mungu atamuadhibu adui yenu.[339]

Wanawake hawakuruhusiwa kutoka nje. Pia wasingeweza kutoka nje wenyewe. Kama ambavyo hadhi ya Imam (a.s.) isivyoweza kumruhusu mwan-

[339] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 298

amke yeyote kutoka nje, wanawake hao hawakutoka nje kwa sababu ya wao kuwepo kwenye daraja la wasiokosea.

Kwa hiyo, pale ambapo watu wa familia ya Imam walipokuwa wakimsikia anakariri, 'Hapana nguvu na uwezo isipokuwa kutoka kwa Allah, Aliye juu, Mwenye nguvu,' walikuwa na wakishusha pumzi ya faraja.

Kwa kuwa Imam alikwisha kuja kambini mara moja au mbili  hata baada ya kuaga, watu wa familia yake walimngojea arudi.

## FAMILIA YA IMAM (A.S.) WASOMA *NAUHA* WAKIMZUNGUKA DHULJANAH

Katika siku hizo, Waarabu waliwafundisha farasi wao vema kwa ajili ya vita kwa sababu farasi ni mnyama anayeweza kufundishwa vema. Mara tu mpandaji wake akiuliwa, farasi anaonyesha athari maalum.

Watu wa familia ya Imam (a.s.) walikuwa wanangojea kusikia sauti fulani au kumwangalia Imam (a.s.) hapo nje. Ghafla wakamsikia Dhuljanah analia. Walikwenda kwenye mlango wa hema wakidhani kwamba Imam (a.s) amewasili lakini badala yake wakamuona Dhuljanah akiwa peke yake na tandiko lake likiwa linaning`inia. Walianza kupiga kelele wakisema: "Yaa Husaina, Yaa Muhammada" na wakamzunguka Dhuljanah kutoka pande zote. (Kulia kwa huzuni ni sehemu ye maumbile ya mwanadamu. Mwanadamu anapotaka kuonyesha huzuni yake, hulia, huzungumza na mbingu, wanyama au wanadamu wengine) na wote walianza kulia kwa namna moja au nyingine.[340]

Imam aliwaamuru watu wa familia yake wasilie lakini aliwaruhusu walie baada ya yeye kuuliwa Shahidi. Kwa hiyo, walianza kulia kwa sauti kubwa.

## SWALI LA KUHUZUNISHA LA SAKINA KWA DHULJANAH

Imesimuliwa kwamba Husain (a.s.) alimpenda sana binti yake Sakina. Baadaye, binti huyu akawa hodari na maarifa mengi sana na wanazuoni

[340] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 60

wote wanazungumza kuhusu yeye kwa heshima.[341] Imam Husain (a.s.) alimpenda sana Sakina naye Sakina alikuwa anampenda baba yake sana sana.

Imeandikwa kwamba Sakina alikuwa na desturi ya kughani mashairi ya kupasua moyo hivyo kwamba kila mtu aliguswa na kuvutika. Wakati watu wa familia walimzunguka Dhuljanah na kuomboleza, Sakina alizungumza na Dhuljanah na akasema, "Ewe farasi mtiifu wa baba yangu! Niambie iwapo baba yangu alipewa maji au aliuawa akiwa na kiu?"[342]

Ilitokea wakati gani? Ilitokea pale ambapo Imam alianguka kutoka kwenye mgongo wa farasi wake.

وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ

**"...na punde watajua waliodhulumu ni mgeuko gani watakao geuka?"** **(Sura Ash-Shu'araa 26 : 227)**

[341] Wanazuoni wengi wa India na Pakistan wanasimulia kwamba binti yake Imam Husain (a.s.) Sakina mwenye umri wa miaka minne, alifia jela huko Syria na amezikwa huko.(Rizwani)

[342] *Masaib al-Masuumiin*, uk. 320

# MAJILISI 50

## WAKATI MGUMU SANA KWA WANAFAMILIA WA IMAM (A.S.)

Tarehe 11 ya Muharram ilikuwa siku ngumu sana kwa wanafamilia wa Imam Husain (a.s.). Kama tukichambua vipengele vyote hasi na chanya (vibaya na vizuri) kuhusu tukio la Karbala, tunaweza kuhisi kwamba tukio la Karbala linapiga picha ya mfano wa mazungumzo baina ya Malaika na Mwenyezi Mungu wakati wa kuumbwa kwa Nabii Adam (a.s.) na jibu ambalo Mwenyezi Mungu aliwapa. Malaika walisema:

قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ وَنَحْنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ

**".....Utaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu, na hali sisi tunakutakasa kwa sifa Zako na kukutaja kwa utakatifu Wako? Akasema (Mwenyezi Mungu): Hakika mimi nayajua msiyoyajua."**
**(Sura Al-Baqarah 2 : 30)**

Malaika walitabiri maovu mengi wakati wa uumbwaji wa wanadamu katika asili yao na yote yalionyeshwa ndani ya Karbala. Kwa upande mwingine, Mwenyezi Mungu alisema, "Enyi malaika wangu! Nyinyi mnaona upande mmoja wa sarafu na sio upande ule unaonga`ra zaidi, ambao unaonyesha ukuu wa mwanadamu." Ubora huu wa mwanadamu ulionekana dhahiri ndani ya Karbala.

Hivyo, uwanja wa vita wa Karbala ulikuwa wa kushangaza sana na wa mtihani.

## UFIDHULI WA ADUI

Yazid alifanya vitendo vya kifidhuli ndani ya Karbala, ambavyo vilikuwa havijawahi kufanywa na yeyote au vimefanywa na watu wachache sana. Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa hakuna mfano unaoweza kulinganishwa na matendo ya kifidhuli kama hayo. Mojawapo ya vitendo hivyo ni kumuua kishahidi kijana au mtoto mbele ya mama zao. Hapo Karbala watu nane waliuliwa mbele ya mama zao au kukatwa vichwa au kukatwa vipande vipande. Miongoni mwao, watatu walikuwa vijana na watano walikuwa ni watoto.[343]

## KIFO CHA KISHAHIDI CHA ALI ASGHAR

Miongoni mwa mashahidi hao wanane, mmojawao alikuwa Abdullah, ambaye anajulikana zaidi kama Ali Asghar. Mama zao mashahidi hao walikuwepo Karbala. Kwa mujibu wa vitabu vya kuaminika vya historia, mtoto huyu mchanga wa Imam Husain (a.s.) aliuliwa kishahidi nje ya hema. Imam Husain (a.s.) aliingia ndani na akasema, "Dada Zainab! Mlete huyo mtoto wangu anayenyonya ili nimuage."[344]

Inasimuliwa kwamba Bibi Zainab alimpeleka mtoto kwa Imam. Imam (a.s.) akamchukua mtoto huyo mikononi mwake na akataka kumbusu. Mama wa mtoto huyo alisimama kwenye mlango wa hema akitazama tukio hili ambapo mshale ulitupwa kwa amri ya Umar bin Saad; ambao ulipenya kwenye shingo ya kichanga huyo.

Shahidi mwingine kama huyo ni Qasim, ambaye alikuwa na uso unaopendeza kama mwezi. Mama yake pia alikuwepo hapo Karbala.[345] Hata hivyo, mama yake Mtukufu Ali Akbar, Laila, hakuwepo Karbala. Ingawaje inasimuliwa kwa ujumla kwamba Bibi Laila alikuwepo hapo Karbala, ukweli ni kwamba jina lake halijaandikwa popote katika matukio ya Karbala.[346]

---

[343] *Absarul Ain,* uk. 130

[344] ***Munatahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 693**

[345] Jina la mama yake Qasim lilikuwa Ramla. Alikuwa Umme Walad. *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 263

[346] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 675

# BIBI ZAINAB ALIHISI ANA DENI KWA HUSAIN (A.S.)

Zainab alimuona mwanawe, Aun bin Abdullah bin Ja`far Tayyar anauliwa kishahidi mbele ya macho yake ndani ya Karbala. Watoto wawili wa Abdullah bin Ja`far Tayyar walifuatana na Imam Husain (a.s.) kwenda Karbala na wote waliuliwa kishahidi. Mmojawao alikuwa mtoto wa Bibi Zainab.[347] Ni ukweli uliothibitishwa kwamba ni mtoto mmoja tu wa Bibi Zainab aliyeuliwa kishahidi ndani ya Karbala. Tabia ya daraja la juu ya Bibi Zainab inafaa kufahamika kwamba hakuna miongoni mwa vitabu vya historia ambacho kimeandika kwamba alilia kabla au baada ya kufa kishahidi mwanae mpendwa katika kumkumbuka. Ilielekea kwamba kila alipotaka kuita jina la mwanae, alikuwa akiacha kufikiri kwamba ingekuwa ni sababu ya kutomheshimu kaka yake, Husain. Maana yake ni kwamba, alikuwa akifikiria kwamba mwanae hakutosheleza kama mhanga kwa kaka Husain. Mathalani, Bibi Zainab alitoka mbio nje ya hema alipouliwa Shahidi Ali Akbar na akalia, "Ewe kaka yangu! Ewe mpwa wangu!"[348] Hata hivyo, hakuna mtu aliyemuona Bibi Zainab akionyesha huzuni sana wakati mwanae alipouliwa kishahidi.

Mmojawapo wa vijana kati ya watoto wa Muslim Aqiil pia aliuliwa kishahidi mbele ya mama yake. Mama huyo alikuwa ni Rukayya, mtoto wa Imam Ali (a.s.).[349]

(Mashahidi wote wale walikuwa ni kutoka dhuria wa Mtukufu, Abu Talib).

Mashahidi wawili au watatu walitokana na masahaba wa Imam Husain (a.s). Mmojawao alikuwa Abdullah bin Umair Kalbi,[350] ambapo haijulikani ni masahaba gani ambao walikuwa wazazi wa hao mashahidi wengine vijana.[351] Hawa vijana wawili pia waliuliwa kishahidi mbele ya mama zao. Nimekwishazungumza kuhusu wao kwenye hotuba zangu za nyuma za maombolezo (Majalis).

347 Mtoto wa pili wa Abdullah bin Ja`far alikuwa Muhammad ambaye jina la mama yake lilikuwa 'Khausa.' *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 262.

348 Kwenye *Irshad* imeandikwa ifuatavyo, Shaykh Mufid, uk. 239 na *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 674; '*Yaa ukhayyah wabna ukhayyaah.'*

349 Jina la huyu mtoto wa Muslim lilikuwa Abdullah. *Absarul Ain*, uk. 130

350 Kijana huyu alikuwa Wahab bin Abdullah bin Habbab Kalbi ambaye ndio kwanza ameoa karibuni tu. (Rizwani)

351 Jina la mtoto huyu lilikuwa Amr bin Junada Ansari. *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 253

## MAMA AMBAYE MWANAE ALIKATWA KICHWA MBELE YAKE

Mtoto wa umri wa miaka kumi kutoka familia ya Husain aliuawa kishahidi baada ya Shahada ya Imam Husain (a.s.). Sikumbuki jina lake. Wakati palipotokea vurugu hapo kambini baada ya kifo cha kishahidi cha Imam Husain (a.s.), mtoto huyu alikimbia na kutoka nje. Imeandikwa kwenye vitabu vya msiba wa Karbala kwamba mtoto huyo hakuweza kuelewa kilichokuwa kinaendelea na alitoka nje akiwa amechanganyikiwa. Msimulizi anasema kwamba yeye hawezi kusahau kwamba kulikuwepo na hereni kwenye masikio ya mtoto huyo na mama yake alikuwa amesimama karibu naye ambapo ghafla dhalimu mmoja alijitokeza na akamkata kichwa mtoto huyo.[352]

Kifo cha kishahidi cha mtoto mwingine zaidi, ambacho kilikuja kuwa sababu ya huzuni kwa Imam Husain (a.s.) ni cha Abdullah bin Hasan. Mtoto huyu wa Imam Hasan (a.s.) alikuwa na umri wa miaka kumi. Mama yake alikuwepo Karbala.[353] Alilelewa chini ya uangalizi wa Imam Husain (a.s.). Imam Husain (a.s.) alikuwa anampenda sana ukumbusho huyu wa kaka yake. Inasimuliwa kwamba wakati Imam Husain (a.s.) alipokuwa amelala kwenye vilima vya ufiadini katika sekunde zake za mwisho, mtoto huyu alitoka nje ya mahema na akakimbia kuelekea kwenye uwanja wa vita. Bibi Zainab alimkamata lakini mtoto huyo aliweza kumponyoka na akakimbia huku akisema, "Naapa kwa jina la Allah siwezi kumwacha ammi yangu peke yake." Alipofika bondeni aliangukia juu ya mwili wa Imam Husain (a.s.). Utukufu ni wa kwake Mwenyezi Mungu! Huu ni uvumilivu uliotukuka kwa jinsi ilioje! Ni jinsi gani subira ya Husain ilivyo kuu! Ni jinsi gani moyo wa Husain ulivyo mtulivu! Imam Husain (a.s.) alimchukua mtoto huyo mikononi mwake. Mtoto huyo alianza kuzungumza na Imam (a.s.). Muuaji alijitokeza akiwa na upanga ili amkate kichwa Imam. Mtoto huyo akasema, "Ewe mwana wa haramu! Unataka kumuua ammi yangu?"[354] Mara tu mkandamizaji huyo aliponyanyua upanga tayari kukata kichwa cha Imam, mtoto huyo aliweka mikono yake pale upanga ulipolenga na matokeo yake mikono yote miwili ikakatwa. Mtoto huyo alilia kutaka asaidiwe, "Ewe ammi yangu!

[352] Jina la mtoto huyu lilikuwa Muhammad bin Abi Saiid bin Aqiil. *Maqtal-e-Husain*,Muqarram, uk. 280

[353] *Absarul Ain* , uk. 130

[354] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 241; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 153; Imeandikwa kama ifuatavyo kwenye *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 700: "Ewe mwana wa mtu mchafu! Mwenyezi Mungu akulaani wewe! Unataka kumuua ammi yangu?"

Nisaidie." Imam Husain (a.s.) alishusha pumzi, "Ewe kumbukumbu ya kaka yangu! Kuwa na subira. Hivi punde utakutana na baba yako na babu yako."

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu na kwa Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)."

# MAJILISI 51

## BIBI ZAINAB AONGOZA MSAFARA

Historia ya Karbala ni historia ambayo kwamba ndani yake wanamume na wanawake wametoa michango yao muhimu. Katika historia hii kila upande umekuwa na michango yao lakini pakiwepo na tofauti kwamba wanamume walichangia bila kuvuka mipaka yao na wanawake hivyo hivyo. Na huu ndiyo muujiza wa Uislamu kwa sababu hautaki mtu awe mnunuzi wa Jahannam. Dunia ya leo inapaswa pia kukubali kwamba wanamume na wanawake wanayo mipaka yao. Kama sio leo, ukweli huu utakubalika huko siku za baadae.

Imam Husain (a.s.) aliwachukua watu wa familia yake na kufuatana nao kwenda Karbala kwa sababu alitaka tabia ya wanawake ipambwe na ionyeshwe katika historia hii ya kudumu. Alitaka Bibi Zainab atoe mchango wake kama kiongozi katika utengenezaji wa historia hii, lakini akiwa amebakia kwenye mipaka ya jinsia ya kike na si kuvuka mipaka popote pale.

Tabia ya Bibi Zainab ilianza kuonekana mara tu baada ya Alasiri ya Ashura. Sasa alionekana kama kiongozi wa familia ya Imam (a.s.) kwa sababu Imam Sajjad (a.s.), ambaye ndiye tu mwanamume aliyebaki hai, alikuwa mgonjwa sana na Bibi Zainab alikuwa anamuuguza. Ilikuwa ni amri ya Ibn Ziyad kwamba hapana mwanamume yeyote miongoni mwa dhuria wa Imam Husain (a.s.) anabaki hai. Kwa hiyo, majaribio kadhaa yalifanywa kutaka kumuua Imam Sajjad (a.s.) lakini adui akasema, "Atajifia mwenyewe kwa maradhi. Kwa nini tumuue?"[355] Huo ulikuwa ni utashi wa Mwenyezi Mungu, ambao ulitaka kuweka uzao wa Imam Husain (a.s.) kuwa hai daima milele.

### "TUPITISHE KATIKATI YA UWANJA WA VITA"

Watu wa familia ya Imam Husain (a.s.) walichukuliwa mateka mnamo tarehe 11 ya mwezi wa Muharram na walilazimishwa kupanda wanyama (nga-

[355] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 242; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 61

mia au punda) kwa matandiko ya mbao. Hawakuruhusiwa kuweka nguo kwenye makalio hayo kwa sababu jeshi la wakandamizaji walitaka wateseke zaidi hasa. Watu wa familia hiyo walisema, "Tafadhalini sana, kwa ajili ya Allah, tupitisheni katikati ya uwanja wa vita (ili tupate kuwaaga wapendwa wetu ambao wameuawa kishahidi)."[356]

## BIBI ZAINAB AOMBOLEZA KWENYE MWILI WA KAKA YAKE

Ni miguu ya Imam Sajjad tu ndiyo iliyofungwa kwenye tumbo la kipando chake kwa sababu yeye alikuwa mgonjwa ambapo wengine walikaa huru kwenye vipando vyao. Walipofika kwenye uwanja wa vita wote walijiangusha kutoka kwenye vipando vyao. Bibi Zainab alipofika kwenye mwili wa Imam Husain (a.s.), alimuona akiwa katika hali ambayo kamwe hajapata kumuona nayo kabla ya hapo. Aliona kwamba mwili wa kaka yake ulikuwa umelala bila kufunikwa sanda na alikuwa amekatwa kichwa. Hatimaye aliusemesha mwili ule uliokuwa umekatwa kichwa, "Nanitolewe mhanga kwa ajili yako, Ewe kaka yangu! Umeteseka kwenye mabalaa na umeondoka hapa duniani. Umeondoka hapa duniani na kui yako." Baada ya hapo alilia sana hivyo kwamba Wallahi maadui na hata marafiki wakalia pia.[357]

## WAJIBU WA BIBI ZAINAB

Pamoja na kwamba mkusanyiko wa kwanza wa maombolezo (Majilisi) katika kumkumbuka Imam Husain (a.s.) ulianzishwa na Bibi Zainab, kamwe hakuwa mzembe kuhusu wajibu wake. Kumtunza Imam Sajjad (a.s.) ilikuwa mojawapo ya wajibu wake.

Kwa hiyo, alikuwa na kawaida ya kutupa jicho kukagua uso wake mara kwa mara. Bibi Zainab alipoona kwamba Imam Sajjad (a.s.) alikuwa haweza kujidhibiti baada ya kuona mwili wa Imam Husain (a.s.) ambao kichwa chake kimekatwa na haukufunikwa nguo, alihisi kwamba yeye Imam Sajjad naye angefariki dunia kutokana na maumivu. Haraka sana aliondoka pale ulipokuwa mwili wa Imam Husain (a.s.) na alikwenda kwa Imam Sajjad (a.s.) na akasema, "Ewe mtoto wa ndugu yangu! Kwa nini upo ka-

[356] *Luhuuf*, uk. 132; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 58
[357] *Luhuuf*, uk. 134; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 58; *Maqtal-e-eHusain,* Muqarram, uk. 307

tika hali hii? Inaonekana kama vile roho yako itaondoka kwenye mwili wako." Imam Sajjad (a.s.) alijibu kwa sauti nyembamba, "Shangazi! Kwa nini nisione uchungu nikiona watu wa karibu yangu na wapendwa wangu wamelala kwa kuuawa kishahidi?" Halafu Bibi Zainab alimliwaza Imam Sajjad (a.s.).[358]

## HADITHI ILIYOSIMULIWA NA UMMU AIMAN

Ummu Aiman alikuwa bibi mashuhuri. Kwa dhahiri huyu alikuwa kijakazi wa Bibi Khadija wakati alipokuwa msichana na baadaye aliachiwa huru. Baada ya kuachiwa huru, aliishi nyumbani kwa Mtume. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akimheshimu sana bibi huyu. Alitumia muda mrefu akiwa ndani ya nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Bibi huyu alimsimulia Bibi Zainab hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Baada ya kusikia hadithi hii, Bibi Zainab alikwenda kwa baba yake, Amirul-Mu'minin ili aithibitishe. Bibi Zainab alisema, "Ewe baba! Nimesikia hadithi hii kutoka kwa Umm Aiman." Halafu akarudia hadithi hiyo kwa baba yake. Baada ya kusikia hadithi, Amirul-Mu'minina alisema Ummu Aiman alisimulia kwa sahihi.[359]

Bibi Zainab alimliwaza Imam Sajjad (a.s.) na akamsimulia hadithi hii pale alipokuwa hawezi kujidhibiti baada ya kuona miili ya wale watu wa karibu yake na wapendwa wake waliouawa kishahidi. Kwenye hadithi hiyo imetamkwa kwamba tukio la Karbala lina umuhimu ambao unahusishwa nalo. Hivyo, baada ya kuona mazingira hayo, hawezi akadhani kwamba baba yake ameuawa na ndiyo mwisho wa kila kitu. "Hapana mpwa wangu, hapana. Ni hadithi ya babu yetu kwamba pale ambapo mwili wa Imam Husain (a.s.) umelala baada ya kuuawa kishahidi[360] panaweza kuwa kaburi la Husain kesho, ambalo litakuwa linatembelewa na wafuasi wetu."

Endapo falsafa ya Shahidi itaelezwa kaburi kubwa la Husain lingekuwa Qibla ya Waislamu.

---

[358] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 179; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 718

[359] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 183

[360] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 179; *Kamiluz Ziaraat*, uk. 259

## MSAFARA WA MATEKA NDANI YA KUFA

Kama vile ilivyo leo, ilikuwa tarehe 11 ya Muharram ndani ya Karbala. Ibn Saad alibakia Karbala kuona wapiganaji wake waliokufa vitani wanazikwa lakini miili ya Imam Husain (a.s.) na masahaba wake iliachwa bila kufunikwa. Watu wa familia ya Imam walikamatwa (yaani katika mkesha wa tarehe ya 12 ya Muharram) hapo Karbala na kupelekwa Kufa. Umbali wa kutoka Karbala kwenda Kufa ni farsakh kumi na mbili (takribani maili 36). Walikuwa wamepanga kwamba wafungwa waingie Kufa huku ngoma zikipigwa kuashiria ushindi wa Yazid kuonyesha nguvu zake. Kwa njia hii, akili zao duni zilipanga kutoa pigo la mwisho kwa Ahlul-Bayt wa Mtume (s.a.w.w.).

Walichukuliwa katika hali ambayo kwamba Bibi Zainab alikuwa hajalala tangu ule mkesha wa Ashura. Vile vichwa vitukufu vya mashahidi vilivyotundikwa kwenye ncha za mikuki vilitangulia kupelekwa Kufa.[361] Sijui ilikuwa wakati gani wa siku hiyo (kufuatana na hadithi moja, saa mbili au tatu zilikwishapita baada ya jua kuchomoza mnamo tarehe 12 ya Muharram). Mara tu baada ya wafungwa kuingia jijini, vile vichwa vya mashahidi vili          letwa mbele kuwalaki mateka hao.[362] Hali ya watu wa familia ya Imam (a.s.) kwa wakati huu haiwezi kuelezeka kwa maneno.

## HOTUBA YA BIBI ZAINAB ILIKUMBUSHA MOJA YA HOTUBA ZA ALI (A.S.)

Enyi waombolezaji!

Hebu fikiria! Mabinti wa Ali na Fatima wanaonekana kwenye milango ya Kufa. Watu wanatazama matukio hayo. Hii ni Kufa ile ile iliyotawaliwa na Imam Ali (a.s.). Binti yake Ali, Zainab alikuwa na ubainifu wa sifa na upekee wa nafsi (Zainab kwenye soko la Kufa?!) kama ilivyothibitishwa na hotuba yake yenye fasaha.

Inasimuliwa kwamba Bibi Zainab akiwa na uchungu aliteua muda muafaka wa kutoa hotuba yake na aliashiria. Imeandikwa kwamba hapakuwepo na kelele mahali pote ya kiasi kwamba mtu angeweza kusikia neno. Hata hivyo, mara tu baada ya kutoa ishara, pakawa kimya kizito kana kwamba

[361] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 718

[362] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 718

watu waliacha kupumua na kengele za saa ziliacha kutoa sauti.[363] Hata wapanda farasi nao walisimama (bila shaka, kama wapanda farasi wakisimama na vipando vinasimama vyenyewe).

## HESHIMA NA STAHA YA BIBI ZAINAB

Bibi Zainab alitoa hotuba ambayo kuhusu hiyo msimulizi anasema: "Wallahi, sijapata kuona mwanamke (*Khafra*) ambaye ana umashuhuri wa uanamama na heshima vinavyobubujika kutoka kwenye hotuba yake."[364]

Neno '*Khafra*' ni la muhimu sana katika maelezo haya ambalo maana yake ni mwanamke anayeheshimiwa. Kama vile ilivyosemwa kuhusu hotuba yake, maana yake ni, "Wallahi sijapata kuona mwanamke ambaye ana umashuhuri wa uanamama na heshima vinabubujika kutoka kwenye hotuba yake." Haitakuwa ni jambo la kutia chuku kusema kwamba Bibi Zainab alikuwa na mchanganyiko wa ujasiri wa Imam Ali (a.s.) na heshima ya uanamama kwenye hotuba yake.

Imam Ali aliitwa Amirul-Mu'minina miaka ishirini iliyopita kabla hapo Kufa na alitawala hapo kwa takribani miaka mitano. Imam Ali (a.s.) alikuwa ametoa hotuba nyingi kutoka kwenye mimbari ya Kufa. Watu walikuwa hawajasahau jinsi hotuba za Imam Ali (a.s.) zilivyokuwa kwa sababu hazikuwa na kufanana na hotuba ya mtu mwingine. Kwa hiyo, msimulizi anasema kwamba wakati Bibi Zainab alipotoa hotuba, ilikuwa kama vile Ali amekuwa na uhai kwa mara nyingine na nafsi ya Ali ilikuwa inazungumza kutoka kwenye mwili wa Zainab.

Msimulizi anasema kwamba wakati hotuba fupi ya[365] Bibi Zainab ilipokwisha, yeye aliona kwamba kila mtu alikuwa anauma kucha zake. Ilikuwa kama vile Bibi Zainab alikuwa ameonyesha tabia ya wanawake kama inavyotakiwa na Uislamu. Ni kwamba Uislamu unamtaka mwanamke kuwa shaksia iliyojaa heshima, uadilifu na utakatifu.

Katika msingi huu, wanawake pia wametimiza wajibu wao wa kubakia kwenye mipaka yao kwa kadiri ambavyo mchango wenye matokeo yaliyotarajiwa uliofanywa na wanamume katika kutengeneza historia ya Kar-

[363] *Amali*, Shaykh Mufid, uk. I98; Luhuuf, uk. 146; *Biharul Anwar,* Juz. 45, uk. 108-162

[364] *Amali*, Shaykh Mufid, uk. 198; Luhuuf, uk. 146; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 108-162

[365] Tafsiri ya hotuba hii yenye ufasaha ya Bibi Zainab ipo mahali pengine kwenye kitabu hiki.

bala. Kana kwamba historia ya Karbala, ambayo imepita kwenye hatua za ukamilifu wa binadamu imekuja kuwepo kupitia ushirikano wa wote, wanamume na wanawake.

Hakuna nguvu wala uwezo isipokuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Aliyeko Juu na Muweza wa Yote.

# MAJILISI 52

## BIBI ZAINAB KWENYE BARAZA LA IBN ZIYAD

Lazima utakuwa umesikia mara kadhaa kwamba shaksia tukufu za watu wa Imam Husain (a.s.), masahaba wake na wanafamilia wake zina sifa bainishi kwa sababu ya dhamira yao ya kukataa fedheha katika msiba wa Karbala. Waliweza kukamatwa mateka, walifungwa pingu za minyororo, walivishwa mikanda mizito ya chuma shingoni, walijeruhiwa, waliuliwa kishahidi lakini hawakuweza kuvumilia mzigo wa fedheha hata kama wanawake watakuwa mateka.

Inasimuliwa kwamba, wakati familia ya Imam walipofanywa mateka na kupelekwa kwenye baraza la Ibn Ziyad, wanawake, pamoja na wale wa kutoka familia ya Mtume (saww) ikiwa ni pamoja na wake na wajakazi wa masahaba wa Imam Husain (a.s.) walimzunguka Bibi Zainab na walimfunika asionekane. Bibi Zainab alikuwa mrefu; kwa hiyo, alionekana hata baada ya kuzungukwa na wanawake wengine. Yeye hakumsalimia mtawala baada ya kuingia kwenye baraza la Ibn Ziyad.

Ibn Ziyad alikuwa akifikiri kwamba alikwishachukua nguvu zote za Ahlul-Bayt baada ya msiba wa Karbala. Fikira zake duni zilikuwa kwamba amewafanya Ahlul-Bayt kuwa wanyonge na alikuwa anatarajia kwamba wangeanguka chini ya miguu yake na kuomba msamaha. Kwa hiyo, alikuwa ametarajia kwamba angalau Bibi Zainab angemsalimia hata kama kwenye msingi wa ridhaa ya Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, binti wa Ali alidhamiria kuyavunja kabisa matarajio ya Ibn Ziyad. Na Ibn Ziyad likasirishwa kwa kitendo hiki cha yeye kutoheshimiwa. Labda alikuwa hatambui kwamba roho za familia ya Mtume (s.a.w.w.) hazikuwa tayari kutishiwa. Bibi Zainab alipoketi chini,[366] yeye Ibn Ziyad aliuliza kwa kiburi. "Ni nani huyu mwanamke mwenye kujivuna?" Au aliuliza, "Kwa nini hakunisalimia?" au ali-

[366] Kwa kawaida, wafungwa wa kivita hawawezi kuketi bila ruhusa ya kamanda wa jeshi lenye ushindi, lakini Bibi Zainab aliketi kwenye kiti chake ndani ya baraza la Ibn Ziyad bila ya ruhusa yake na kuvunja kiburi chake. Bibi Zainab alihakikisha kwamba yeye ndiye aliyekuwa mshindi halisi na sio yeye Ibn Ziyad. (Rizwani)

uliza, "Ni nani mwanamke huyu asiyejali watu wengine?" (Maswali yote haya yanaonekana. Mojawapo lina neno '*Mutakabbir*' na lingine lina neno '*Munkir*'). Hakuna mtu aliyejibu swali la Ibn Ziyad. Alirudia swali lake kwa mara nyingine tena lakini hakupata jibu lolote. Aliporudia kwa mara ya tatu au ya nne, mwanamke mmoja akasema, "Huyu ni Zainab, binti yake Ali bin Abi Talib (a.s.)."

Ibn Ziyad alijaribu kuwadanganya watu. Akasema, "Sifa zote zimwendee Mwenyezi Mungu kwani amewafedhehesha nyinyi. Amewaua na kuweka hadharani uwongo wenu." Yule aliyelaaniwa aliendelea kumdhihaki Bibi Zainab kwa maneno yake.

Bibi Zainab alikuwa na wajibu mkubwa sana mabegani mwake wakati huu. Baada ya kusikia maneno yake, yule Bibi mwenye dhamira alisema kwa namna ya dharau, "Shukurani zote ni zake Mola ambaye alimpa utume Muhammad Mustafa na heshima kwetu na alitupatia muujiza wa kutotenda makosa sisi watu wa nyumba ya Mtume (s.a.w.w.). Unachokisema wewe sio sahihi." Halafu akaendelea kusema:

"Ewe Ibn Ziyad! Aliyefedheheshwa ni yule ambaye ni mtenda dhambi na muongo. Sisi hatuko hivyo! Sisi tuna heshima. Uwongo si desturi ya watu wa kweli. Uwongo upo mbali sana na sisi. Ewe mwana wa Marjana! Mwenyezi Mungu na akuangamize!"[367]

Macho ya Ibn Ziyad yaligeuka kuwa mekundu kwa hasira baada ya kusikia maneno hayo. Alitoa sauti kama nyoka wa jangwani na akasema, "Hivi bado umebakiwa na nguvu? Unazungumza kwa namna ile ile hata baada ya kuteseka sana? Hivi bado mmelengea juu ya dhamira yenu?"

Ingawaje "Mwana wa Marjana" ni maneno matatu, yanaelezea hadithi fulani, ambayo ilifichua tabia duni ya Ibn Ziyad. Mama yake Ibn Ziyad, Marjana alikuwa mwanamke mzinifu. Bibi Zainab alielekeza usikivu wa kila mtu aliyekuwepo kwenye baraza hilo kwenye ukweli huu kwa kumwita yeye "Mwana wa Marjana."

Ibn Ziyad alimuamuru mnyongaji wake "kumkata kichwa mwanamke huyo."(Bibi Zainab). Vivyo hivyo, alipomsemesha Imam Sajjad (a.s.), naye alijibu bila kusita. Hivyo, Ibn Ziyad alimuamuru mnyongaji wake kumkata

[367] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 243; Luhuuf, uk. 160; *Biharul Anwar,* Juz. 45, uk. 115-117; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 735; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 324.

kichwa kijana huyo pia. Aliposikia amri hii, Bibi Zainab alinyanyuka kutoka pale alipoketi, akamshika Imam Sajjad (a.s.) na kumweka karibu naye na akasema,

"Wallahi huwezi kumua huyu isipokuwa labda unikate kichwa mimi."[368]

Imeandikwa kwamba Ibn Ziyad aliwatazama kwa muda kidogo na halafu akasema, "Ni jinsi iliyoje uhusiano wa damu unashangaza!"

"Ninaona kwamba kama ninataka kumuua kijana huyu, itanibidi nimuue mwanamke huyu kwanza."[369]

Hapana nguvu na uwezo isipokuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Aliyeko Juu na Mwenye nguvu."

[368] *Irsahad*, Shaykh Mufid, uk. 244; *Biharul Anwar*, Juz, 45, uk. 117; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 325
[369] *Falsafa Akhlaq*, uk. 57-59

# MAJILISI 53

## WAUAJI WA IMAM HUSAIN (A.S.) WALIUPA UHALIFU WAO SURA YA KIDINI

Kila mfumo unahitaji kuungwa mkono kiitikadi na kidini ili uweze kunusurika. Kwa hiyo, kila mfumo hutaka msaada wake uwe katika msingi fulani wa falsafa au fikira, hata kama ni fikira ya kidini, iliyoganda kwenye nyoyo za watu, ili asitokee mtu wa kupinga mfumo huo. Utawala wa Yazid nao pia usingenusurika bila ya kuegemea kwenye aina fulani za itikadi.

Usije ukafikiri kwamba walikuwa wapumbavu sana na wakifikiri kwamba kila kitu kimemalizika baada ya vita vya Karbala na hapakuwa na haja ya kufanya lolote kuhusu jambo hilo. Haikuwa hivyo. Baada ya tukio hili la msiba, kila mara utawala ulikuwa unajishughulisha kupanga jinsi ya kuwafanya watu wawe wanajishughulisha kwa hili na lile ili walazimike kufikiri kwamba kila chochote kilichokuwa kinatokea kilikuwa ni kwa upendeleo wa utawala huo. Ili kuweza kupata radhi ya tabaka la kidini, ni lazima kwa utawala kupatia harakati zake muonekano wa kidini. Kwa hiyo, msaada wa Kadhi Shuraih uliihitajika ili kwamba watu waweze kutosheka kisomi na namna yao ya kufikiri iweze kubadilika. Fikira hii ilifuzu hadi mnamo Alasiri ya siku ya Ashura huko Karbala.

Imam Baqir (a.s.) anasema kwamba watu elfu thelathini walikuwa wamekusanyika hapo Karbala kumuua mjukuu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kwa nini? Walitaka kupata ukaribu kwa Mwenyezi Mungu baada ya kumwaga damu ya mtoto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).[370] Walikuwa wakimshambulia Imam Husain (a.s.) kwa mapanga ili wapate Pepo. Viongozi wa watu hao walihongwa mifuko ya dhahabu kwa ajili ya kutekeleza jambo hili, kama ambavyo Farazdaq amesema; wakati watu walikuwa hawajui kabisa kuhusu ukweli huu. Viongozi waliowapotosha watu kwenye njia zao ni wale ambao walijaza mifuko yao kwa hongo. Upekee wa utawala wa Ibn Ziyad ulikuwa kwamba aliupatia uhalifu wake muonekano wa kidini ili awadanganye watu.

[370] *Biharul Anwar*, Juz. 44, uk. 298

Kwa upande mwingine Yazid alikuwa na doa kwa sababu ya tabia yake ya ulevi. Ilipotokea akasisimka baada ya kulewa sana alikuwa anasema undani wake. Halafu alikuwa hawezi kujidhibiti na alikuwa akisema ukweli. Aliwahi kusema kwamba asingekubali chochote. Tabia hii ilimuumbua. Vinginevyo, Yazid pia angewapotosha watu kupitia mashambulizi kama hayo ya kisomi.

Baada ya mauaji hayo makubwa ya kishahidi, Ibn Ziyad aliwakusanya watu kwenye msikiti mkuu wa Kufa kuwajulisha kuhusu jambao hili. Alijaribu pia kukipatia kifo cha kishahidi cha Imam Husain (a.s.) muonekano wa kidini kwa wakati huo. Alivaa barakoa la utakatifu na akasema, "Ninamshukuru Allah ambaye ametoa ushindi kwa ukweli na watu wakweli akamuua muongo, mtoto wa muongo ambaye alikuwa na tabia ya kudanganya watu."[371] Ibn Ziyad alitaka watu wamshukuru Mwenyezi Mungu na mamia ya watu walifanya hivyo. Hata hivyo, palikuwepo na mtu mmoja kipofu kwenye mkusanyiko ambaye pamoja na kwamba alikuwa haoni kwa macho yake ya kimaumbile lakini aliweza kuzingatia ya mbele. Aliuzuia mpango huo wa Ibn Ziyad.

## KIPOFU HAKURUHUSU HILA YA IBN ZIYAD KUFAULU

Alikuwepo muungwana mmoja aliyeitwa Abdullah Ibn Afif.[372] Mwenyezi Mungu amrehemu. Wakati mwingine hutokea watu wakathubutu kuyaweka maisha yao rehani na kuokoa dunia yote kwa kujitoa mhanga. Suala la Abdullah bin Afif linafanana na mfano huo hapo juu. Hakuweza kuona kwa macho yake. Alipoteza jicho lake moja kwenye vita vya Jamal na akapoteza jicho lingine kwenye vita vya Siffiin akiwa mpiganaji wa jeshi la Imam Ali (a.s.). Alikuwa hafanyi kazi kwa sababu ya upofu wake na hakuweza kushiriki hata kwenye Jihad kwa sababu ya ulemavu wake. Kwa hiyo alikuwa na kawaida ya kutumia muda wake mwingi kwenye ibada. Siku hiyo, alikuwa anaswali ndani ya msikiti wa Kufa. Mara baada ya kusikia maneno ya Ibn Ziyad, alisimama na akasema, "Ewe Ibn Ziyad! Wewe ni muongo na baba yako

[371] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 244; *Luhuuf*, uk. 163; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 119. Maneno ya Ibn Ziyad ndani ya Masjid Kufa yameandikwa kama ifuatavyo kwenye Maalimul Madarasatain, Juz. 3, uk.186: "Sifa zote ni stahiki Yake Allah kwani aliifanya kweli na watu wa ukweli washinde na alimsaidia bwana wa waumini, Yazid bin Muawiyah na kundi lake na kumuua muongo Husain bin Ali na wafuasi wake." (Rizwani)

[372] Abdullah bin Afif Azudi

alikuwa muongo pia,"[373] Baada ya hapo, Abdullah bin Afif aliendelea kuongea hadi watu wakamsukuma na akaanguka chini. Akakamatwa na akauawa Shahidi lakini tayari barakoa la Ibn Ziyad lilikuwa limepasuliwa.[374]

## MANTIKI YA IBN ZIYAD ILIEGEMEZWA KWENYE MABAVU

Ibn Zyad aliye haramu katika maana zote mbili yaani alikuwa haramu kwa kuzaliwa na alikuwa na kitabia ya kishetani pia. Kwa kawaida, kwenye jamii ambazo watu wake wameelekea kwenye dini, watawala madhalimu hutumia mantiki ambayo imeegemezwa kwenye mabavu ili kuweza kuhalalisha ukandamizaji wao. Wanahusisha kila kitendo chao na Mwenyezi Mungu. Wanasema kwamba kila kitu kilikuwa hivyo kwa sababu ya Utashi wa Mwenyezi Mungu. Kama isingekuwa hivyo, tukio hilo lisingetokea. Lolote linalotokea ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Ameridhia. Mantiki hii ya udhalimu ni mantiki ya Ibn Ziyad. Alipokabiliana na Bibi Zainab, alihusisha mlolongo wa matukio kwa Mwenyezi Mungu na akasema, "Sifa zote ni stahiki yake Allah ..."

Maelezo haya yana maana nyingi sana iliyofichwa ndani humo.

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwani amewafedhehesheni nyinyi. Amewaua na kufichua uongo wenu. Yaani mlieneza fitina ya kushangaza miongoni mwa Waislamu."[375]

---

[373] "Ewe adui wa Mwenyezi Mungu! Kwa hakika wewe ni muongo na baba yako alikuwa muongo na mtu aliyekufanya gavana pia ni muongo na baba yake pia alikuwa muongo. Ewe mtoto wa Marjana!"

[374] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 244; *Luhuuf*, uk. 164; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 119

[375] Baada ya uchunguzi wa kina kuhusu jambo hili, mtu anahitimisha kwamba watawala hawa wa kidikteta walieneza dini kwa kulazimisha kwa sababu kupitia humo waliweza kuonekana hawana hatia katika makosa yote. Watu huchukulia uhalifu wao kuwa ndiyo hatima ya mtu na hunyamaza na kufikiri kwamba hiyo ni sehemu ya dini yao. Watawala dhalimu wa Bani Umayyah walitoa mchango muhimu katika kueneza imani ya majaaliwa.

Watu wa familia ya Imam walipochukuliwa mateka hadi Kufa kwenye baraza la Ibn Ziyad baada ya tukio la Karbala, alimwambia Bibi Zainab: "Sifa zote ni stahiki yake Mwenyezi Mungu ambaye amewafedhehesha nyinyi, amewaua na kufichua uongo wa madai yenu." Bibi Zainab alimpinga kwa kusema: "Sifa zote ni stahiki yake Mwenyezi Mungu ambaye ametupendelea sisi na Mtume Wake, Muhammad (s.a.w.w.), na familia yake. Na ametutakasa sisi kabisa tusije kutenda dhambi. Humfedhehesha muovu mkuu tu na hufichua sura ya fisadi muongo. Wanamume kama hao hawapo miongoni mwetu, shukurani zote ni stahiki yake Mwenyezi Mungu." Ibn Ziyad akasema, "Unafikiria ni vipi Mwenyezi Mungu ameitendea Nyumba yenu?"

Zainab akajibu "Mwenyezi Mungu amewaamulia wao kifo na walisonga mbele (kwa ujasiri) kwenye mapumziko yao." Akaendelea: "Mwenyezi Mungu atatukusanya nyinyi na sisi pamoja. Mtatetea udhuru wenu Kwake na sisi tutakuwa wapinzani wenu mbele Yake."

Halafu Ibn Ziyad alimuuliza Imam Sajjad (a.s.): “Jina lako nani?” akajibu, “Ali bin Husain.” Ibn Ziyad akasema, “Hivi Mwenyezi Mungu hakumuua Ali bin Husain kule Karbala?” Imam Sajjad (a.s.) akasema, “Kaka yangu, Ali, aliuawa kishahidi na watu.” Ibn Ziyad akasema, “Kwa kweli Allah Mwenyezi alimuua huyo.” Imam Sajjad (a.s.) akasema:

اللَّهُ يَتَوَفَّى الْأَنْفُسَ حِينَ مَوْتِهَا وَالَّتِي لَمْ تَمُتْ فِي مَنَامِهَا

**“Mwenyezi Mungu huzipokea roho zinapokufa. Na zile zisizokufa wakati wa kulala kwake.” Qur`ani Tukufu Sura Az-Zumar 39:42** Na:

وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ أَنْ تَمُوتَ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ كِتَابًا مُؤَجَّلًا

**“Na nafsi haiwezi kufa ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kama ilivyoandikwa ajali yake” Qur`ani Tukufu Sura Aal-Imran 3:145.**

Yazid alimwambia Imam Sajjad (a.s.) kuhusu ukandamizaji kule Karbala. “Baba yako alivunja uhusiano na mimi na aliikana haki yangu na akapigana na mimi ndani ya utawala wangu. Vyovyote vile Mwenyezi Mungu alivyomfanyia kama malipo unaona mbele ya macho yako.” Imam Sajjad (a.s.) akasema:

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِنْ قَبْلِ أَنْ نَبْرَأَهَا

**“Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujaziumba....”** Qur`ani Tukufu Sura Al-Hadid 57:22.

Yazid alimwambia mwanae, Khalid ajibu lakini hakujibu. Yazid akasema: “Mwambie:

وَمَا أَصَابَكُمْ مِنْ مُصِيبَةٍ فَبِمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ

**“Na misiba inayowasibu ni kwa sababu ya yaliyotendwa na mikono yenu.”** Qur`ani Tukufu Sura Ash-Shura 42:30.

Ibn Ziyad na Yazid walilihusisha tukio la Karbala na Mwenyezi Mungu na wakasema kwamba udhalimu wote uliotokea Karbala ulifanywa na Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, Imam Sajjad (a.s.) na Bibi Zainab waliikataa mantiki yao na wakasema, “Mwenyezi Mungu hakutufanyia udhalimu sisi. Wewe na wafuasi wako ndiyo mliofanya udhalimu huo.”

Wasimulizi waliowaunga mkono makhalifa watatu wamesimulia hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa lengo la kuthibitisha uhalali wa imani ya majaaliwa. Imesimuliwa kutoka kwa Abu Huraira kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema “Niulizeni mimi.” Hata hivyo, kila mmoja alinyamaza kimya kwa sababu ya heshima yake. Halafu mtu alikwenda akaketi karibu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Akauliza, “ Ewe Mjumbe wa Allah Mwenyezi! Nini maana ya Uislamu?” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema, “Ni kutokumshirikisha yeyote na Mwenyezi Mungu, kusimamisha swala, kulipa Zakat, na kufunga saumu mnamo mwezi wa Ramadhani.” Muulizaji akasema, “Hayo ni sahihi.” Halafu akauliza tena, “Imani ni nini?” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema, “Kumuamini Mwenyezi Mungu, malaika Wake, vitabu Vyake, kukusanyika mbele Yake, Mitume Wake, na majaaliwa kamili ni imani.” Muulizaji akasema, “Hayo ni sahihi.”

Hitimisho la hadithi tisa za kwanza za *Sahih Muslim,* kwenye “Kitab al-Qadr” ni kwamba mara tu baada ya kijusi kuumbwa ndani ya tumbo la uzazi, Mwenyezi Mungu huamuru malaika Wake kukadiria kipato, tabia na mwenendo. Pia huamuru kuandika kama mtoto huyo atakuwa na bahati au hapana. Wakati wowote mtu anapokuwa bado yupo tumboni, inaamuliwa kwamba ataingia Peponi au Jahannam na uamuzi huu haubadiliki kamwe. Kwa hiyo mwanadamu analazimishwa katika vitendo vyake. (Allamah Sayyid Murtadha Askari, *'Ahya-e-din mein Ahlul-Bayt ka kirdar*, Juz. 2, uk.387) - Rizwani.

Hebu fikiria juu ya hilo! Mtu ambaye ameshindwa vita kwa dhahiri amefedheheshwa kwa mantiki ya Ibn Ziyad. Ina maana kwamba mtu ambaye ameuawa vitani ni kama aliyeshindwa. Ushindi humfedhehesha na kummaliza yeye. Kwa maneno mengine, hawezi kusemekana kuwa anafuata njia iliyonyooka. Kama angekuwa kwenye njia iliyonyooka basi angeshinda. Alimaanisha kusema kwamba kwa kuwa aliweza kuwashinda Ahlul-Bayt, huo ulikuwa ni uthibitisho kwamba wao walikuwa wanafuata njia isiyo sahihi.

## KIWANGO CHA FEDHEHA KULINGANA NA MANENO YA BIBI ZAINAB

Bibi Zainab (s.a.) alimjibu Ibn Ziyad akasema, "Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia utume na kwa sababu sisi tunatoka katika familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)."[376]

"Sio kila yeyote anayekufa akiwa kwenye uwanja wa vita hafedheheshwi kwa sababu kiwango cha fedheha ni kitu kingine kabisa."[377]

Kiwango cha kutoheshimika hutegemea na kutafuta haki na ukweli. Yeyote anayejitoa mhanga katika njia ya Allah Mwenyezi hawezi kufedheheka. Anayeaibishwa ni yule anayedhulumu, na yule anayekataa haki. Kiwango cha kuaibishwa au kutofedheheshwa ni ama kwa kuwa katika njia iliyonyooka au njia ya upotofu. Katika msingi wa fedheha, yeyote anayeuliwa si lazima awe muongo. Bendera ya ukweli au uongo ni mtu mwenyewe, malengo yake, maneno yake na matendo yake. Ingawaje kaka yangu, Husain (a.s.) ameuawa Shahidi, ataitwa mkweli. Kama angekuwa bado hai basi pia angeitwa mkweli. Hata hivyo, hata kama wewe utauawa, utabakia kuwa ni muongo bado. Kama ukiwa hai basi pia utaitwa muongo." Baada ya majibu haya yenye kuponda, Bibi Zainab akamshambulia Ibn Ziyad kwa ukali kabisa kwa maneno yake na akashikwa na butwaa. Bibi Zainab akasema, "Ewe mwana wa Marjana!" Marjana alikuwa mama yake Ibn Ziyad na alikuwa hapendi mtu yeyote amuite kwa jina hilo la mama yake kwa sababu mama huyo alikuwa anajulikana sana kwa tabia yake ya uasherati na ukahaba."[378]

---

376 Imeandikwa ifuatavyo kwenye *Irshad*, Shaykh Mufid na *Biharul Anwar*; Sifa zote anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye alitupa heshima sisi kupitia kwa Mtume Wake."

377 *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 244; *Luhuuf*, uk. 160; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 117.

378 Luhuuf, uk. 160; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 116

## IBN ZIYAD AAMURU BIBI ZAINAB AUAWE

Ibn Ziyad hakuwa na majibu kwa kauli na maneno kama: “”Ewe mtoto wa Marjana! Ewe mtoto wa mwanamke mzinifu! Fedheha ni kwa ajili ya mtoto wa Marjana kwa sababu ipo katika majaaliwa yake.”

Kwa hiyo, Ibn Ziyad alikasirika sana na akamuamuru muuaji wake amkate kichwa mwanamke huyo. Khawarij mmoja (Adui wa Ali) alikuwepo kwenye baraza ya Ziyad wakati huo. Mtu huyu aliposikia amri ya Ibn Ziyad, busara yake ya heshima ya Uarabu ilifura na akamwambia Ibn Ziyad,[379] “Ewe Amiri! Uko timamu na akili zako sawa sawa? Unazungumza na mwanamke na kwamba pia, ni ambaye amevumilia masimanzi mengi yasiyo na ukomo. Kaka zake wameuawa na amepoteza watu wa karibu yake na wapendwa wake.”

## JINA LA ALI LAWACHUKIZA MAADUI

Imam Sajjad (a.s.) alipelekwa mbele ya Ibn Ziyad. Ibn Ziyad alimuita Imam Sajjad (a.s.) kwa sauti ya kupaza kama Firaun. “Wewe ni nani?” Imam akasema, “Mimi ni Ali mtoto wa Husain.”

Ibn Ziyad akauliza, “Hivi Mwenyezi Mungu hakumuua Ali bin Husain kule Karbala?” (Kwa mara nyingine kitendo hicho kilihusishwa na Mwenyezi Mungu) ili kwamba watu waweze kuhakikishiwa kwamba Yazid alikuwa sahihi. Imam Sajjad (a.s.) akajibu, “Kwa hakika, kazi ya kuchukua roho za kila mtu ni jukumu la Mwenyezi Mungu lakini kaka yangu aliuliwa Shahidi na watu (na wala sio Allah).”

Ibn Ziyad akasema, “Ali mmoja na Ali mwingine?[380] Ni nini yote hii? Baba yako aliwaita watoto wake wote Ali? Jina lako wewe ni Ali na ndugu yako naye ni Ali? Hapakuwepo na jina lingine lolote?” Imam Sajjad (a.s.) akajibu. “Baba yangu alikuwa anampenda baba yake sana. Alipenda kuwapa watoto wake jina la baba yake ambapo wewe unamfikiria baba yako kuwa fedheha kwako.”

---

[379] Jina la mtu huyu linatajwa kama Amr bin Harith katika *Irshad* ya Shaykh Mufid, uk. 244; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 116.

[380] Imeandikwa katika *Damaus Sujum*, Uk. 251 kwamba imepokewa kutoka kwa Yahya bin Hasan katika *Manaqib* kwamba Yazid alimwambia Imam Sajjad (a.s.), “Ni ajabu iliyoje kwamba baba yako amewaita watoto wake wawili jina la Ali!” Imam Sajjad akajibu, “Baba yangu alimpenda baba yake na alitaka kuwaita watoto wake wote wanamume kwa jina la Ali.”

## NGAO YA IMAM SAJJAD (A.S.)

Ibn Ziyad hakutarajia kuwa Imam Sajjad (a.s.) angezungumza neno lolote mbele yake kwa sababu kwa maoni yake yeye hakuna mfungwa ambaye angethubutu kuzungumza. Yeye alidhani Imam Sajjad (a.s.) angekubaliana naye aliposema kwamba hiyo ilikuwa kazi ya Allah na wakubali jaala yao. Hata hivyo, alipoona kwamba Imam Sajjad (a.s.) alithubutu kusema kwa uhuru pamoja na kwamba yeye ni mateka, akasema "Unathubutuje kunijibu mimi kama hivyo?"[381] Alikasirika na kutoa mlio kama wa nyoka wa jangwani na akamuamuru muuaji wake, "Nenda ukamkate kichwa kijana huyu."

Inasimuliwa kwamba Ibn Ziyad aliwatazama kwa sekunde chache halafu akasema, "Ninaona kwamba kama nikitaka kumuua kijana huyu, ni budi nimuue mwanamke huyu kwanza."[382] Kwa hiyo, aliacha kumuua Imam Sajjad (a.s.).

Ndiyo, hii ni tabia muhimu ya Ahlul-Bayt kwamba walipigana dhidi ya imani ya majaaliwa, jambo ambalo hadi leo bado linaendelea kuaminiwa na linatafsiriwa kama ni haki. Kwa maneno mengine, Ahlul-Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walithibitisha kwamba maneno kama "mwanadamu hawajibiki kwa lolote" au "si kazi ya mwanadamu kujaribu kuleta mabadiliko katika jamii" au "lolote linalotokea lilipangwa kutokea" yaani "hakuna mchango unaotakiwa kufanywa na mwanadamu katika jamii hii" yalikuwa ya uongo kabisa na waliyapiga vita.

[381] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 244; *Luhuuf,* uk. 162; *Biharul Anwar,* Juz. 45, uk. 117

[382] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 244; Luhuuf, uk. 162; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 117.

# MAJILISI 54

## ROHO ZETU HAZIWEZI KUFUNGWA NYORORO

Inasimuliwa kwamba wakati watu wa familia ya Imam walipofikishwa kwenye baraza la Ibn Ziyad, wanawake wa familia ya Imam na vijakazi walimzunguka Bibi Zainab ambaye alikuwa mrefu kwa kimo na kwa hiyo alionekana katikati kama johari iliyozungukwa na walinzi wake.

Ibn Ziyad alimfahamu Bibi Zainab kama alivyowajua watendaji wa baraza lake. Alitarajia kwamba Bibi Zainab angemsalimia baada ya kuingia kwenye ukumbi (kama ilivyo desturi). Hata hivyo, binti yake Ali hakumsalimia.

Bibi Zainab alitaka kuthibitisha na kweli alithibitisha kama iliyotarajiwa kwamba Ibn Ziyad asingeweza kuzikamata nyoyo zao kama alivyoifunga nyororo miili yao na kuwaweka kizuizini. Hapana kabisa! Alithibitisha hilo kwamba nyoyo zao zilikuwa ni nyoyo za binadamu zilizokamilishwa, si nyoyo zilizojitengeneza zenyewe bali hizi zilikuwa nyoyo takatifu. Kwa hiyo, nyoyo zao wala zisingeweza kudhibitiwa au kuuawa. Kwa hiyo, Bibi Zainab hakumsalimia.

Tukio hili lilimkasirisha Ibn Ziyad na akasema, "Ni nani mwanamke huyu mwenye majivuno?" Hakuna mtu aliyejibu. Alirudia swali lake mara mbili au mara tatu na hatimaye akapata jibu, "Huyu ni Zainab, binti yake Ali bin Abi Talib (a.s.)"[383] Halafu Bibi Zainab alimshutumu sana Ibn Ziyad hivyo kwamba hakuweza kusema neno. Ibn Ziyad alilazimika kumuamuru muuaji wake 'kumkata kichwa mwanamke huyo.'

### BIBI ZAINAB KWENYE BARAZA LA YAZID

Bibi Zainab alipopelekwa ndani ya baraza la Yazid (*Green Palace*),hapo pia alionyesha ufahari ule ule. Hata baada ya kupitia kifungoni na hatua arobaini

[383] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 243; *Luhuuf*, uk. 160; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 115-117; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 735; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 324

za safari, dhamira yake haikuathirika. Moyo wake ulikuwa haujavunjika na dhamira na subira yake vilionekana zaidi ndani ya baraza la Yazid.

Hotuba ya Bibi Zainab ndani ya baraza la Yazid haina kifani hapa duniani. Hapa ningependa kusimulia kauli moja tu iliyopo ndani ya hotuba hiyo. Bibi Zainab alisema, "Ewe mtoto wa Muawiyah! Unaweza kujaribu kutumia kila njia ya kushambulia lakini kumbuka kwamba hutaweza kuzima hii "nuru ya wahyi" ambayo imeteremka ndani ya nyumba yetu. Wewe na falme yako mtaangamizwa hapa duniani. Jina lako litakuwa neno la kutusi lakini jina na ujumbe wa kaka yangu vitakuwepo daima milele.[384] Shamba alilopanda kaka yangu litakuwa la kijani daima milele. Kaka yangu, Husain ni chanzo cha mzinduko kwa wacha-Mungu. Dunia yote itakuwa mpenzi wa kaka yangu."

Kwa nini Bibi Zainab alikuwa anaamini kwamba jina la Yazid lingedhalilishwa na ujumbe wa Husain ungeenea kila mahali? Ilikuwa hivyo kwa sababu alikuwa ana imani kuhusu maumbile ya binadamu. Mwenyezi Mungu amemuumba mwanadamu pamoja na "kupenda haki." Kama asemavyo mshairi maarufu, Iqbal:

**Musa Firaun na Shabbir na Yazid**

**Nguvu hizi mbili pinzani zilikuwepo**
**tangu mwanzo wa uumbwaji.**
**Uhuishaji wa haki unatoka kwenye nguvu za Shabbir.**
**Na hatimaye batili huishia katika kukata tamaa na kifo.**
**Wakati uhusiano wa Ukhalifa ulipokatwa kutoka Qur`ani.**
**Sumu iliyeyushwa ndani ya mdomo wa uhuru.**
**Wakati kiongozi wa Umma bora sana alipotaka**
**Kueneza kijani kama wingu linyeshavyo mvua.**
**Haya yalinyesha juu ya ardhi ya Karbala na kupita**
**Yakiacha nyuma shamba la maua mekundu yakaenda zao.**
**Hivyo kwamba udhalimu unaangamizwa daima**
**Mawimbi ya damu yaliasisi bustani.**

[384] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 135

## "MTUME ALIKUWA AKIIBUSU MIDOMO HIYO.

Pamoja na kwamba Yazid alikuwa anachukuliwa kuwa miongoni mwa washairi fasaha wa Arabuni, alibaki hana la kusema mbele ya mantiki ya Bibi Zainab. Wawakilishi wa nchi zisizo za Kislamu na maofisa wa ngazi za juu wa kijeshi walikuwepo kwenye baraza hilo. Kwa hiyo, alikuwa akabiliwe na fedheha kubwa.[385] Yazid alijaribu sana kumnyamazisha Bibi Zainab lakini hakufaulu na halafu akafanya kosa kubwa ili aweze kumnyamazisha Bibi Zainab. Alijiambia mwenyewe kwamba ilikuwa lazima amdhibiti mwanamke huyu kwa namna ambayo watu wengine hawatajua kama amenyamazishwa. Kwa kweli, maneno ya Bibi Zainab yalibadilisha hali yake (Yazid). Kwa hiyo, alifanya kosa, ambalo siwezi kulieleza kwa urefu. Nitasema tu kwamba kitendo hiki cha Yazid hakikupendwa na mmojawapo wa watendaji wa baraza.[386] Alipiga kelele:

"Ewe Yazid! Simamisha kichapo cha hanzerani yako. Wallahi mimi nimewahi kuona kwa macho yangu kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akibusu midomo hiyo."[387]

[385] *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 355

[386] Abu Barza Salami

[387] *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk.354; *Falsafa Akhlaq*, uk. 220-221

# MAJILISI 55

## ZAINAB - MRITHI WA UMASHUHURI WA ALI NA FATIMA

Umashuhuri wa Bibi Zainab ni jambo la kweli. Kwamba aliupata kupitia malezi ya kwenye mapaja ya Bibi Zahra na Imam Ali (a.s.) pia ni jambo ambalo halina mjadala. Hata hivyo, baada ya msiba wa Karbala, Bibi Zainab alibadilika sana; yaani kwamba umashuhuri alioupata baada ya Karbala ulikuwa mkubwa zaidi.

Tumeona kwamba Bibi Zainab hakuweza kujidhibiti mara mbili au mara tatu katika mkesha ule wa Ashura. Alilia sana wakati mmoja hata akapoteza fahamu na kuanguka kwenye mapaja ya Imam Husain (a.s.) ambaye baadaye alimliwaza kwa maneno yake. Imam Husain (a.s.) alisema, "Ninahofia Shetani anaweza akakushinda na kukupora subira yako."[388]

Wakati Imam Husain (a.s.) alipomuuliza Bibi Zainab, "Kwa nini unafanya mambo namna hii? Wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuweza kuishi milele, nani ambaye angeweza? Hukumuona babu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akifariki dunia? Babu yangu alikuwa bora kuliko mimi, baba yangu pia alikuwa bora kuliko mimi na kaka yangu Hasan na mama Fatimah pia walikuwa bora kuliko mimi." Bibi Zainab akajibu, "Ewe kaka yangu! Walipokufa wote wewe ulikuwa kimbilio langu la mwisho lakini baada ya wewe kuondoka hakutakuwa na kimbilio tena."

Hata hivyo, mara tu baada ya jua kuchomoza mnamo siku ya Ashura na Bibi Zainab akamuona Imam Husain (a.s.) anaelekea kwenye lengo lake akiwa na dhamira nzito; mabadiliko ya namna fulani yalitokea kwenye shaksia yake hivyo kwamba hata chembe ndogo tu ya utu haikubakia kwa yeyote ambaye alimpinga yeye. Imam Sajjad (a.s.) anasema, "Tulikuwa watu kumi na mbili kwa jumla, na wote tulifungwa kwa kamba moja. Ncha moja ya kamba hiyo ilifungwa kwenye mkono wangu na nyingine kwenye mkono wa shangazi yangu Zainab."[389]

[388] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 232; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 2

[389] Luhuuf, uk. 178; *Damaus Sujum*, uk. 247-248; *Muntahaiul Amaal,* Juz. 1, uk. 764

## WAFUNGWA NDANI YA KASRI YA YAZID

Inasimuliwa kwamba mateka, wakiwa wamefungwa kwenye kamba walifika Damascus mnamo tarehe 2 mwezi wa Safar.[390] Kwa hiyo, Bibi Zainab alibakia mateka kwa siku ishirini na mbili. Alikuwa anateseka mfululizo kwa kubughudhiwa na matatizo kwa siku ishirini na mbili. Wafungwa walipelekwa kwenye baraza la Yazid wakiwa katika hali mbaya sana. Kasiri ya Yazid iliitwa jina la '*Qasr-e-Khazra*' (Kasri ya Kijani), na ilijengwa na baba yake, Muawiyah. Umaridadi wa kasri hiyo ulishangaza macho ya watazamaji.

Baadhi ya waandishi wa historia wamesema kwamba watu walipita katikati ya mabaraza makubwa saba kuweza kufika kwenye baraza la mwisho ambako ndiko Yazid aliketi kwenye kiti cha enzi kilichotapakaa vito vya thamani. Mbali na wawakilishi matajiri wa nchi zingine walikuwa na kawaida ya kuketi kwenye viti vilivyotengenezwa kwa dhahabu au fedha.[391] Hali ilikuwa ni hiyo siku wafungwa walipofikishwa kweye ikulu yake.

Wakati Zainab mwenye huzuni alipofika kwenye kasri hii ya kifahari, mlipuko wa hisia uliibuka nafsini mwake na matokeo yake ni kwamba alitoa hotuba ambayo ilisababisha ghasia kubwa sana kiasi kwamba Yazid alipigwa butwaa na hakuweza kusema neno pamoja na yeye kuwa mashuhuri kwa ufasaha wake.

## HOTUBA YA BIBI ZAINAB NDANI YA BARAZA LA YAZID

Yazid alipokosa majibu kwa Bibi Zainab, alianza kuimba beti za Abdullah bin Zibari Sahmi hali amefunga mdomo,[392] ambazo zilijaa imani ya kishirikina na alitunga beti hizo alipokuwa mshirikiana. Alikuwa anajivunia ushindi wake wa dhahiri. Ghafla, Bibi Zainab alinyanyua sauti yake akisema:

"Ewe Yazid! Hivi unadhani kwamba umefunga njia zetu zote hapa duniani na mbinguni kwa kutufanya sisi tuzurure hapa na pale kama wafungwa wa kawaida? Hivi unadhani kwamba heshima yako itaongezeka na hadhi yetu itapungua kwa sababu ya hali hii?"[393]

---

[390] Imeandikwa ifuatavyo kwenye *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 248; 'Waliingia Damascus mnamo tarehe 1 mwezi wa Safar na walisimamishwa hapo Baabus Saat.'

[391] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk.759

[392] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 766

[393] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 133

"Ewe Yazid! Umejaza hewa nyingine zaidi kwenye ubongo wako.[394] Unafikiri kwamba umefunga njia zetu zote kwa kutufunga na tupo chini ya ulinzi wa watumishi wako. Wallahi, kwa wakati huu wewe ni mtu mmoja muovu sana na duni mno kwa maoni yangu. Wala sikufikirii wewe kuwa ni mtu unayefaa kuongea na mimi."

## BIBI ZAINAB ALETA MAPINDUZI NDANI YA SYRIA

Tazama, watu hawa wametoa muhanga kila kitu katika njia ya Mwenyezi Mungu isipokuwa imani yao na utu wao wa kiroho. Hata baada ya kujua haya, huwezi kuamini kwamba shaksia ya mfano bora kama hii inaweza kuibua hamasa ndani ya watu hivyo kwamba inaweza kuleta mapinduzi, kama alivyoleta mapinduzi ndani ya Syria? Hotuba ya Bibi Zainab (s.a.) iliwatetemesha watu sana hivyo kwamba Yazid alihofia mjibizo wa umma na akalazimika kubadili njia zake na akawapeleka wafungwa Madina kwa heshima kubwa. Halafu akajaribu kukwepa kutokuhusika na uhalifu huu mbaya sana kwa kusema, "Mwenyezi Mungu amlaani Ibn Marjana. Yote haya yametokea kwa sababu yake. Sikumuamuru afanye hivi." Ni kazi ya mikono ya nani? Nani aliyemlazimisha Yazid kusema hivi? Ilikuwa ni mafanikio ya binti yake Ali.

Bibi Zainab alisema mwishoni mwa hotuba yake: "Ewe Yazid! Kwa hiyo panga vyovyote utakavyotaka kupanga, na utekeleze njama zako, na zidisha juhudi zako, kwani Wallahi, kamwe hutaweza kufuta utajo wetu, wala hata hutaweza kuua wahyi (ulioteremshwa kwetu)."[395] Bibi Zainab alithubutu kuongea mbele ya mtawala huyo dhalimu ambaye watu walimuogopa kwa sababu elfu moja na walimuita "Amiri wa Waumini."

"Ewe Yazid! Tumia udanganyifu wako wote ulionao hadi moyo wako utosheke. Jaribu njia zote. Ongeza kasi ya juhudi zako na utimize matakwa yako. Hata hivyo, kumbuka kwamba pamoja na yote haya, wala hutaweza kuharibu jina letu katika dunia hii au kuweza kupunguza heshima yetu au kusitisha kuenea kwa maoni yetu. Ni wewe ndiye utakayeangamizwa."

---

[394] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 133; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 358

[395] *Luhuuf*, uk. 185; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 135

Kama mshairi Iqbal asemavyo:

Hadithi ya mapenzi ina sura mbili: Karbala na Damascus

Moja iliandikwa na Husain na nyingine na Zainab.

Bibi Zainab alitoa hotuba kama hiyo kwenye baraza ambamo Yazid alikuwa amechanganyikiwa na ile hali ya majivuno iliyojaa ndani ya kichwa chake iliondolewa. Akawa amekasirika sana. Alifanya kitendo cha woga ukosa haya ili amnyamazishe Bibi Zainab; alinyanyua henzirani yake na akaanza kukosa adabu kwa kuanza kuchezea midomo mitukufu na meno ya Imam Husain (a.s.).[396]

**Kwa jina la Allah na kwa Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Mwenyezi (s.a.w.w.)**

[396] *Matqal-e-Husain*, Muqarram, uk. 354

# MAJILISI 56

## FAMILIA YA IMAM NDANI YA JELA LA SYRIA

Enyi waombolezaji!

Kwa kuwa hizi ni siku za maombolezo, ningependa kusema machache kuhusu mateso ya familia ya Imam Husain (a.s.). Hizi ni siku ambapo familia ya Imam ilipelekwa Syria, ingawaje haiwezekani kusema kwa uhakika siku ngapi zilipita tangu walipopelekwa Syria, lakini kufuatana na riwaya ya kuaminika, waliwasili Damascus tarehe 2 mwezi wa Safar.[397] Pia kufuatana na lolote lililoandikwa kwenye vitabu vya msiba wa Karbala, familia ya Imam ilizuiliwa kwenye jela ya kuta nne katika kipindi cha siku hizi.

Jela ambamo familia ya  (a.s.) waliwekwa wala hapakuwepo na kivuli kutokana na mwanga wa jua wakati wa mchana, au baridi wakati wa usiku. Ilikuwa ni kizuizi cha kuta nne tu ndimo walimokuwamo, ili wasiweze kutoroka.

Maelezo ya hapo juu yameandikwa na waandishi wa tukio la Karbala.[398] Sasa swali linalojitokeza ni kwamba familia ya Imam (a.s.) ilikaa jela kwa muda gani? Hakuna jibu kamili kwa swali hili, kama ilikuwa siku chache, wiki chache, au miezi michache. Imeandikwa kwenye vitabu vya msiba wa Karbala kuhusu hili, kwamba mtu alimuona Imam Sajjad (a.s.) amekaa kwenye lango la jela siku moja. Alipoona jinsi ngozi ya uso wake ilivyosawijika, alimuuliza Imam (a.s.) sababu ya hali hiyo. Imam alijibu, "Tuliwekwa kwenye jela ambapo hapakuwepo na kinga dhidi ya jua na baridi."[399]

Muda ambao familia ya Imam (a.s.) ilikaa Syria ulikuwa na mateso Makali sana kwao. Inasimuliwa na Imam Sajjad (a.s.) mwenyewe kwa sababu wakati moja aliulizwa, "Ewe bwana! Ni hatua gani ilikuwa na mateso sana kwenu? Ilikuwa ni ile safari ya kutoka Karbala kwenda kufa? Au kutoka

[397] Imeandikwa kama ifuatavyo kwenye *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk.348: Waliingia Damascus mnamo tarehe 1 ya mwezi wa Safar na walisimamishwa hapo Baabus Saa`at

[398] *Luhuuf*, uk. 188; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 771

[399] *Anwar-e-Numaniya*, Juz. 3, uk. 252; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 277

Kufa kwenda Syria? Au safari ya kutoka Syria kwenda Madina?" Imam (a.s.) akajibu, "Ash-Shaam, Ash-Shaam."[400] Safari a kwenda Syria ilikuwa ngumu sana kuliko sehemu zote. Sababu kubwa ilikuwa pale watu wa familia ya Imam (a.s) walipaswa kuingia ndani ya baraza la Yazid ambapo kila kitu cha kuwadhalilisha wao kiliwekwa.

Imam Sajjad (a.s.) anasema, "Miongani mwetu, watu kumi na mbili walifungwa kwa kamba moja. Ncha moja ya kamba hiyo ilifungwa kwenye mkono wangu na ncha nyingine ilifungwa kwenye mkono wa shangazi yangu Zainab. Tulifikishwa kwenye baraza la Yazid tukiwa katika hali hiyo ambapo Yazid alikuwa ameketi kwenye kiti chake cha kifalme akiwa amezungukwa na watendaji wake." Pia katika hali hii, Imam Sajjad (a.s.) alitoa maelezo ambayo yalimdhalilisha Yazid mbele ya kila mtu. Yazid hakutarajia kabisa kwamba mfungwa angeweza kuzungumza naye namna hiyo.

Imam Sajjad (a.s.) alimsemesha Yazid akasema, "Utaniruhusu niseme kitu?"[401] Yazid alitoa ruhusa lakini kwa sharti kwamba asije akasema kitu kichafu. Imam (a.s.) akasema, "Haiwezekani kwa mtu kama mimi kusema kitu kichafu kwenye baraza kama hili. Nitazungumza mantiki." (Kwa hakika Imam alisema hivi ili watu watambue kuhusu ukweli na waamke kutoka kwenye usingizi wao wa ujinga) "Yazid ameketi kwemye kiti chake cha enzi kama khalifa wa Mtume (s.a.w.w.). Itakuwaje kama Mtume akitokea hapa na kutuona sisi ambao ni dhuria wake, tupo katika hali hii?"[402]

**Kwa jina la Allah na kwake Allah na juu ya dini ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.).**

[400] *Tadhkiratush Shuhada,* uk. 412

[401] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 764; *Damaus Sujum*. uk. 247

[402] *Ishnal ba Qur`an*, Juz. 5, uk. 57

# MAJILISI 57

## WAFUNGWA WALIOHUISHA HISTORIA YA KARBALA

Historia ya Karbala ilihuishwa na wafungwa wa Karbala yaani wao ni walinzi wa umashuhuri wa Karbala. Upumbavu mkubwa sana wa watawala wa Bani Umayyah ulikuwa ni kuwakamata watu wa familia ya Imam (a.s.) kama mateka na kuwatembeza kwenye mitaa ya masoko ya mji Kufa na Syria. Kama wasingekuwa wamefanya hivyo, labda wangeweza kufaulu kupotosha historia ya tukio la Karbala au angalau wangeweza kuficha ukweli wake kwa kiasi fulani. Hata hivyo, walichimba Makaburi yao kwa mikono yao na wakafanya kitendo ambacho kilisababisha familia ya Imam (a.s.) kupata fursa ya kuhuisha historia ya Karbala daima milele.

Utawala wa Bani Umayyah haukutarajia kwamba wanawake na watoto waliodhikika wangenufaika na fursa hii kwa ukamilifu. Wangwezaje kufikiria hili? Walifanya propaganda ya uongo ili wafanikishe lengo lao.

### IMAM SAJJAD (A.S.) AHUTUBIA MKUSANYIKO WA SWALA YA IJUMAA

Ilikuwa siku ya Ijumaa huko Syria na watu walikuwa wanajiandaa kwa swala. Yazid alilazimika kuhudhuria swala kwa sababu labda angehitajika kuongoza swala (kwa sasa siwezi kuwa na uhakika kuhusu hilo). Ni lazima kwamba hotuba mbili zenye manufaa zitolewe kabla ya Swala ya Ijumaa. Baada ya hapo Swala inapaswa ianze kwa sababu hizi hotuba mbili huwa badala ya rakaa mbili za Swala ya Adhuhuri na Swala ya Ijuamaa huwa na rakaa mbili tu.

Mwanzoni kabisa msemaji wa serikali alipanda kwenye mimbari. Alimsifu Yazid na Muawiyyah kama kawaida na akahusisha mambo mazuri kwao. Halafu akasema mambo mabaya kuhusu Imam Ali (a.s.) na Imam Husain (a.s.) na akawalaani kana kwamba ( Mungu apishe mbali), walikuwa wameacha dini na wakafanya vitendo kama hivyo.

Imam Sajjad (a.s.) aliita kwa sauti ya kupaza, "Ewe msemaji! Unauza radhi ya Muumbaji kwa ajili ya kumfurahisha kiumbe."[403] Halafu akasema, "Ewe Yazid! Je, ninaweza kusimama kwenye vipande vile vya mbao na nizungumze?" Hii ni ajabu iliyoje! Ahlul-Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walizingatia hata mambo madogo katika akili zao. Mathalani, Yazid aliitwa 'Amiri wa Waumini' kwenye baraza lake lakini Ahlul-Bayt hawakumuita hivyo na hata hawakumuita kwa cheo chake. Walimuita kwa jina lake yaani 'Yazid.'[404] Wote wawili Imam Sajjad (a.s.) na Bibi Zainab (s.a.) walifuata mwenendo huo. Wakati huo, Imam Sajjad (a.s.) hakuiita mimbari ile kuwa ni 'mimbari' lakini aliita 'vipande vya mbao'. Mbao yenye ngazi tatu iliyoonekana kutokea hapo ilikuwa na msemaji duni sana aliyeipanda. Imam (a.s.) aliuliza kama angeruhusiwa kupanda kwenye vile vipande hivyo vya mbao na aongee japo maneno machache.

Yazid alimnyima ruhusa hiyo Imam (a.s.). Watu waliokusanyika hapo walimuunga mkono Imam kwa sababu alitokea Hijaz na walijua kwamba mazungumzo ya watu wa Hijaz yalikuwa yakuvutia sana. Pia walisisitiza Yazid amruhusu kwa sababu walitaka kuona mtindo wa uzungumzaji wa Imam (a.s.), lakini Yazid hakuruhusu. Mwanawe Yazid akasema, "Baba! Tafadhali mruhusu. Tunataka kumsikia kijana huyu kutoka Hijaz." Yazid akasema. "Ninawaogopa watu hawa." Hata hivyo, watu walisisitiza sana hivyo kwamba Yazid alilazimika kumruhusu.[405] Pia alitambua kwamba kama angeendelea kutaka uhalali zaidi, ingezidi kufichua udhaifu na woga wake; kwa hiyo alimruhusu.

Tazama, Imam Sajjad (a.s.) alikuwa mgonjwa na mateka wakati huo kwa sababu ya Mapenzi ya Mwenyezi Mungu (baada ya hapo, hakuugua tena, alipona na akaendelea na maisha kama Maimam wengine). Pia, kama inavyosimuliwa kwa kawaida kutoka kwenye mimbari, Imam (a.s.) alikuwa amefungwa kwa minyororo na alikuwa na mkanda mzito wa chuma ambao ulifungwa kwenye shingo yake. Alikwisha safiri hatua arobaini akiwa katika hali ile hadi kufika Syria. Pamoja na hayo, alipopanda kwenye mimbari hiyo alifanya nini? Alisababisha shauku kwa watu kiasi kwamba Yazid akajutia kosa lake.

[403] *Luhuuf*, uk. 188; *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 137
[404] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 137
[405] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 138; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 352

## EWE MUADHINI! NYAMAZA

Alianza kuhisi kwamba watu wangemrukia na kumuua. Kwa hiyo, alifikiria njia ya kujihami. Muda wa swala uliwadia. Alimuamuru Muadhini kusoma Adhana (wito kwa swala) kwani swala ilikuwa inacheleweshwa. Mara tu Muadhini alipopaza sauti Imam akanyamaza. Muadhini akatamka, "*Allah Akhbar, Allah Akhbar*." Halafu akasema, "Ninashahidilia kwamba hakuna mungu ila Allah" na Imam akarudia maneno hayo. Muadhini aliposema, "Ninashudilia kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah," Imam (a.s.) alivua kilemba chake na akasema, "Ewe Muadhini! Kwa ajili ya Muhammad, nyamaza," Halafu akamgeukia Yazid na akasema, "Ewe Yazid! Huyu mtume ambaye anashuhudiwa hapa ni yupi? Ni babu yako au babu yangu mimi? Halafu Imam akawageukia watu na akasema, "Enyi watu! Hivi mnatujua sisi ni nani? Ambao mmetukamata mateka? Baba yangu ni nani, Husain ambaye ameuawa Shahidi?"[406]

Watu walikuwa hawajui ukweli hadi wakati huo. Lazima utakuwa umesikia kwamba Yazid aliwaachia watu wa familia ya Imam Husain (a.s.) na akawarudisha kwao Madina kwa heshima.

Nu'man bin Bashir alikuwa mtu mpole na mwenye urafiki. Alipewa kazi ya kuwapeleka Madina watu wa familia ya Imam (a.s.) na kushughulikia mahitaji yao na kudumisha heshima yao. Hivi uliwahi kustaajabu tu kwa nini ilitokea hivyo? Hivi Yazid alibadilika haraka tu na kuwa mtu mwema? Hivi fikira zake zilibadilika ghafla? Hapana, hapana kabisa. Kwa uhalisia, jamii ya Damascus ilikuwa imebadilika. Lazima utakuwa umesikia kwamba Yazid alikuwa akimlaani Ibn Ziyad baadae na kumshutumu kwa makosa yote. Akawa na desturi ya kusema kwamba yeye hakumuagiza amuue Imam Husain (a.s.)[407] na kwamba Ibn Ziyad alifanya yote hayo kwa uamuzi wake mwenyewe.

Haya yote yalitokeaje? Yote haya yalitokea kwa sababu Imam Sajjad (a.s.) na Bibi Zainab (s.a.) waligueza mtiririko wa matukio.

[406] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 139; *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 353
[407] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 247; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 784

# MAJILISI 58

## GEREZA LA SYRIA

Waandishi wa historia wameandika kwamba mwanzoni watu wa familia ya Imam (a.s.) walipata matatizo mengi sana ndani ya gereza la Syria. Gereza hilo la kuta nne ambamo waliwekwa lilikuwa halina kinga dhidi ya jua na baridi. Hivyo, waliteseka usiku na mchana.[408] Hata hivyo, haukupita muda mrefu ambapo Yazid alijutia kosa lake la kisiasa. Hatuwezi kusema kwamba alitubu dhambi zake; lakini alitambua kwamba makosa yake kwenye siasa yangethibitisha kuwa ya hatari katika mamlaka yake ya utawala.

Baada ya hapo akawa na kawaida ya kumshutumu Ibn Yazid mara kwa mara. Alikuwa akisema, "Mwenyezi Mungu amlaani huyu mwana wa Marjana! Kamwe sikumwambia kupaka mikono yake kwa damu ya Husain. Nilimwambia ampore kilemba chake na aniletee lakini yeye akamkata kichwa na akaniletea. Mimi sikumuamuru kumuua Husain bin Ali (a.s.). Ibn Ziyad alimuua kwa hiari yake."

Yazid alirudia maneno yote haya mara nyingi. Hata hivyo, yote yalikuwa ni uongo. Alitaka kujiengua kwenye kosa hili kwa kuzungumza kwa namna hiyo na alijaribu kuuhamisha uhalifu wake kwa Ibn Ziyad ili kuhakikisha usalama wa utawala wake.[409] Ili aweze kuokoa utawala wake, alijaribu kuwahamisha wafungwa na kuwaweka kwenye sehemu nzuri zaidi. Kama angewaweka sehemu ile ile, watu wangesema, "Sawa, sasa tunaelewa kwamba Ibn Ziyad Alikuwa ndiye mpangaji mkuu wa kila kitu ndani ya Karbala lakini yeye hayupo hapa na wewe ndiye mwenye mamlaka yote. Sasa kwa nini unawatesa wafungwa hawa vibaya hivi?" Kwa hiyo, aliamuru wafungwa wahamishwe kwenye nyumba iliyokuwa karibu na kasiri yake. Baadaye alimuachia huru Imam Sajjad (a.s.) na kumruhusu kwenda mahali popote ndani ya Syria. Mara nyingi alimualika Imam Sajjad (a.s.) kuungana naye

[408] Luhuuf, uk. 188; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 771

[409] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 244; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, uk. 784

kwenye chakula cha mchana au cha jioni.[410] Hata alimuuliza Imam siku moja, "Hivi nikitubu toba yangu itakubaliwa?"[411]

Hapana nguvu wala uwezo isipokuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Aliye Juu na Mwenye nguvu

[410] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 244; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 1, 783; *Damaus Sujum*, uk. 265. Mhadhara huu haukurekodiwa zaidi kwa sababu ilikuwa mwisho wa kaseti.

[411] *Ashnai ba Qur`an*, Juz. 5, uk. 249-250

# MAJILISI 59

## IMAM SAJJAD (A.S.) – MFANO HALISI WA UPENDO

Shaksia ya Imam Sajjad (a.s.) ilikuwa mfano kamili wa upendo. Alikuwa upendo ulioonekana katika kila kipengele. Wakati wowote alipomuona mtu mgeni njiani, akiwa hana msaada, masikini na fukara, alikuwa akimliwaza na kumchukua na kumpeleka nyumbani kwake na kumtunza.[412]

Siku moja aliona kundi la watu wakoma (kwa kawaida, watu huwaepuka wakiogopa kwamba watawaambukiza ugonjwa huo),[413] aliwachukua na kuwapeleka nyumbani kwake na akawatunza vizuri.3 Nyumba ya Imam Sajjad iliyobarikiwa ilikuwa kimbilio la watu masikini, mayatima na wasiojiweza.

### KUHUDUMIA MSAFARA WA KWENDA HIJJA

Huyu ni mwana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.). Hata hivyo, hakusafiri na msafara ambamo walikuwepo watu waliomfahamu vema. Alikuwa na kawaida ya kungojea msafara unaotoka mbali sana ambamo hakuwemo mtu anayemtambua na alijiunga na msafara huo kama msafiri. Hatimaye, msafara kama huo ulifika na Imam aliruhusiwa kujiunga nao. Siku hizo, ilichukua siku kumi au kumi na mbili kusafiri kwa farasi au ngamia kufika mwisho wa safari. Imam (a.s.) aliuhudumia msafara huo katika kipindi hicho na aliendelea kusafiri kwa ajili ya Hijja. Wakati wa safari hiyo, mtu mmoja alijiunga na msafara huo naye akamtambua Imam (a.s.). Al-

[412] Muntahaiul Amaal, Jz. 2, uk. 15.

[413] Katika siku za zamani, watu walikuwa wakiuchukulia ukoma kama ugonjwa wa kuambukiza. Babu yake Imam Sajjad, imam Ali amani juu yao wote, pia aliwahudumia wakoma. Hii inathibitisha kwamba ugonjwa huu sio wa kuambukiza. Wakati jambo hili lilipotajwa kwenye moja ya vitabu vya Ustaadh Mutahhari, alipokea simu kutoka kwenye kituo cha ukoma kinachoendeshwa na wamishenari wa Kikristo. Walimuuliza: "Hivi ni kweli kwamba Imam Ali na Imam Sajjad waliwahudumia wakoma?" Yeye aliwajibu pamoja na ushahidi, nao walivutiwa sana na elimu na tabia ya msaada ya Maimam wetu (a.s.) na wakaomba rejea ambazo walipatiwa. (Ridhwani).

ipomuona Imam anawahudumia watu wa msafara, aliwauliza watu hao, "Hivi mnamjua mtu huyu anayewahudumia?"

Watu hao wakajibu kwamba hawamjui mtu huyo ni nani. Walichojua tu ni kwamba kijana huyo ni mtu wa Madina na alikuwa mtu mwema. Mtu huyo akasema, 'Ni sahihi kwamba hamumjui mtu huyu ni nani. Kama mngemtambua mtu huyu msingemtuma na kumruhusu awahudumie." Watu hao wakauliza kwa wasi wasi, "Wewe unamjua huyu?" Mtu huyo akajibu, "Ndiyo, ni mwana wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, huyu ni Ali mtoto wa Husain."

Mara tu watu walipotambua kwamba alikuwa Imam Sajjad (a.s.) walikwenda kwake wanakimbia na kuanguka miguuni pake. Watu hao wakasema "Ewe mtoto wa Mtume wa Allah! Kwa nini unatufanya tutende dhambi? Endapo tungethubutu kukudharau mahali popote, adhabu ya Mwenyezi Mungu ingetuangukia sisi. Wewe ni bwana wetu. Wewe keti hapa. Sisi tutakuhudumia." Imam (a.s.) akasema: "Hapana, kila ninapojiunga na msafara ambamo wamo watu wanaonitambua hawaniruhusu mimi kuwahudumia. Wao husema kwamba watanihudumia mimi; lakini mimi nataka kusafiri na msafara ambamo hakuna watu wanaonitambua ili nipate fursa ya kuwahudumia mahujjaji."[414]

## KULIA NA KUOMBA DUA KWA IMAM SAJJAD (A.S.)

Imam Sajjad (a.s.) hakupata fursa kubwa kama baba yake, Imam Husain (a.s.) au Imam Ja`far Sadiq (a.s.) kwa sababu mazingira ya kisiasa yalikuwa hayafai wakati wa kipindi chake. Hata hivyo, mtu ambaye anataka kuutumikia Uislamu, mara zote kwake ni wakati unaofaa kwake isipokuwa njia hutofautiana.

Tunaweza kukadiria hali hii kutokana na ukweli kwamba Imam Sajjad (a.s.) aliacha baada yake hazina ya muongozo kwa ajili ya Shi'ah katika namna ya dua. Alifanya kazi yake vizuri sana kupitia dua hizi. Watu wengine wana maoni kwamba kwa kipindi chochote Imam Sajjad (a.s.) alichoishi baada ya baba yake, kwa kuwa yeye hakupigana kwa upanga alipuuza mambo mengi yaliyohusiana na harakati za Karbala. Hata hivyo, hilo sio kweli. Imam Sajjad (a.s.) kwa kweli alitumia kila dakika katika kuhuisha harakati za Karbala.

[414] *Biharul Anwar*, Juz. 46, uk. 69; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 13

Imam Zainul Abidiin (a.s.) alikuwa anaomboleza mara kwa mara. Alifanya hivyo kwa kumbukumbu ya nani? Hivi hali ya Imam (a.s.) ilikuwa kama ya yule mtu anayelia bila lengo wakati hisia zake zimeumizwa? Hivi kuomboleza huku hakukuwa na maana kwamba Imam alitaka kuhuisha kumbukumbu za msiba wa Karbala? Hivi si kwamba Imam hakutaka watu wasahau kwa nini Imam Husain (a.s.) alijitoa mhanga maisha yake na ya wale wote waliouawa kishahidi pamoja naye? Hii ndiyo ilikuwa sababu hasa iliyomfanya Imam aomboleze; na wakati mwingine alikuwa anaomboleza sana.

Siku moja mtumishi mmoja alimuuliza Imam (a.s.), "Ewe bwana! Utaendelea kuomboleza hadi lini?" (alidhani kwamba Imam alikuwa anaomboleza kwa ajili ya ndugu zake) Imam (a.s.) akasema, "Unasema nini? Yakuub alihuzunika kwa ajili ya Yusuf mmoja tu na Qur`ani tukufu inasimulia hisia zake kwamba: **"Macho yake yaligeuka kuwa meupe kwa sababu ya huzuni."[415]** Ambapo mimi nimeona Yusuf kumi na nane wanauawa kishahidi mbele yangu, ambao wote walianguka kwenye ardhi ya Karbala mmoja baada ya mwingine."[416]

[415] **Surat Yusuf (12:84)**

[416] Biharul Anwar, Juz. 45, uk. 149; Seeri dar Seerat-e-Aimma-e-Athaar, uk. 112-114

# MAJILISI 60

## KIFO CHA KISHAHIDI CHA IMAM MUSA KADHIM (A.S.)

Kama inavyojulikana vema, leo ni usiku wa kifo cha kishahidi cha Imam wetu wa saba, Imam Musa Kadhim (a.s.). Alizaliwa mnamo mwaka wa 128 A.H. Hiki ni kipindi ambapo utawala wa Bani Umayyah ulikuwa kwenye kilele chake wakati alipouliwa kishahidi ndani ya jela la khalifa wa Bani Abbasi, Haruun Rashid mnamo mwaka wa 183 A.H. Alikuwa na umri wa miaka hamsini na tano wakati huo. Aliishi miaka ya mwisho wa maisha yake katika jela na alipewa sumu na kufa kishahidi ndani ya jela hiyo.[417]

Mshairi wa Kiarabu anasema:

"Watu wananidhihaki kwamba nilifungwa. Ninasema kwamba hayo si mapungufu. Hivi upo upanga wowote Mkali usiowekwa ndani ya ala?

"Hivi hamuoni kwamba simba anapozeeka, anakuwa na tabia ya kuishi kwenye tundu lake ambapo wanyama duni hukimbia hapa na pale?"

Maulana Rumi alisimulia kisa kwenye sehemu ya kwanza ya *Mathnawi* yake. Baada ya Nabii Yusuf (a.s.) kustahimili balaa lake, kutumbukizwa kisimani, akawa mtumwa na kuishi jela kwa miaka mingi, mmoja wa marafiki zake wa utotoni alimwendea. Maulana Rumi anasema:

"Siku moja rafiki wa utotoni wa Nabii Yusuf (a.s.) alikwenda kumtembelea. Akamkumbusha kuhusu uonevu na wivu wa kaka zake. Yusuf (a.s.) akajibu, "Sisi ni simba na matukio yale yalikuwa minyororo. Hata kama simba akifungwa kwa minyororo lakini hadhi yake haitaathirika. Hata kama shingo ya simba huyo inafungwa nyororo, itakuwa ni bora zaidi kuliko nyingine zilizofungwa."

Rafiki yake akauliza, "Hali yako ilikuwaje ulipokuwa jela na pale ulipokuwa kisimani?" Akajibu, "Hali yangu ilikuwa kama mwezi, ambao hupunguza awamu zake na hatimaye hutoweka na kisha kuwa mwezi kamili

[417] *Muntahaiul Amaal*,Juz. 2, uk. 287 na 366

na kutokeza tena. Ngano hufukiwa ndani ya ardhi lakini huota tena. Halafu husagwa kwenye kinu kuwa unga lakini thamani yake huongezeka na kuwa mkate baadaye. Wakati ngano hii ikisagwa na meno, hugeuka kuwa uhai, akili na utambuzi."

Kwa kuwa sehemu kubwa ya maisha yake ilitumika gerezani, hali ya Imam Musa Kadhim (a.s.) ni sawa na ile ya Nabii Yusuf (a.s.). Imetamkwa ndani ya Qur`ani tukufu kwamba mabibi wa Misri walijaribu kumtongoza Yusuf (a.s.) lakini yeye alichagua kwenda jela ili kuokoa imani yake na kutunza nguo zake za uchamungu zisitiwe doa.

قَالَ رَبِّ السِّجْنُ أَحَبُّ إِلَيَّ مِمَّا يَدْعُونَنِي إِلَيْهِ ۖ وَإِلَّا تَصْرِفْ عَنِّي كَيْدَهُنَّ أَصْبُ إِلَيْهِنَّ وَأَكُنْ مِنَ الْجَاهِلِينَ

فَاسْتَجَابَ لَهُ رَبُّهُ فَصَرَفَ عَنْهُ كَيْدَهُنَّ ۚ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

ثُمَّ بَدَا لَهُمْ مِنْ بَعْدِ مَا رَأَوُا الْآيَاتِ لَيَسْجُنُنَّهُ حَتَّىٰ حِينٍ

**"Akasema: Ewe Mola Wangu! Gereza linapendeza zaidi kwangu kuliko haya wanayoniitia. Na kama hutaniondolea vitimbi vyao nitawaelekea na nitakuwa miongoni mwa wajinga. Basi Mola Wake akamwitikia na akamuondoshea vitimbi vyao; hakika Yeye ni Msikizi, Mjuzi. Kisha ikawadhihirikia baada ya kuona ishara ya kuwa wamfunge kwa muda." [Sura Yusuf 12:33-35]** [418]

[418] Iblisi alimwambia Mwenyezi Mungu kwamba atauonyesha uovu kuwa kitu kizuri kwa watu na atamwelekeza kila mmoja kwenye upotofu lakini hila zake hazitafanikiwa kwa waja wema wa Mwenyezi Mungu. Allah akamjibu akasema: "Kwa hakika hutakuwa na mamlaka kwa waja Wangu waadilifu. Ni wale tu ambao wamepotea ndiyo watakaokutii wewe."

Mwenyezi Mungu akawasilisha mfano wa Nabii Yusuf (a.s.) kama mja muadilifu akasema:

وَلَقَدْ هَمَّتْ بِهِ ۖ وَهَمَّ بِهَا لَوْلَا أَنْ رَأَىٰ بُرْهَانَ رَبِّهِ ۚ كَذَٰلِكَ لِنَصْرِفَ عَنْهُ السُّوءَ وَالْفَحْشَاءَ ۚ إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُخْلَصِينَ

**"Na hakika (mke) alimtamani naye angelimtamani kama asingeona dalili ya Mola Wake. Hivyo ndivyo ilivyokuwa ili tumwepushie uovu na uchafu. Hakika yeye ni katika waja Wetu waliotakaswa."** [Sura Yusuf 12:24]

Wivu wa ndugu ulimtupa Nabii Yusuf (a.s.) ndani ya kisima na tamaa ya ngono isiyokubalika ya mabibi wa Misri ilimpeleka gerezani. Akawa mfungwa kwa miaka mingi.

فَلَبِثَ فِي السِّجْنِ بِضْعَ سِنِينَ

**"Basi (Yusuf) akakaa gerezani miaka kadhaa."** **(Surah Yusuf 12:42).**

Yusuf alipata utume akiwa gerezani na alipotoka gerezani alikuwa mtakatifu zaidi, mkamilifu zaidi na aliyedhamiria zaidi.

Yusuf (a.s.) alikuwa mtume, ambaye alitupwa kisimani kwa sababu ya kosa la yeye kupendwa zaidi na baba yake na alifungwa gerezani kwa kutambua haki, utakasifu na uchaji Mungu. Kutoka kwenye dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Imam Musa Kadhim (a.s.) alifungwa gerezani kwa miaka mingi kwa sababu watu walimpenda yeye na walimuona kuwa anafaa zaidi kwa uongozi kuliko Haruun Rashid. Tofauti pekee iliyopo ni kwamba Yusuf (a.s.) aliachiwa huru kutoka gerezani ambapo Haruun Rashid alimuua Imam kwa sumu akingali gerezani.

أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

**"Au wanawahusudu watu kwa alichowapa Mwenyezi Mungu katika fadhila Yake?"** **(Sura An-Nisaa 4:54)**

Bila shaka, wakatia wowote ule watu wenye wivu wanapoona radhi ya Mwenyezi kumpendelea mtu, huwa wanaona wivu na huanza kumsumbua mtu huyo.

Zulaikha alinuia kutenda tendo ovu kwenye chumba ambamo hamkuwa na mtu mwingine isipokuwa yeye na Nabii Yusuf (a.s.). Katika hali kama hiyo, kama Nabii Yusuf angekuwa hajaona ile dalili ya Mola wake angemuua Zulaikha au angetimiza matakwa yake kwa sababu alikuwa mfano bora wa uzuri wa sura, na Nabii Yusuf (a.s.) alikuwa ni madaha yaliyotoka kwa Mwenyezi Mungu. Pia, Nabii Yusuf (a.s.) alikuwa kijana na hajaoa na mazingira ya chumba kilichofungwa huhamasisha hisia za uovu. Pamoja na yote hayo, Nabii Yusuf hakutenda uovu kwa sababu tayari alikwishaona uthibitisho wa Mola Wake. Alikuwa mteule wa Allah na kutoka kwenye kundi la waja wema. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu akamuweka mbali na uovu. Uthibitisho aliouona Nabii Yusuf (a.s.) ulikuwa ni matokeo ya kitendo kizuri cha mtu na kitendo kibaya cha mtu. (*Islami Aqaid-Qur`an ki nazar mein*, Sayyid Murtaza Askari, kilichochapishwa na Jame Taalimaat-e-Islam, Pakistan) – Ridhwani.

Beti mbili za Kiarabu ambazo nilizinukuu mwanzoni mwa mhadhara huu pia zina maana ile ile. Kwamba, **"Watu wananidhihaki kwamba nilifungwa. Ninasema kwamba hayo si mapungufu. Hivi upo upanga wowote Mkali usiowekwa ndani ya ala? Hivi hamuoni kwamba simba anapozeeka, anakuwa na tabia ya kuishi kwenye tundu lake ambapo wanyama duni hukimbia hapa na pale?"**

Baada ya hapo mshairi anasema:

"Nyota ndogo hazionekani hadi jua lizame.

"Moto hubakia umefichwa ndani ya mawe na hauwezi kutumika hadi pale unapolipuliwa kwa kutumia zana.

"Kama kufungwa gerezani sio kutokana na uhalifu wa kimaadili, gereza si mahali pabaya."

Endapo mtu ametenda wizi, mauaji, kusema uongo, kueneza fitina na mahakama ikamtia hatiani na kumfunga gerezani; kwa kweli hii itakuwa ni sababu ya fedheha. Ni sababu ya kuvunjika kwa heshima na hata kama hakufungwa gerezani kwa sababu ya makosa haya, ni aibu. Hata hivyo, endapo mtu anakwenda gerezani kwa sababu ya kupigania haki na kupinga udhalimu, hicho ni chanzo cha fahari.

Gerezani ni mahali ambapo heshima ya mtu mwema huongezeka. Watu wanakwenda huko kumuona na wanaona fahari kuonana naye. Yeye hahitaji kwenda kwa watu.

Halafu mshairi huyo anasema:

"Machozi yalipokuwa yanatiririka kutoka machoni na moto wa shauku uliwashwa ndani ya moyo, nilimwambia aliyedhikika asiwe na wasi wasi kwa kuwa miguu yake ilifungwa minyororo. Minyororo hii ni pambo la wanaume."

## ATHARI ZA GEREZA KWA UHALIFU WA KUPENDA UHURU

Mambo mawili yanafaa kutajwa hapa. Kwanza kabisa, mateso anayopata mtu kwa kuunga mkono haki sio sababu ya masikitiko. Badala yake mateso hayo ni chanzo cha fahari. Ni muhimu kwa nukta hii kwamba tunatupa

jicho la haraka kwenye historia ambayo imejaa matukio kama hayo, ambamo watu mashuhuri walipoteza maisha yao kwa heshima; walifungwa na kuumia kwa mateso na ukatili. Mateso haya si tu ni sababu ya fahari kwa viongozi hao lakini pia ni kwa wanadamu wote.

Jambo jingine ni kwamba kuuvumila udhalimu kama huo ni njia ya kukamilisha roho ya ubinadamu. Maisha ya starehe za dunia ni kisababishi cha tabia mbaya na hupunguza ujasiri. Hakuna kitu kinachoweza kupunguza ujasiri, kuzalisha tabia mbaya na kuharibu maisha ya mtu zaidi kuliko maisha ya starehe za kidunia.

Nafsi hupata nguvu kutokana na kupitia kwenye dhiki na matatizo, na pia huimarishwa, na hapo dhahabu ya uwepo wa binadamu huwa safi zaidi na yenye nguvu. Almuradi mtu hakabiliwi na majanga na matatizo, utu wake haukamiliki. Mabadiliko hayawezi kutokea bila ya kuvunjika kwa utu. Maulana Rumi anasema kwamba mbegu ya ngano hutegwa wakati inapofukiwa kwenye ardhi. Hupasuka humo na huo ndiyo unakuwa mwisho wake. Baada ya hapo, huondoka na kuelekea kwenye hatua ya juu zaidi. Baada ya siku chache, hutokeza nje ikiwa katika umbo la mmea ukiwa na machipukizi mengi yenye kubeba mbegu ndani yake. Ngano inapochanganywa na udongo ardhini, huashiria mwanzo wa mabadiliko yake. Halafu ngano hii husagwa kwenye kinu na kuwa unga. Unga wa ngano hugeuka kuwa mkate. Wakati mkate unapotafunwa na meno, huyeyuka na ngano hugeuka kuwa akili na utambuzi baada ya kupita katika hatua mbali mbali.

## SHERIA YA VINYUME NA MIGONGANO

Sheria ya maumbile inaitwa "sheria ya migongano." Kufuatana na falsafa, kama hakuna ukinzani hakutakuwa na uwezekano wa muendelezo wa manufaa kutoka kwenye chanzo asili cha neema. Ni kweli kwamba ipo aina fulani ya mageuzi ndani ya kila mtu.[419]

Kama tukiangalia upande mwingine tunaona kwamba kila kitu kilichopo hukutana na vitu fulani katika hatua mbali mbali za mabadiliko, ambazo ni muhimu na zenye manufaa kwa kitu hicho katika hatua hiyo. Mathalani, ganda la tunda hulipatia tunda vuguvugu au kaka la yai, ambalo hulinda kiini cha yai na uteyai.

[419] *Al-Hikmatul Mutaliyyah fil Asfaar al-Aqliyyatur Rabaahu,* Juz. 7, uk. 77.

Ngozi hizi ni muhimu na zenye manufaa almuradi vuguvugu ni vuguvugu na yai linabakia kuwa yai. Kama mbegu ya tunda inataka kuendelea na kuwa mti au yai linataka kuwa kifaranga na halafu kuwa kuku mzima, halina njia nyingine isipokuwa kuvunja mipaka ya kaka la yai na kuwa huru.

Mipaka hii na kuta huvunjika kama matokeo ya ukinzani wa kimaumbile, na vikwazo huharibiwa na chemchem ya neema ya kimungu huanza kutiririka.

Kama matokeo ya matatizo haya, watu jasiri na wenye akili kupita kiasi na watu waadilifu huzaliwa. Nguvu na uwezo hutokeza upya. Viongozi mashuhuri walilazimika kuvumilia mateso na matatizo mengi na ni baada ya hapo tu ndipo waliweza kuongoza dunia kwenye mapinduzi makubwa.

## BIBI ZAINAB KUBRA

Historia yetu ya kidini ina mifano mingi kama hii. Bibi Zainab Kubra ni mmojawapo wa wanawake hao ambaye ni sababu ya fahari kwa Uislamu. Historia inasimulia kwamba mabalaa ya hatari na ukatili wa Karbala ni mambo ambayo yalimfanya Bibi Zainab kuwa imara zaidi. Bibi Zainab hakuwa kama yule yule wa zamani aliporudi Madina kama alivyoondoka. Alikuwa amebadilika sana baada ya kurudi kutoka Syria. Vitendo vigumu alivyofanya na kufanikiwa wakati wa kipindi alipokuwa mfungwa vilikuwa tofauti kabisa na vile vya Karbala ambapo kaka yake mashuhuri alikuwa bado hai na alikuwa na wajibu mdogo mabegani mwake.

Dkt. Aisha binti al-Shati ni mmoja wa wanawake wa Kiarabu wa wakati wetu ambao wamepata sifa stahilifu. Ameandika kitabu kiitwacho, *Batlatu Karbala* – Mwanamke shujaa wa Karbala. Kitabu hiki kimetarjumiwa kwa lugha ya Kiajemi na kilichapishwa mara kadhaa. Ameandika kwamba sababu zilizomfanya Bibi Zainab kuwa maarufu ni mabalaa ya Karbala. Matukio ya Karbala ndiyo yaliyosababisha Bibi Zainab kutoa hotuba kali ndani ya baraza la Yazid, ambayo wote mmeisikia.[420]

Mshairi wa Kiarabu Abu Tamaam anasema:

"Kama mti wa mshubiri hauchomwi moto

hakuna awezaye kutambua harufu yake nzuri."

[420] *Biharul Anwar*, Juz. 45, uk. 133

Saadi naye pia amewasilisha methali hii hivi:

"Neno la kawaida hutokeza tu

wakati moyo unapojaa huzuni."

"Kama mti wa mshubiri ambao hautoi

harufu nzuri hadi uchomwe moto."

Rudaki anasema:

"Dhiki kali sana huzaa

Ubora, umashuhuri na uongozi."

## KUSEMA NA KUTAMANI UKWELI

Imam Musa Kadhim (a.s.) alifungwa gerezani kwa 'kosa' kwamba alisema kweli na alikuwa na imani na uchaji Mungu. Kuna usemi wa Imam (a.s.), ambao alimuambia mmoja wa Shi'ah wake: "Angalia, ogopa hasira ya Mwenyezi Mungu. Sema kweli wakati wote hata kama inaonekana kusababisha maangamizi kwa sababu wawokovu wako upo humo; na kumbukumbu ya ukweli kamwe haielekezi kwenye uharibifu. Badala yake ukweli ni wakovu wa mwisho. Wakati wote jiweke mbali na uongo hata kama kuna wakovu wa wazi ndani yake, ukumbuke kwamba uongo huo hautakupatia wewe wakovu aslani."[421]

Shaykh Mufiid anaandika kwamba Imam Musa Kadhim (a.s.) alikuwa mcha-Mungu mkuu, mwanasheria, mhisani na mwenye jamala wa zama zake.[422] Kila wakati alikuwa akijisalimisha kwa Mola Wake na kuonyesha unyenyekevu wake. Alikuwa na desturi ya kuomba dua kila mara; **"Ee Allah! Ninaomba faraja wakati wa kufa na msamaha wakati wa hesabu ya matendo."[423]**

Alikuwa na kawaida ya kutafuta waombaji. Alikuwa na desturi ya kujaza fedha tasilimu, unga na tende kwenye chombo na kupita anagawa miongoni

[421] *Biharul Anwar*, Juz. 78, uk. 319
[422] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 292
[423] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 296

mwa watu masikini wa Madina kwa njia mbali mbali. Watu hao masikini wala hawakuwa wanamjua mhisani wao huyo ni nani.[424]

Imam Musa Kadhim (a.s.) alikuwa hafadhi wa Qur`ani tukufu asiye na mfano wa kulinganishwa ambaye aliijua kwa moyo. Alikuwa akiisoma Qur`ani kwa utamu kabisa hivyo kwamba iligusa nyoyo za watu. Wasikilizaji walikuwa wakilia wanaposikia usomaji wake. Watu wa Madina walimpa jina la *'Zain al-Mutahajjidin'* (Mbora zaidi miongni mwa wale wanaofanya ibada usiku).[425]

## GEREZA LA BASRA

Mnamo mwaka wa 179 A.H. Haruun aliondoka Baghdad kwenda Hijja. Alikwenda Madina kwanza na akamuita Imam (a.s.). Watu wa Madina walishituka. Palitokea machafuko miongoni mwa watu. Haruun aliamuru kwamba Imam apelekwe Basra mara moja wakati wa giza la usiku baada ya kumfunika kwenye kipando chake. Aliamuru kwamba Imam akakabidhiwe kwa Isa bin Ja`far, kiongozi wa Bani Abbasi hapo Basra. Mtu huyu alikuwa gavana wa Basra na binamu yake Haruun kwa upande wa kuumeni kwake. Imam (a.s.) alipelekwa huko na akafungwa gerezani. Haruun aliamuru kwamba kipando kingine zaidi kufunikwe na kupelekwa kuelekea Kufa ili kwamba watu waamini kwamba Imam (a.s.) alikuwa anapelekwa Kufa. Hivyo, watu wasingekuwa na wasi wasi kwani Kufa ilikuwa ndiyo kituo kikuu cha wapenzi na Shi'ah wa Imam na kwamba Imam (a.s.) asingedhuriwa huko. Hata kama baadhi ya watu wangejaribu kumrudisha Imam (a.s.) Madina, wangekwenda Kufa.[426]

Imam Musa Kadhim (a.s.) alikuwa mfungwa gerezani huko Basra kwa mwaka moja. Haruun alimwambia Isa kummaliza Imam akiwa ndani ya gereza lakini Isa hakukubali. Aliandika katika majibu yake, "Kila mara nimemuona mtu huyu akiwa katika ibada katika mwaka wote uliopita. Mtu huyu hana mapungufu katika ibada. Niliwateuwa watu fulani kumchunguza endapo huwa ananilaani mimi katika dua zake au hapana? Nikatambua kwamba huwa hasemi kitu chochote isipokuwa hujiombea huruma kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mimi siko tayari kushiriki katika mauaji ya mtu kama

[424] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 296
[425] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 298
[426] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 300; *Biharul Anwar*, Juz, 48, uk. 207-221; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 337

huyu. Wala sitaki hata kumweka ndani ya gereza kwa muda mrefu zaidi. Kwa hiyo mrudishe au nitamuachia huru."[427]

## GEREZA LA BAGHDAD

Haruun aliamuru kwamba Imam apelekwe Baghdad na kufungwa kwenye gereza la Fadhl bin Rabii. Haruun alimuamuru Fadhl bin Rabi pia kumuua Imam (a.s.) lakini alikataa pia. Halafu, Haruun alimkabidhi Imam (a.s.) kwa Fadhl bin Yahya Barmiki ili awe mfungwa wa gereza lake.[428] Fadhl bin Yahya alitenga chumba ndani ya nyumba yake kwa ajili ya Imam mtukufu na pia aliamuru kwamba pawepo na uangalizi wa karibu sana wa Imam (a.s.). Alipewa taarifa kwamba Imam huwa anaswali, huomba dua na kusoma Qur`ani Tukufu usiku na mchana na hufunga saumu mara nyingi. Yeye hashughuliki na jambo lolote isipokuwa ibada. Fadhl bin Yahya aliamuru kwamba Imam (a.s.) anapaswa kuheshimiwa na akawa anaangalia yeye mwenyewe binafsi kuhusu mambo ya kumliwaza Imam (a.s.).

Wapasha habari walimpa taarifa Haruun kuhusu hali hii. Haruun hakuwa Baghdad alipopata taarifa hizi. Mara moja Haruun aliandika barua ya kumkaripia Fadhl bin Yahya na akaamuru kwamba Imam auawe. Hata hivyo, Fadhl bin Yahya hakuwa tayari kufanya hivyo. Haruun hakuridhika kabisa. Aliandika barua tofauti tofauti kwa Sindi bin Shakik na Abbas bin Muhammad na akazituma kupitia mtumishi wake binafsi kwa jina la Masrur. Pia, alimuamuru Masrur kuchunguza kwa siri na kama Musa bin Ja`far (a.s.) alikuwa anaishi kwa starehe kwenye nyumba ya Fadhl bin Yahya basi huyo Fadhl achapwe viboko. Amri ilikubaliwa na Fadhl bin Yahya akachapwa viboko. Masrur aliandika maelezo yote kuhusu shughuli zake na akampelekea Haruun.[429]

Haruun aliagiza kwamba Imam (a.s.) akabidhiwe kwa Sindi bin Shahik kutoka kwenye ulinzi wa Fadhl bin Yahya. Sindi hakuwa Mwislamu na ni mtu mwenye moyo mgumu. Pia, wakati fulani Haruun aliwahi kutangaza hadharani kwamba Fadhl bin Yahya alikataa kutii amri zake, akamlaani na akawataka watu wamlaani. Hatimaye, watu wasio na huruma walimlaani

[427] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 300; *Biharul Anwar,* Juz. 48, uk. 233; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 338
[428] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 300
[429] *Irshad*, Shaykh Mufid, uk. 301; *Munatahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 341

Fadhl bin Yahya ili wamfurahishe Haruun.[430] Wakati baba yake Fadhl bin Yahya Barkimi, yaani Yahya bin Khalid Barmiki aliposikia habari hizo, alipanda farasi na alikwenda kuomba radhi kwa niaba ya mwanae. Haruun akakubali kumsamehe.[431] Hatimaye mtukufu Imam (a.s.) aliuliwa kishahidi kwa sumu ndani ya gereza la Sindi.[432]

## AFISA WA CHEO CHA JUU AMTEMBELEA IMAM

Siku moja Haruun alimpeleka mtu kumtembelea Imam ndani ya gereza la Sindi. Sindi alifuatana na huyu afisa wa cheo cha juu. Mjumbe huyu alipokutana na Imam (a.s.), Imam akamuuliza, "Unataka nini?" Yeye Akajibu, "Khalifa amenituma kuja kukutembelea wewe."

Imam (a.s.) akasema, "Nenda kamwambie khalifa wako kwamba kila siku ya mateso yangu hupunguza siku moja ya furaha yake. Wakati utakuja ambapo wote sisi wawili tutakuwa mahali pamoja. Madhalimu wataadhibiwa kwa matendo yao hapo.[433]

## KUTOSHEKA KWA IMAM MUSA KADHIM (A.S.)

Wakati alipokuwa kwenye gereza la Haruun, Haruun alipeleka ujumbe kwa Imam kupitia kwa Fadhl bin Rabii. Fadhl anasema kwamba alipofika gerezani, Imam alikuwa anajishughulisha na ibada ya Swala. Hakuthubutu kukaa pale kwa sababu ya kicho juu ya Imam. Alisimama akiwa ameegemea upanga wake. Imam wala hakuwa na habari naye hata baada ya kumaliza Swala yake. Imam akaanza kuswali Swala inayofuata. Baada ya hapo, Imam alikuwa anakaribia kuanza kusali Swala ya tatu ndipo alipoingilia kati na akasema:

"Khalifa amenituma nije kwako ili niwasilishe salamu zake kwako. Ameniomba nisitie mwanzoni cheo cha Amiri wa Waumini kabla ya jina lake na nitaje jina lake kama ndugu yako, Haruun. Anataka kukupa taarifa kwamba palikuwepo na kutokuelewana kwa sababu ya habari zisizosahihi. Sasa inajulikana kwamba wewe hauna makosa lakini yeye anataka kwamba wewe

---

[430] *MuntahaiulAmaal*, Juz. 2, uk. 341

[431] *MuntahaiulAmaal*, Juz. 2, uk. 341

[432] *Biharul Anwar*, Juz. 48, uk. 247

[433] *Al-Muntazim*, Juz. 9, uk. 88

ukae karibu naye wakati wote na usirudi Madina. Sasa imeamuliwa kwamba wewe utakaa karibu naye, anataka kujua wewe unapenda kula chakula gani. Mimi nimeteuliwa kushughulikia maliwazo yako."

Baada ya kusikia haya, Imam alimjibu Fadhl kwa sentensi mbili. Imam (a.s.) alisema, "Sina fedha ya kwangu mwenyewe ambayo ninaweza kutumia na sina tabia ya kuomba fedha hivyo kwamba niweze kukuomba wewe."[434]

Imam (a.s.) alionyesha kujitegemea kwake na kukinai kwake ndani ya haya maneno mawili na akathibitisha kwamba magereza hayawezi kudunisha shauku yake. Aliposema haya, Imam (a.s.) alinyanyuka na kuanza Swala yake nyingine kwa Takbir (*Allahu Akbar*).

> **"Ee Mola! Mzidishie neema Musa bin Ja`far ambaye alikuwa mrithi muadilifu, kiongozi wa wacha Mungu, aliyekuwa na siri za Nuru Tukufu ya ki-Mbingu, mtu mwenye shaksia adhimu na moyo uliotulia. Mwenye hekima na athari za elimu. Amani iwe juu yake kiongozi huyo ambaye aliyekuwa akikesha usiku kucha hadi asubuhi na kumuabudu Allah na kuomba msamaha mfululizo."[435]**

[434] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 339
[435] *Mafaatihul Jinaan*, Ziarat Imam Musa bin Ja`far Beest Guftar, uk. 161-173

# MAJILISI 61

## KIFO CHA KISHAHIDI CHA IMAM RIDHA

Leo ni siku ya maadhimisho ya kifo cha kishahidi cha Imam Ali Ridha (a.s.), kwa hiyo, nitanukuu hadithi fulani ili tuweze kujiunganisha na neema za uwepo wake mtukufu. Hadithi hii inaitwa *'Hadith Tauhiid'* na *'Hadith Silsilatuz Dhahab'* yaani hadithi ambayo nyororo yake ya wasimulizi ina wasimulizi ambao ni safi kama dhahabu.

### HADITH SILSILATUZ DHAHAB

Mathalani, kama hadithi inasimuliwa na msimulizi kutoka kwa Ahmad kutoka kwa Mahmuud kutoka kwa Khalid kutoka kwa Muhammad bin Muslim hadi inafika kwa Imam maasumin, wasimulizi walioko katikati wanaitwa nyororo (*Silsila*) yaani nyororo ya wapokezi.

Hadithi nitakayosimulia hapa, inaitwa '*Hadith Silsilatuz Dhahab*' - Hadithi ambayo nyororo yake ni ya dhahabu. Ni ulinganisho uliofanywa na wengine. Kwa nini? Kwa sababu ni usimuliaji hadithi ambao Imam Ridha (a.s.) amesema:

"Ninasimulia hadithi hii kutoka kwa Mtukufu baba yangu, Musa bin Ja`far kutoka kwa baba yake Mtukufu, Ja`far bin Muhammad kutoka kwa baba yake Mtukufu, Muhammad bin Ali kutoka kwa baba yake Mtukufu Ali bin Husain, kutoka kwa baba yake Mtukufu Husain bin Ali kutoka kwa baba yake Mtukufu Ali bin Abi Talib (a.s.) kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kutoka kwa malaika mkuu Jibril kutoka kwenye ubao na kalamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Muweza wa Yote."[436]

Sasa basi, ni nyororo ipi ya wapokezi inayoweza kuwa safi kama dhahabu kuliko hii? 'Ya Dhahabu' inatumika kwa kitu ambacho kwamba hakuna kitu kingine kinachoweza kufikiriwa kulinganishwa nacho kwa ubora wake.

[436] *Biharul Anwar*, Juz. 49, uk. 126; *Muntahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 453

## IMAM RIDHA (A.S.) ASIPITISHWE SEHEMU ZENYE SHI'AH WENGI

Tukio hili lilitokea huko Nishapur, ambalo linathibitisha ni kiasi gani watu hususani watu wa Irani waliwapenda Maimam (a.s.). Hata baada ya juhudi kubwa ya wale waliokuwa wanauunga mkono ukhalifa wa Bani Abbasi, inashangaza kwamba Maamuun alimfanya Imam Ridha (a.s.) kuondoka Madina kwa heshima zote ili kuonyesha diplomasia, jambo ambalo halitazungumziwa hapa kwa urefu.[437] Hata hivyo, alikwishatoa amri kwa siri kwamba Imam asipitishwe kwenye miji mikubwa inayokaliwa na Mashia wengi. Kwa hiyo, Imam alipitishwa kwenye maeneo yasiyokaliwa na Mashia na ambayo watu wa humo walikuwa hawamjui. Angalia heshima ya wazi aliyopewa Imam Ridha (a.s.) na Maamuun na hila yake ya kisiasa iliyokuwa imefichwa. Ndiyo sababu Imam (a.s.) hakupelekwa Qum, ambako kulikuwa ndio kituo cha Mashia. Mbali ya hili, Baghdad, Makao makuu ya ukhalifa haikuwa kituo cha kundi moja tu.

Sehemu hii ilikuwa inakaliwa na makundi yote. Ilikuwa inawezekana kumpeleka Imam pale lakini hakupitishwa huko kwa kuogopa hali ya uadui uliokuwepo dhidi ya Maamuun kwa sababu ya kuwepo kwake yeye hapo. Vivyo hivyo, pia Imam (a.s.) hakufanywa apitie mji wa Kufa na alipitishwa kwenye njia zisizojulikana hadi Nishapur. Sababu ni kwamba hawakutarajia kuwa wangekabiliana na uchangamfu mwingi kama huo na kwamba watu wangetoka majumbani mwao kwa idadi kubwa kwenye mji huu wa zamani sana wa Khorasan katika kumkaribisha Imam (a.s.).

## IMAM RIDHA (A.S.) NDANI YA NISHAPUR

Kipando cha Imam kilipofika Nishapur, umati mkubwa wa watu ulikusanyika kumkaribisha. Wanamume, wanawake vijana na wazee, kila mtu alimkaribisha kwa shangwe.[438] Wanachuoni wa jiji pia walikusanyika kwa mapenzi

[437] Watu wenye kuvutiwa wasome kitabu cha Ustaadh Mutahhari, kiitwacho *Siirat Aimma Athar.*

[438] Katika siku hizo, mji wa Nishapur ulikuwa ndio katikati ya Khorasan. Ilikuwa inaitwa Khorasani ya kati au Khorasan ya kusini. (Haikujumuisha miji ya Mawaraun Nahr, ambayo ipo kaskazini mwa Khorasan). Kulikuwa na miji mikubwa kama Balkh, Bukhara na Merv lakini katikati ya Khorasan ya sasa ilikuwa Nishapur. Tus ipo farsakh nne magharibi mwa Mash'had Sharif. Kuna kaburi la Firdausi hapo Tus. Katika siku hizo, Tus ilikuwa ni vitongoji vidogo. Ile sehemu ya Mash'had Sharif ya sasa ilikuwa na vitongoji viwili tu vidogo. Moja ya vitongoji hivyo ilikuwa ikiitwa Sanabad. Imam ar-Ridha (a.s.) amezikwa kwenye sehemu hii. Kitongoji kingine kiliitwa

juu ya Imam. Mwanachuoni mashuhuri kabisa wa jiji aliomba apewe heshima ya kushika hatamu za kipando cha Imam Ridha (a.s.). Hivyo, mwanachuoni mashuhuri kabisa wa Nishapur alipewa heshima hii.

Imam (a.s.) hakuruhusiwa kusimama mahali popote na watu wa Haruun. Alitakiwa kupita kwenye kila eneo kwa haraka kiasi iwezekanavyo. Kwa upande mwingine, watu walitaka sana kipando cha Imam kusimama kwa muda fulani. Hata hivyo, askari wenye silaha walikataa kutoa ruhusu wakisema kwamba walikuwa na haraka kwani Maamuun alikuwa anawangojea wao. Kama wakichelewa wataadhibiwa.

## NGOME YA TAUHIID

Watu walimuomba Imam mtukufu, "Ewe bwana! Tunataka uache kumbukumbu, ambayo itabaki na sisi daima milele. Hivyo, tunakuomba utupatie zawadi ya kitu wakati unapita na zawadi bora sana ingekuwa ni ile ya kutusimulia sisi hadithi, ambayo tunaweza kuindika na kuwa nayo daima milele."

Usemi wa kwamba watu elfu kumi na mbili walikusanyika wakiwa na kalamu ya dhahabu na karatasi kuandika hadithi na kwa hiyo, inaitwa '*Hadith Silsilatudh Dhahab*' hauna maana kabisa. Inaitwa 'Hadithi Silsilatudh

---

Naughan, ambacho ni mashuhuri kama mtaa wa Naughan hata leo. Sehemu hii ipo mwishoni mwa jiji la Mash'had. Umashuhuri wa kihistoria wa sehemu hii ni kwamba Haruun alipatwa na maradhi hapa alipokuwa njiani kwenda Khorasan. Halafu maradhi yake yakazidi sana hivyo alifariki dunia hapo na akazikwa Sanabad.

Tunajua kwamba Haruun amezikwa kwenye kaburi kubwa la Imam Ridha miguuni mwa kaburi lake katikati ya kuba. Kaburi la Imam Ridha (a.s.) halipo katikati ya kuba. Sababu ni kwamba kaburi la Haruun lipo katikati ya kuba na Maamuun alitaka Imam Ridha azikwe miguuni mwa kaburi la baba yake. Hata hivyo, kama ambavyo imesimuliwa kwenye riwaya nyingi, hali ya mambo yasiyo ya kawaida ilitokea na kusababisha Imam kuzikwa kichwani mwa kaburi lake. Mapema kuba hili liliitwa "*Baq-a`h haruniyyah*"

Dibil Khuzai alikuwa mshairi wa kushangaza. Katika istilahi ya kileo, anaweza kuitwa mshairi wa kimapinduzi. Kufuatana na maoni yangu, mshairi kama Dibil hajazaliwa katika zama zetu. Alikuwa na kawaida ya kusema kwamba alitembea huko na huko akiwa amebeba msalaba wake mabegani mwake kwa miaka hamsini. Ina maana, Dibil alinukuu beti kama hizo kwa mfululizo kwa miaka hamsini, jambo ambalo lingesababisha kifo chake wakati wowote. Dibli alikuwa mshairi ambaye aliwakasirisha Bani Abbasi. Mathalani:

"Yapo Makaburi mawili ndani ya Tus. Mmojawpo ni la kiumbe bora sana na jingine ni la kiumbe muovu sana na ukweli huu ni somo zuri.

Hivi yule umuovu anaweza kunufaika kutoka kwa yule mbora? Hivi yule mbora anaweza kuathiriwa na uchafu wa yule muovu? Kwa hakika hapana."

Kwa kawaida, beti hizi zingewakasirisha sana Bani Abbas. (Ustaadh Mutahhari)

Dhahab' kwa sababu kila mmoja wa wasimulizi wake ni maasum. Mahali hapa palikuwa kituo cha wasimulizi wa hadithi na hivyo, Imam (a.s.) aliombwa kusimulia hadithi.

Inasimuliwa kwamba Imam (a.s.) alipochungulia nje kutoka kwenye pazia la kipando chake na watu wakamuona, waliguta kwa mshangao ghafla tu, "Inaonekana kana kwamba tunamtazama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)."[439] Shauku ya watu ikaongezeka. Halafu Imam (a.s.) akasema:

**"Ninasimulia hadithi hii kutoka kwa mtukufu baba yangu kutoka kwa mtukufu baba yake na kuendelea vivyo hivyo hadi kufika kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na halafu kutoka hapo hadi kwenye ubao na kalamu na hatimaye Mwenyezi Mungu akasema, "Lile tamko la, 'hapana Mungu isipokuwa Allah',ndiyo ngome Yangu na yeyote anayeingia kwenye ngome Yangu atakuwa salama kutokana na adhabu Yangu."[440]**

Mtu anapoingia kwenye ngome ya tauhiid, kila kitu kinafuata baada ya hapo takriban kwa njia ile ile kama ambavyo herufi zote zinavyofuatwa na herufi A. Msingi wa dini ni *Tauhiid* - imani ya Mungu mmoja.

**Sifa za mwanzo na za mwisho ni stahiki**

**yake Mwenyezi Mungu**

**Na Mwenyezi Mungu amrehemu Muhammad**

**na kizazi chake tohara na kitakatifu**

**Na laana iwe juu ya maadui wao wote**

**tangu sasa hadi Siku ya Kiyama.**

## HOTUBA YA BIBI ZAINAB KUBRA NDANI YA SOKO LA KUFA

"**Sifa zote ziwe juu ya Mwenyezi Mungu na rehema za Mungu zimwendee baba yangu Muhammad na kizazi chake chema na cha mfano.**

[439] *Muntahaiul Amaal*, Juz. 2, uk. 451

[440] *Tauheed*, Saduuq, uk. 25; *Biharul Anwar*, Juz. 49, uk.127

**"Enyi watu wa Kufa, Enyi watu ambao ni walaghai na wadanganyifu:[441] Mnalia machozi? Na machozi yenu kamwe yasikauke na kilio chenu cha sauti za kupaza kamwe kisikome.[442] Nyinyi ni kama mwanamke anayefumua vipande vidogo vidogo uzi ambao yeye mwenyewe ameusokota kwa umadhubuti kabisa. Imani yenu si lolote bali ni udanganyifu na usaliti. Hivi wapo miongoni mwenu isipokuwa wapotovu, wasiofedheheka, wanaojivuna, wenye chuki, mwenye kujisifu mno, adui na watukanaji? Miongoni mwenu wapo wenye hila kama mmea unaopendeza unaokua kwenye uchafu, au madini ya fedha juu ya kaburi. Kwa hakika uovu ndio kitu ambacho nafsi zenu zimekitanguliza mbele yenu. Mwenyezi Mungu hafurahikiwi nanyi na mtadumu milele kwenye adhabu.**

**Mnalia na kuomboleza? Kweli, Wallahi! Lieni bila kikomo na mcheke bali kidogo tu, kwani kitendo chenu kilikuwa chenye fedheha ya kutisha sana hivyo kwamba kamwe hamtaweza kukilipia. Mnawezaje kutakasa uhalifu wa kumuua bwana kijana wa Mwisho wa Mitume, moyo wa ujumbe, bwana wa vijana wa Peponi, kimbilio la waungwana wenu, hifadhi ambayo mlikimbilia wakati wa mateso, uthibitisho kwenu wa kimungu unaong`ara, bwana wenu aliyelinda mwenendo wa Mtume.**

**Ni dhambi ya kutisha kiasi gani mliyofanya! Nendeni zenu, hapatakuwepo na msamaha juu yenu. Kwa hakika juhudi zenu zilishindwa, mikono yenu imepata hasara na matazamio yenu yamekuwa bure. Mmejifanya wenyewe kustahili ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Fedheha na udhalili vimeshushwa juu yenu.**

**Ole wenu! Mnajua jinsi mlivyopasua ini la Mtume wa Mwenyezi Mungu? Ni akina nani katika jinsia ya wanawake wa nyumba yake mliowavua stara na kuwaadhiri hadharani? Damu yake gani mliyomwaga? Heshima yake gani mliyokashifu?**

[441] Kwenye maelezo inasema: "Kuvunja Kiapo"

[442] Kwenye maelezo inasema: "Machozi yenu hayatakoma kutoka, na maombolezo yenu hayatatulia."

**Kwa hakika kabisa kitendo chenu kina ubaya wa kuhatarisha na kuchukiza, hivyo kwamba kilijaza ardhi na mbingu kinyaa. Mnastaajabu kwamba ilinyesha damu? Kwa hakika adhabu ya Akhera ni yenye fedhehesha daima zaidi na milele, na hamtasaidiwa. Msichukulie kirahisi kucheleweshwa kwa adhabu ya kwamba haiharakishwi kwa hofu ya kukosekana ulipizaji kisasi. Bila shaka yoyote Allah anatazama."** Halafu akaghani beti zifuatazo:

**Enyi watu wa Kufa! Mtatoa majibu gani wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) atakapowaulizeni nyinyi, "Mlifanya nini? Mlikuwa umma wa mwisho. Kwa nini mliwatendea watu wa familia yangu, kizazi changu na utakatifu wangu uovu wa namna hii? Kwa nini mliwafanya baadhi yao kuwa mateka ambapo wengine mliwafanya waogelee kwenye damu?**

**Hayo yalikuwa ndio malipo ya huduma yangu kama mjumbe kwamba mlifanya mambo kama haya kwa ndugu zangu?**

**Nahofia kwamba msije mkawa mnayo haki ya ile adhabu na iwaangukie kama ile iliyoonyeshwa kwa jamii ya Aad.[443] (Rizwani).**

[443] *Maqtal-e-Husain*, Muqarram, uk. 387; *Nuurul Absaar*, Shablanji, uk. 167. Imenukuliwa kutoka: *Hayatul Imam al-Husain bin Ali*, Baqir Sharif Qarashi, Juz. 3, uk. 335.

# MWISHO

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHJI AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu

21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo

47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar

73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali

99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa

125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu

151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Mshumaa.
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi

177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

# MUHTASARI

# MUHTASARI